**15 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

## MAJADILIANO YA BUNGE

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Tano – Tarehe 15 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa, tuketi.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo iliwasilishwa mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. PROF. JOYCE L. NDALICHAKO K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**SPIKA:** Ahsante sana.

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## MASWALI NA MAJIBU

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali tunaanza na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto, sasa aulize swali lake.

Na. 319

### Hitaji la Gari la Wagonjwa Hospitali ya Wilaya Lushoto

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka Gari jipya la Wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Lushoto kwa kuwa lililopo limechakaa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Dkt. Festo Dugange, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto mwaka 2023/2024 imepokea magari mawili ya kubebea wagonjwa na kupelekwa katika Vituo vya Afya vya Mlola na Mtae. Kwa sasa Hospitali ya Wilaya ya Lushoto inatumia gari la

kubebea wagonjwa kutoka kwenye Kituo cha Afya Mlola wakati taratibu za matengezo ya gari la hospitali ya wilaya zikiendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ununuzi wa magari ya wagonjwa kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya nchini; na Hospitali ya Wilaya ya Lushoto itapelekewa gari.

**SPIKA:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi, swali la nyongeza.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Spika, ninakushuku na nina maswali mawili ya nyongeza. Tuna vituo vya afya zaidi ya vitatu katika Jimbo la Lushoto, lakini chenye gari la wagonjwa ni kituo kimoja tu cha Mlola: -

Je, Serikali haioni kuwa kuna haja ya kuongeza bajeti ya kuwa na magari mawili ili kurahisisha usafiri kwa wagonjwa wetu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, wananchi wa Lushoto wamejenga zahanati mbili, Kata ya Kilole ambayo ni Mbeleyi na Kata ya Makanya ambayo ni Mdando. Hata hivyo, zahanati zile wamejenga kwa nguvu zao na hazijaisha: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza fedha kwa ajili ya kumalizia zahanati zile ili kuondoa usumbufu kwa wanaosafiri kufuata huduma za afya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kama ambavyo katika mwaka wa fedha 2023/2024 Serikali ilipeleka magari mapya mawili ya wagonjwa katika Halmashauri ya Lushoto, tunafahamu kwamba vipo vitu vya afya ambavyo vinahitaji magari ya wagonjwa, na tunafahamu kwamba safari ni hatua; tutaendelea kununua magari haya kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tayari magari mawili yamekwenda; na nimhakikishie kwamba, vituo vingine vya afya vitaendelea kupewa magari ya wagonjwa kwa kadri ambavyo tutakuwa tumeweka kwenye bajeti.

Mheshimiwa Spika, kwa swali la pili, kuhusu vituo vya afya katika kata hiyo, Kituo cha Afya Mbeleyi na Mdando. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Ofisi ya Rais - TAMISEMI tulikwishafanya tathmini na kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa ujenzi na ukamilishaji wa vituo vya afya katika kata zote za kimkakati, zikiwemo kata hizo mbili ambapo kuna Kituo cha Afya cha Mdando na Mbeleyi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Shekilindi kwamba Serikali itaendelea kupeleka fedha na tutahakikisha kwamba tunapeleka fedha kwa ajili ya vituo hivyo vya afya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abubakari Asenga, swali la nyongeza.

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kata ya *Msola Station* Kipo umbali wa kilometa 22 mpaka Mkamba: -

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa *(ambulance*) katika Kituo cha Afya cha Kata ya *Msola Station*?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Asenga, kwa sababu alikwishaleta hoja hiyo na tunatambua kuwa kituo kile cha afya kinahudumia wananchi wengi, lakini pia kiko umbali mkubwa kutoka kituo cha afya chenye gari la wagonjwa; tayari tumekiweka kwenye mpango wa vituo vya afya ambavyo vitapelekewa magari ya wagonjwa hivi karibuni.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini, sasa aulize swali lake.

Na. 320

**Kukarabati Barabara za Pembezoni Tabora Mjini**

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA** aliuliza: -

Je, upi mkakakati wa Serikali kukarabati barabara za pembezoni Tabora Mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mheshimiwa Zainabu Katimba, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2023/2024, shilingi milioni 585.2 zilitumika kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 46.6, ujenzi wa kalavati 4 za box, ujenzi wa kalavati 10 za mduara, ukarabati wa daraja moja na ujenzi wa mitaro mita 500 za urefu katika kata za Ikomwa, Ifucha, Itetemia, Uyui, Misha, Itonjanda na Ndevelwa.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2024/2025, zimetengwa shilingi milioni 703.7 ambapo kazi za kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 61, ujenzi wa kalavati 2 za *box*, ujenzi wa kalavati 20 za mduara katika kata za Uyui, Tumbi, Kabila, Ikomwa, Ifucha, Ntalikwa, Itonjanda na Ndevelwa zimekwishaanza kufanyika na zinatarajiwa kukamilika ifikapo Julai 2025.

Mheshimiwa Spika, serikali itaendelea kuihudumia miundombinu ya barabara na madaraja zikiwemo barabara za pembezoni mwa Mji wa Tabora kwa kuzijenga, kuzikarabati na kuzifanyia matengenezo kulingana na upatikanaji wa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, swali la nyongeza.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya

nyomngeza. Kwanza, ninaipongeza Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan. Sisi Tabora Mjini kwa kweli ndiyo maana tunaitwa Toronto, miundombinu yetu mingi imekuwa ni mizuri yakiwemo madaraja makubwa mawili yamekamilika. Katika kata ya Kabila (Daraja la Igombe) limekamilika na Ifucha pia tunaishukuru sana Serikali.

Mheshimiwa Spika, nina swali moja tu la nyongeza. Baada ya mvua hizi kunyesha kuna miundombinu mingi Tabora ambayo imeharibika sana. Ukianzia Kata ya Misha, ukipita Masagala mpaka unatokea Kata ya Mapambano, lakini unapokwenda Mzunguko kuanzia Kata ya Mtendeni, unaenda Kata ya Uyui, Kata ya Kakola mpaka Ikomwa kutokea Kabila barabara hizo sehemu nyingine hazipitiki kabisa.

Je, Serikali ina mkakati gani wa dharura wa Serikali kuhakikisha barabara hizi zinapitika katika kipindi hiki?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba kumjibu Mheshimiwa Mwakasaka; kwamba kama nilivyojibu kwenye majibu ya msingi kwamba, katika mwaka huu wa fedha 2024/2025 shilingi milioni 703.7 zimetengwa kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye barabara hizi kwenye barabara hizi katika kata alizozitaja.

Mheshimiwa Spika, fedha hizi zinatarajia kufikia kilometa 61; pia kujenga box karavati mbili na ujenzi wa karavati za mduara 20 kwenye kata ikiwemo Uyui, Tumbi, Kabila, Ikomwa, Ifucha, Ntalikwa, Itonjanda pamoja na Ndevelwa. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, kwamba, Serikali inaendelea na utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa barabara katika maeneo haya.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba mvua nyingi ambazo zimekuwa zikinysha zinaleta madhara na kuna baadhi ya maeneo ambayo mawasiliano yanakatika. Ndiyo maana Serikali ya Awamu ya Sita katika bajeti ya mwaka huu 2024/2025 imetenga bajeti ya ya dharura ya shilingi bilioni 71 ambayo hiyo

inatumika kurudisha mawasiliano katika maeneo ambayo mawasiliano yamekatika kabisa. Kwa hiyo, ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali inatambua mazingira yanayojitokeza na hata mazingira ambayo yanajitokeza katika Jimbo lako la Tabora Mjini tunachukua hatua za dharura kuhakikisha tunafikia maeneo kama uliyoyajataja kwa ajili ya kuhakikisha tunarudisha mawasiliano ili wananchi waweze kutumia barabara hizi ambazo zinawanufaisha kiuchumi, lakini zinawasaidia kufika katika huduma za msingi za kijamii. Tutaendelea kufanya hivyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Rita Kabati, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Barabara ya Mtandika – Msosa kilomita 16 ambayo ipi Ruaha Mbuyuni katika Wilaya ya Kilolo, hii barabara kwa kweli ina changamoto kubwa na imekata mawasiliano: -

Je, Serikali iko tayari sasa kurekebisha zile sehemu ambazo zimekatika mawasiliano ili iweze kupitika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, inafanya uwekezaji mkubwa sana katika kuimarisha barabara hizi za Wilaya zinazosimamiwa na *TARURA*. Ndiyo maana tutaona kwamba katika kipindi cha Awamu ya Sita bajeti ya *TARURA* imeongezeka maradufu. Hapo mwanzo bajeti ya *TARURA* kila mwaka ilikuwa ni bilioni 275, lakini tunavyozungumza tunatarajia katika mwaka wa fedha 2025/2026 bajeti ya *TARURA* itakuwa ni trilioni 1.8.

Mheshimiwa Spika, vilevile, ukiacha bajeti hiyo tu kunakuwa na bajeti ya dharura. Mathalani, katika mwaka huu wa bajeti tuna bilioni 71 kama bajeti ya dharura. Kazi kubwa ya bajeti hii ya dharura ni kufanya au kuchukua hatua za dharura kurudisha mawasiliano kwenye maeneo ambayo barabara zimekata mawasiliano ili wananchi waweze kuzitumia.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, niweze kumwagiza Meneja wa TARURA Mkoa wa Iringa, pamoja na wa wilaya waweze kufuatilia babaara hii ya Mtandika – Msosa aliyoitaja Mheshimiwa Ritta Kabati, na waweze kuiweka katika mpango kwa ajili ya kuhakikisha kwamba mawasiliano yanarejeshwa ili wananchi waweze kuitumia barabara hii ambayo inawanufaisha kiuchumi, lakini itawasaidia kufikia huduma za msingi za kijamii.

**SPIKA:** Mheshimiwa Kenneth Nollo, swali la nyongeza.

**MHE. KENNETH E. NOLLO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *Box* karavati ya Mayamaya – Mpondali iko kwenye *package* ya Miradi ya kuendeleza miji na tayari mkandarasi amepatikana: -

Je, ni lini Mkandarasi atafika *site* kuanza kazi ya ujenzi wa *box* karavati hiyo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie nafasi hii kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI kumkumbusha wajibu wa msingi Meneja wa *TARURA* wa Mkoa wa Dodoma pamoja na Meneja wa *TARURA* Wilaya ya Bahi kuhakikisha kwamba Mkandarasi huyu aliyepatikana anaweza kukabidhiwa kazi *(site)* na aweze kuanza kutekeleza Mradi huu kwa mujibu wa ratiba ya kazi ambayo ipo katika mkataba.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa George Natany Malima, Mbunge wa Mpwapwa, sasa aulize swali lake.

Na. 321

**Ujenzi wa Kingo za Korongo Mji wa Mpwapwa**

**MHE. GEORGE N. MALIMA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa kuimarisha kingo za korongo linalopita katikati ya Mji wa Mpwapwa ili kuzuia mmomonyoko na madhara kwa wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii kwa niaba ya Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Mheshimiwa Danstan Kitandula, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kutokea kwa korongo linalopita Katikati ya Mji wa Mpwapwa kumesababishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi ikiwemo uwepo wa mvua nyingi pamoja na shughuli zisizoendelevu za ukataji miti, kilimo na ufugaji katika safu za Milima Kiboriani. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Serikali kupitia Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa inaendelea kufanya tathimini ya kina ya ujenzi wa kingo za korongo linalopita katikati ya Mji wa Mpwapwa. Lengo la tathmini hiyo ni kubainisha gharama za ujenzi wa ukuta katika kingo hizo ili kupunguza mmomonyoko wa udongo na kunusuru maisha na makazi ya watu wa Mpwapwa. Kwa muktadha huo, ujenzi wa kuimairisha kingo hizo utaanza baada ya tathmini ya kina kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kutoa wito kwa halmashauri zote nchini kuendelea kusimamia kikamilifu Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura 191 ili kuzuia shughuli za kibinadamu na kuelimisha jamii juu ya utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa George Malima, swali la nyongeza.

**MHE. GEORGE N. MALIMA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa jibu zuri la Serikali, lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wananchi wa Mpwapwa wangependa kusikia: -

Je, ni lini hiyo tathmini ya kina itakamilika ili ujenzi uanze mara moja?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; ili kuweka uzito wa changamoto hii kule Mpwapwa: -

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari kutembelea Mpwapwa ili kujionea mwenyewe madhara yaliyosababishwa na hilo korongo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, jambo hili ni la dharura kwa hiyo Serikali inalifanyia kazi kwa udharura katika kuhakikisha kwamba tathmini hii inakamilika ndani ya kipindi kifupi. Ninaomba Mheshimiwa Mbunge awe na Subira wakati jambo hili linafanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na kutembelea eneo hilo, Serikali iko tayari, itatuma wataalamu wake ikiongozana na Waziri husika ili kuweza kwenda kujionea.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 322

**Kuboresha Makazi ya Askari Polisi Manispaa ya Shinyanga**

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA** aliuliza: -

Je, nini mpango wa Serikali wa kuboresha makazi ya Askari Polisi Manispaa ya Shinyanga kwa kuwa ni duni sana?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali inatambua uchakavu wa nyumba za makazi ya askari polisi katika manispaa ya Shinyanga na mikoa yote kwa ujumla hapa nchini. Katika Manispaa ya Shinyanga zipo jumla ya nyumba 84 za makazi ya askari polisi ambazo ni chakavu. Tathmini ya uchakavu kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati nyumba hizo imeshafanyika na kiasi cha fedha shilingi 1,848,000,000 kinahitajika.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutenga fedha toka kwenye Bajeti yake kila mwaka wa fedha ili kuweza kukarabati nyumba za makazi ya askari polisi hapa nchini zikiwemo za Manispaa ya shinyanga. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imekwishafanya tathmini na kubaini nyumba 84 pamoja na fedha bilioni 1.8: -

Je, ni lini ukarabati utaanza?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; katika Halmashauri ya Shinyanga kuna kituo cha afya ambacho ni chakavu tagnu enzi za mkoloni, na pale ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Shinyanga: -

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuhakikisha kwamba inajenga kituo kipya cha kisasa?

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imeshafanya tathimini na kubaini nyumba 84 pamoja na fedha shilingi bilioni 1.8. Je, ni lini ukarabati utaanza?

Swali la pili, katika Halmashauri ya Shinyanga kuna kituo cha afya ambacho ni chakavu toka enzi za Mkoloni na pale ni Makao Makuu ya Halmashauri ya Shinyanga. Je, ni nini mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba inajenga kituo kipya cha kisasa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Christina Christopher Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama tulivyojibu jibu la msingi, tathimini ishafanyika na ukarabati utaanza huu mwaka wa fedha 2026/2027.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuhusu mkakati wa kujenga kituo kipya kwenye Manispaa ya Shinyanga, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikijenga vituo vya polisi kupitia bajeti ya Serikali pamoja na mfuko wa tuzo na tozo. Kwa hiyo, tumechukua kituo hicho alichokitaja kwenye manispaa hiyo, tutakiingiza kwenye mpango na kutengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wote mliyosimama niliwaona, maswali yawe mafupi.

Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, swali la nyongeza.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Spika, Zima Moto Wilaya ya Tarime, hawana gari, hawana ofisi. Kwa hiyo utendaji wao kazi ni mgumu kwelikweli na wanashusha hadhi ya jeshi hilo.

Je, ni lini Serikali itatoa huduma hizo muhimu kwa watu wale wafanye kazi kwa heshima? Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Tarime Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Zima Moto, Serikali imeshaagiza na kununua magari 150 kwa ajili ya wilaya zote hapa nchini, ikiwepo na Wilaya ya Tarime.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu ofisi, nitoe wito kwa Mheshimiwa Mbunge na halmashauri itenge eneo tayari kwa ajili ya kuingiza kwenye mpango na kujenga Ofisi ya Zima Moto katika Halmashauri ya Tarime. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Zacharia Paulo Issaay, swali la nyongeza.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Mbulu ni wilaya kongwe nchini, makazi ya Askari Polisi na Magereza katika wilaya hiyo ni chakavu sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuweza kujenga makazi mapya na kukarabati yale yaliyopo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zacharia Issaay, Mbunge wa Mbulu Mjini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kila mwaka imekuwa ikitenga fedha kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa makazi ya Askari Polisi na Magereza hapa nchini. Na hiki cha mji wa Mbulu pia tutakichukua kuingiza kwenye mpango na kutengewa fedha kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Flatei Massay, swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, Jimbo la Mbulu Vijijini ina vituo vitatu vya Polisi na Mheshimiwa Naibu Waziri, unavijua na hakuna makazi kabisa ya polisi. Je, lini unaweka hata bajeti ya kujenga makazi haya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Flatei Massay, Mbunge wa Mbulu Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, Serikali inatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa makazi ya Askari Polisi. Kwa hivyo alivyovitaja vya Wilaya ya Mbulu Vijijini pia tutavichukua tayari kuingiza kwenye mpango na kutengewa fedha kwa ajili ya kufanyia ujenzi. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, makazi ya Askari wa Jeshi la Magereza nchini ni chakavu sana, hasa Gereza la Tarime na Gereza la Matongo, lililopo Mkoa wa Simiyu. Ninataka kujua mkakati wa Serikali kuhakikisha kwamba wanaboresha makazi haya ya Askari wa Jeshi la Magereza?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu kwenye jibu la msingi, Serikali imekuwa ikifanya tathimini ya uchakavu wa makazi ya Askari Polisi na Magereza hapa nchini na nimuhakikishie Mheshimiwa Esther, pia na ya Tarime tutaingiza kwenye mpango na tayari kwa ajili ya kufanyiwa ukarabati. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Minza Mjika, swali la nyongeza.

**MHE. MINZA S. MJIKA:** Mheshimiwa Spika, majengo ya Askari Polisi Mkoa wa Simiyu ni hakuna kabisa tuseme hivyo, lakini Wilaya ya Maswa ni wilaya ambayo ni kongwe, haina kabisa majengo ya Askari Polisi na majengo yaliyopo yamechakaa kabisa yapo chini ya kiwango. Je ni lini Serikali itajenga makazi mapya?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Minza Mjika, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, tutachukua nyumba za Askari Polisi ambazo hazipo kabisa kwenye Wilaya ya Maswa ili tuingize kwenye mpango na kutengewa bajeti kwenye miaka ya fedha ianyokuja. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maryam Azan Mwinyi, swali la nyongeza.

**MHE. MARYAM AZAN MWINYI:** Mheshimiwa Spika, je ni lini Serikali itazifanyia ukarabati makazi ya Polisi, nyumba zilizopo Kengeja na mkoani, mkoa wa Kusini Pemba? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Serikali imekuwa ikitenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ukarabati wa nyumba za Askari Polisi kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, mkoani kule Pemba. Lakini nimuhakikishie pia maeneo haya aliyoyataja pia tutakaa na Mheshimiwa Mbunge, tutaingiza kwenye mpango tayari kwa ajili ya kutengewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa makazi hayo. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Mhandisi Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 323

**Kuwaandaa Wanawake wa Tanga na Kilimo cha Mbogamboga**

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE** aliuliza: -

Je, upi mkakati wa kuwaandaa Wanawake wakulima wa mbogamboga Mkoani Tanga kwenye mpango wa Tanga kuwa *hub* ya kilimo cha mbogamboga?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa *engineer* Mwanaisha Ulenge, kama ifuatavyo: -

Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imekiwezesha Kituo cha Utafiti cha Mlingano *TARI* kuwa kituo mahiri katika uzalishaji wa mazao ya viungo, karafuu na mboga. Pia Wizara inaendelea kutoa mafunzo ya kanuni na teknolojia bora za kilimo cha mboga kushirikiana na sekta binafsi ikiwemo *TAHA* kujenga vituo na miundombinu ya kuhifadhi mazao ya mbogamboga ikiwemo vyumba vya baridi na kutoa mafunzo ya ukusanyaji, ufungashaji na uhifadhi wa mazao kabla ya kusafirishwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa majibu mazuri ya Serikali, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali imechagua Mkoa wa Tanga kuwa miongoni mwa kanda zitakazozalisha *hot culture*, hamuoni haja sasa yakutengeneza fikra za vifungashio, kumlinda mlaji na kuongeza thamani za mbogamboga zinazolimwa na wanawake wa Mkoa wa Tanga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kwa kuwa sasa tumeona magari ya kuchimba visima vya umwagiliaji vimeshaingia nchini. Je, Serikali hamuoni haja ya kutoa kipaumbele kwa Mkoa wa Tanga kuchimbiwa umwagiliaji ili zile mboga kwa sababu ni mazao ya haraka yalete tija. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Eng. Ulenge, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali sasa hivi na Mkoa wa Tanga ni mmoja wa mpango huo, wataalamu wa wizara wameshaanza kufanya tathimini ndani ya Mkoa wa Tanga kwa mazao yote, kwa maana ya viungo, matunda na mbogamboga ili kuanzisha mfumo wa ukusanyaji wa mazao na namna ya kuyauza na kuyafungasha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni mchakato ambao tunaendelea nao, na *feasibility study* inaendelea katika maeneo yote ambayo ni maeneo yaliyoteuliwa kama maeneo ya uzalishaji wa mbogamboga na viungo. Kwa hiyo, nataka nimtoe hofu na niwaambie wananchi wa Mkoa wa Tanga kwamba ni jambo ambalo Serikali inalifanyia kazi na hivi karibuni tutakuwa na taarifa rasmi kwa ajili ya kuanza kutekeleza.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji wa visima, nataka niseme tu kwa Wabunge wote, mikoa yote itapewa kipaumbele. Lakini tutawapa vipaumbele maeneo ambayo tayari tathimini ya awali imeshafanyika, mpaka sasa tathimini ya awali imeshafanyika kwa halmashauri 75 ambazo zitaanza kufanyiwa huu utaratibu na utaratibu wa uchimbaji wa visima hivi, hivi karibuni Serikali itautangaza kwa kuwa na mwongozo, tutakuwa na skimu ya wakulima watako chimbiwa bure kwa 100% lakini watakuwepo wakulima ambao watakuwa wanachangia gharama kidogo ili waweze kuchimbiwa.

Mheshimiwa Spika, mfumo wa uchimbaji hautakuwa kila mkoa kupelekewa gari, Serikali imenunua magari zaidi ya 22, 23 ambayo mpaka tarehe 15 Juni, yatakuwa yamefika yote, *then* tutatangaza ni mkoa gani tunaanza kuchimba. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, tusubiri baada ya hiyo *public announcement* itakayofanyika kila mkoa utafahamu magari yatakwenda lini katika mkoa husika.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza, Mheshimiwa Dkt. Thea Ntara, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. THEA M. NTARA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba zile mbegu zinazouzwa madukani zote zina ubora na zina bei nafuu ili wanawake waweze kuzinunua kwa uhakika?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ntara, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, suala la ubora Serikali imeendelea kuongeza uwezo wa taasisi yetu ya udhibiti ya Mbegu ya *TOSCI* na msimu ujao wa Kilimo Wakulima wataona kuna *new label* ambayo inawekwa katika mifuko yote iliyopo sokoni, hilo la kwanza.

Mheshimiwa Spika, la pili, ili kutatua tatizo la mbegu *fake*, Serikali imeamua sasa hivi kusajili upya wauzaji wa vijijini, wa mikoani na kuubadili mfumo wa usambazaji na wasambazaji wote wataingizwa kwenye *database* maalum.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kupunguza gharama, Serikali imeanza kuweka ruzuku katika mbegu; tumeanza Ngano, Alizeti na sasa tumeingiza zao la Mahindi. Malengo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba tunapunguza gharama za Mbegu kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile tumeanza kuihusisha sekta binafsi kuanza kutumia mashamba ya Serikali ambayo yalikuwa

hayatumiki kabisa yamegeuka mapori kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wetu wa mbegu ili kuweza kuhakikisha kwamba *availability* na *affordability* inatokea sokoni. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Angeline Mabula, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Manispaa ya Ilemela inao Wakulima wachache wanaolima mbogamboga kutokana na eneo kuwa dogo. Je, Serikali haioni sasa ili kuongeza tija kwa wakulima wale kuwaanzishia vitalu nyumba ili waweze kuzalisha mazao kwa tija?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mabula, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nikiri ameshakuja ofisini kwangu, tumeshakaa na nataka nimuhakikishie yeye na wakulima wadogo wa Wilaya ya Ilemela, Serikali inaanza kulifanyia kazi baada ya bajeti ya mwaka huu, skimu ya Wakulima wa Ilemela na maeneo hayo; *Lake Victoria* yote wataona ndani ya bajeti ya Serikali tumeweka mpango kwa ajili yao. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Saashisha Mafuwe, swali la nyongeza

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Katika Jimbo la Hai, wapo wananchi wengi wanaolima zao la Nyanya kwa wingi na kufanya zao hili kuwa sokoni kwa wingi na bei yake kushuka.

Je, ili kudhibiti thamani ya zao hili la Nyanya, Serikali ina mpango gani wa kujenga kiwanda cha kuchakata zao la Nyanya katika Jimbo la Hai, ili thamani ya zao hili iweze kuongezeka? *(Makofi)*

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, nataka nijibu swali la Mheshimiwa Saashisha...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, naomba nisiseme sasa hivi tuna mpango kwa ajili ya Hai lakini nimelipokea, tunaweza kukaa pamoja kujadili, kuangalia *scale* kama ambavyo tumekaa pamoja ku-*unlock* matatizo ya masoko mawili katika jimbo lako kwa ajili ya Wakulima wa mbogamboga. Kwa hiyo, nikuombe tu kwamba mimi na wewe tupate muda tuweze kujadili, tutatuma wataalamu tuangalie ili tuwe na mpango, kila eneo lina mpango wake.

Mheshimiwa Spika, lakini kuhusu kuongeza thamani nataka niwahakikishie Wabunge, kwenye bajeti tutakayokuja nayo tutakuwa na mpango maalum wa uongezaji wa thamani ambao utasimamiwa na Wakulima wadogo *(backyard processing)* kwa mazao yote ili tuweze kuongeza thamani ya mazao yetu sasa hivi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, naomba radhi, nilikuwa namaanisha kuuliza swali linalofuata, samahani sana. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, swali lake litaulizwa, naona Wabunge wawili mmesimama, mwenye majibu? Wewe ndio una majibu? Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, kwa niaba yake.

Na. 324

**Ujenzi Bwawa la Yongoma - Same**

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA K.n.y. MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA** aliuliza: -

Je, lini ujenzi wa Bwawa la Yongoma - Same utaanza baada ya kukamilika kwa usanifu wa kina?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kaboyoka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilikamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bwawa la Yongoma lenye ukubwa wa mita za ujazo 5.8 katika mwaka 2023/2024. Baada ya usanifu kukamilika, mradi huo umewekwa kwenye mpango wa ujenzi kwa mwaka 2025/2026. Kukamilika kwa ujenzi wa bwawa hilo kutawezesha kumwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 1,800 na kunufaisha wakulima 11,150 katika kata za Fidia, Ndungu, Kalemawe na Bendera.

**SPIKA:** Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, swali la nyongeza.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. Kwa kuwa kata alizozitaja ambazo ni Maore, Ndungu, Kalemawe, Kihurio na Bendera, zimeathiriwa sana na ukame kutokana na hali ya mabadiliko ya tabia ya nchi na kwa kuwa wananchi wanashughulika na Kilimo. Je mnamkakati wa kumaliza bwawa hilo haraka ili wananchi waweze kufaidika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili, kuna mradi wa *BBT* katika Wilaya ya Muleba, Kata ya Kamachumu, Kata ya Ruhanga, Kijiji Makongola na mradi huo wananchi wanapanda …. na unaendelea vizuri lakini kuna tatizo kubwa sana la maji ya kumwagilia. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba maji yanapatikana ili mradi huu uweze kuwa na tija. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa kumaliza mradi huu wa Yongoma kwa haraka? Ndiyo, ni mpango wa Serikali na ndio maana tumeshakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina

na tumeweka kwenye bajeti ya mwaka 2025/2026 kwa ajili ya utekelezaji wa bwawa na eneo linalofaa kwa Kilimo.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ukanda ule wakati wa kiangazi, wakati wa masika wanapata maji mengi sana kwa muda mfupi, wakati wa kiangazi wanakuwa na ukame. Kwa hiyo, niwahakikishie tu wananchi wa maeneo hayo kwamba Serikali itaanza kujenga bwawa hili katika Mwaka wa Fedha wa 2025/2026 pamoja na eneo la hekta zaidi ya 1,000 ambazo zitakuwa ni kwa ajili ya Kilimo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mradi wa *BBT* wa Kagera, kwanza niseme tu niwakupongeze viongozi wa Serikali wa mkoa lakini nitumie nafasi hii kuwahakikishia na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mbunge nikushukuru kwa wewe kuwa sehemu ya wakulima wa eneo lile, nakushukuru sana.

Mheshimiwa Spika, nikuhakikishieni tatizo la barabara zile kilometa chache tunaziweka kwenye bajeti ya mwaka kesho na tutawachimbia visima, kwa sababu tayari usanifu umeonyesha kwamba upatikanaji wa maji yapo, tutaleta magari kwa ajili ya uchimbaji kwenye eneo lile. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, swali la nyongeza.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kupata nafasi hii, naomba kuuliza swali langu la nyongeza ambalo Mheshimiwa Waziri ni la muhimu sana. Kwa kuwa Bwawa la Yongoma linahitajika sana kwenye kata zilizotajwa hapo. Je, Serikali hamuoni kwamba mchukue ujenzi wa bwawa hili kama mkakati mkubwa wa Serikali? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mama Kilango, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, yeye mwenyewe alinipeleka tukatembelea Ndungu, tukatembelea hadi kule juu milimani na

ameona Serikali imeanza kutekeleza mradi wa Mlimani, tumeanza kutekeleza mradi wa skimu ya Ndungu. Nikuhakikishie Mheshimiwa Mama Kilango na wananchi wa Same, kama tulivyowaahidi kwenye mkutano pale kijijini mimi na wewe, mradi huu tutautekeleza na tutajenga bwawa hili na skimu hii kama inavyotarajiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Jackson Kiswaga, swali la nyongeza.

**MHE. JACKSON G. KISWAGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kuuliza swali. Je, ni lini sasa Serikali itakamilisha usanifu wa kina katika Bwawa la Magubike katika Kata ya Nzihi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, kama ifuatavyo; -

Mheshimiwa Spika, wataalam wapo hatua za mwisho kumalizia Bwawa la Magubike na nikuahidi Mheshimiwa Kiswaga, kwenye bajeti ya mwaka kesho 2025/2026 Magubike itakuwepo na tutaanza ujenzi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Venant Daud Protas, swali la nyongeza.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Bwawa la Goeko awamu ya kwanza lipo asilimia 98, tuna awamu ya pili na Mkandarasi ameshapatikana. Ni lini sasa Mkandarasi atakwenda kukabidhiwa *site* na kuanza ujenzi wa Bwawa la Goeko ambalo katika historia ni bwawa kubwa? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venant, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kwanza nimshukuru kwa *support* anayotoa kwenye mradi wa Goeko kama Mbunge, Mkandarasi ameshapatikana, mkataba umeshasainiwa na sasa tumepeleka maombi Wizara ya Fedha kwa ajili ya kupata *advance payment*

kwa ajili ya yeye kwenda *site*. Nimuhakikishie tu kwamba mradi ule *phase two* unahusisha bwawa hilo kulikamilisha na vilevile kujenga jumla ya hekta 3,000 ambazo tulitembelea pamoja mimi na yeye kukagua lile eneo. Nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia swali la nyongeza. Ningependa kujua ujenzi wa Bwawa la Kidete utakamilika lini, ili kupunguza maporomoko ya Mto Mkondoa Wilayani Kilosa? Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naomba tu nimwambie Mheshimiwa Ishengoma, kwamba Bwawa la Kidete ni moja ya mabwawa muhimu, kwa maana ya ukanda wa yale mabwawa matano yote, kwa ajili ya kuondoa matatizo ya mafuriko katika Wilaya ya Kilosa na Serikali itaendelea kusukuma kuhakikisha hiyo miradi yote inakamilika kwa wakati.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke, swali lake litaulizwa kwa niaba yake...

Haya nawaona Wabunge watatu mmesimama, sasa Mbunge mwenye majibu ni yupi kati yenu? Haya naambiwa, aaah! ni huyu huku eeh? Haya sawa, Mheshimiwa Zuberi Mohamedi Kuchauka, kwa niaba ya Mheshimiwa Dorothy George Kilave.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Afya, Mheshimiwa Dorothy George Kilave, Mbunge wa Temeke swali lake litauliza kwa niaba yake yake. Haya, ninawaona Wabunge watatu mmesimama, sasa Mbunge mwenye majibu ni yupi kati yenu? Haya ni huyu huku, haya, sawa.

Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, kwa niaba ya Mheshimiwa Dorothy George Kilave. *(Makofi)*

Na. 325

**Kuongeza Majengo Hospitali ya Rufaa Temeke**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA K.n.y MHE. DOROTHY G. KILAVE** aliuliza: -

Je, kuna mpango gani wa kuongeza majengo katika Hospitali ya Rufaa ya Temeke?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Wizara inaendelea na maboresho ya miundombinu ya Hospitali za Rufaa za Mikoa Nchini ambapo kwa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Temeke, Wizara inaendelea na maandalizi ya michoro ya usanifu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Huduma za Kliniki za Kibingwa na Bima. Utekelezaji wa ujenzi wa jengo hilo unatarajiwa kuanza katika mwaka 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninashukuru kwa majibu mazuri yanayotia matumaini kutoka Serikalini lakini nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, sambamba na ujenzi huo, bado Temeke kuna changamoto ya watumishi hasa wa Madaktari Bingwa. Je, Serikali ipo tayari inapofanya tathmini ya ujenzi huo iende sambamba na kuongeza watumishi kwenye hospitali hiyo? *(Makofi)*

Swali la pili, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Lindi ni hospitali chakavu, ni hospitali ya siku nyingi sana. Je, Serikali ipo tayari kuifanyia ukarabati hospitali hiyo ili iendane na wakati uliopo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ninaomba nijibu maswali mawili ya Kaka yangu Mheshimiwa Kuchauka, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Spika, moja ni kweli kwamba kuna baadhi ya maeneo kuna upungufu wa Madaktari Bingwa lakini ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Kuchauka, katika hospitali zenye Madaktari Bingwa wengi moja wapo ni Temeke, lakini ni kweli tunapoongeza hili jengo na kwa sababu ya idadi ya watu tupo tayari pia kuongeza Madaktari Bingwa ili kukabiliana na namba ya watu itakayokuwepo kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, swali lako la pili, kuhusu Hospitali ya Mkoa wa Lindi, hii ni mojawapo ya hospitali za Mikoa ambazo huu upembuzi yakinifu na michoro inatengenezwa kwa ajili ya kuhakikisha inakuwa nayo mpya na kufanana na hospitali zingine za Mikoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge nimewaona, shukrani zetu nimeshapokea, kwa hiyo msinishukuru tena kwa sababu muda wetu unakimbia, pia upande wa Serikali huna haja ya kumtaja Mbunge ikiwa nimeshamtaja.

Mheshimiwa Aysharose Mattembe, swali la nyongeza.

**MHE. AYSHAROSE N. MATTEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa, ujenzi wa Jengo la *Covid-19* katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Singida umekuwa ukisuasua.

Je, ni upi mkakati wa Serikali wa kupeleka fedha za kutosha ili kumalizia ujenzi wa jengo hilo?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mbunge kwamba jengo hilo ni kweli kumekuwepo na tatizo analolisema na tayari mambo yameshafanyika Wizarani ya kuweza kulirekebisha hilo tatizo na nimhakikishie kabla ya Disemba jengo hilo litakuwa limemalizika. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA:** Mheshimiwa Spika, Hospitali yetu ya Rufaa ya Mkoa wa Kagera majengo mengi yamechakaa sana hasa *OPD* na wodi. Ningependa kuja Serikali ni lini itafanya ukarabati majengo hayo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba hospitali yao ni ya zamani na majengo mengi ni ya zamani, mengine yamefanyiwa ukarabati lakini bado ni yale ya zamani. Kwa hiyo, hii ni hospitali mojawapo ambayo michoro yake inachorwa kwa ajili ya kuja sasa na mkakati wa kuijenga upya na kubomoa yale majengo ya chini na kujenga majengo ya kwenda juu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Martha Mariki, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA F. MARIKI:** Mheshimiwa Spika, Je, ni lini Serikali itatenga fedha kwa ajili ya umaliziaji wa Jengo la Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Katavi? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Mkoa wa Katavi ni mojawapo ya hospitali nzuri sana na mpya ambazo Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan amezijenga na amezindua hivi karibuni, lakini ni kweli kama anavyosema kuna jengo ambalo halijamaliziwa kama ambavyo amesema.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwenye bajeti ya mwaka huu fedha zinatengwa kwa ajili ya kumalizia kazi iliyopo pale. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wodi nyingi za Hospitali ya Rufaa ya Ligula, Mkoani Mtwara zimechakaa.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati wodi hizo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, Mtwara ni mojawapo ya eneo ambalo limepata bahati sana katika kazi ambazo zimefanywa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu kilometa tatu tu kutoka hospitali hiyo ya Mkoa imejengwa hospitali nzuri sana ya Kanda ya Kusini.

Mheshimiwa Spika, pia ni kweli kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge anasema hospitali yao ni ya zamani imechakaa sana na ni mojawapo kama ambavyo nimesema kwenye hospitali zetu zote za zamani ni mojawapo ya hospitali ambazo michoro inatengenezwa kwa ajili ya kuja na mkakati baada ya kumaliza hospitali za Mikoa ambayo ilikuwa haina hospitali kabisa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO:** Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya cha Kimea, Wilaya ya Muleba kilijengwa majengo mawili ya wodi za mama na mtoto kipindi kirefu hayakumalizika.

Je, ni lini Serikali itakamilisha ukarabati wa hayo majengo mawili?

**SPIKA:** Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Mheshimiwa hilo swali lako ni la TAMISEMI kwa kweli, sasa tukimpa Mheshimiwa Waziri hapa!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, nipo.

**SPIKA:** Haya, Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu kwa Mheshimiwa Mbunge.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Muleba kwamba, tunafahamu walishaleta orodha ya vituo vya afya viwili ambavyo Serikali ya Awamu ya Sita ilishapeleka fedha kwa ajili ya ujenzi wa majengo lakini hayajakamilika, ninamhakikishia kwamba Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha majengo haya ya vituo vya afya. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, swali la nyongeza.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Spika, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Kigoma, Hospitali ya Maweni mpaka sasa imechukua muda mrefu kukamilisha jengo la utawala.

Je, ni lini Serikali itakamilisha jengo la utawala la hospitali hiyo? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme tu, Hospitali ya Mkoa wa Kigoma ni kweli ilikuwa na hali mbaya ya majengo kwa sababu ni hospitali ya zamani lakini kama Mheshimiwa Mbunge anavyokumbuka, hospitali hii ni mowapo ya hospitali alizozitembelea Mheshimiwa Rais kuzindua majengo mazuri sana yaliyojengwa kwenye eneo hilo. Kwa hiyo, ukiilinganisha Hospitali ya Mkoa ya Maweni iliyokuwepo na ya sasa kwa kweli hospitali hiyo imekuwa nzuri sana, na ni moja wapo ya hospitali zinazofanya vizuri sana nchini ipo kwenye *top three* ya hospitali zinazofanya vizuri kwenye nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, ninamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa katika bajeti ya mwaka huu kwa kazi inayoijua inayoendelea pale nayo inatengewa fedha kwa ajili ya kumaliza kazi hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Wizara ya Maji, Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, Mbunge wa Karatu, sasa aulize swali lake.

Na. 326

**Hitaji la Huduma ya Uhakika ya Maji – Karatu**

**MHE. DANIEL A. TLEMAI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatimiza ahadi yake ya kupeleka Shilingi Bilioni 4.5 Karatu ili wananchi wapate huduma ya uhakika ya maji?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kwa niaba ya Wizara ya Maji, Mheshimiwa Maryprisca Mahundi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maji inayolenga kuboresha huduma ya majisafi na salama kwa wananchi wa Karatu Mjini. Katika mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya shilingi 1,371,878.043 zimetolewa kwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Karatu *(KARUWASA)* ikiwa ni sehemu ya ahadi ya Serikali ya kuboresha huduma ya maji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Spika, fedha hizo zimewezesha kukamilisha utekelezaji wa Mradi wa Maji Ayalabe na kuanza kwa utekelezaji wa Mradi wa Maji Bwawani Na. 3 ambayo kwa pamoja inanufaisha zaidi ya watu 18,880 kwa maeneo hayo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kutoa kipaumbele cha kupeleka fedha za utekelezaji wa miradi ya maji katika Jimbo la Karatu kadri fedha zinavyopatikana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Awack Tlemai, swali la nyongeza.

**MHE. DANIEL A. TLEMAI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya maswali ya Serikali, nina swali moja la nyongeza.

Je, kwa kuwa ahadi imechukua miaka miwili toka Serikali itoe ahadi, nini mkakati wa Serikali ili kupunguza adha ya upungufu wa maji katika Mji wa Karatu? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI K.n.y WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, mkakati wa Serikali kuhakikisha Mji wa Karatu unapunguza kadhia ya maji, kwanza mradi huu ambao tayari tumeweka fedha zaidi ya Shilingi Bilioni 1.3 mwaka huu wa fedha 2025/2026 Wizara imetenga Shilingi Milioni 864 kuhakikisha kazi zitaendelea na kadri fedha zinavyopatikana basi tutahakikisha mradi huu unawekewa fedha ili uweze kukamilika.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo Serikali itaendelea kuboresha mambo mbalimbali kama uchimbaji wa kisima ambacho kitakuwa zaidi ya mita 200, lengo ni kuhakikisha tunaweza kupata vyanzo vingine vya maji na kuweza kusambaza. Vilevile, visima ambavyo tayari vilichimbwa Wizara itahakikisha inakwenda kuviendeleza kwa kuhakikisha sasa vinasambaza katika maeneo yote yaliyokusudiwa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mliosimama nimewaona lakini sasa Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu hapa kwa niaba ya Wizara. Yeye hayupo tena kwenye hiyo Wizara lakini kwa kweli nimewaona. Sasa ninaona kidogo mmesimama wengi, kwa hivyo, mniwie radhi kidogo kwa sababu Mheshimiwa anajibu swali kwa niaba ya Wizara nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Uchukuzi, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, sasa aulize swali lake.

Na. 327

**Hitaji la Uzio Uwanja wa Ndege Urambo**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza: -

Je, lini Uwanja wa Ndege Urambo utawekwa uzio ili kuimarisha usalama?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Kihenzile, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inakubaliana na pendekezo la ujenzi wa uzio ili kuimarisha usalama katika Kiwanja cha Ndege Urambo na tayari suala hili limejumuishwa katika rasimu ya Mpango Mkakati wa *TAA* wa miaka mitano ijayo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwepo kwa mpango huo, *TAA* inaendelea na utekelezaji wa maagizo ya Kitaifa kuhusiana na ulinzi na usalama, ikiwemo ushirikishwaji wa wananchi kulinda mipaka kupitia uhamasishaji wa ulinzi shirikishi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Wizara, ninaipongeza kwa kufanya usafi katika Uwanja wa Urambo, ambapo sasa Uwanja unapendeza kwa kuwa upo katikati ya Mji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:

Swali la kwanza, kwa kuwa uwanja huo upo katikati ya mji. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuweka utaratibu maalum wa kudumu wa usafi ili tusiwe tunangojea mpaka hali iwe mbaya ndiyo tuombe? *(Makofi)*

Swali la pili, kwa kuwa uwanja upo katikati ya Mji kwa ajili ya usalama na kupendezesha Mji pia. Je, Serikali haioni kuna umuhimu wa kuweka taa angalau za *solar* katika uwanja huo wa ndege? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa niaba ya Serikali kupitia Waziri wetu Mheshimiwa Prof. Mbarawa, tunapokea shukurani zake kwa sababu wachache ambao wakitendewa wema huwa wanashukuru. Wiki mbili zilizopita Mheshimiwa Sitta, alisimama hapa na akatoa ushauri wake na Serikali ikachukua jambo lake kwa uzito unaostahili, ikatekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimpongeze kwa jinsi ambavyo amekuwa mfuatiliaji makini wa maendeleo kwenye eneo lake. Amekuwa ni mmoja wa Wabunge wa kuigwa ambaye kila wakati anafuatilia maendeleo ya eneo lake. Ameleta maswali mawili la pili ni kama ushauri.

Swali lake la kwanza, nimhakikishie sisi kama Serikali tunajipanga kufanya jambo alilolieleza la usafi kuwa endelevu. Kwa hiyo, kila wakati tutajitahidi kuhakikisha kwamba usafi unafanyika katika Kiwanja hiki cha Ndege cha Urambo. *(Makofi)*

Swali lake la pili, Mheshimiwa Mbunge anaulizia kuhusiana na taa. Nimhakikishie kwamba Serikali imelipokea jambo hili kama ushauri, ninailekeza Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini iende kwenye eneo hilo ikatazame gharama zilizopo na kisha tutazame tunachoweza kukifanya ili kama alivyosema moja tuimalize ulinzi na usalama lakini pili tupendezeshe Mji wake wa Urambo, lakini tatu tuweze kuondoa vibaka pengine na wavamizi katika eneo hilo ambao wangeweza kuwa changamoto katika uendeshaji wa shughuli za wananchi za kila siku. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwita Getere, swali la nyongeza.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru. Tumekuwa na ahadi ya muda mrefu sana ya Uwanja wa Ndege wa Musoma, na sasa tumeambiwa kwamba miezi michache iliyopita kwamba utamalizika.

Je, ni lini uwanja huo sasa utamalizika ili wananchi wa Musoma wapate haki ya kupanda ndege?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninampongeza Mheshimiwa Getere kwa kuuliza swali katika wa Uwanja wa Musoma ambao kimsingi wote tunafahamu, kihistoria huo ni Mkoa ambao Baba wa Taifa alikuwa anatokea ni Mkoa wenye madini, ni Mkoa wenye utalii.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kutambua uzito na umuhimu wa uwanja huu ulikwishafanya uamuzi wa kutenga fedha na ujenzi ulishaanza na hivi ninavyozungumza tupo asilimia 58.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge pamoja na Wabunge wetu wa Mkoa wa Mara kwamba tunaendelea na taratibu za ndani mara tu tutakapokamilisha taratibu za kifedha tutaukamilisha uwanja huo ili uanze kutumika na wananchi kwa sababu imekuwa ni kilio cha muda mrefu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 328

**Usajili wa Waendesha Bodaboda Nchini**

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaanzisha utaratibu wa kuwasajili waendesha bodaboda nchini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Mheshimiwa Mwanaidi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Serikali inao mkakati wa kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara ndogondogo nchini wakiwemo waendesha bodaboda ambapo hadi kufikia tarehe 11 Mei, 2025 waendesha pikipiki (bodaboda) 3,032, Mwanaume 2,921 na Wanawake 111, walikuwa wamesajiliwa kwenye mfumo wa utambuzi, usajili na utoaji wa vitambulisho vya kidijitali.

Mheshimiwa Spika, usajili huo ni wa hiari na umeanza Machi, 2024 na unatekelezwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kupitia Dawati la Uratibu Wafanyabiashara Ndogondogo ambalo limeanzishwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa zote 184 nchini. Hivyo, zoezi la usajili linaendelea kwa kushirikiana na Maafisa waliopata mafunzo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Asha Abdullah Juma, swali la nyongeza.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Spika, ninashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, tunatambua umuhimu wa sekta hii ya wanabodaboda inavyosaidia kuzalisha ajira kwa vijina. Ni jukumu la mamlaka kuhakikisha kwamba vijana hawa wanabaki salama lakini vijana wengi wanaendelea kupata ajali wengine wanapoteza maisha wanakuwa vilema.

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba katika huo usajili vijana hawa wanapewa sharti la kwanza kwamba ni lazima watumie kofia ngumu wakati wanaposafirisha abiria?

Swali la pili, Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba ni lazima kila mwendesha (bodaboda) pikipiki awe amesajiliwa ili kuweza kuwaratibu vizuri na siyo jambo la hiari kama ulivyoeleza Mheshimiwa Waziri ili hawa watu wanaweza kuratibiwa vizuri? Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM:** Mheshimiwa Spika, ninapenda kujibu swali la Mheshimiwa Asha, kwanza ninapenda atambue kuwa usajili wowote wa vyombo vya moto ambavyo vinaendeshwa barabara basi anastahiki au ni lazima awe na kofia ngumu. Pia nitoe wito kwa wananchi kuwaelekeza kwamba mtu yeyote au mwananchi yeyote asikubali kupakiwa katika chombo cha miguu miwili ambacho kinaendeshwa barabarani bila ya kuvaa kofia ngumu kwa usalama wao na maisha yao.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili, kama nilivyoeleza bodaboda wote wamesajiliwa au vyombo vya moto vyote vimesajiliwa. Huu usajili ambao unaendelea ni kwa kuwawezesha kiuchumi wafanyabiashara hao ili biashara zao au kazi zao ziweze kukua na kuhakikisha kwamba hawana wasiwasi na maisha na Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amefanya hivi kuhakikisha kwamba wananchi wake wote basi wanakuwa na maisha ambayo hayana matatizo wala changamoto yoyote. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ahsante sana kwa majibu yako ya kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge. Wizara ya Ujenzi, Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, sasa aulize swali lake.

Na. 329

**Ujenzi wa Barabara Mpya ya Mombo hadi Lushoto kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga upya barabara ya Mombo hadi Lushoto yenye kilometa 36 kwa kiwango cha lami ili kukidhi mahitaji ya sasa?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Mheshimiwa Mhandisi Godfrey Kasekenya Msongwe, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TANROADS*, imekamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina wa barabara ya Mombo – Lushoto yenye urefu wa kilometa 36 kwa ajili ya kuifanyia ukarabati mkubwa kwa kiwango cha lami. Kwa sasa Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuanza ukarabati huu, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Rashid Shangazi, swali la nyongeza.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Spika, barabara hii imejengwa zaidi ya miaka 30 iliyopita na kwa kweli imejengwa katika vipimo vya kizamani ambavyo ni upana wa mita sita na hata jana barabara hii imepata changamoto maporomoko yameiziba kwa muda. Sasa kwa kuwa Serikali inakiri kwamba imeshafanya upembuzi wa kina na usanifu; je, ipo tayari kutafuta fedha kwa haraka ili kwenda kukarabati barabara hii?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kipande cha barabara kutoka Nyasa - Mlalo kwenda Majulai, mkandarasi alikuwepo *site* kwa muda lakini sasa ameondoka. Ningependa kujua hali ipoje sasa ni lini mkandarasi yule atarejea ili kwenda kuendelea na ujenzi katika kipande kile?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ninaomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara ya Mombo – Lushoto yenye urefu wa kilometa 36 ni ya zamani, ni nyembamba na ni barabara ambayo inapita kwenye miinuko mikali na mawe. Tunakiri kwamba imekuwa ni kawaida kila zinaponyesha mvua (eneo lina mvua nyingi sana) huwa kunakuwa na maporomoko ya mawe.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge tumeweka timu ya wataalamu ambao mpaka sasa hivi tunavyoongea wapo eneo hilo, kila mawe yanapoanguka kwa sababu ya ufinyu wa barabara huwa wanayaondoa.

Mheshimiwa Spika, Serikali tumeshafanya usanifu kwa ajili ya kuipanua hiyo barabara na tunatafuta chanzo cha uhakika kwa sababu hiyo barabara ndiyo barabara pekee ya muhimu inayoingia huko Lushoto ambako kuna uzalishaji mkubwa sana. Kwa hiyo Serikali tumeshafanya usanifu, tunatafuta chanzo cha uhakika ili kuweza kuipanua na kuiweka kwenye viwango vya sasa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala lake la pili, hii barabara ya kutoka Nyasa kwenda Majulai ni sehemu tu ya barabara ambayo inatoka Lukozi - Nyasa hadi Mng'alo, tunaijenga kwa awamu hatujasimama. Tayari tumejenga kilometa 2.8 na kilometa tatu ambazo tunaenda kuzijenga tayari tumeshapata mkandarasi na muda wowote tunasaini ili tukamilishe hizo kilometa tatu ambazo tutazifanya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Noah Lemburis Saputu Mollel, swali la nyongeza.

**MHE. NOAH L. S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, barabara ya Mianzini – Sambasha – Ngaramtoni, mkandarasi amesimama kwa muda mrefu sasa hafanyi kazi yoyote. Je, ni lini Serikali itapeleka pesa kumpa mkandarasi huyo ili barabara hiyo iendelee kutengenezwa kwa sababu ni ya mjini?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Ukiachilia mbali hali ya mvua inayoendelea lakini ukweli ni kwamba mkandarasi huyo hajaondoka *site* ila amepunguza ile kasi ya kutengeneza hiyo barabara. Tayari tumeshapokea maombi yake na tunashughulikia hati za malipo ili aweze kuongeza kasi mara baada ya kumlipa fedha.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Midimu, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER L. MIDIMU:** Mheshimiwa Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza. Barabara ya kutoka Bariadi – Itilima – Kisesa – Meatu – Singida ipo kwenye Ilani. Je ni lini Serikali itajenga kwa kiwango cha lami? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Barabara anayoisema ni ya mkoa na ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba ipo kwenye hatua za usanifu. Kwa hiyo ipo inasanifiwa ili iweze kuingia kwenye ujenzi kwa kiwango cha lami.

**SPIKA:** Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Handeni – Kibirashi – Songe sasa hivi magari yanatumia zaidi ya saa sita kwa sababu kwa mvua zinazonyesha maeneo mengi yana mashimo. Je, nini mpango wa Serikali wa kuhakikisha kwamba barabara hiyo inafanyiwa ukarabati ili iweze kupitika muda wote? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Sambamba na swali la Mheshimiwa Kigua, maeneo mengi ya nchi ambapo mvua zinanyesha kwa kweli hasa hizi barabara za kiwango cha changarawe kulikuwa na changamoto kwa sababu ya mvua.

Mheshimiwa Spika, tumetenga fedha za matengenezo ikiwepo hiyo barabara ya Kibirashi kwenda Songe. Nimhimize tu Mheshimiwa, nimpe maelekezo Meneja wa Mkoa wa Tanga kuhakikisha kwamba anaweka timu katika eneo hilo ili kuweza kukwamua hayo magari tukisubiri mvua ikatike halafu tuweze kuikarabati kwa kiwango ambacho tunakihitaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, tunakushukuru sana kwa majibu yako kwa maswali ya Waheshimiwa Wabunge.

Tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza cha maswali kutoka kwenu na majibu kutoka upande wa Serikali. Sasa nitaleta tangazo nililonalo hapa mbele, nalo linahusu wageni walioko Bungeni asubuhi hii. Tutaanza na wageni waliokaa Jukwaa la Spika.

Tutaanza na wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa ambaye ni Waziri wa Uchukuzi. Yupo Profesa Godius Kahyarara ambaye ni Katibu Mkuu; yupo Ndugu Ludovick Nduhiye, Naibu Katibu Mkuu; Balozi Ernest Mangu, Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (*TPA*); Ndugu Ally Karavina, Mwenyekitii wa Bodi Shirika la Reli Tanzania *(TRC);* Ndugu Juma Fimbo, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Usimamizi wa Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA);* Captein Mussa Mandia, Mwenyekiti wa Bodi Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC);* Dkt. Khamisi Mwinyimvua, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Usimamizi wa Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA);* Dkt. Ulingeta Mbamba, Mwenyekiti wa Bodi Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT)*. *(Makofi)*

Yupo pia, Profesa Hamad Ame, Mwenyekiti wa Bodi Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA);* Ndugu Augustus Fungo, Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri Ardhini *(LATRA CCC);* Jaji Ally Mshibe, Mwenyekitii wa Bodi Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA);* Dkt. Ladislaus Chang'a, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA);* Ndugu Masoud Faki, Mkurugenzi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa Zanzibar, Ndugu Masanja Kadogosa, Mkurugenzi Mkuu Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana, ninaamini wote hawa ni watumiaji wazuri wa reli yetu ya kisasa kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaye, Ndugu Salim Msangi, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania *(TCAA);* Ndugu Mohamed Salum, Mkurugenzi Mkuu shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC);* Ndugu Erick Hamis, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO*); Profesa Tumaini Gurumo, Mkuu…

Waheshimiwa Wabunge, pamoja na kwamba mnazungumza na wajumbe subirini niketi kwanza. Ninaona mmehalalisha mjadala baada ya makofi kwa Masanja Kadogosa, subirini kwanza nimalize kusoma wageni, nikishaketi mtaendelea na mjadala muhimu kabisa mnaoendelea nao.

Waheshimiwa Wabunge, tunaye Ndugu Erick Hamis, Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO);* Profesa Tumaini Gurumo, Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es salaam *(DMI);* Ndugu Sadiki Minja, Naibu Mkurugenzi Mtendaji *Tanzania - Zambia Railway (TAZARA),* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye *CPA*. Habibu Suluo, Mkurugenzi Mkuu Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA);* Mahandisi Peter Ulanga, Mkurugenzi Mkuu Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL);* Ndugu Angela Mushi, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji Kampuni ya Meli ya Ushirikiano wa Tanzania na China *(SINOTASHIP);* Ndugu Innocent Kyara, Katibu Mtendaji Baraza la Walaji *(TCAA CCC)*. *(Makofi)*

Tunaye Ndugu Aristid Kanje, Mkuu wa Chuo cha Usafiri wa Anga *(CATC);* Dkt. Lufunyo Hussein, Mkuu wa Chuo cha Bandari Dar es Salaam; Ndugu Damas Mwajanga, Mkuu wa Chuo cha Reli Tabora *(TIRTEC);* Dkt. Prosper Mgaya, Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT);* Ndugu Daudi Goodluck, Katibu Mtendaji, Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Usafiri za Ardhini *(LATRA CCC);* Ndugu Mahmoud Mabuyu, Mwakilishi Shirika la Chakula Duniani (*WFP*), karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi na hawa ni familia yake.

Yupo Ndugu Edina Kiposa ambaye ni Mama mzazi wa Mheshimiwa Naibu Waziri, karibu sana. Ameongozana na mdogo wa Mheshimiwa Naibu Waziri ambaye ni Ndugu Bedon Kilupula, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao sasa wageni mbalimbali wageni wenu. Tunao wageni 39 wa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu ambaye ni Naibu Spika, hawa ni wanafunzi, waalimu na wafanyakazi wa *Malaika Schools* kutoka Kigamboni Jijini Dar es salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni 100 wa Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamisi ambaye ni Naibu Waziri, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, hawa ni viongozi wa mwanamke salama kutoka mikoa yote Tanzania bara, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunaye mgeni wa Mheshimiwa Hassan Seleman Mtenga ambaye ni Dkt. Joseph Mtenga ambaye ni ndugu yake kutoka Wizara ya Afya Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Constantine John Kanyasu ambaye ni ndugu zake kutoka Mkoani Geita. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Augustine Holle Vuma ambao ni wafanyakazi wa *Magna Attorneys* kutoka Masaki, Dar es salaam. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Husna Juma Sekiboko ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Kenneth Ernest Nollo ambao ni wapiga kura wake kutoka Bahi. *(Makofi)*

Wageni sita wa Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ambao ni ndugu zake kutoka Busega. *(Makofi)*

Wageni watano wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni viongozi wa na wajumbe wa Chama cha Ufugaji Tanzania kutoka Bunda Mkoani Mara. *(Makofi)*

Wageni 28 wa Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya ambao ni wanakwaya wa kwaya ya Mtakatifu Gasper Del Bufalo kutoka parokia ya Kisasa Jijini Dodoma, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo. Wapo wanafunzi 23 na mhadhiri mmoja kutoka Chuo Kikuu cha Iringa, karibuni sana. *(Makofi)*

Wanafunzi 60 na waalimu sita wa shule ya awali na msingi Bernhard Bendel Kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulio nao asubuhi hii Bungeni na wengine tutaendelea kuwatangaza kadri watakavyopata fursa ya kuingia hapa ndani. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. BARAKA I. LEONARD – KATIBU WA BUNGE:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, sasa nimwite Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa aje awasilishe hoja yake.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia kukutana hapa tukiwa na afya njema….

**SPIKA:** Mheshimiwa subiri kidogo, Waheshimiwa Wabunge, tupunguze sauti kidogo tumsikilize Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Waziri, endelea.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii ya kipekee kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu na kutimiza miaka minne katika uongozi wake imara na maono yake yaliyoleta maendeleo makubwa nchini.

Mheshimiwa Spika, pamoja na masuala mengine, Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kujenga, kuendeleza na kuboresha huduma katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya uchukuzi. Ni dhahiri kuwa tumeona uthubutu na maendeleo makubwa ambayo yameendelea kutekelezwa katika sekta ya uchukuzi yakiwemo: ujenzi na uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR*, maboresho ya bandari, ujenzi na ukarabati wa meli pamoja na viwanja vya ndege, uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania ikiwemo ununuzi wa ndege, ununuzi wa rada za hali ya hewa, na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa umahiri wake mkubwa wa kuendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, kwa uongozi wake makini. Ni wazi kuwa Mheshimiwa Waziri Mkuu ameendelea kutumikia nchi yetu kwa umahiri mkubwa kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais katika nafasi hiyo ambayo ameendelea kuwatumikia Watanzania kwa umakini na kuonesha uwezo mkubwa katika kutekeleza ipasavyo majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa uongozi wako mahiri katika kuliongoza Bunge letu Tukufu. Aidha, niendelee kukupongeza kwa jinsi unavyoendelea kutekeleza kwa weledi majukumu ya nafasi ya Urais wa Umoja wa Mabunge Duniani, nafasi ambayo ni heshima kubwa kwako na kwa nchi yetu. Watanzania tunaendelea kukuombea katika utekelezaji wa majukumu yako hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Naibu Spika kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yake katika kukusaidia wewe Mheshimiwa Spika kuliongoza Bunge hili. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wote wa Bunge kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso, Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango Malecela na pia, ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati. Kamati hii imeendelea kutoa ushauri wenye tija na kuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Sekta ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa simanzi kubwa ninaungana na Bunge na Watanzania wote kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa familia husika na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Makamu wa Rais wa Kwanza na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Cleopa David Msuya, kilichotokea Tarehe Saba, Mwezi Mei, Mwaka huu 2025. Hakika, alikuwa na mchango mkubwa katika kulitumikia Taifa hili. Aidha, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha Dkt. Faustine Ndugulile, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na

Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani, Kanda ya Afrika, kilichotokea Tarehe 27 Novemba, Mwaka jana 2025. Hakika tutaendelea kuthamini na kuenzi mchango wake katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi. Amiin.

Mheshimiwa Spika, kipekee napenda kumshukuru Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake ambayo imetoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka 2024/2025, pamoja na kuonesha Dira na Mwelekeo wa Taifa letu kwa mwaka wa fedha 2025/2026 katika sekta mbalimbali, ikiwemo Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa uniruhusu nitoe Taarifa ya Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/2025, pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Wizara ya Uchukuzi (Fungu – 62) iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2.729, kwa ajili ya matumizi ya kawaida na fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 114.74 ni za Matumizi ya Kawaida ya Wizara na taasisi zake na shilingi 2.614 ni za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, Mwaka huu 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya shilingi trilioni 1.674 sawa na asilimia 61.34 ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizopokelewa, shilingi bilioni 100.11 ni fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni sawa na asilimia 87.25 ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa na shilingi trilioni 1.574 ni fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, ambazo ni sawa na asilimia 60.21 ya Bajeti ya Maendeleo iliyoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Uchukuzi baada ya kupokea fedha hizo iliendelea kutekeleza Miradi ya Maendeleo na shughuli

mbalimbali zilizopangwa katika Mwaka 2024/2025, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Udhibiti wa Huduma za Uchukuzi. Katika kuimarisha huduma za uchukuzi nchini Wizara, kupitia Mamlaka ya Udhibiti, imeendelea kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Udhibiti wa Usafiri Ardhini. Serikali, kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini *(LATRA),* imeendelea kusimamia na kudhibiti usafiri katika sekta ndogo za reli, barabara, pamoja na kuanza maandalizi ya awali, kwa ajili ya udhibiti wa usafiri wa waya. Aidha, *LATRA* imeendelea na jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa, ili kuboresha usalama na ubora wa huduma katika usafiri ardhini.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya *LATRA* yanapatikana kwenye kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti, kuanzia Ukurasa wa 10 hadi 16.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga. Mamlaka ya Usafiri wa Angani *(TCAA)* imeendelea kusimamia Sekta ya Usafiri wa Anga kwa kutoa huduma za udhibiti wa anga, viwanja vya ndege, pamoja na kutoa huduma ya uongozaji ndege viwanja vya ndege 15. Vilevile, *TCAA* imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege zinazoruka na kupita katika Anga la Burundi kwa urefu wa futi 24,500 kutoka usawa wa bahari, ambalo limekasimiwa kwa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani.

Mheshimiwa Spika, kuanzia Mwezi Julai, Mwaka 2024 hadi Machi Mwaka huu, *TCAA* imetekeleza majukumu mbalimbali na maelezo yake ya kina yanapatikana kwenye Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia Ukurasa wa 16 hadi 24.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Udhibiti wa Usafiri Majini. Katika kuimarisha usafiri majini Serikali, kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania *(TASAC),* imeendelea kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini katika Eneo la Tanzania Bara; udhibiti wa

huduma za bandari na watoa huduma za usafiri majini, kutoa huduma ya biashara ya meli kwa bidhaa mahsusi na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za usafiri majini.

Mheshimiwa Spika, Katika kipindi cha Julai, Mwaka 2024 hadi Machi Mwaka 2025, *TASAC* imetekeleza majukumu mbalimbali. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia Ukurasa wa 24 hadi 31.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Udhibiti wa Huduma za Hali ya Hewa. Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* imeendelea na utoaji wa huduma za hali ya hewa, pamoja na kudhibiti na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini. Aidha, *TMA* imeendelea kuhimili katika viwango vya utoaji wa huduma Kimataifa, ambapo imetoa huduma za utabiri hali ya hewa wa kila siku, utabili wa siku 10 na ule wa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai Mwaka 2024 hadi Machi mwaka 2025, *TMA* imetekeleza majukumu mbalimbali. Maelezo ya kina yanapatikana kwenye Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti kuanzia Ukurasa wa 31 hadi 36.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utoaji wa Huduma za Uchukuzi; Huduma za Bandari. Wizara, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania *(TPA),* imeendelea kusimamia Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za kibandari, kulinda mazingira na usalama wa bandari kwa viwango vinavyokubalika na kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; hadi kufikia Mwezi Machi Mwaka 2025, Serikali imeendelea na uboreshaji wa bandari hiyo, ikiwemo uboreshaji wa Gati Namba 8 mpaka 11 na Gati Namba 12 mpaka 15, ambapo upembuzi yakinifu na uboreshaji wa Gati hizo umekamilika. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya kupokelea mafuta, pamoja na matanki 15 ya mafuta yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 378,000 umeendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 25.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika, uboreshaji wa Bandari ya Tanga unaendelea, ili kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena kwenda Kanda ya Kaskazini na nchi za jirani. Maboresho yaliyofanyika hadi hivi sasa ni pamoja na kuongeza kina cha maji kutoka mita tatu hadi mita 13 na upanuzi wa eneo la kuingia na kutokea bandarini, lenye upana wa mita 73 na eneo la kugeuzia meli kuwa na kipenyo cha mita 800.

Mheshimiwa Spika, Serikali, kupitia *TPA,* imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Gati jipya na *conveyer belt* katika Bandari ya Kisiwa Mgao, ambayo ni maalum, kwa ajili ya kuhudumia shehena chafu (*dirty cargo),* kama vile makaa ya mawe na saruji. Katika kuendelea na utekelezaji wa mradi huo, tayari usanifu wa kina umekamilika. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na hatua za maandalizi, kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Spika, lengo la mradi huu ni kuiwezesha Bandari ya Mtwara iendelee kutoa huduma kwa ufanisi bila kuathiri mazingira. Aidha, Serikali imekamilisha kuhuisha upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa ujenzi wa Bandari Mpya ya Mbegani iliyopo Bagamoyo. Ujenzi wa bandari hiyo ya kimkakati utachochea shughuli za viwanda na biashara katika Eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi la Bagamoyo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na utekelezaji wa Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo ujenzi wa bandari ya sakafu ngumu *(pavement)* yenye ukubwa wa hekta tano, kwa ajili ya kuhifadhi shehena umefikia asilimia 96.6. Bandari hiyo imeendelea kuhudumia makasha kutoka Bandari ya Dar es Salaam na hivyo, kuongeza ufanisi na kupunguza msongamano katika Jiji la Dar es Salaam. Aidha, katika kuboresha Biashara ya Tanzania na nchi za jirani na kulifanya Eneo la Bandari Kavu ya Kwala kuwa ya kimkakati zaidi Serikali imetoa maeneo, kwa ajili ya kuhudumia shehena za nchi ya Rwanda, *DRC*, Burundi, Zambia, Uganda, Malawi, Sudan Kusini na Zimbabwe; nchi hizo zimeanza uendelezaji wa maeneo husika. Pia, Mwezi Aprili, Mwaka 2025, nchi yetu imepewa takribani hekta 15, kwa ajili ya kujenga Bandari Kavu katika Eneo la Kasumbalesa huko *DRC*.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hatua hizo Serikali, pia, imeendelea kuboresha bandari zilizopo katika Maziwa Makuu nchini. Hadi kufikia Mwezi Machi, Mwaka 2025, Serikali imesaini Mkataba wa Uboreshaji wa Bandari ya Kigoma iliyopo katika Ziwa Tanganyika unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuingilia bandarini na jengo la abiria. Mradi huu wa usanifu na ujenzi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Japan kupitia Shirika lake la *JICA*.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali, kupitia *TPA,* imeendelea kuboresha bandari zilizopo katika Ziwa Victoria, ambapo uboreshaji wa Bandari ya Bukoba umefikia asilimia 96. Vilevile, uboreshaji wa Bandari ya Kemondo umekamilika na kwa sasa uko katika kipindi cha uangalizi. Pia, uboreshaji wa Bandari ya Mwanza *North* umefikia asilimia 58. Katika Ziwa Nyasa, Serikali imeendelea na uboreshaji wa Bandari ya *Mbamba Bay,* ili kuweza kuhudumia wananchi wa maeneo hayo na Nchi jirani za Malawi na Msumbiji, ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi Katika Uendelezaji na Uendeshaji wa Bandari Nchini. Kwa lengo la kuongeza ufanisi wa bandari nchini Serikali imeendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari kwa kuingia ubia na Kampuni ya *DP World* na Tanzania *East Africa Gateway Terminal Limited* katika kuendeleza na kuendesha baadhi ya maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, ushirikishwaji huo wa sekta binafsi, pamoja na manufaa mengine, umeleta mafanikio mbalimbali, kama ifuatavyo: -

(i) Kuongezeka kwa mapato yanayotokana na kodi ya forodha kutokana na shughuli za kibandari. Ambapo katika kipindi cha Julai, Mwaka 2024 hadi Februari, Mwaka 2025 jumla ya shilingi trilioni 8.26 zimekusanywa, sawa na ongezeko la shilingi trillion 1.18, ikilinganishwa na shilingi trilioni 7.08 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho Mwaka 2023/2024 kabla ya kushirikishwa kwa waendeshaji binafsi katika Bandari ya Dar es Salaam;

(ii) Kupungua kwa gharama za uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam kutoka shilingi bilioni 775.01 hadi kufikia shilingi bilioni 685.16. Sawa na punguzo la asilimia 30;

(iii) Kupungua kwa muda wa kusubiri meli nangani kutoka wastani wa siku 46 hadi siku saba kwa meli za mizigo mchanganyiko na kichele na meli za makasha Gatini kutoka wastani wa siku 10 hadi siku tatu;

(iv) Kuongezeka kwa wastani wa shehena ya makasha inayohudumiwa kwa mwezi kutoka makasha 17,000 hadi makasha 25,000. Sawa na ongezeko la asilimia 47.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla hatua hii ya ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuendeleza na kuendesha bandari nchini, imechangia kufikiwa mapema kwa lengo la Mpango Kabambe wa *TPA* wa miaka 20 uliowekwa kuhudumia tani milioni 30 za shehena, ifikapo Mwaka 2029/2030. Hata hivyo, matokeo ya uendeshaji wa bandari hadi kufikia Mwezi Machi, 2025 tayari ufanisi wa uhudumiaji wa shehena wa bandari zote nchini umefikia tani milioni 27.55 na kwa mwenendo huu lengo la kufikia tani milioni 30 litafikiwa mapema kabla ya muda wake uliowekwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utendaji wa huduma za kibandari na utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa bandari nchini kupitia *TPA,* umeoneshwa kwenye Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti, kuanzia Ukurasa wa 36 mpaka 46.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Huduma za Usafiri wa Reli; Shirika la Reli Tanzania *(TRC)*. Katika kuchagiza ukuaji wa uchumi Serikali, kupitia Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* imeendelea kuboresha huduma ya uchukuzi kwa njia ya reli kwa kusimamia na kuendeleza miundombinu ya reli nchini kwa *Meter Gauge Railway* yenye urefu wa kilomita 2,707, kujenga reli mpya ya kiwango cha *Standard Gauge* kwa awamu, ambapo awamu ya kwanza ina jumla ya kilometa 1,219 na awamu ya pili ina jumla ya kilometa 1,590 za njia kuu na hivyo, kufanya reli hiyo ya *SGR* kuwa na mtandao wa jumla ya kilometa 2,809 ambazo ni zaidi ya kilometa

102, ikilinganishwa na *MGR* iliyojengwa kabla ya kupata uhuru. Pia, Serikali imeendelea na ujenzi wa *SGR* kwa maeneo mengine, yakiwemo Ushoroba wa Kusini na Kaskazini kwa kadiri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, katika kurahisisha usafiri kwa wananchi, sambamba na utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati akihutubia Taifa, Mwezi Desemba, 2023; alielekeza kuanza uendeshaji wa treni katika *SGR,* Kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara, kupitia *TRC,* ilianza rasmi huduma ya uendeshaji wa treni katika *SGR,* Tarehe 14 Juni, Mwaka 2024 kwa safari kati ya Dar es Salaam na Morogoro na Tarehe 25 Julai, Mwaka 2024 kwa safari ya Dar es Salaam mpaka Dodoma. Kutokana na mafanikio haya, nimpongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuonesha uthubutu katika kuendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika ujenzi wa miundombinu ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tangu kuanza kwa safari za treni katika *SGR,* hadi kufikia Mwezi Machi, Mwaka 2025, *TRC* imesafirisha jumla ya abiria 2,054,828 na kuwezesha kukusanya mapato ya jumla ya shilingi bilioni 60.25. Usafiri wa treni katika *SGR* umepunguza muda wa safari kutoka saa tisa, zilizokuwa zinatumika kwa usafiri wa barabara, hadi kufikia saa tatu kati ya Dar es Salaam na Dodoma na hivyo kuwezesha muda uliopunguzwa kutumika katika shughuli nyingine za uzalishaji mali. Aidha, Serikali inaendelea na kukamilisha taratibu za kuanza usafirishaji wa mizigo kwa *SGR,* kuanzia Mwezi Juni, Mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali iliahidi kuendelea na ujenzi wa *SGR*. Hivyo, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeendelea kutekeleza ujenzi wa *SGR* kwa Awamu ya Kwanza, ambapo hadi kufikia Mwezi Machi,Mwaka 2025, ujenzi umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kipande cha Dar es Salaam – Morogoro ni asilimia 99.72, ambacho kinajumuisha ujenzi wa njia ya kuingilia bandarini *(port link),* uliyofikia asilimia 91.78. Kipande cha Morogoro – Makutupora, chenye urefu wa Kilometa 422, umefikia asilimia 97.98. Kipande cha tatu cha Makutupora – Tabora umefikia asilimia 14.53; kipande cha nne, Tabora – Isaka, umefikia asilimia 6.65 na kipande cha tano, kutoka Mwanza – Isaka, umefikia asilimia 63.16.

Mheshimiwa Spika, pia, Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa *SGR* kwa awamu ya pili, ambapo ujenzi wa *SGR* kutoka Tabora – Kigoma, yenye urefu wa kilometa 506, umefikia asilimia 7.88. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa reli hii kutafungua biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za ukanda huo, zikiwemo Burundi na *DRC*.

Mheshimiwa Spika, katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020, Ibara ya 30(a), Serikali iliahidi kuendelea kunufaika na fursa za kijiografia kwa kubuni na kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati, ili nchi iweze kunufaika zaidi na fursa. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali, kupitia *TRC,* imesaini Mkataba wa Ujenzi wa *SGR* Kipande cha Uvinza – Musongati, chenye kilometa 240 mnamo Tarehe 29 Januari, Mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kusainiwa kwa mkataba huu ni matokeo ya ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Burundi. Kukamilika kwa reli hii kutaunganisha Nchi ya Burundi na Bandari ya Dar es Salaam, sambamba na kufungua Nchi ya Tanzania kikanda na kurahisisha ufanyaji biashara kati ya Tanzania, Burundi na *DRC*.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali, kupitia *TRC,* imeendelea kufanya ununuzi wa vifaa mbalimbali vya treni, ikiwemo ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo, kwa ajili ya kutoa huduma ya usafiri kwenye *SGR*. Hadi kufikia Mwezi Machi, Mwaka 2025, mabehewa 71 ya abiria, vichwa vya treni vya umeme 17 na seti 10 za treni ya mchongoko zimewasili nchini na kuanza kutoa huduma. Pia, mabehewa 264 ya mizigo katika ya mabehewa

1,430 yaliwasili nchini Tarehe 11 Desemba, Mwaka 2024 na hatua za majaribio ya mabehewa hayo zimekamilika.

Mheshimiwa Spika, vilevile, Serikali imeendelea na uendelezaji na uendeshaji wa *MGR*. Kutokana na umuhimu wake, Serikali inaendelea na ukarabati wa njia ya *MGR* ya Kaliua – Mpanda, yenye urefu wa kilometa 210, ambapo umefikia asilimia 24.04, pamoja na kusaini Mkataba wa Ununuzi wa Malighafi za Matengenezo, ikiwemo reli, mataruma na vifungashio, kwa ajili ya kukarabati Njia ya Reli ya Tanga – Arusha na Ruvu – *Mruazi junction*.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa miradi mbalimbali ya *TRC* unapatikana kwenye Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti, kuanzia Ukurasa wa 46 hadi 59.

Mheshimiwa Spika, Kuhusu Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)*. Ili kuendeleza huduma ya reli, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* inayomilikiwa kwa hisa za asilimia 50 kwa 50 kati ya Tanzania na Zambia, imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam, Tanzania na *New Kapiri Mposhi* huko Zambia.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla, utendaji wa Reli ya *TAZARA* umekuwa wa kusuasua na umeendelea kudorora kila mwaka. Kutokana na hali hiyo nchi wanahisa (Tanzania na Zambia) zimeamua kuchukua hatua ya makusudi ya kuiboresha *TAZARA*. Mathalani, Serikali ya Awamu ya Sita kwa kushirikiana na Serikali ya Jamhuri ya Zambia na Serikali ya watu wa China kupitia Kampuni ya *CCECC* zimeingia makubaliano ya kuboresha uendeshaji wa *TAZARA*. Makubaliano hayo yalifanyika tarehe 04 Septemba mwaka jana Jijini Beijing China, mbele ya Marais wa Nchi zote tatu. Mkakati huu pamoja na mambo mengine, umelenga kumpata mwekezaji mahiri ambaye atawekeza katika kuiendeleza na kuiendesha *TAZARA* kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu. Kwa sasa nchi wanahisa zinaendelea kukamilisha taratibu ikiwemo za kufanya majadiliano ili kukubaliana na namna gani utekelezaji huo utafanyika kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi wanahisa. Utendaji kazi wa

*TAZARA* umeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti, kuanzia ukurasa wa 59 hadi 63.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma katika Maziwa Makuu. Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania *(TASHICO)* ambayo inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100 imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji katika maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika, na Nyasa, ndani na nje ya nchi zikiwemo nchi jirani za Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, DRC, Zambia, na Malawi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kuanzia Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu *TASHICO* ilisafirisha abiria 210,588 ikilinganishwa na abiria 198,080 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia 6.31. Kwa upande wa mizigo *TASHICO* ilisafirisha tani 58,605.78 ikilinganishwa na tani 33,288.44 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho Mwaka wa Fedha 2023/2024, sawa na ongezeko la asilimia 76.05.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri katika Maziwa Makuu, Serikali iliahidi kuboresha huduma za usafiri katika Maziwa Makuu kwa kujenga na kukarabati meli. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu Serikali kupitia *TASHICO* imeendelea kujenga meli mpya na kukarabati meli zilizopo katika Ziwa Victoria na Tanganyika, ambazo utekelezaji wkae umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo; MV. Sangara umefikia asilimia 98, na MV. Liemba wamefikia asilimia 15. Aidha, maandalizi ya kuanza ukarabati wa meli ya MV. Mwongozo yanaendelea baada ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati huo. Utendaji kazi wa *TASHICO* umeonyeshwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 64 hadi 67.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za viwanja vya ndege. Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* imeendelea kusimamia, kuendesha na kuendeleza viwanja vya ndege vya Serikali 61 Tanzania bara. Hadi kufikia mwezi Machi, mwaka huu Serikali kupitia *TAA* imeendelea na uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha ambapo ujenzi wa jengo la abiria umekamilika na kazi ya ukungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege unaendelea.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kazi ya ukamilishaji wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege Mwanza imefikia asilimia 13; kazi ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi umefikia asilimia 69; na upembuzi yakinifu na usanifu wa awali wa Kiwanja cha Ndege cha Njombe umekamilika na taratibu za utwaaji wa ardhi unaendelea ili kazi ya ujenzi iweze kuanza. Vilevile, wakandarasi wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi; mradi wa ujenzi wa jengo la abiria, jengo la mnara wa kuongozea ndege, kituo cha hali ya hewa na kituo cha zimamoto katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara wamekabidhiwa maeneo ya mradi na taratibu za malipo ya awali zinaendelea.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kunakuwa na usalama wa ndege zinazotumia Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, Serikali imeona umuhimu wa kujenga mnara wa kuongozea ndege katika kiwanja hicho ambapo maandalizi yake yanaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na mpango wa kudumu wa kutatua changamoto za usalama katika usafiri wa anga katika Mkoa wa Kagera. Katika utekelezaji wa mpango huo, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi imependekeza eneo jipya litakalofaa kwa ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha daraja la 4C ambacho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege zinazobeba abiria hadi 220 kwa wakati mmoja. Pendekezo hilo linaonesha eneo la Kyabajwa lililopo Wilaya ya Misenyi kufaa zaidi kwa ajili ya ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege. Kwa sasa taratibu za utwaaji ardhi zinaendelea. Utendaji kazi wa *TAA* pamoja na miradi mbalimbali umeoneshwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 67 hadi 72.

Mheshimiwa Spika, kuhusu huduma za usafiri wa anga, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imeendelea kufufua *ATCL* kwa kununua ndege, kuboresha karakana za matengenezo ya ndege na kutekeleza mikakati ya kuongeza ubora na usalama katika utendaji ili kutoa huduma ya usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali imekamilisha ununuzi wa ndege aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* na kufanya *ATCL* kuwa na jumla ya ndege 16. Uwepo wa ndege hizo umeendelea kuiwezesha *ATCL* kupanua mtandao wa safari kwa kurejesha safari na kuifanya *ATCL* kuwa na vituo 27

vinavyotoa huduma. Kati ya vituo hivyo vituo 15 ni vya ndani ya nchi, vituo tisa ni vya kikanda, na vituo vitatu ni vya kimataifa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Julai, mwaka jana hadi Machi, mwaka huu *ATCL* imesafirisha abiria 876,357 sawa na ongezeko la abiria 25,697 ikilinganishwa na abiria 850,660 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Pia, *ATCL* ilisafirisha tani 5,869.81 za mizigo sawa na ongezeko la tani 835.61 ikilinganishwa na tani 5,034.2 zilizosafirishwa katika Mwaka wa Fedha 2023/2024. Utendaji kazi wa *ATCL* umeoneshwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti, kuanzia ukurasa wa 72 hadi 76.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utoaji wa mafunzo katika vyuo vya mafunzo vya kisekta. Serikali imeendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za usafiri na usafirishaji kwenye vyuo vya kisekta, ikiwemo, *NIT*; *DMI*, Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania, Chuo cha Bandari Dar es Salaam; Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania, na Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kwa lengo la kujenga uwezo katika kutumia wataalamu wa ndani na kupunguza gharama za kusomesha wataalamu nje ya nchi ili kuwa na wataalamu toshelevu na kutoa huduma katika sekta ya usafiri na usafirishaji. Utendaji kazi wa Vyuo vyetu unapatikana kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti, kuanzia ukurasa wa 78 hadi 91.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mafanikio ya miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya uchukuzi. Sambamba na maelezo niliyoyatoa hapo juu, ninaomba kwa muhtasari niainishe mafanikio yaliyopatikana katika sekta ya uchukuzi kwa kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwanza kwa kuanza na uendeshaji wa Reli ya *SGR* na kuendelea na ujenzi wa reli hiyo. Tanzania imeweka historia ndani na nje ya Bara la Afrika kwa kujenga na kuanza uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR*. Hatua hii ni kubwa na ya kupongezwa kwani imekuwa ya kipekee tangu kupata uhuru wa nchi yetu. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan,

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetekeleza kwa vitendo maono ya nchi yetu ambapo uendeshaji wa reli ya kisasa ya *SGR* ulianza rasmi tarehe 14 Juni, mwaka jana kwa safari kati ya Dar es Salaam hadi Morogoro, na tarehe 25 Julai, mwaka jana kwa safari kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma. Pamoja na hatua hiyo, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia *TRC* inatarajia kuanza uendeshaji wa treni ya mizigo kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma ifikapo mwezi Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuanza uendeshaji wa reli ya kisasa katika kipande cha Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na ujenzi wa reli ya kisasa; ambapo kabla ya kuingia madarakani *TRC* ilikuwa imeanza ujenzi wa reli ya kisasa kwa vipande viwili tu ambavyo ni kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro chenye urefu wa kilometa 300 na Morogoro hadi Makutupora chenye urefu wa kilometa 422. Aidha, ninapenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza kwa vitendo ambapo tangu imeingia madarakani imefanikisha kupatikana kwa fedha za kuendelea na kuanza ujenzi wa Reli ya *SGR* kwa vipande vifuatavyo; Makutupora – Tabora; Tabora – Isaka yenye urefu wa kilometa 165; Tabora – Kigoma yenya urefu wa kilometa 506; Isaka – Mwanza yenye refu wa kilometa 341; na Uvinza – Musongati yenye urefu wa kilometa 240. Kazi ya ujenzi katika vipande hivyo inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ununuzi wa ndege, tangu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, ndege saba zimenunuliwa na kuifanya *ATCL* kuwa na ndege mpya 15. Ndege hizo zimewezesha *ATCL* kupanua huduma za usafiri na usafirishaji ndani na nje ya nchi ambapo kwa sasa ndege zetu kupitia *ATCL* zinatoa huduma katika vituo 27 ikilinganishwa na vituo 23 ilivyohudumia mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuendelea kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji katika Maziwa, Serikali ya Awamu ya Sita imeweka historia ya kuendelea kujenga na kukarabati meli mbalimbali. Mathalani, katika kuendelea na ujenzi wa meli kwa vitendo, ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu umeendelea na hadi kufikia Machi, mwaka huu umefikia asilimia

96 kutoka asilimia 40 iliyofikiwa mwezi Machi, 2021 wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani. Aidha, meli ya MV. Umoja yenye uwezo wa kubeba kwa wakati mmoja mizigo yenye tani 1,200 ukarabati wake umekamilika na kuanza kutoa huduma, ambapo kwa sasa inafanya safari kwenda nchi za Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uboreshaji wa huduma za Bandari Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuchukua mikakati madhubuti katika kuendeleza bandari nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya maboresho makubwa katika Bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mwanza, na Bandari za Maziwa Makuu, na kuendelea kushirikisha sekta binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari. Kutokana na juhudi hizi mafanikio makubwa yameanza kupatikana. Mathalani, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022, shehena ya mizigo iliyohudumiwa katika Bandari za Tanzania imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 15.23 kwa mwaka kutoka tani milioni 20.78 zilizohudumiwa mwaka 2021/2022 hadi kufikia tani milioni 27.55 zilizohudumiwa mwaka 2023/2024. Kwa kasi hii, inaonesha kuwa lengo lililowekwa na *TPA* katika Mpango Kabambe la kufikia tani milioni 30 ambalo lilikuwa lifikiwe mwaka 2029/2030, sasa linafikiwa mapema zaidi kutokana na mikakati madhubuti inayoendelea kutekelezwa chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu miundombinu na huduma katika Viwanja vya Ndege, mwezi Mei 2023, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania imewezesha nchi kushika nafasi ya nne barani Afrika kwa ubora wa ulinzi katika viwanja vya ndege kupitia ukaguzi uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani *(ICAO)* wa masuala ya ulinzi kwa kupata ufaulu wa asilimia 86.70.

Mheshimiwa Spika, kuhusu udhibiti wa Usafiri wa Anga. Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ufungaji wa mfumo wa mawasiliano kwa njia ya sauti baina ya waongoza ndege na marubani katika viwanja vya ndege 12 na vituo 18. Mfumo huo

umewezesha kuimarisha usalama wakati wa kutua na kuruka kwa ndege.

Mheshimiwa Spika, Serikali inayoongozwa na Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imewezesha Chuo cha *NIT* kupata ndege mbili mpya za mafunzo na ithibati ya kuanza kutoa mafunzo ya urubani. Mafunzo hayo yataanza kutolewa mwezi Juni, mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo ya miaka minne, Serikali pia imepata mafanikio katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai mwaka jana hadi Machi, mwaka huu kama ifuatavyo:-

(i) Kuwasili kwa vitendea kazi vinavyotumika katika uendeshaji wa Reli ya *SGR* ambavyo ni vichwa vya treni vya umeme17, seti za treni ya umeme za *EMU* 10 (mchongoko) na mabehewa 264 ya mizigo;

(ii) Kukamilisha ukarabati wa mabehewa ya mizigo 350 kati ya mabehewa 600 na mabehewa ya abiria 33 kati ya mabehewa 37 ambayo yameanza kutoa huduma katika Reli ya *MGR;*

(iii) Kuongezeka kwa mizigo iliyosafirishwa kwa kutumia Kampuni ya Ndege Tanzania ambapo hadi kufikia Machi mwaka huu, *ATCL* imesafirisha tani 5,869.81 ikilinganishwa na tani 3,658.60 za mizigo zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 60.41;

(iv) Kuongezeka kwa idadi ya abiria waliosafirishwa na *ATCL* ambapo abiria 876,357 wamesafirishwa sawa na ongezeko la abiria 25,707 ikilinganishwa na abiria 850,650 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/2024;

(v) Kuendelea kuboreshwa kwa Kampuni ya Ndege ya *ATCL* kulikowezesha pamoja na mambo mengine, kurejesha

safari katika vituo mbalimbali na kuifanya *ATCL* kuwa na jumla ya vituo 27;

(vi) Kupokelewa kwa ndege moja aina ya *Boeing 787-8 Dreamliner* iliyowasili nchini tarehe 20 Agosti, mwaka jana;

(vii) Kuendelea kutoa huduma katika Bandari Kavu ya Kwala ambapo hadi kufikia Machi, mwaka huu ilihudumia makasha 805;

(viii) Kukamilisha ununuzi wa boti maalum itakayotoa huduma ya uokozi katika Ziwa Victoria. Boti hiyo tayari imepokelewa nchini tarehe 31 Machi, mwaka huu; na

(ix) Serikali kupitia *TAA* imefanikiwa kupata tuzo ya mshindi wa kwanza kutoka Baraza la Viwanja vya Ndege Afrika kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kwa kuwa kiwanja chenye huduma bora za usalama kwa mwaka 2024 kwa viwanja vya ndege vya Afrika vyenye miruko zaidi ya 50,000.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita yanapatikana kwenye Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti, kuanzia ukurasa wa 101 hadi 119.

Mheshimiwa Spika, kuhusu changamoto na mikakati ya kuzitatua. Wizara ya Uchukuzi imekabiliwa na changamoto mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu yake. Changamoto hizi na mikakati ya kuzitatua zimeoneshwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 120 hadi 123.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Uchukuzi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vyake ambavyo ni pamoja na kuendelea na ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* katika Ushoroba wa Kati, kununua vitendea kazi na kuboresha reli zilizopo, kuendelea kuboresha Kampuni ya Ndege Tanzania, Kuboresha miundombinu na huduma katika bandari nchini, Kuimarisha usalama na mawasiliano kwenye usafiri na usafirishaji

katika Maziwa Makuu Nchini; Uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege, kuendelea na ujenzi wa meli mpya na ukarabari wa meli zilizopo; na Kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza vipaumbele vya Wizara Fungu 52 na taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/2026 imetengewa jumla ya shilingi 2,746,485,018,000, ambapo kati ya fedha hizo shilingi 125,438,950,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 2,621,046,068,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Aidha, Fedha za matumizi ya kawaida zilizotengwa zinajumuisha shilingi 46,654,340,000 kwa ajili ya mishahara ya watumishi na shilingi 28,784,610,000 kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Vilevile Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa zinajumuisha shilingi 2,452,512,444,000 fedha za ndani na shilingi 168,533,624,000 fedha za nje. Vipaumbele na bajeti iliyotengwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 vimeainishwa kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 123 hadi 125.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Miradi ya Maendeleo inayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kutekeleza miradi mbalimbali ikiwemo ya kielelezo. Miradi ya kielelezo iliyotengewa fedha ni mradi wa ujenzi wa reli ya kisasa *(SGR)*, uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania, Uboreshaji wa usalama wa usafiri na usafirishaji katika Bahari na Maziwa Makuu, mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha, mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara, mradi wa ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro, mradi wa ujenzi na uendelezaji wa viwanja vya ndege vya mikoa ikiwemo Mkoa wa Lindi; na Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba. Maelezo ya kina na kazi zitakazofanyika katika mwaka wa fedha 2025/2026 na fedha zilizotengwa kwa kila mradi yameainishwa katika Kitabu changu cha Hotuba ya Bajeti, kuanzia ukurasa wa 126 hadi 145.

Mheshimiwa Spika, shughuli nyingine zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/2026 zinapatikana kwa kina kwenye kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 146 mpaka 178.

Mheshimiwa Spika, shukrani, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2024/2025, Wizara imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kutekeleza majukumu yake na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika Kipindi husika. Matokeo hayo yamepatikana kutokana na ushirikiano wa wadau wa Sekta ya Uchukuzi wa ndani na nje ya Wizara, wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote waliotoa michango mbalimbali ya hali na mali na wale walioshiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Shukrani za kipekee ninaziwasilisha kwenu Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushauri na michango yao ambayo imewezesha Wizara kuimarisha utendaji katika kutoa huduma za usafiri na usafirishaji hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia nitumie nafasi hii kuwapongeza na kutambua michango inayotolewa na viongozi wanaonisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kwa kuanza na Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Kihenzile, Katibu Mkuu, Prof. Kahyarara na Naibu Katibu Mkuu Bwana Ludovick Nduhiye. Halikadhalika, napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taifa kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninaomba nitumie fursa hii adhimu**,** kwa niaba ya Wizara kutoa shukrani na kuwatambua wadau wote wa Wizara ikiwa ni pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia rasilimali fedha katika utekelezaji wa programu, miradi na mipango mbalimbali ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee niruhusu niwatambue wafuataao: Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini *(IMO)*; Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga *(ICAO)*; Shirika la Hali ya

Hewa Duniani *(WMO)*; Benki ya Maendeleo ya Afrika *(AfDB)*; Benki ya Dunia *(WB)*; Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan *(JICA)*; Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea Kusini *(KOICA)*; Ujerumani *(KfW); Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO);* Shirika la Maendeleo la Ufaransa *(AFD)*; Jumuiya ya Umoja wa Ulaya *(EU)*; Benki ya Uwekezaji ya Ulaya *(EIB);* Shirika la Chakula Duniani *(WFP)*; Shirika la Maendeleo la Marekani *(USAID); Trade Mark Africa*; Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)*; Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika - *SADC*; Nchi za Urusi; Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE); Uingereza; Marekani; Uholanzi; Japan; India; China; Denmark; Korea Kusini; Ufaransa; Ubelgiji; Ujerumani na Uturuki; Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya *NSSF* na *PSSSF*; Taasisi za fedha za *CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC na TCB* na Asasi mbalimbali za kiraia; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sikuwataja hapa si kwa sababu ya umuhimu wao bali ni kutokana na wingi wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Spika, muhtasari wa maombi ya fedha ya Wizara ya Uchukuzi katika mwaka wa fedha 2025/2026. Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 2,746,485,018,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 125,438,950,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 2,621,046,068,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania kwa ujumla kuhusu utendaji wa Sekta ya Uchukuzi. Naomba majedwali hayo yachukuliwe kama sehemu ya hotuba yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (www.uchukuzi.go.tz)

Mheshimiwa Spika, majedwali ya taarifa na takwimu mbalimbali kuhusu Wizara ya Uchukuzi yameainishwa katika kitabu changu cha hotuba ya bajeti kuanzia ukurasa wa 186 hadi 234.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA UCHUKUZI MHESHIMIWA PROF. MAKAME MNYAA MBARAWA (MB.), AKIWASILISHA BUNGENI MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A: UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu iliyochambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/25 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likubali kupokea, kujadili na kuidhinisha Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/26.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema, usalama, amani na utulivu katika Taifa letu na kutuwezesha kukutana tena katika siku hii ya leo kuendelea kutekeleza majukumu ya kuwatumikia Watanzania. Ninamuomba Mwenyezi Mungu atuongoze vyema katika kujadili Hotuba hii ya Wizara ya Uchukuzi na Bajeti ya Serikali kwa ujumla ili tuweze kuendeleza nchi yetu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi imeendelea kutekeleza kazi zake kulingana na Hati ya Mgawanyo wa Majukumu iliyotolewa tangu kuanzishwa kwake mwezi Agosti, 2023. Kwa heshima kubwa, niendelee kumshukuru Mheshimiwa Rais kwa miongozo ambayo ameendelea kunipa katika kipindi changu chote ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita. Ni dhahiri kuwa katika kipindi hiki kumekuwa na mafanikio makubwa katika

sekta mbalimbali ikiwemo uchukuzi kwa kuendeleza miundombinu mbalimbali na kuimarisha udhibiti wa huduma zinazotolewa katika sekta hii.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii ya kipekee kumpongeza na kumshukuru kwa dhati Jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuliongoza Taifa letu na kutimiza miaka minne (4) katika uongozi wake imara na maono yake yaliyoleta maendeleo makubwa nchini. Pamoja na masuala mengine, Mheshimiwa Rais ameendelea kuweka mkazo na kipaumbele katika kujenga, kuendeleza na kuboresha huduma katika sekta mbalimbali ikiwemo sekta ya uchukuzi. Ni dhahiri kuwa tumeona uthubutu na maendeleo makubwa ambayo yameendelea kutekelezwa katika sekta ya uchukuzi yakiwemo: ujenzi na uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR; maboresho ya bandari; ujenzi na ukarabati wa meli pamoja na viwanja vya ndege; kuboresha shughuli za utafutaji na uokoaji katika Maziwa Makuu; uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ikiwemo ununuzi wa ndege; ununuzi wa rada za hali ya hewa; na uendelezaji wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia katika vyuo vinavyosimamiwa na Wizara ikijumuisha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI).

5. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi hiyo ya maendeleo umeendelea kwa ufanisi na kuleta tija katika kuchochea ukuaji wa sekta mbalimbali nchini zikiwemo za kilimo, mifugo, utalii, madini, viwanda na biashara. Sote ni mashuhuda kuwa miradi iliyokamilika na kuanza kutoa huduma za usafiri na usafirishaji imekuwa chachu ya ukuaji wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Vilevile, kutokana na umahiri wake katika ubunifu na utendaji, tunu za Taifa letu zikiwemo: Utu, Uzalendo, Uadilifu, Umoja, Uwazi, Uwajibikaji na lugha ya Taifa zimeendelea kuimarika na kuifanya nchi yetu kuwa mfano mzuri wa kuigwa na Mataifa mbalimbali.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pongezi na shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa namna

anavyoendelea kumsaidia Mheshimiwa Rais katika utendaji na kuongoza nchi yetu kwa ajili ya kuwaletea maendeleo wananchi na Taifa kwa ujumla na kuongeza ufanisi katika utendaji wa Serikali.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile nimpongeze Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Kiongozi wa shughuli za Serikali Bungeni, kwa uongozi wake makini. Ni wazi kuwa kiongozi huyu ameendelea kutumikia nchi yetu kwa umahiri mkubwa kwa lengo la kuimarisha usimamizi wa shughuli za Serikali.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati, kwa kuendelea kuaminiwa na Mheshimiwa Rais kuhudumu katika nafasi hiyo. Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ameendelea kuwatumikia Watanzania kwa umakini na kuonesha uwezo mkubwa katika nafasi yake kwa kutekeleza ipasavyo majukumu yake.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kukupongeza wewe binafsi kwa umahiri na uwazi uliouonesha katika kipindi unachoendelea kutumikia Taifa letu. Ni wazi kuwa Bunge limekuwa mahiri na la mfano kimataifa kwa jinsi linavyoendesha shughuli zake. Aidha, niendelee kukupongeza kwa jinsi unavyoendelea kutekeleza kwa weledi majukumu ya nafasi ya Urais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), nafasi ambayo ni heshima kubwa kwako na kwa nchi yetu. Watanzania tunaendelea kukuombea katika utekelezaji wa majukumu yako ya ndani na nje ya nchi.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** aidha, nimpongeze Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb.), Naibu Spika kwa kuendelea kutekeleza vyema majukumu yake katika kumsaidia Spika kuliongoza Bunge. Vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza Wenyeviti wa Bunge, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga (Mb.), Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama (Mb.) na Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika (Mb.) kwa kuendelea kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

11. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa naomba kuishukuru na kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu inayoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Selemani Moshi Kakoso (Mb.) na Makamu Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb.). Sambamba na viongozi hao wa Kamati, niwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Kamati hii imeendelea kutoa ushauri wenye tija na kuwa chachu ya kuongeza ufanisi katika utendaji wa Wizara. Napenda pia kuishukuru Kamati kwa uchambuzi makini iliyoufanya kwenye Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/25 na Mpango wa makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26. Maoni na ushauri wa Kamati uliotolewa umeiwezesha Wizara kukamilisha maandalizi ya Mpango wa makadirio ya mapato na matumizi tunaouwasilisha leo mbele ya Bunge lako Tukufu.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa simanzi kubwa niungane na Bunge na Watanzania wote kutoa pole kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kwa familia husika na Taifa kwa ujumla kufuatia kifo cha aliyekuwa Makamu wa Rais wa Kwanza na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayati **Cleopa David Msuya** kilichotokea tarehe 7 Mei 2025, hakika alikuwa na mchango mkubwa katika kulitumia Taifa hili. Aidha, nitoe pole kwa Bunge lako Tukufu kufuatia kifo cha **Dkt. Faustine Engelbert Ndugulile** aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kigamboni na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Kanda ya Afrika kilichotokea tarehe 27 Novemba, 2024. Hakika tutaendelea kuthamini na kuenzi mchango wake katika Bunge hili na Taifa kwa ujumla. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awapumzishe mahali pema peponi.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee napenda kumshukuru Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa hotuba yake ambayo imetoa hali ya utekelezaji wa jumla katika utendaji wa Serikali kwa mwaka 2024/25 pamoja na kuonesha dira na mwelekeo wa Taifa letu kwa mwaka 2025/26 katika sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Uchukuzi. Pia, niwapongeze Waheshimiwa Mawaziri

wote waliowasilisha hotuba zao kabla ya hotuba yangu, ambao kwa ujumla kila mmoja ameelezea utekelezaji wa mwaka 2024/25 na mpango wake kwa mwaka 2025/26.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo hayo ya utangulizi, naomba sasa uniruhusu nitoe taarifa ya mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2024/25 pamoja na Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/26.

B: MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZAKE KWA MWAKA WA FEDHA 2024/25

15. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Sekta ya Uchukuzi imeendelea kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Uchumi kwa Taifa hili. Mchango huo umewezesha kuendelea kukua kwa sekta nyingine za uzalishaji zikiwemo sekta za kilimo, madini, utalii, viwanda na biashara. Kwa mujibu wa Taarifa ya Ofisi ya Taifa ya Takwimu Tanzania (NBS) kwa mwaka 2023, Sekta ya Uchukuzi ilikua kwa asilimia 4.1 na kuchangia katika Pato la Taifa kwa asilimia 7.2. Kimsingi sekta hii katika mwaka 2024/25 imeendelea kuwa kichocheo katika ukuaji wa uchumi ikiwemo kuanza uendeshaji wa SGR ambayo ni miongoni mwa miradi ya kimkakati katika Sekta ya Uchukuzi na Taifa kwa ujumla.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta hii ni moja kati ya sekta zinazochangia fedha za kigeni kupitia mauzo ya huduma za Uchukuzi (Trade in Services). Kwa mujibu wa Taarifa za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kipindi cha kuanzia Julai 2024 hadi kufikia Machi 2025, Sekta ya Uchukuzi ilichangia mauzo ya kiasi cha Dola za Marekani bilioni 2.48 ya fedha za kigeni sawa na ongezeko la asilimia 8.30 ikilinganishwa na Dola za Marekani bilioni 2.29 zilizopatikana katika mauzo katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/24. Kwa ujumla sekta hii hutoa mchango mkubwa katika sekta mbalimbali ikijumuisha sekta ya Utalii ambapo mchango huo wa mauzo ya usafirishaji huainishwa kila mwaka kupitia taarifa inayoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

17. ***Mheshimiwa Spika,*** mchango huo wa fedha za kigeni unaotolewa na Sekta ya Uchukuzi unatokana na kodi za ushuru wa forodha, kodi ya ongezeko la thamani (VAT) na kodi nyingine, hususan inayotokana na mafuta ya petroli na dizeli pamoja na ajira za Watanzania walioajiriwa au kujiajiri katika biashara za uendeshaji wa bandari, usafiri na usafirishaji kwa njia ya maji, barabara, reli na anga. Kwa ujumla sekta mbalimbali zimeendelea kufungamanishwa na huduma za uchukuzi na kuwezesha biashara ndani ya nchi, kikanda na kimataifa.
18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi (Fungu 62) iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,729,676,417,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 114,744,476,000** ni za Matumizi ya Kawaida ya Wizara na Taasisi zake na **Shilingi 2,614,931,941,000** ni za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2025 Wizara ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 1,674,448,400,698.31** sawa na **asilimia 61.34** ya bajeti yote ya Wizara iliyoidhinishwa.

Bajeti ya Matumizi ya Kawaida
19. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya **Shilingi 114,744,476,000** zilizoidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, **Shilingi 86,661,930,000** ni fedha za Mishahara na **Shilingi 28,082,546,000** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) kwa ajili ya Wizara na Taasisi zake. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 100,111,641,231.41** sawa na **asilimia 87.25** ya bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyoidhinishwa zilikuwa zimetolewa. **Bajeti ya Miradi ya Maendeleo**

20. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi ilitengewa jumla ya **Shilingi 2,614,931,941,000** kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 2,524,369,202,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 90,562,739,000** ni fedha za nje. Hadi kufikia Aprili, 2025 jumla ya **Shilingi 1,574,336,759,466.90** sawa na **asilimia 60.21** ya bajeti yote ya Maendeleo iliyoidhinishwa zilitolewa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi baada ya kupokea fedha hizo, iliendelea kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli mbalimbali zilizopangwa katika mwaka 2024/25. Lengo

ni kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za uchukuzi zinazozingatia usalama, uhakika na unafuu wa gharama nchini na kuimarisha biashara kati ya Tanzania na nchi nyingine.

B.1. UDHIBITI NA UTOAJI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI B.1.1. UDHIBITI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI

22. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za uchukuzi nchini, Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA), Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za uchukuzi kama ifuatavyo:

UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kusimamia na kudhibiti usafiri katika sekta ndogo za reli, barabara pamoja na kuanza maandalizi ya awali kwa ajili ya udhibiti usafiri wa waya. Aidha, LATRA inalo jukumu la kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vinavyodhibitiwa ili kuboresha usalama na ubora wa huduma katika usafiri ardhini.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) imeendelea kudhibiti na kutoa huduma mbalimbali, zikiwemo leseni na vibali ambapo kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, LATRA ilitoa jumla ya leseni 250,096 za usafirishaji ikiwa ni sawa na ongezeko la leseni 8,283, ikilinganishwa na leseni 241,813 zilizotolewa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2023/24. Kati ya leseni hizo, leseni 38,334 ni za mabasi ya abiria, leseni 155,041 ni za magari ya mizigo na leseni 56,721 ni za magari ya kukodi.

Mifumo ya Ufuatiliaji wa Usafiri Ardhini

25. ***Mheshimiwa Spika,*** LATRA imeendelea kuimarisha usalama kwa kufanya ufuatiliaji wa mwenendo wa mabasi ya masafa marefu na treni za TAZARA na TRC kwa kutumia mfumo wa Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Magari (Vehicle Tracking System - VTS). Hadi kufikia Machi, 2025 mabasi yote ya masafa marefu ambayo ni 11,826 yaliyopewa leseni yalikuwa yameunganishwa kwenye mfumo wa VTS. Mfumo unaonesha kuwa, wastani wa

mabasi 8,969 yanatuma taarifa kila siku, sawa na asilimia 76 ya mabasi yote. Aidha, mabasi 2,857 yaliyobaki ambayo ni asilimia 24 ni mabasi yaliyosimama kutoa huduma kwa sababu mbalimbali zikiwemo ajali na matengenezo. Wamiliki wote wa mabasi yaliyounganishwa na mfumo wamepewa akaunti za VTS ili waweze kufuatilia mabasi yao na kuchukua hatua stahiki kulingana na makosa yanayojitokeza. Vilevile, ili kuleta ufanisi zaidi na baada ya LATRA kutumia mfumo wa VTS miaka nane (8), katika mwaka 2024/25, imefanyika tathmini ya kina ya teknolojia zinazotumika katika mfumo huo. Lengo la tathmini hiyo ni kujua uwezo wa mfumo huo na hivyo kuendelea kuongeza wigo wa matumizi yake.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua ya kuongeza wigo wa kufuatilia mwenendo wa mabasi, LATRA imewezesha upatikanaji wa taarifa za mabasi kupitia mfumo wa Taarifa kwa Abiria (Passenger Information System - PIS) ulioounganishwa na VTS. Kwa kupitia mfumo huo, abiria anaweza kufuatilia taarifa za mabasi kupitia kiunganishi ***pis.latra.go.tz.*** Aidha, mfumo huu unamwezesha mtumiaji kuwasiliana na watoa huduma wa LATRA na kutoa mrejesho/ malalamiko na kupatiwa msaada kupitia namba 0800 110019/20.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** LATRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) na wadau wengine inaendelea kufanya maboresho ya mfumo wa usimamizi wa usafiri ardhini (Railway and Road Information Management System - RRIMS) ambao unasajili watoa huduma na vyombo vyao, kuchakata taarifa za maombi ya leseni pamoja na kusajili na kuthibitisha madereva. Maboresho haya yamefanywa kwa kuzingatia mirejesho ya watumiaji wa mfumo na kwa sasa, mfumo huo umewekwa kwenye simu za viganjani (LATRA App) ili kurahisisha matumizi na kuleta ufanisi. Niendelee kuwasisitiza Watanzania, hususan madereva na kuwataka kuendelea kujisajili katika mfumo huu ili kuimarisha udhibiti nchini.

Utoaji wa Tiketi za Kielektroniki kwa Mabasi ya Abiria na Usafiri wa Treni

28. ***Mheshimiwa Spika***, maendeleo na maboresho makubwa yamefanyika ili kuboresha huduma za usafiri wa umma kwa

mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani kwa kuanza kutoa Tiketi za Kielektroniki kuanzia mwezi Julai, 2022. LATRA kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo: Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA), Jeshi la Polisi Tanzania (TPF), Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), Shirika la Reli Tanzania (TRC), watoa huduma wa tiketi za kielektroniki (e-ticketing vendors) pamoja na Chama cha Wamiliki wa Mabasi Tanzania (TABOA) imekamilisha ujenzi wa Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao. Mfumo huu unarahisisha utoaji wa huduma za usafiri wa mabasi yaendayo mikoani na nchi jirani na ambao ni mahsusi kwa ajili ya kukusanya takwimu zote muhimu za kisekta pamoja na kudhibiti nauli za mabasi.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao, pia husaidia kutambua abiria walio kwenye chombo cha usafiri (passengers manifest) hasa inapotokea dharura, mfumo huu Mkuu wa Tiketi Mtandao, tayari unawezesha abiria kukata tiketi za mabasi na treni (SGR na MGR) kupitia dirisha moja. Hadi sasa mfumo huu kwa upande wa treni unafanya kazi kwa ukamilifu. Aidha, kwa upande wa mabasi utakamilika mara tu baada ya kukamilika usajili wa mifumo iliyokidhi vigezo vya kuendelea kutoa huduma ya tiketi mtandao ambapo jumla ya mifumo 14 ya watoa huduma (e-Ticketing Vendors) imeunganishwa kwenye Mfumo Mkuu wa Tiketi Mtandao baada ya kukidhi viwango. Kazi hii ya kuunganisha mifumo inatarajiwa kukamilika na kuanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai, 2025. Aidha, taarifa zinazokusanywa na mfumo huu zinawezesha kutambua mchango wa sekta ya usafiri wa umma (mabasi na treni) kwenye mapato ya Serikali.

Udhibiti wa Madereva na Wahudumu wa Vyombo Vinavyodhibitiwa

30. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha weledi na kudhibiti mwenendo wa madereva barabarani, LATRA imeendelea kusajili, kuthibitisha na kufuatilia mienendo ya madereva wakiwa barabarani kupitia mifumo ya TEHAMA. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya madereva 7,232 walisajiliwa kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Usafiri Ardhini (RRIMS) na kutahiniwa kupitia Mfumo wa Kutahini Madereva (Drivers Testing System - DTS) ambapo kati ya hao madereva 1,550 walithibitishwa. Serikali imeweka utaratibu wa lazima wa

madereva wa safari za usiku kwa mabasi ya abiria kuwa na kitufe cha utambuzi (i-Button). Aidha, Serikali inaendelea kuboresha mfumo huo ili utumike kuthibitisha madereva wa treni. Kwa upande wa usajili wa wahudumu hadi kufikia Machi 2025, LATRA ilisajili wahudumu 560 baada ya kupewa mafunzo ambayo yalitolewa kwa kushirikiana na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE).

Udhibiti Usafiri wa Waya (Cable Transport)

31. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu usafiri kwa njia ya waya, katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, LATRA ilishirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Wizara ya Maliasili na Utalii, Wakala wa Misitu (TFS), Wakala wa Wanyamapori (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (TANAPA), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Halmashauri za Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Iringa, Mbeya, Pwani na Dar es Salaam pamoja na Sekta Binafsi katika kutambua uwepo, fursa, utayari na mahitaji ya udhibiti wa huduma hii nchini. Aidha, wadau mbalimbali kutoka ndani na nje ya nchi wameonesha utayari wa kuwekeza katika usafiri kwa njia ya waya. Kutokana na fursa hiyo, Wizara ya Uchukuzi inaandaa Kanuni za Udhibiti wa Usafiri wa Waya baada ya kupokea maoni ya wadau mwezi Desemba 2024 pamoja na kufanya maombi ya mabadiliko ya muundo wa LATRA ili kuwe na kitengo mahsusi katika udhibiti wa usafiri huo.

Kufikisha Huduma Karibu na Wananchi

32. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kupanua wigo wa huduma ili kufikia wananchi kiurahisi zaidi. Pamoja na jitihada za kuboresha huduma za udhibiti kupitia mifumo ya TEHAMA, katika kipindi cha mwaka 2024/25, LATRA imefungua ofisi ndogo 10 katika maeneo mbalimbali ya kimkakati, ambayo ni Stendi za Magufuli, Tegeta na Mbagala za jijini Dar es Salaam; na Halmashauri za Same, Korogwe, Nzega, Masasi, Makambako, Ifakara na Kahama. Hii inafanya jumla ya Ofisi za LATRA kuwa 37 nchi nzima, ambazo zinajumuisha Ofisi 26 za Makao Makuu ya mikoa yote na Ofisi Maalum ya Kituo cha Mikocheni ambayo ni kwa ajili ya kusimamia Mfumo wa VTS.

UDHIBITI WA HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) imeendelea kusimamia sekta ya usafiri wa anga kwa kutoa huduma za udhibiti wa anga, viwanja vya ndege, usalama na masuala ya kiuchumi. Aidha, TCAA inaendelea kutoa huduma za uongozaji ndege katika viwanja vya ndege 15 vya Dar es Salaam, Zanzibar, Mwanza, Bukoba, Arusha, Pemba, Tabora, Kigoma, Dodoma, Iringa, Songwe, Mtwara, Tanga, Songea na Kilimanjaro. Pia, TCAA imeendelea kudhibiti viwanja vya ndege vinavyomilikiwa na Taasisi za Serikali pamoja na Sekta Binafsi. Hatua hii inalenga kuboresha utoaji wa huduma, kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii na kuhakikisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za uendeshaji wa viwanja vya ndege nchini. Vilevile, TCAA imeendelea kutoa huduma za uongozaji ndege zinazoruka na kupita katika anga la juu la Burundi kwa urefu wa futi 24,500 kutoka usawa wa bahari, ambalo limekasimiwa kwa Tanzania na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO).

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya ndege 17 zilizosajiliwa zilifanyiwa ukaguzi na kupewa vyeti vya awali vya ubora wa anga (Certificate of Airworthiness). Ndege hizo ni: Cessna 208 tano (5), ATR mbili (2), Gulfstream moja (1), Helikopta za Airbus AS350B3 tatu (3), Boeing 787 Dreamliner moja (1), Pilatus PC12/47E moja (1), Embraer 120ER moja (1), Microlight moja (1), Cessna 152 moja (1) na Cameroon A450 moja (1). Aidha, ndege mbili (2) ziliondolewa kwenye daftari la usajili kufuatia kufikia ukomo wa mikataba ya ukodishaji. Vilevile, jumla ya ndege 142 zilifanyiwa ukaguzi ndani ya nchi na kupewa vyeti vya ubora wa kuendelea na shughuli za usafiri wa anga. Hadi kufikia Machi 2025, daftari la usajili wa ndege nchini lina jumla ya ndege 467.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TCAA, imeendelea kufanya mapitio na kusaini Mikataba ya Usafiri wa Anga (Bilateral Air Services Agreements - BASA) kati yake na nchi nyingine ili kufungua soko la usafiri wa anga. Hatua hii inalenga kuboresha huduma za usafiri wa anga, kuvutia mashirika mapya kutoa huduma nchini na kuimarisha ushindani katika sekta hiyo. Aidha, katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali imefanya majadiliano ya mikataba ya usafiri wa anga na nchi 14 katika Mkutano wa

Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAN2024) uliofanyika mwezi Desemba, 2024 jijini Kuala Lumpur, Malaysia. Kutokana na mkutano huo, Tanzania iliingia mikataba mipya mitatu (3) na nchi za Uzbekistan, Benin na Latvia ambapo hadi kufikia mwezi Machi 2025, Tanzania ilikuwa imeingia mikataba ya BASA na jumla ya nchi 88, ikilinganishwa na nchi 85 zilizokuwa na mikataba hiyo katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2025, jumla ya mashirika 30 ya ndege za kimataifa yameendelea kutoa huduma kwa utaratibu wa mikataba ya usafiri wa anga baina ya Tanzania na nchi nyingine (BASA) ikilinganishwa na mashirika 25 yaliyotoa huduma katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ongezeko la mashirika ya ndege za kimataifa limechangiwa na kuendelea kukua kwa soko la usafiri wa anga nchini kutokana na umahiri wa Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ameendelea kutangaza vivutio vya utalii nchini, hususan kupitia filamu ya Tanzania *The Royal Tour* na kuvutia watalii na hatimaye kuvutia mashirika mapya ya ndege kuanzisha safari zao nchini Tanzania.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mikakati ya kuimarisha Sekta ndogo ya Anga, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga imeongezeka na kufikia abiria 6,037,444, ikilinganishwa na abiria 5,080,920 waliotumia usafiri huo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 18.8. Ongezeko hili limetokana na kuendelea kuimarika kwa biashara ya usafiri wa anga nchini, hususan kutokana na uboreshaji mkubwa wa miundombinu ya usafiri wa anga.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya abiria waliotumia usafiri wa anga ndani ya nchi imeendelea kuongezeka. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi kufikia Machi 2025, idadi ya abiria waliosafiri ndani ya nchi imefikia 3,201,362, ikilinganishwa na abiria 2,769,192 waliosafiri katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2023/24. Hili ni sawa na ongezeko la asilimia 15.6. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri kimataifa imefikia 2,836,082, ikilinganishwa na abiria 2,311,728 waliosafiri katika kipindi kama

hicho cha mwaka wa fedha 2023/24, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 22.6.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mizigo iliyosafirishwa kwa kutumia usafiri wa anga imeongezeka. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025, jumla ya tani 33,112.5 za mizigo zilisafirishwa ikilinganishwa na tani 27,532 za mizigo zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2023/24. Kati ya mizigo hiyo, tani 30,637.2 zilisafirishwa nje ya nchi na tani 2,475.3 zilisafirishwa ndani ya nchi. Ongezeko la mizigo inayosafirishwa linatokana na kuendelea kuimarika kwa usafiri wa anga pamoja na ununuzi wa ndege ya mizigo ya ATCL jambo ambalo limechangia kuongeza kwa usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TCAA imeendelea kuongoza ndege za mashirika ya ndani na kimataifa ambapo hadi kufikia Machi 2025, jumla ya miruko ya safari za ndege ilikuwa 222,307, ikilinganishwa na miruko 205,968 katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/24. Kuongezeka kwa kiwango cha usafirishaji wa abiria, mizigo na miruko ya ndege kunatokana na ukuaji wa biashara ya usafiri wa anga duniani, kuongezeka kwa mashirika mapya ya usafiri wa anga yanayokuja nchini, pamoja na kurejeshwa kwa baadhi ya njia za ndege (routes) na njia za kupitia (en-routes).

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha usalama wa usafiri wa anga, Serikali imeendelea kuboresha mawasiliano ya sauti baina ya mwongoza ndege na rubani ambapo ufungaji wa mitambo ya mawasiliano ya sauti umekamilika katika kituo mbadala cha mawasiliano kwa dharura (Back-up Center) pamoja na viwanja vya ndege 12 ambavyo ni Julius Nyerere International Airport (JNIA), Pemba, Abeid Amani Karume International Airport (AAKIA), Kilimanjaro (KIA), Tanga, Dodoma, Arusha, Tabora, Kigoma, Mtwara, Mwanza na Songwe.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ufungaji wa mitambo kwenye vituo 18 (VHF relay stations) kwa ajili ya mawasiliano ya anga la juu umekamilika. Vituo hivyo vilivyofungwa mitambo husika ni Gairo (Morogoro), Matogoro (Songea), Michakaini (Pemba),

Nambunga (Newala-Mtwara), Lolkisale (Arusha), Kwenjugo (Handeni - Tanga), Mwaseni (Rufiji - Pwani), Kitulo (Njombe), Kaluwe (Mbeya), Mwisi (Igunga - Tabora), Kasulu (Kigoma), Nyamanyama (Biharamulo - Kagera), Ndisso - Sitalike (Katavi), Muganza (Butiama - Mara), Mugumu (Serengeti), Oldean Malanja (Ngorongoro - Arusha), Lubuli (Dodoma) na Ngoli (Dodoma).

43. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi, 2025 TCAA ilitekeleza kazi nyingine kama ifuatavyo: -

i. Kufunga mifumo ya kutoa taarifa za hali ya hewa kwa njia ya sauti ya redio (D-ATIS) katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere (JNIA) na Abeid Amani Karume (AAKIA). Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 60, ambapo JNIA kazi ya ufungaji, mafunzo kwa wataalam na upokeaji wa mradi (Site acceptance) yamekamilika na shehena ya mitambo kwa ajili ya Kiwanja cha AAKIA inatarajiwa kuwasili kabla ya mwishoni mwa mwezi Mei 2025;
ii. Kupatikana kwa mkandarasi wa mradi wa Mfumo wa Kuruka na Kutua kwa Ndege kwa kutumia msaada wa vifaa vya kielektroniki (ILS) katika kiwanja cha ndege cha JNIA ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 5;
iii. Kupatikana kwa Mkandarasi wa ujenzi wa Chuo cha Kisasa cha Usafiri wa Anga (CATC) ambapo ujenzi huo utachukua miaka mitatu (3) na unalenga kuboresha miundombinu ya kutoa mafunzo kwa wataalam wa usafiri wa anga ndani na nje ya nchi; na
iv. Kufanya ukaguzi wa usalama wa usafiri wa anga kwa kuzingatia viwango vya ICAO. Ukaguzi huu umehusisha mashirika ya ndege (AOC Holders), vituo vya matengenezo (AMOs), wahandisi wa ndege (AML Holders), na ndege zilizosajiliwa nchini. Taarifa za ukaguzi zimeingizwa katika mfumo wa ICAO USOAP *Online Framework*. Kupitia taarifa hizo, nchi yetu imeendelea kuaminika kiudhibiti katika masuala ya anga na kufanya mashirika ya ndege kuendelea kufanya safari zake nchini na kuondoa hoja zilizojitokeza wakati wa ukaguzi.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** kama ambavyo nimekuwa nikiahidi kwa Watanzania kuhusu uimarishaji wa usimamizi wa masuala ya usalama wa usafiri wa anga, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa sasa Serikali imeanzisha rasmi Kitengo cha Uchunguzi wa Ajali za Ndege baada ya Muundo wa Wizara kuhuishwa na kupitishwa na Mamlaka zinazohusika mwezi Machi, 2024. Hii ilikuwa ni mwendelezo wa maamuzi ya Serikali ya Mwaka 2009 ya kuhamisha majukumu ya Uchunguzi wa Ajali za Ndege kutoka ndani ya idara iliyokuwa chini ya Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania (TCAA). Madhumuni ya kuanzishwa kwa Kitengo cha Uchunguzi wa Ajali za Ndege ni kuzuia ajali au matukio kwa kufanya uchunguzi wa kina wa ajali na matukio ya ndege kwa wakati bila kuegemea upande wowote, ili kubaini vyanzo na sababu za ajali na matukio ikiwa ni pamoja na kutoa mapendekezo ya usalama yanayokusudiwa kuzuia kujirudia kwa ajali na matukio.

45. ***Mheshimiwa Spika,*** kuanzishwa kwa Kitengo cha Uchunguzi wa ajali za Ndege ni kukidhi matakwa ya Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO), ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 26 ya Mkataba wa Chicago (Chicago Convention) wa Mwaka 1944 ukisomwa pamoja na Kiambatisho cha 13 (Annex 13). Mkataba huo unataka shughuli za uchunguzi wa ajali za ndege kuwa chini ya kitengo huru kisichoingiliwa na mamlaka nyingine zinazohusika na usafiri wa anga, ili kuhakikisha kunakuwa na ufanisi katika utendaji kazi na kuepuka mgongano wa maslahi.

UDHIBITI WA USAFIRI MAJINI

46. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (TASAC) imeendelea kusimamia ulinzi na usalama wa vyombo vya usafiri majini katika eneo la Tanzania Bara; udhibiti wa huduma za bandari na watoa huduma za usafiri na usafirishaji; kutoa huduma ya biashara ya meli kwa bidhaa mahsusi; na kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na shughuli za usafiri majini.

Udhibiti wa Watoa Huduma za Usafirishaji Majini

47. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TASAC imeendelea na usimamizi wa watoa huduma zinazodhibitiwa kwa kutoa leseni/vyeti vya usajili kwa watoa huduma waliokidhi vigezo na

kusimamia utekelezaji wa masharti ya leseni hizo. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya watoa huduma 1,556 zinazodhibitiwa walisajiliwa na kupewa leseni. Baada ya usajili huo, TASAC iliendelea kufanya ufuatiliaji, tathmini na kutoa maelekezo kuhusu utekelezaji wa vigezo na viwango vya ubora wa huduma kwa watoa huduma za bandari na usafiri majini.

Usalama wa Vyombo vya Usafiri Majini

48. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kutekeleza miongozo yake ikiwemo Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ambayo katika Ibara 59(c) pamoja na mambo mengine, Serikali iliahidi kuboresha usalama wa usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ununuzi wa boti maalum ya kisasa ya matibabu (Modern Ambulance Boat) yenye vifaa vya uokoaji, huduma za dharura za afya na matibabu ndani ya Ziwa Victoria umekamilika. Boti hiyo imewasili nchini tarehe 31 Machi, 2025 katika Bandari ya Mtwara na taratibu za boti hiyo kuanza kutoa huduma zinaendelea.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** TASAC imeendelea kuratibu shughuli za utafutaji na uokoaji kupitia Vituo vya Utafutaji na Uokoaji Majini vilivyopo Dar es Salaam na Mwanza. Kutokana na uratibu huo, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025, jumla ya matukio 22 ya ajali yaliripotiwa. Serikali kupitia TASAC imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali kwa lengo la kupunguza ajali za vyombo vya usafiri majini ikiwemo kuendelea kutoa elimu, kubaini changamoto na kushirikiana na wadau katika kuzitatua. Aidha, TASAC imeendelea kusambaza taarifa za hali ya hewa kwa wadau wa usafiri majini kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kutuma ujumbe mfupi kwa njia ya simu.

50. *Mheshimiwa Spika,* katika kipindi hicho, TASAC ilifanya kaguzi za usalama kwa meli kubwa 63 za ndani na za kimataifa zenye ujazo wa tani 50 na kuendelea zinazofanya shughuli katika maeneo ya Tanzania. Kufuatia kaguzi hizo, vyeti vya ubora vilitolewa kwa vyombo vilivyothibitika kukidhi matakwa ya kiusalama. Aidha, vyombo vidogo 14,787 vyenye ujazo wa chini ya tani 50 vilifanyiwa ukaguzi ili kuhakikisha kuwa ni salama na

vinaendeshwa na mabaharia wenye sifa ambapo vyombo 10,675 sawa na asilimia 72.19 ya vyombo hivyo vilikidhi matakwa ya kiusalama na kupewa vyeti vya ubora. Kasoro zilizojitokeza mara kwa mara katika kaguzi za vyombo vidogo ni pamoja na kukosekana kwa vifaa vya kujiokoa, vifaa vya zimamoto na vifaa vya kuongoza vyombo na mawasiliano. Kaguzi hizo zilifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Mwanza, Kigoma, Kagera, Mara, Mbeya, Pwani, Lindi, Rukwa na Geita.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha usalama wa usafiri na usafirishaji katika Ziwa Victoria, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Jamhuri ya Uganda chini ya uratibu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kupitia Kamisheni ya Bonde la Ziwa Victoria, zimeendelea kutekeleza Mradi wa Kikanda wa kuboresha Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria wenye lengo la kuimarisha huduma za utafutaji na uokoaji pindi inapotokea ajali katika Ziwa hilo. Hadi kufikia Machi, 2025 utekelezaji wa mradi huo ambao pamoja na shughuli nyingine, unahusisha ujenzi wa Kituo Kikuu cha Kikanda cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokoaji katika Ziwa Victoria kinachojengwa Ilemela Jijini Mwanza ambacho ujenzi wake umefikia asilimia 71. Kukamilika kwa kituo hicho kutaimarisha usalama wa usafiri na usafirishaji katika Ziwa Victoria.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi huo pia unahusisha ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokoaji katika Ziwa Victoria kwenye maeneo mbalimbali. Ujenzi wa vituo hivyo umefikia hatua mbalimbali kama ifuatavyo: Kanyala - Sengerema umefikia asilimia 68; Nansio - Ukerewe umefikia asilimia 71; na Musoma Mjini umefikia asilimia 80. Pamoja na ujenzi wa vituo hivyo, ununuzi wa boti mbili (2) za Utafutaji na Uokoaji zitakazotumika katika Ziwa Victoria umefikia asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika kabla ya mwisho wa mwaka 2025.

Usimamizi na Udhibiti wa Utoaji wa Mafunzo ya Usafiri Majini

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kusimamia utekelezaji wa miongozo ya kimataifa, TASAC imeendelea kutekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Mafunzo, Utoaji vyeti na Utendaji kazi kwa Mabaharia wa mwaka 1978 pamoja na mabadiliko yake (International Convention on Standards of Training, Certification and Watch-keeping for seafarers – STCW 1978 as amended) ili

kuhakikisha kuwa vyombo vya usafiri majini vinaendeshwa na mabaharia wenye sifa, vigezo na uzoefu unaostahili. Hadi kufikia Machi 2025, TASAC ilitoa jumla ya vyeti 10,270. Kati ya vyeti hivyo, vyeti vya ustadi (Certificates of Proficiency - COP) vilikuwa 9,459, vyeti vya kumbukumbu za kazi kwa Mabaharia (Continuous Discharge Certificates – CDC) vilikuwa 729 na vyeti vya umahiri kwa maofisa wa meli (Certificates of Competency - COC) vilikuwa 82. Kutokana na utekelezaji mzuri wa mkataba wa STCW, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweza kukidhi viwango vya ukaguzi wa utekelezaji wa Mkataba huo, ambapo jina la Tanzania litaendelea kuwepo katika nchi safi (Whitelist) miongoni mwa wanachama wa Shirika la Bahari Duniani (IMO) zinazotekeleza Mkataba huo. Hii ni baada ya taarifa ya Ukaguzi huo kupitishwa na wataalam wa IMO Januari 8, 2025 na jina litapitishwa rasmi katika kikao cha 110 cha kamati ya Usalama ya Shirika la Bahari Duniani - Maritime Safety Comitee (MSC 110).

Uwakala wa Forodha kwa Shehena za Kipekee

54. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza jukumu la kipekee la ugomboaji wa shehena, TASAC imeendelea kutoa huduma za Uwakala wa Forodha kwa Shehena za Kipekee (exclusive mandate) kwa mujibu wa kifungu cha 7 cha Sheria ya Uwakala wa Meli Tanzania, Sura 415 na marekebisho ya Sheria ya Fedha Na. 5 ya mwaka 2022. Kutokana na jukumu hilo, hadi kufikia Machi, 2025 TASAC iliwapatia mafunzo mbalimbali watumishi 24 wanaotekeleza majukumu ya ugomboaji na uondoshaji wa shehena zilizoainishwa kisheria; kuhusu maandalizi ya taratibu za utendaji kazi (Internal Operating Procedures-IOPs); na kufanya tathmini ya ufanisi na uwezo wa ugomboaji na *uondoshaji* wa shehena.

Kongamano la Kimataifa na Mkutano Mkuu wa Saba (7) wa Shirikisho la Mamlaka za Udhibiti wa Usafiri Majini Afrika

55. ***Mheshimiwa* Spika,** Serikali kupitia TASAC iliratibu na kupewa heshima ya kuwa mwenyeji wa Kongamano la Kimataifa na Mkutano Mkuu wa saba (7) wa Shirikisho la Mamlaka za Udhibiti wa Usafiri Majini Afrika (7th Conference of the Association of African Maritime Administrations – AAMA and the General Assembly) lililofanyika kuanzia tarehe 29 Novemba hadi 1 Desemba, 2024 Jijini Dar es Salaam, Tanzania. Kongamano hilo

huwakutanisha wadau wa Sekta ya Usafiri Majini kutoka nchi mbalimbali duniani kwa ajili ya kujadili, kubadilishana uzoefu, kuibua fursa na kujifunza mikakati ya kuboresha usimamizi wa usafiri na usafirishaji majini. Mikakati iliyojadiliwa ni pamoja na: ushirikiano baina ya nchi wanachama wa Shirika la Bahari Duniani katika kuimarisha usalama na ulinzi wa usafiri majini; namna ya kujenga uwezo na utoaji wa mafunzo kwa wataalam katika sekta ya usafiri majini; na mikakati endelevu ya kulinda mazingira ya Bahari. Kufanyika kwa Kongamano hilo la Kimataifa pamoja na Mkutano Mkuu wa AAMA katika Taifa letu kumeleta mafanikio ya kiuchumi na kumeipa nchi yetu fursa mbalimbali za kiuchumi hususan katika sekta ya usafiri majini. Kongamano hilo lilihudhuriwa na takribani washiriki 300 kutoka nchi mbalimbali barani Afrika zikiwemo Kenya, Ghana, Angola, Msumbiji, Nigeria, Afrika ya Kusini na Cape Verde.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na utekelezaji huo, TASAC imetekeleza kazi nyingine katika kipindi cha mwaka 2024/25 ambazo ni pamoja na: Kuandaa kanuni saba (7) za kutoa mwongozo kuhusu udhibiti, usalama na ulinzi wa vyombo vya usafiri na usafirishaji majini; na kuwajengea uwezo watumishi kwa kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na udhibiti, uwakala wa forodha, ugomboaji, uondoshaji shehena mahsusi na huduma saidizi ili kuongeza weledi na kuboresha utendaji kazi unaoendana na mabadiliko ya teknolojia. Hadi kufikia Machi, 2025 watumishi zaidi ya 140 walihudhuria mafunzo ya kujengewa uwezo.

UDHIBITI WA HUDUMA ZA HALI YA HEWA

57. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea na utoaji wa huduma za hali ya hewa pamoja na kudhibiti na kuratibu shughuli za hali ya hewa nchini. Aidha, majukumu mengine ni pamoja na kupima na kufuatilia mifumo ya hali ya hewa, kufanya tafiti za kisayansi juu ya mabadiliko ya hali ya hewa nchini, kubadilishana taarifa za hali ya hewa katika mtandao wa mawasiliano wa dunia (Global Telecommunication System - GTS) kulingana na makubaliano ya kimataifa pamoja na kuiwakilisha Tanzania katika masuala ya hali ya hewa kikanda na kimataifa. Aidha, TMA imeendelea kushirikisha wadau

mbalimballi katika utekelezaji wa majukumu yake na hivyo kuweza kutoa huduma kwa ufanisi zaidi.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** TMA imeendelea kuhimili katika viwango vyake vya utoaji wa huduma kimataifa, ambapo imetoa huduma za utabiri wa kila siku, siku 10 na ule wa muda mrefu. Aidha, TMA imeendelea kutoa tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa ili kuhakikisha usalama wa watu na mali zao, ambapo usahihi wa utabiri nchini umeendelea kuwa katika kiwango cha juu cha asilimia 86 ikilinganishwa na asilimia 70 ya kiwango cha usahihi kinachokubalika na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO). Kutokana na ufanisi huu, TMA imeendelea kuaminiwa na WMO na kuifanya nchi yetu itambulike kikanda na kimataifa katika nyanja za hali ya hewa. Kutokana na kuaminiwa huko, Tanzania kupitia TMA imepewa jukumu la kusaidia nchi nyingine katika baadhi ya masuala ya uboreshaji wa Huduma za Hali ya Hewa yakiwemo: kuweka na kuendesha mifumo ya udhibiti wa ubora katika utoaji wa huduma hizo katika maeneo ya usafiri wa Anga, mifumo ya uchakataji, ubadilishanaji na usambazaji wa *data*. Nchi zilizosaidiwa hadi sasa ni pamoja na Namibia na Burundi. Aidha, TMA imepokea maombi ya kuzisaidia nchi za Uganda, Zimbabwe, Sudan ya Kusini, Siera Leoni, Gambia, Zambia na Guinea na majadiliano na nchi hizo yanaendelea.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59(j), Serikali iliahidi kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa ikiwemo ununuzi wa Rada na vifaa vya hali ya hewa. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia TMA imekamilisha uboreshaji (upgrading) wa rada mbili (2) za hali ya hewa zilizokuwepo katika mikoa ya Mwanza na Dar es Salaam ili kuendana na teknolojia ya kisasa ya uendeshaji na kuleta ufanisi zaidi katika utoaji wa huduma.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha huduma za hali ya hewa kwenye sekta ndogo ya usafiri wa anga, Serikali ilikamilisha ufungaji wa mitambo miwili (2) ya kutoa huduma za hali ya hewa katika viwanja vya ndege vya Iringa na Bukoba. Aidha, TMA ilifanyiwa ukaguzi wa kimataifa wa utekelezaji wa mfumo wa

kudhibiti ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa katika sekta ya usafiri wa anga kuanzia tarehe 03 hadi 14 Machi, 2025. Kutokana na ufanisi uliobainika, TMA imeendelea kukidhi vigezo vya kumiliki cheti cha ubora (ISO 9001: 2015) katika sekta ya usafiri wa anga.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kununua na kufunga mitambo na vifaa vya hali ya hewa ikiwemo seti ya mitambo 20 ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe (Automatic Weather Station – AWS) ambapo ufungaji wa mitambo hiyo unaendelea. Aidha, seti ya mitambo 15 ya kupima hali ya hewa kilimo (Agro – synoptic station) imenunuliwa ambapo seti 10 za mitambo hiyo zimefungwa katika vituo vya Kibaha, Naliendele, Kilwa Masoko, Lyamungo, Mlingano, Hombolo, Matangatuwani, Kizimbani, Uyole na Mbinga.

62. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini, Serikali kupitia TMA imeendelea kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo ya kuweka mifumo ya kisasa ya uchakataji wa data na uandaaji wa utabiri. Mathalan, TMA iko katika hatua za mwisho za ununuzi wa mtambo wenye mfumo wa kisasa wa kuandaa utabiri ambao utengenezaji wake umekamilika nchini Ufaransa na kwa sasa taratibu za kuusafirisha kuja nchini zinaendelea.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** TMA imeendelea kutoa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kupitia Ofisi zake tisa (9) zilizopo katika bandari za Malindi - Unguja, Mkoani - Pemba, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Ziwa Victoria katika Bandari ya Mwanza, Ziwa Tanganyika katika Bandari za Kigoma na Karema na Ziwa Nyasa katika Bandari ya Itungi na hivyo kuongeza mchango wa TMA katika uchumi wa buluu.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhabarisha Umma wa Watanzania kuhusu taarifa za hali ya hewa, Serikali imeongeza wigo wa kutoa taarifa za hali ya hewa kwa umma kwa kusaini mikataba ya utangazaji wa taarifa hizo na vituo sita (6) vya redio za jamii ambazo ni Machesha FM (Katavi), Point FM (Dodoma), Kings FM (Njombe), Mum FM (Morogoro), Ileje FM (Mbeya) na

City FM (Dar es Salaam) pamoja na vituo viwili (2) vya televisheni vya St Bongo (Dar es Salaam) na Mahaasin TV (Mwanza). Hatua hii imewezesha kuwa na jumla ya vyombo vya habari 116 vinavyohusisha vituo 86 vya redio, vituo 19 vya televisheni, magazeti matatu (3) na Televisheni Mtandao (on-line TV) nane (8).

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TMA imeendelea kufanya tafiti mbalimbali zinazohusiana na masuala ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya tafiti tano (5) zimefanyika na kuchapishwa katika majarida mbalimbali ya kisayansi ya kimataifa. Tafiti hizo ni pamoja na: tathmini ya matukio ya mvua kubwa na namna ya kukabiliana na hali mbaya ya hewa nyanda za juu kusini mwa Tanzania; tathmini ya halijoto ya Bahari ya Hindi; tathmini ya hali mbaya ya hewa na athari zake kwenye ajali za Baharini; tathmini ya joto nchini katika msimu wa Vuli; na tathmini ya athari za mabadiliko ya tabianchi katika kilimo. Aidha, matokeo ya tafiti hizi yameendelea kutumika katika kuwezesha sekta za kiuchumi na kijamii kuwa himilivu dhidi ya athari za hali mbaya ya hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuchochea maendeleo endelevu.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mazingira ya kufanyia kazi na kujenga uwezo kwa watumishi, Serikali kupitia TMA imeendelea na ujenzi wa jengo la Kanda ya Mashariki na Kituo cha Kufuatilia Matukio ya Tsunami ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 61. Vilevile, watumishi 96 wanaendelea na mafunzo ndani na nje ya nchi, ambapo kati ya watumishi hao, saba (7) ngazi ya shahada ya uzamivu, 47 ngazi ya shahada ya uzamili, 28 ngazi ya shahada na 14 ngazi ya stashahada.

B.1.2. UTOAJI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI HUDUMA ZA BANDARI

67. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeendelea kusimamia Bandari za Mwambao wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu kwa kuendeleza miundombinu na utoaji wa huduma za kibandari; kuweka taratibu na kanuni kwa watoa huduma za bandari nchini; kusimamia huduma za bandari, kulinda mazingira na

usalama wa bandari kwa viwango vinavyokubalika; na kuweka mazingira mazuri yatakayowavutia wawekezaji.
Aidha, TPA imeendelea kupanua wigo wa soko la huduma za kibandari kwa kushirikisha na kusimamia Sekta Binafsi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari ili kuongeza ushindani na kuleta tija zaidi.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 TPA ilihudumia tani milioni 23.18 za shehena ikiwa ni ongezeko la asilimia 11.87 ikilinganishwa na tani milioni 20.72 za shehena iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Aidha, kwa upande wa uhudumiaji wa makasha, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, TPA ilihudumia makasha 831,866 sawa na ongezeko la asilimia 3.32 ikilinganishwa na makasha 805,167 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ongezeko hilo la shehena na makasha limetokana na mikakati mbalimbali inayoendelea kutekelezwa ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA inaendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 ambayo katika Ibara ya 59b(i-vi) inasisitiza uboreshaji na uimarishaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za bandari nchini. Katika kutekeleza ibara hiyo, TPA imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa bandari nchini zikiwemo bandari za ukanda wa mwambao wa Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na Bandari Kavu. Aidha, TPA imeendelea na juhudi mbalimbali za kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa na mitambo ya kisasa kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika bandari nchini.

70. ***Mheshimiwa Spika***, kwa upande wa uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, hadi kufikia Machi, 2025 Serikali imeendelea na uboreshaji wa Bandari hiyo ikiwemo uboreshaji wa Gati Na. 8 - 11 na Gati Na. 12 - 15 ambapo Upembuzi Yakinifu wa kuboresha Gati hizo umekamilika. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya kupokelea mafuta pamoja na matanki 15 ya mafuta (tank farms) yenye uwezo wa kuhifadhi kiasi cha mita za ujazo 378,000 umeendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 25.

Halikadhalika, uboreshaji wa Bandari ya Tanga unaendelea ili kuongeza uwezo wa kuhudumia shehena kwenda kanda ya Kaskazini na nchi jirani. Maboresho yaliyofanyika mpaka sasa ni pamoja na kuongeza kina kutoka mita tatu (3) hadi mita 13 na upanuzi wa eneo la kuingia na kutoka bandarini lenye upana wa mita 73 na eneo la kugeuzia meli na kuwa na kipenyo cha mita 800.

71. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TPA imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Gati jipya na *Conveyer belt* katika Bandari ya Kisiwa Mgao ambayo ni maalum kwa ajili ya kuhudumia shehena chafu (dirty cargo) kama vile makaa ya mawe na saruji. Katika kuendelea kutekeleza mradi huu, tayari usanifu wa kina (*detailed engineering design)* umekamilika. Kwa sasa Mkandarasi anaendelea na hatua za maandalizi (mobilization stage) kwa ajili ya kuanza ujenzi. Lengo la mradi huu ni kuiwezesha bandari ya Mtwara iendelee kutoa huduma kwa ufanisi bila kuathiri mazingira. Aidha, Serikali imekamilisha kuhuisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali wa ujenzi wa bandari mpya ya Mbegani iliyopo Bagamoyo. Ujenzi wa Bandari hiyo ya kimkakati utachochea shughuli za viwanda na biashara katika eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone) wa Bagamoyo.

72. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Bandari Kavu ya Kwala umekamilika; ujenzi wa uzio wenye mzunguko wa kilomita 2.9 umekamilika; mtandao wa reli ya MGR wenye urefu wa kilomita 1.3 umekamilika; na ujenzi wa yadi ya sakafu ngumu (pavement) yenye ukubwa wa hekta tano (5) kwa ajili ya kuhifadhi shehena unaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 96.6. Bandari Kavu hii imeanza kutoa huduma kwa kupokea makasha kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwa kutumia njia ya reli na barabara.

73. ***Mheshimiwa Spika***, katika kutekeleza mkakati wa kuboresha biashara baina ya Tanzania na nchi za kikanda na kulifanya eneo la Kwala kuwa la kimkakati zaidi, Serikali ilitoa maeneo kwa ajili ya kuhudumia shehena ya nchi za Rwanda, DRC, Burundi na

Zambia. Aidha, Serikali imetenga maeneo kwa ajili ya nchi za Uganda, Malawi, Sudan Kusini na Zimbabwe. Nchi hizo kwa sasa zimeanza uendelezaji wa maeneo hayo ambapo Burundi imeanza ujenzi wa uzio na DRC inakamilisha Upembuzi Yakinifu. Kwa upande mwingine, nchi yetu inaendelea kupanua ushirikiano wa kidiplomasia katika masuala ya uchukuzi ambapo baadhi ya nchi zinaendelea kushirikiana katika kuimarisha zaidi biashara. Mathalan, mwezi Aprili, 2025 Tanzania imepokea takribani hekta 15 kwa ajili ya kujenga bandari kavu katika eneo la Kasumbalesa nchini DRC.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na uboreshaji wa bandari zilizopo katika Bahari ya Hindi, Serikali pia imeendelea kuongeza wigo wa huduma zake za kibandari kwa kujenga na kuboresha bandari zilizopo katika Maziwa Makuu nchini. Hadi kufikia Machi 2025, Serikali imekamilisha taratibu za kumpata Mkandarasi wa kufanya maboresho ya Bandari ya Kigoma iliyopo katika Ziwa Tanganyika unaohusisha ujenzi wa barabara ya kuingia bandarini na jengo la abiria. Mradi huu wa usanifu na ujenzi unatekelezwa kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Serikali ya Jamhuri ya Watu wa Japan kupitia Shirika la JICA; na Serikali Jamhuri ya Watu wa China. Mkataba wa ujenzi wa mradi huo kati ya TPA na M/s SHIMIZU Corporation umesainiwa mwezi Januari, 2025 na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA imeendelea kuboresha bandari zilizopo katika Ziwa Victoria ambapo uboreshaji wa Bandari ya Bukoba umefikia asilimia 94 na kazi zinazoendelea kufanyika ni pamoja na: ujenzi wa gati ya kuhudumia shehena ya magari (RO-RO), kizuia upepo (wind breaker), ujenzi wa eneo la maegesho ya magari pamoja na ujenzi wa jengo la abiria. Vilevile, uboreshaji wa Bandari ya Kemondo umekamilika na kwa sasa upo katika kipindi cha uangalizi (Defect Liability Period). Pia, uboreshaji wa Bandari ya Mwanza North umefikia asilimia 58 na kwa upande wa uboreshaji wa Bandari ya Mwanza South utaanza baada ya kukamilika kwa baadhi ya miundombinu ya Bandari ya Mwanza North ili kutoathiri shughuli za kibandari. Maboresho haya yatawezesha

kuhudumia meli kubwa kama vile MV. Mwanza inayotarajiwa kutoa huduma katika Ziwa Victoria.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia imeendelea na uboreshaji wa bandari zilizopo katika Ziwa Nyasa ili kuweza kuhudumia wananchi wa maeneo hayo na nchi jirani za Malawi na Msumbiji. Mradi huo unajumuisha uboreshaji wa Bandari ya Mbamba Bay ulioanza tarehe 27 Januari 2024 unaotarajiwa kukamilika tarehe 26 Januari, 2026 ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 26. Uboreshaji wa Bandari hii utachochea ukuaji wa uchumi katika Ushoroba wa Kusini mwa nchi kwa kuunganisha nchi za Malawi na Msumbiji.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza wigo wa huduma za bandari nchini, TPA kupitia ofisi zake zilizo nje ya nchi imeendelea kufanya jitihada kubwa za kimasoko katika kujitangaza na kutafuta fursa zaidi za kibiashara kwa nchi jirani zinazotumia Bandari za Tanzania zikiwemo nchi za Rwanda, Burundi, Uganda, Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Zimbabwe ambapo kutokana na jitihada hizo shehena iliyosafirishwa kwenda nchi jirani imeongezeka hadi kufikia tani milioni 8.24 katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kutoka tani milioni 6.91 katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 19.24. Kupitia mikakati hiyo ya kujitangaza, Serikali ya Tanzania na Serikali ya DRC zimesaini makubaliano ya kuimarisha usafirishaji wa shehena kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwenda DRC kwa kuendeleza miundombinu ya bandari ambapo DRC imeanza ujenzi wa bandari mpya na ya kisasa ya Kalemie ambapo kukamilika kwake kutaimarisha usafirishaji wa shehena kwenda DRC kupitia bandari za Karema na Kigoma katika Ziwa Tanganyika. Aidha, hatua hii itachochea zaidi ufanyaji wa biashara kati ya DRC na Tanzania hususan kupitia Bandari ya Dar es Salaam.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuongeza ufanisi wa bandari, Serikali kupitia TPA imeendelea na ununuzi wa vifaa na mitambo kwa ajili ya kuboresha utoaji wa huduma katika Bandari nchini. Hadi kufikia Machi 2025, TPA imefanikiwa kununua na kupokea vifaa na mitambo 18 sawa na asilimia 50 ya lengo la kununua mitambo na vifaa 36. Aidha, katika kuimarisha

upatikanaji wa umeme, TPA kwa kushirikiana na TANESCO imejenga kituo kidogo cha umeme (*substation*) cha kv33 na *line* ya umeme wa msongo wa kati kutoka kituo cha Ilala hadi Bandari ya Dar es Salaam yenye urefu wa kilomita 5.

79. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utendaji, TPA imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wake ambapo watumishi 2,125 walihudhuria mafunzo kati ya watumishi 2,494 waliopangwa kuhudhuria mafunzo sawa na asilimia 85.20 ya lengo. Kati ya hao, watumishi 1,808 walishiriki mafunzo ya vikundi, watumishi 250 walishiriki mafunzo ya kitaaluma, watumishi watano (5) walishiriki mafunzo ya muda mfupi na watumishi 62 walishiriki mafunzo ya muda mrefu.

Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Uendelezaji na Uendeshaji wa Bandari Nchini

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi wa bandari, Serikali imeendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika uendeshaji wa shughuli za bandari nchini kwa kuingia ubia na Kampuni za DP World na Tanzania East Africa Gateway Terminal Limited (TEAGTL) katika kuendeleza na kuendesha baadhi ya maeneo ya Bandari ya Dar es Salaam. Lengo la kushirikisha Sekta Binafsi ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari nchini ili kuziwezesha zichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi wa Taifa letu na maendeleo ya wananchi kwa ujumla. Wawekezaji hao wamewezesha upatikanaji wa vifaa na mitambo ya kisasa na mifumo ya TEHAMA inayoendelea kuleta ufanisi katika uendeshaji wa shughuli za kibandari.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** maboresho na ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na manufaa mengine, umeleta mafanikio yafuatayo: -

i. Kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za kibandari, ambapo katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2024 hadi kufikia mwezi Februari 2025, mapato yatokanayo na Kodi ya Forodha kutoka Bandarini yanayokusanywa kutokana na shughuli za kibandari yamefikia Shilingi trilioni 8.26 ambalo ni ongezeko la Shilingi trillion 1.18 ikilinganishwa na makusanyo ya jumla

ya Shilingi trilioni 7.08 yaliyokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24.

ii. Kupungua kwa gharama za uendeshaji katika Bandari ya Dar es Salaam, ambapo gharama hizo zimepungua hadi kufikia Shilingi bilioni 685.16 sawa na punguzo la asilimia 30 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 975.01 zilizotumika katika uendeshaji katika kipindi kama hicho kabla ya kushirikishwa kwa waendeshaji binafsi katika bandari hiyo;

iii. Kupungua kwa muda wa kusubiri meli nangani kutoka wastani wa siku 46 hadi wastani wa siku saba (7) kwa meli za mizigo mchanganyiko (General cargo) na kichele (Bulk cargo);

iv. Kupungua kwa muda wa kuhudumia meli za makasha gatini kutoka wastani wa siku 10 hadi siku tatu (3);

v. Kuongezeka kwa wastani wa shehena ya makasha inayohudumiwa kwa mwezi kutoka makasha (TEUs) 17,000 hadi makasha (TEUs) 25,000 ambalo ni ongezeko la asilimia 47; na

vi. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato yasiyo ya kikodi yanayokusanywa na taasisi mbalimbali za umma zinazotoa huduma bandarini.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa ujumla hatua hii ya ushirikishwaji wa Sekta Binafsi katika kuendeleza na kuendesha bandari nchini, pamoja na kuleta faida za moja kwa moja kama zilivyoainishwa hapo, pia imechochea shughuli nyingine za kiuchumi katika sekta mbalimbali na katika maeneo mengi kutokana na kuimarika kwa utoaji huduma na hivyo kuleta ufanisi stahiki. Aidha, hatua hii imeendelea kuiwezesha bandari ya Dar es Salaam kuwa lango la kibiashara kikanda na kimataifa. Vilevile, ushirikishwaji huu umechangia kufikiwa mapema kwa lengo la Mpango Kabambe wa TPA wa miaka 20 (2021/22 – 2044/45) ulioweka shabaha ya bandari zote nchini kuhudumia tani milioni 30 za shehena ifikapo mwaka 2029/30. Hata hivyo, matokeo ya uendeshaji wa bandari hadi kufikia mwezi Machi, 2025 tayari ufanisi wa uhudumiaji wa shehena wa bandari zote nchini umefikia tani milioni 27.55 na matarajio ya Serikali hadi kufikia mwisho wa mwaka wa fedha wa 2024/25, ni kuwa na lengo la tani milioni 30 litafikiwa.

HUDUMA ZA USAFIRI WA RELI Shirika la Reli Tanzania (TRC)

83. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuchagiza ukuaji wa uchumi, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) imeendelea kuboresha huduma ya uchukuzi kwa njia ya reli kwa kusimamia na kuendeleza miundombinu ya reli nchini kwa reli iliyopo ya *Meter Gauge Railway* (MGR) yenye urefu wa kilomita 2,707; kujenga reli mpya ya kiwango cha *Standard Gauge Railway* (SGR); na kutoa huduma ya usafirishaji wa abiria na mizigo. Aidha, ujenzi wa reli ya SGR unatekelezwa kwa awamu ambapo awamu ya kwanza ina jumla ya kilomita 1,219 na awamu ya pili kilomita 1,590 za njia kuu na hivyo kufanya reli hiyo kuwa na mtandao wa jumla ya kilomita 2,809 ambazo ni zaidi ya kilomita 102 ikilinganishwa na reli ya MGR iliyojengwa kabla ya kupata uhuru. Pamoja na hatua hiyo, Serikali itaendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa maeneo mengine yakiwemo ushoroba wa Kusini na Kaskazini kwa kadri ya upatikanaji wa rasilimali fedha.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TRC imeendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo na abiria kupitia reli ya MGR ambapo hadi kufikia Machi 2025, tani 183,048 za mizigo zimesafirishwa ikilinganishwa na tani 240,439 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/24 sawa na upungufu wa tani 57,391. Kwa upande wa utoaji wa huduma ya usafiri wa reli ya mjini kutoka Stesheni ya Kamata kwenda Ubungo na Pugu, TRC imesafirisha jumla ya abiria 1,963,734 sawa na upungufu wa abiria 272,689 ikilinganishwa na abiria 2,236,423 waliosafirishwa kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/24. Upungufu huo umesababishwa na uchache wa vitendea kazi uliotokana na kuchelewa kuwasili kwa vipuri kutoka nje ya nchi vinavyohitajika kwa ajili ya ukarabati wa vitendea kazi pamoja na ubovu wa njia ambao unapelekea ajali za treni mara kwa mara.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa abiria wa masafa marefu, hadi kufikia Machi, 2025, abiria 374,997 walisafirishwa sawa na ongezeko la abiria 54,483 ikilinganishwa na abiria 320,514 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/24. Ongezeko hilo limetokana na uboreshaji wa huduma.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kurahisisha usafiri kwa wananchi sambamba na utekelezaji wa maagizo ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akihutubia Taifa mwezi Desemba, 2023 alielekeza kuanza uendeshaji wa treni katika reli ya SGR kipande cha Dar es Salaam hadi Dodoma. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia TRC ilianza rasmi huduma ya uendeshaji wa treni kupitia reli ya SGR tarehe 14 Juni, 2024 kwa safari kati ya Dar es Salaam na Morogoro na tarehe 25 Julai, 2024 kwa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma. Aidha, huduma hii ya uendeshaji wa treni kupitia reli ya SGR ilizinduliwa rasmi tarehe 01 Agosti, 2024 na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kutokana na mafanikio haya, nimpongeze kwa dhati Mheshimiwa Rais kwa kuonesha uthubutu katika kuendelea kufanya uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya reli.

87. ***Mheshimiwa Spika,*** tangu kuanza kwa safari za treni kupitia reli ya SGR hadi kufikia Machi 2025, TRC imesafirisha jumla ya abiria 2,054,828 na kuwezesha kukusanya mapato ya jumla ya Shilingi bilioni 60.25. Aidha, usafiri kwa kutumia reli ya SGR umepunguza muda wa safari kutoka saa tisa (9) hadi saa tatu (3) kwa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma na hivyo kuwezesha muda uliopunguzwa kutumika katika shughuli zingine za uzalishaji mali na kuongeza tija katika biashara na uchumi kwa ujumla.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa usafirishaji wa mizigo, taratibu za kuanza uendeshaji kwa reli ya SGR zinaendelea na tayari Serikali inatekeleza mikakati ya kuongeza upatikanaji wa mizigo ndani ya nchi kwa kuhamasisha Shoroba za Kiuchumi kandokando na sehemu zinazofikika na huduma za miundombinu ya Usafirishaji (Transport and Logistics Economic Corridors). Usafirishaji wa mizigo kupitia reli ya SGR unatarajiwa kuanza mwezi Juni, 2025 baada ya Serikali kukamilisha taratibu za kuandaa mazingira ya kuwezesha kufanyika kwa shughuli hiyo. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Taasisi ya Ushoroba wa Kati (Central Corridor Transit Transport Facilitation Agency - CCTTFA), Mfuko wa Chakula Duniani (WFP) na Watumiaji wakubwa wa Bandari za Tanzania wa ndani na nje ya nchi ambao wanatarajia kutumia fursa hiyo pindi itakapoanza kutoa huduma.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia inaendelea kuhamasisha Shoroba kubwa tatu (3) ambazo zitachochea upatikanaji wa mizigo ndani ya nchi. Shoroba hizo ni: Ushoroba wa Baridi (Cold Chain) unaohusisha mizigo ya nyama, samaki, matunda, mbogamboga na maua; Ushoroba wa Njano (Yellow Chain) unaohusisha mizigo ya madini; na Ushoroba wa Kichele (General Cargo Chain) unaohusisha mizigo mingine, hususan mizigo mikubwa (bulk cargo) pamoja na mizigo ya viwandani na kilimo ikiwemo pembejeo. Utekelezaji wa mkakati huu umeanza kuzaa matunda ambapo makampuni makubwa na wateja wa muda mrefu wamejitokeza kwa ajili ya majadiliano.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), ambao katika kipengele cha 5.7 Serikali iliahidi kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa reli ya Kati kwa kiwango cha SGR. Halikadhalika, katika Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 Ibara ya 58(e)(ii) na Ibara ya 59(d), Serikali iliahidi kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR. Hivyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali imeendelea kutekeleza mradi wa ujenzi wa reli ya SGR kwa awamu ya kwanza na ya pili ambapo hadi kufikia Machi 2025, ujenzi wa reli ya SGR awamu ya kwanza ya kutoka Dar es Salaam – Mwanza yenye urefu kilomita 1,219 za njia kuu pamoja na ujenzi wa vipande viwili vya awamu ya pili vya Tabora - Kigoma (Km 506) na Uvinza - Musongati yenye urefu wa kilomita 240 za njia kuu (Tanzania Km 156 na Burundi km 84) umeendelea kutekelezwa.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi mwezi Machi 2025, utekelezaji wa kipande cha kwanza cha kutoka Dar es Salaam – Morogoro (km 300) umefikia asilimia 99.72 na kazi zinazoendelea ni ujenzi wa njia kuingia bandarini (port link) umefikia asilimia 91.78 na ujenzi wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme umefikia asilimia 99.98. Aidha, utekelezaji wa kipande cha pili cha kutoka Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 97.98 na kazi zinazoendelea ziko katika hatua mbalimbali za utekelezaji ambazo ni pamoja na ujenzi wa vivuko vya juu umefikia asilimia 88.52; ujenzi wa stesheni umefikia asilimia 98.52; na ujenzi wa uzio umefikia asilimia 95.12.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa kipande cha tatu cha kutoka Makutupora – Tabora (km 368) umefikia asilimia 14.53 na kazi zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa kina ambao umefikia asilimia 54.98; ujenzi wa kambi; na ukataji wa miinuko na ujazaji mabonde pamoja na utwaaji wa ardhi. Halikadhalika, utekelezaji wa kipande cha nne cha kutoka Tabora – Isaka (km 165) umefikia asilimia 6.65 ambapo kazi zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa kina; utafiti wa udongo na miamba; ujenzi wa kambi, machimbo ya kokoto pamoja na utwaaji wa ardhi. Vilevile, utekelezaji wa kipande cha tano cha kutoka Mwanza – Isaka (km 341) umefikia asilimia 63.16 na kazi zinazoendelea ni usanifu wa kina; ujenzi wa tuta; majengo ya stesheni; madaraja na vivuko vya binadamu na wanyama; utandikaji wa reli; ujenzi wa mifumo ya mawasiliano na umeme pamoja na utwaaji wa ardhi.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa lengo la kuhakikisha uchumi wa nchi unakua kwa kufungua masoko ya nje ya nchi, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa reli ya SGR kwa awamu ya pili ambapo ujenzi wa reli ya SGR kutoka Tabora – Kigoma (Km 506) umeanza na utekelezaji wake umefikia asilimia 7.88. Kazi zinazoendelea ni pamoja na utwaaji wa ardhi; ujenzi wa kambi; usanifu pamoja na usafirishaji wa mitambo na vitendea kazi. Aidha, kukamilika kwa ujenzi wa reli hii kutafungua biashara kati ya Tanzania na nchi jirani za ukanda huo zikiwemo Burundi na DRC.

94. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 Ibara ya 30(a) Serikali iliahidi kuendelea kunufaika na fursa zake za kijiografia kwa kubuni na kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati ili nchi iweze kunufaika zaidi na fursa hizo. Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali kupitia TRC imesaini mkataba wa ujenzi wa reli ya SGR kipande cha Uvinza – Musongati (Km 240) mnamo tarehe 29 Januari, 2025. Kusainiwa kwa mkataba huu ni matokeo ya ushirikiano kati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Burundi. Kukamilika kwa reli hii kutaunganisha nchi ya Burundi na Bandari ya Dar es Salaam sambamba na kufungua nchi ya Tanzania kikanda kwa kuwezesha na kurahisisha ufanyaji biashara kati ya nchi hizo.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** dhamira ya Serikali ni kujenga reli ya SGR katika maeneo mbalimbali ya nchi. Katika kutekeleza lengo hili, Serikali inaendelea kutafuta fedha kutoka kwa wadau mbalimbali wa maendeleo ikiwa ni pamoja na wawekezaji kwa utaratibu wa ubia baina ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP). Upatikanaji wa rasilimali fedha utawezesha ujenzi wa reli ya SGR kwa maeneo yaliyobaki yanayojumuisha reli ya SGR ya kutoka Kaliua – Mpanda – Karema (km 321); Isaka – Rusumo – Kigali (km 371); Mtwara – Mbamba Bay na matawi (Spurs) ya Liganga na Mchuchuma (km 1,000); Tanga – Arusha – Musoma (km 1,028); Reli ya Jiji la Dar es Salaam (km 166); na Reli ya Jiji la Dodoma (km 107).

96. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri na usafirishaji, Serikali kupitia TRC imeendelea kufanya ununuzi wa vichwa vya treni, mabehewa na mitambo kwa ajili kutoa huduma ya usafiri kwenye reli ya SGR. Hadi kufikia Machi 2025, Serikali imekamilisha ununuzi wa mabehewa ya abiria 89 ambapo mabehewa 71 kati ya hayo yamewasili nchini na mabehewa 18 yaliyosalia yanatarajiwa kuwasili kwa nyakati tofauti ndani ya mwaka 2025. Aidha, ununuzi wa vichwa vya treni vya umeme 17 umekamilika na tayari vimepokelewa na kuanza kutoa huduma. Pia, ununuzi wa seti 10 za treni ya mchongoko (Electric Multiple Unit – EMU) kwa ajili ya abiria umekamilika ambapo seti zote 10 zimewasili nchini na seti tano (5) zimekamilisha majaribio na kuanza kutoa huduma. Halikadhalika, hatua za utengenezaji wa mabehewa 1,430 ya mizigo zinaendelea na tayari awamu ya kwanza ya mabehewa 264 ya mizigo yamewasili nchini tarehe 11 Desemba, 2024 na hatua za majaribio zimekamilika.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na uendelezaji wa reli ya SGR, reli ya MGR imeendelea kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi nchi jirani. Kutokana na umuhimu wake, Serikali imeendelea kukarabati reli hiyo ya MGR katika maeneo mbalimbali kupitia Mfuko wa Reli, ambapo hadi kufikia Machi, 2025 ukarabati wa njia ya reli ya MGR ya Kaliua - Mpanda (Km 210) unaendelea na umefikia asilimia 24.04. Kazi zinazoendelea ni pamoja na usanifu wa njia na madaraja, ufungaji wa mtambo

wa kuchakata kokoto, ufungaji wa mitambo katika kiwanda cha kutengeneza mataruma ya zege na shughuli za kimazingira.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali kupitia TRC imesaini Mikataba ya ununuzi wa malighafi za matengenezo ikiwemo reli, mataruma na vifungashio kwa ajili ya kukarabati njia ya reli ya Tanga - Arusha na Ruvu - Mruazi junction. Sambamba na hayo, TRC inaendelea kutekeleza mradi wa ukarabati wa miundombinu ya njia ya reli kutoka Dar es Salaam hadi Isaka awamu ya pili (Tanzania Intermodal Rail Project - TIRP II) unaohusisha ukarabati wa njia ya reli, ujenzi wa madaraja, makalavati na ujenzi wa vituo vya kuhudumia mizigo vya Ilala na Isaka ambapo kazi ya usanifu imekamilika na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa njia kwa maeneo korofi katika kipande cha Dar es Salaam - Tabora (Km 257.4) na Tabora - Isaka (Km 135) zinaendelea. Aidha, Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya reli ya MGR kipande cha Tanga - Arusha (Km 626) na kipande cha Kilosa – Gulwe - Igandu zinaendelea. Pia, ukarabati wa Vichwa vya treni na Mabehewa ya reli ya MGR ili kuongeza ufanisi wa reli hiyo umeendelea kutekelezwa ambapo jumla ya mabehewa 350 ya mizigo kati ya mabehewa 600 na mabehewa 33 ya abiria kati ya mabehewa 37 yamekarabatiwa na yameanza kutoa huduma.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** kama Watanzania wanavyoelewa reli ya SGR imeanza kutoa huduma kwa ufanisi kwa takribani mwaka mmoja sasa tangu kuanza kwa huduma hiyo. Pamoja na tunu hii ya Taifa iliyofanikiwa kutokana na maono ya viongozi wetu, kumekuwa na uvamizi na uharibifu wa miundombinu ya reli ikiwemo ya SGR, hususan nyaya za shaba, nyaya za mawasiliano (Optic Fibre cable) na uzio wa usalama. Naomba kupitia Bunge hili Tukufu, kuwasihi Wananchi kuacha tabia ya kijinai ambayo inahujumu uchumi na isiyo na nia njema kwa maendeleo yanayoshamiri katika nchi yetu. Ikumbukwe kuwa, ubadhilifu huu unahatarisha usalama wa abiria na kurudisha nyuma uwekezaji mkubwa uliofanywa kwa kutumia fedha nyingi za Watanzania. Hakika hakuna mtu yeyote atakayepona kwa kubainika anafanya uharibifu kwa nchi yetu na Serikali tayari inaendelea kuwachukulia hatua kali wale wote wanaopatikana na makosa hayo na kamwe haitawaonea huruma. Zoezi hili la kupambana

na wahalifu hao linaendelea kufanyika kwa kutumia vyombo vyote vya Dola ili kuhakikisha inakomesha tabia hii. Kupitia Bunge hili, naomba kutoa rai kwa yoyote atakayeshiriki uharibifu wa miundombinu ya reli nchini atachukuliwa kama mhujumu uchumi.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** maendeleo ya reli nchini yameendelea kushika kasi kutokana na ongezeko la mahitaji ya usafiri na usafirishaji na hivyo kupelekea usafiri wa reli kuhitajika zaidi katika maeneo yote ya Tanzania ikiwemo mikoa ya Kaskazini. Serikali inaendelea kuyafanyia kazi mahitaji haya kwa kuchukua mikakati mbalimbali. Pamoja na mikakati mingine, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, sambamba na Ujenzi wa reli ya SGR na maboresho ya reli ya MGR na matawi yake yanayoendelea kufanyika, Serikali kupitia TRC inaendelea na mikakati mahsusi ya uanzishaji na uboreshaji wa huduma za reli ya Kaskazini inayounganisha Bandari ya Tanga na mikoa ya Kilimanjaro na Arusha na baadaye mikoa ya Shinyanga, Simiyu hadi Mara. Mikakati ya uboreshaji wa reli hii ni ya muda mfupi, kati na mrefu.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mkakati wa muda mfupi, Serikali imeendelea kuhakikisha matengenezo ya reli katika maeneo korofi yanafanyika kwa wakati ili kuepuka kufunga njia. Kwa upande wa utekelezaji wa mkakati wa muda wa kati, tayari mikataba ya ununuzi wa vipuri na vifaa vya matengenezo imesainiwa na malipo ya awali yamefanyika. Kazi hii inatarajiwa kuchukua miaka miwili ambapo itahusisha kuondoa reli chakavu na nyepesi kwa kuweka reli nzito za ratili 80 kwa yadi na kuboresha madaraja kwa kuyaongezea uwezo kutoka tani 13.5 kwa ekseli hadi tani 18.5. Sambamba na mikakati hiyo, mkakati wa muda mrefu unahusisha kuunganisha mikoa hiyo na reli ya kisasa ya SGR kadri ya mahitaji na upatikanaji wa fedha. Hata hivyo, katika hatua za awali, Serikali imekamilisha upembuzi wa awali wa ujenzi wa mtandao wa reli ya SGR yenye urefu wa kilomita 1,028 inayounganisha Bandari ya Tanga na Musoma ili kuyafikia maeneo yenye uzalishaji ikiwemo migodi ya Nikeli katika eneo la Dutwa, *Phosphate* katika eneo la Minjingu na Magadi soda katika eneo la Engaruka. Vilevile, Serikali kupitia TRC imeanza taratibu za manunuzi ya Mkandarasi wa kufanya

Upembuzi Yakinifu ili kuiunganisha Bandari ya Tanga na reli ya kati kwa kiwango cha SGR kwa ajili ya kuiongezea ufanisi wa kuhudumia mizigo kwa haraka kupitia reli ya kati.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** kazi nyingine zinazoendelea kutekelezwa na TRC ni pamoja na:-

i. Kuboresha mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme katika njia ya reli ya MGR ambapo ununuzi wa vipuri kwa ajili ya maboresho ya mfumo wa mawasiliano katika njia ya reli ya MGR umekamilika. Halikadhalika, ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuboresha upatikanaji wa umeme kwenye stesheni za MGR unaendelea;
ii. Kuunda vichwa vya treni tisa (9) kwa ajili ya kuongeza vitendea kazi na kukarabati vichwa vya njia kuu (2) aina ya 88U na vichwa vya sogeza (7) aina ya 64XX. Kazi ya uundwaji na ukarabati wa vichwa hivyo vya treni imekamilika na vimeanza kutoa huduma katika njia ya reli ya MGR;
iii. Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli yenye urefu wa kilomita 6.2 na daraja katika eneo la Godegode – Gulwe katika njia ya MGR. Hadi kufikia Machi, 2025 kazi hiyo imefikia asilimia 72; na
iv. Kuboresha mifumo ya TEHAMA ikiwemo ufungaji wa kamera za CCTV kwa ajili ya ulinzi na usalama katika maeneo ya stesheni na mfumo wa kieletroniki wa ukataji tiketi (eticketing).

Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)

103. ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) inamilikiwa na Serikali za Tanzania na Zambia kwa hisa za asilimia 50 kwa 50. Katika kuendeleza huduma za reli kati ya nchi hizo mbili (2), TAZARA imeendelea kutekeleza jukumu lake la msingi la kutoa huduma za kusafirisha abiria na mizigo kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, TAZARA inalinda na kuimarisha miundombinu ya reli yenye urefu wa jumla ya kilomita 2,153 ambapo, kilomita 1,860 ni za njia kuu, kilomita 293 ni njia za reli zilizoko stesheni na zile za michepuko, pamoja na maeneo yote yaliyo ndani ya hifadhi ya reli (mita 50 pande zote kutoka katikati ya reli).

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, TAZARA imesafirisha tani 71,670 za mizigo ikilinganishwa na tani 115,182 za mzigo zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho 2023/24 sawa na upungufu wa asilimia 37.77. Aidha, kampuni binafsi zimesafirisha mizigo tani 91,471 ikilinganishwa na mizigo tani 136,082 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2023/24 sawa na upungufu wa asilimia 32.78 hivyo kufanya mizigo iliyosafirishwa katika reli ya TAZARA katika kipindi cha Julai 2024 hadi Machi 2025 kufikia jumla ya tani 163,141 ikilinganishwa na tani 251,264 za mzigo zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24 sawa na upungufu wa asilimia 35.07.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu abiria, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, treni za abiria zinazofanya safari kati ya Dar es Salaam, Tanzania na New Kapiri Mposhi, Zambia, zilisafirisha jumla ya abiria 454,312 sawa na upungufu wa asilimia 12.25 ikilinganishwa na abiria 517,752 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Aidha, abiria waliosafirishwa kwa treni ya Udzungwa inayofanya safari kati ya stesheni za Kidatu na Makambako walikuwa abiria 179,303 sawa na upungufu wa asilimia 21.99 ikilinganishwa na abiria 229,873 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2023/24. Pia, treni inayofanya safari jijini Dar es Salaam ilisafirisha abiria 1,083,976 sawa na upungufu wa asilimia 31.52 ikilinganishwa na abiria 1,582,833 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2023/24.

106. ***Mheshimiwa Spika***, kushuka kwa utendaji wa TAZARA kumetokana na uhaba wa vitendea kazi, ikiwemo vichwa vya treni, mabehewa pamoja na uchakavu na uharibifu wa miundombinu ya reli. Aidha, mnamo Mwezi Aprili 2024, miundombinu ya reli ya TAZARA iliharibiwa na janga la mvua za ***El Nino*** katika baadhi ya maeneo kati ya Mlimba na Uchindile na kupelekea kufungwa kwa njia kwa takribani miezi miwili (2). Hali hii ilisababisha Waendeshaji Binafsi na TAZARA kusimamisha huduma na kusababisha baadhi ya wateja waliokuwa na makubaliano ya kusafirisha mizigo kwa njia ya TAZARA kuondoka na kwenda kuingia makubaliano na wasafirishaji wengine. Hali hii

imeleta changamoto katika kuwarejesha baada ya njia kufunguliwa.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka mitano (5) sehemu ya 5.2.3 na Ilani ya Chama cha Mapinduzi Ibara ya 59(f), Serikali iliahidi kuendelea kukarabati miundombinu ya reli na kufanya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya kuboresha huduma zinazotolewa na Mamlaka ya Reli ya TAZARA. Hadi kufikia Machi 2025, pamoja na mikakati mingine, Serikali imekamilisha malipo ya ununuzi wa mashine moja (1) ya kushindilia kokoto na kunyoosha reli (Tamping Machine) ambayo tayari imewasili nchini tarehe 31 Machi, 2025.

108. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na hatua za utekelezaji zinazoendelea ndani ya TAZARA, kwa muda mrefu utendaji wake umekuwa wa kusuasua na umeendelea kudorora kila mwaka. Mathalan, uwezo wa TAZARA kutoa huduma umekuwa ukipungua mwaka hadi mwaka tangu kuanzishwa kwake kutoka tani 1,228,000 za mwaka 1986/87 hadi tani 128,928 katika mwaka 2023/24. Kutokana na hali hii, nchi wanahisa (Tanzania na Zambia) zimeamua kuchukua hatua za makusudi za kuiboresha TAZARA. Katika kuendelea na utekelezaji wa mkakati huo, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita kumesainiwa Hati ya Makubaliano (MoU) ya kuboresha uendeshaji wa TAZARA**.** Makubaliano hayo yalifanyika tarehe 4 Septemba, 2024 Jijini Beijing - China, mbele ya Marais wa nchi zote tatu (Tanzania, Zambia na China). Mkakati huu pamoja na mambo mengine, umelenga kumpata mwekezaji mahiri ambaye atawekeza katika kuiendeleza na kuiendesha TAZARA kwa kuzingatia maslahi mapana ya nchi yetu. Kwa sasa nchi wanahisa zipo katika hatua za mwisho za kukamilisha taratibu za kusaini mkataba na mwekezaji ili kuanza utekelezaji. Ni matumaini yetu kuwa kupitia mkakati huu, TAZARA sasa itapata suluhu ya kudumu na mwelekeo mpya wa uendeshaji. Pamoja na manufaa mengine, mkakati huu utaimarisha usafirishaji wa shehena inayosafirishwa kupitia Bandari ya Dar es Salaam kwenda na kutoka nchi jirani zikiwemo nchi ya Zambia na DRC.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu naomba kutaarifu kuwa hatua hii ya kusainiwa kwa MoU ni ya kihistoria na ya kujivunia katika Taifa letu na Serikali ya Awamu ya Sita. Hii ni

kutokana na ukweli kuwa majadiliano haya yalianza muda mrefu (mwaka 2006) ambapo hadi sasa ni takriban miaka 19. Ni wazi kuwa majadiliano haya yatakamilishwa katika kipindi hiki cha Uongozi wa Serikali ya sasa inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Maboresho yatakayotekelezwa yatazingatia teknolojia ya kisasa na yatajumuisha: ukarabati na uboreshaji wa njia za reli; ununuzi wa mabehewa mapya ya mizigo; ununuzi wa vichwa vya treni vya kisasa; na ufungaji wa mifumo ya uendeshaji inayoendana na mahitaji ya sasa. Kupitia makubaliano haya, TAZARA itakuwa na ufanisi zaidi na itaendana na mikakati mingine inayochukuliwa na Serikali ukiwemo mkakati wa maboresho ya bandari nchini na ujenzi mkubwa wa miundombinu ikiwemo Reli ya SGR unaofanyika nchini kwa sasa.

HUDUMA KATIKA MAZIWA MAKUU

110. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) iliyokuwa
Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) inayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, imeendelea kutoa huduma za usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa ndani na nje ya nchi zikiwemo nchi jirani za Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, DRC, Zambia, na Malawi.

111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 TASHICO ilisafirisha abiria 210,588 ikilinganishwa na abiria 198,080 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 6.31. Kwa upande wa mizigo, TASHICO ilisafirisha tani 58,605.78 ikilinganishwa na tani 33,288.44 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 76.05. Ongezeko hili limetokana na kukamilika kwa ukarabati na kuanza kazi kwa meli ya MV. Umoja ambayo ilianza kutoa huduma mwezi Oktoba, 2023.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za usafiri katika Maziwa Makuu, Serikali kupitia Mpango wa Taifa wa Maendeleo (FYDP III) ukurasa wa 203 kipengele cha 20 na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka

2020 katika Ibara ya 59(c) iliahidi kuboresha huduma za usafiri katika Maziwa Makuu kwa kujenga na kukarabati meli. Serikali kupitia TASHICO imeendelea kukarabati meli zilizopo katika Ziwa Victoria na Tanganyika na kukamilisha taratibu za kuanza ujenzi wa meli mpya ili kuimarisha usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa meli ya MV. Mwanza itakayotoa huduma katika Ziwa Victoria, hadi kufikia Machi, 2025 umefikia asilimia 96 na tayari meli hiyo imefanyiwa majaribio ya mifumo na mitambo, kwa sasa Mkandarasi anaendelea na ufungaji wa samani za ndani ya meli zikihusisha viti na meza. Kwa upande wa ukarabati wa meli inayotoa huduma za uokozi katika Ziwa Victoria (MV. Ukerewe) ulioanza kutekelezwa tarehe 02 Oktoba, 2024 umefikia asilimia 17. Ukarabati wa meli hii unatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2025 kulingana na mkataba. Vilevile, ukarabati wa meli ya MT. Nyangumi yenye uwezo wa kusafirisha shehena ya mafuta lita 410,000 katika Ziwa Victoria upo katika hatua za maandalizi ikiwa ni pamoja na kufanya malipo ya awali kwa Mkandarasi. Meli hii inatarajiwa kuongeza ufanisi wa kuhudumia nchi jirani za Uganda na Sudan Kusini kwa kusafirisha shehena ya mafuta kupitia Ziwa Victoria.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** uboreshaji wa huduma za usafiri na usafirishaji katika Ziwa Tanganyika umeendelea ambapo ukarabati wa meli ya MT. Sangara umefikia asilimia 98. Meli hii ipo katika hatua za mwisho za kukamilika kwake na inategemewa kurahisisha usafirishaji wa mafuta kwenda maeneo mbalimbali zikiwemo nchi za DRC na Burundi. Pia, Serikali inaendelea na ukarabati wa meli ya MV. Liemba katika Ziwa Tanganyika yenye uwezo wa kusafirisha abiria 600 na tani 200 za mizigo kwa wakati mmoja ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 15 na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2026 kwa mujibu wa mkataba. Halikadhalika, Serikali imekamilisha tathmini ya hali ya msawazo (stability) wa meli ya MV. Mwongozo. Tathmini ilipendekeza meli hiyo ikabaratiwe ili iendelee kutoa huduma katika Ziwa Tanganyika ambapo Mkandarasi kwa ajili ya ukarabati wa meli hiyo amepatikana na mkataba umesainiwa.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu unakuwa salama na wa uhakika kwa kuendelea na ujenzi wa meli mpya. Ili kufanikisha azma hiyo, Serikali inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli katika Ziwa hilo chenye uwezo wa kubeba meli yenye uzito wa tani 5,000 na ujenzi wa meli ya kusafirisha mizigo yenye uwezo wa kusafirisha tani 3,500 ambapo utekelezaji wake upo katika hatua za maandalizi baada ya Serikali kufanya malipo ya awali. Ujenzi wa kiwanda hiki na meli mpya katika Ziwa Tanganyika utachochea biashara ya ujenzi wa meli na kuongeza fursa za ajira kwa Watanzania.

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi wa kulihudumia soko la kusafirisha mizigo kwenda nchi jirani za Uganda na Sudan Kusini kutokana na tija itakayotokana na reli ya SGR, Serikali inaendelea na ujenzi wa meli mpya ya kubeba tani 3,000 za mizigo katika Ziwa Victoria ambapo kwa mujibu wa mkataba, ujenzi huo utatekelezwa kwa muda wa miaka miwili (2) na utekelezaji wake upo katika hatua za maandalizi ikiwa ni pamoja na kufanya malipo ya awali kwa Mkandarasi.

HUDUMA ZA VIWANJA VYA NDEGE

117. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) imeendelea kusimamia, kuendesha na kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Serikali 61 Tanzania bara kwa kuzingatia Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania Na.08 ya Mwaka 2024 na Miongozo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa inayohusiana na Usafiri wa Anga. Pamoja na majukumu mengine, TAA inalo jukumu la kutoa huduma bora zenye ufanisi na salama, na vifaa wezeshi kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege inavyovisimamia; na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na umma kuhusu masuala ya kitaifa na kimataifa yanayohusu uanzishwaji, uendelezaji, usimamizi, uendeshaji na utunzaji wa viwanja vya ndege.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha viwanja vyetu vya ndege vinaendelea kuwa salama wakati wote, TAA imeratibu na kuandaa mazoezi ya kupima utayari wa kukabiliana na majanga viwanjani. Hatua hii ni kwa mujibu wa Sheria ya Viwanja vya Ndege Tanzania, ambapo kwa kipindi cha kuanzia Julai, 2024

hadi Machi, 2025 imefanya mazoezi ya kujipima na dharura ya uokozi (Emergency Drills) katika viwanja vya ndege vya Julius Nyerere (JNIA), Dodoma, Songwe na Geita. Pia, leseni za uendeshaji kwa viwanja vya ndege vya Same, Chunya, Ifakara, Biharamulo, Ngara na Njombe zimehuishwa ili kuhakikisha viwanja hivyo vinakidhi viwango vya kitaifa vya uendeshaji.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kuwa na viwanja vya ndege vyenye miundombinu bora, Serikali imeendelea kuboresha na kukarabati viwanja vya ndege nchini. Hadi kufikia Machi, 2025, uboreshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha umeendelea kwa mafanikio makubwa ya utoaji wa huduma kwa abiria ambapo ujenzi wa jengo jipya la abiria pamoja na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA umekamilika. Aidha, kazi ya ufungaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege (AGL) utakaowezesha kiwanja hiki kutoa huduma kwa masaa 24 inaendelea.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hatua hizo, kazi ya ukamilishaji wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege Mwanza imefikia asilimia 13; kazi ya ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi imefikia asilimia 69; na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Awali wa kiwanja kipya cha Ndege cha Njombe umekamilika na taratibu za utwaaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi zinaendelea. Vilevile, wakandarasi wa mradi wa ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi na mradi wa ujenzi wa jengo la abiria, jengo la mnara wa kuongozea ndege, kituo cha hali ya hewa na kituo cha zimamoto katika Kiwanja cha Ndege cha Mtwara wamekabidhiwa maeneo ya mradi na taratibu za malipo ya awali zinaendelea.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha TAA inaendana na kasi ya ukuaji wa shughuli za usafiri wa anga nchini unaosababisha mahitaji ya upanuzi na ujenzi wa viwanja vipya, Serikali imeendelea na juhudi za utwaaji, upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki katika viwanja vya ndege mbalimbali. Hadi kufikia Machi 2025, Serikali imeanza kulipa fidia kwa awamu kwa wananchi wa Kipunguni waliopisha upanuzi wa Kiwanja cha JNIA ambapo hadi kufikia Machi, 2025 Shilingi bilioni 20 tayari zimelipwa. Pia, TAA kwa kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali

imefanikiwa kupata Hati Miliki za Viwanja vya Ndege vya Msalato, Mafia, Liuli, Mbamba Bay, Kondoa na Kongwa na hivyo kupelekea kuwa na jumla ya Hati Miliki 36. Aidha, zoezi la upimaji wa Viwanja vya Ndege vya Dodoma, Manyoni, Ngara na Masasi liko katika hatua za mwisho za ukamilishwaji.

122. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kunakuwa na usalama wa ndege zinazotumia Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, Serikali imeona umuhimu wa kujenga mnara wa kuongozea ndege katika Kiwanja hicho ambapo maandalizi ya awali yanaendelea. Aidha, Serikali inaendelea na mpango wa kudumu wa kutatua changamoto za usalama katika usafiri wa anga katika Mkoa wa Kagera. Katika utekelezaji wa Mpango huo, Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi iliunda Timu ya Wataalam kutoka Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA), Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera na Ofisi ya Kamishna Msaidizi wa Ardhi wa Mkoa wa Kagera kwa ajili ya kufanya Tathimini ya Kina. Timu ya Watalaam ilifanya tathmini hiyo mwezi Januari, 2025 na kupendekeza eneo jipya litakalofaa kwa ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Daraja la 4C ambacho kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege zinazobeba abiria hadi 220 kwa wakati mmoja. Pendekezo hilo lilionesha eneo la Kyabajwa lililopo Wilaya ya Misenyi kufaa zaidi kwa ajili ya ujenzi wa Kiwanja kipya na kuridhiwa. Kwa sasa taratibu za utwaaji ardhi zinaendelea.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na jitihada za kuboresha huduma na kuongeza mapato, Serikali kupitia TAA imeendelea kuboresha na kuimarisha mifumo ya maegesho ya magari (Car Parking System) katika Viwanja vya Ndege vya JNIA, KIA, Songwe, Mwanza, Bukoba, Tabora, Dodoma na Mtwara. Aidha, kwa upande wa mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege (AMIS), Serikali kupitia TAA tayari imefunga mifumo hiyo kwenye viwanja vya JNIA, KIA, Arusha, Bukoba, Dodoma na Songwe. Taratibu za kufunga mifumo hiyo katika viwanja vya ndege vya Mwanza, Iringa, Tabora na Mtwara zinaendelea. Mifumo hiyo husaidia katika kutoa taarifa za miruko, mituo ya ndege na taarifa za abiria na mizigo.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na kasi ya ukuaji wa sekta ya anga na uimarishaji wa utoaji huduma katika Viwanja vya Ndege, TAA imeendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya mara kwa mara ndani na nje ya nchi kwa watumishi wake. Katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, jumla ya watumishi 893 kati ya watumishi 1,516 sawa na asilimia 58.91 ya watumishi walio katika mpango wa mafunzo kutoka katika kada mbalimbali ikiwemo zimamoto na uokoaji, uendeshaji, uhandisi, ulinzi na usalama waliweza kupatiwa mafunzo ya kuwajengea uwezo ili kuongeza tija katika utoaji wa huduma katika viwanja vya ndege nchini.

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TAA imeratibu Mkutano mkubwa wa kikanda wa Baraza la Viwanja vya Ndege Afrika (ACI Africa) uliofanyika tarehe 24 – 30 Aprili, 2025 Jijini Arusha na kuwakutanisha wabobezi na wataalam wa masuala ya usafiri wa anga wapatao 350 kutoka nchi 54 za Bara la Afrika. Mkutano huo umeliletea heshima Taifa letu na kutoa fursa kwa wageni kutambua na kujifunza juu ya mafanikio ambayo nchi yetu imeyafikia kwa upande wa sekta za usafiri wa anga. Aidha, mkutano huo umekuwa moja ya mikakati ya kuendelea kuitangaza Tanzania kimataifa na hivyo kuendelea kuchochea utalii nchini.

HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) inatekeleza Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), ambapo moja ya kipaumbele ni ufufuaji wa ATCL. Katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali imeendelea kufufua ATCL kwa kununua ndege, kuboresha karakana za matengenezo ya ndege, kuboresha mazingira ya kazi na kutekeleza mikakati ya kuongeza ubora na usalama katika utendaji ili kuiwezesha ATCL kuendelea kutoa huduma ya usafiri wa abiria na usafirishaji wa mizigo kwa ufanisi zaidi.

127. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika Mwaka wa Fedha 2024/25 imekamilisha ununuzi wa ndege aina ya Boeing 787-8 Dreamliner. Ununuzi wa ndege hii umeisaidia ATCL kuongeza miruko katika safari za kwenda nchi za China na India. Ndege hii iliwasili nchini

tarehe 20 Agosti, 2024 na kufanya ATCL kuwa na jumla ya ndege 16 zikijumuisha ndege nne (4) za masafa marefu ambazo ni: tatu (3) za abiria aina ya Boeing 787-8 na moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767-300F; ndege sita (6) za masafa ya kati zikijumuisha nne (4) aina ya Airbus A220 – 300, mbili (2) aina ya Boeing 737 Max 9; na ndege sita (6) za masafa mafupi zikiwemo tano (5) aina ya Dash 8 Q400 na moja (1) aina ya Dash 8 Q300.

128. ***Mheshimiwa Spika,*** uwepo wa ndege 16 umeendelea kuiwezesha ATCL kupanua mtandao wa safari kwa kurejesha safari katika kituo cha Johannesburg nchini Afrika Kusini mwezi Novemba 2024, kituo cha Mtwara na kituo cha Iringa mwezi Februari, 2025 na kuifanya ATCL kuwa na vituo 27 vinavyotoa huduma. Kati ya vituo hivyo: vituo 15 ni vya ndani ya nchi ambavyo ni Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Dodoma, Mtwara, Iringa, Kilimanjaro, Kigoma, Mbeya, Geita, Mpanda, Mwanza, Songea, Tabora na Zanzibar; Vituo tisa (9) ni vya kikanda ambavyo ni Bujumbura, Entebbe, Hahaya, Harare, Lusaka, Ndola, Nairobi, Lubumbashi na Johanesburg; na Vituo vitatu (3) ni vya kimataifa ambavyo ni Dubai, Guangzhou na Mumbai.

129. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, ATCL imesafirisha abiria 876,357 sawa na ongezeko la abiria 25,697 ikilinganishwa na abiria 850,660 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Pia, ATCL ilisafirisha tani 5,869.81 za mizigo sawa na ongezeko la tani 835.61 ikilinganishwa na tani 5,034.2 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

130. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali pia, imeendelea kuiboresha ATCL kwa kuiwezesha kuimarisha miundombinu wezeshi ikijumuisha uboreshaji wa karakana za matengenezo ya ndege zilizoko Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA) na Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA). Maboresho hayo yameiwezesha ATCL kuendelea kufanya matengenezo madogo na makubwa ya ndege, kwa kuzingatia miongozo ya matengenezo ya ndege kutoka katika mamlaka husika za ndani na nje ya nchi.

131. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na mikakati hiyo inayoendelea kuboresha utendaji wa ATCL, Kampuni hiyo imeendelea kuwa na mchango katika kuchangia pato la Taifa na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni nchini zinazotokana na utoaji wa huduma zake. Mathalan, katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya Dola za Marekani milioni 104.53 zimepatikana ikilinganishwa na Dola za Marekani milioni 60.07 zilizokusanywa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2023/24, sawa na ongezeko la asilimia 74.01. Sambamba na fedha hizo za kigeni, pia ATCL imeendelea kuchangia katika pato la Taifa ambapo jumla ya Shilingi bilioni 36.06 ikiwa ni Kodi, Ada na Tozo za Kisheria zimekusanywa na Serikali katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Kwa ujumla, ATCL itaendelea kuongeza fedha za kigeni kadri inavyoongeza vituo vya nje ya nchi ambapo pamoja na vituo ilivyokuwa inafanya safari, mwezi Aprili mwaka huu wa 2025 imeanzisha safari katika kituo cha Kinshasa. Aidha, kabla ya mwisho wa mwaka 2025, ATCL itaanzisha safari katika kituo cha Lagos Nigeria. Kuanzishwa kwa safari hizi kutafungua fursa zaidi kati ya Tanzania na Nchi za Afrika Magharibi.

132. ***Mheshimiwa Spika,*** ATCL kwa upande mwingine, imeendelea kuboresha miundombinu na mazingira ya kufanyia kazi kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika utendaji wake. Katika kipindi cha mwaka 2024/25, Kampuni hiyo imeendelea na ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 79 hadi kufikia Machi 2025, ikilinganishwa na hatua ya asilimia 47 iliyokuwa imefikiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kituo cha KIA ni kituo muhimu kwa ajili ya utalii hivyo, ATCL inatarajia kufanya kituo hicho kuwa kitovu kidogo (sub hub). Aidha, ukarabati wa sakafu ya tatu katika Jengo la Ofisi za ATCL Makao Makuu umefikia asilimia 89.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Serikali kupitia ATCL imeendelea kuongeza ajira kwa Watanzania ili kuhakikisha inakidhi matakwa ya uendeshaji wa biashara ya usafiri wa anga ambapo, hadi kufikia Machi 2025, ATCL ilikuwa na watumishi 857 ikilinganishwa na watumishi 792 waliokuwepo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2023/24. Idadi hii inajumuisha marubani 117, wahandisi na mafundi wa ndege 190 na watumishi wengine 550. Pia, ATCL imefanikiwa kuendeleza rasilimaliwatu

hususan wa kada adimu za urubani na uhandisi ndege, kwa kuwapatia mafunzo muhimu ambapo katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi 2025, watumishi 316 walipatiwa mafunzo.

HUDUMA ZA USAFIRISHAJI MAJINI

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Tanzania imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China katika kuboresha huduma za uchukuzi katika Bahari. Mkakati huo umeendelea kutekelezwa na Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) ambayo inamilikiwa kwa uwiano wa asilimia 50:50 kati ya nchi hizo mbili. Aidha, kampuni hii inamiliki meli moja ya mizigo yenye uwezo wa kubeba jumla ya tani 57,000 kwa wakati mmoja. Kwa sasa meli hiyo inaendelea kutoa huduma katika nchi mbalimbali duniani chini ya usimamizi wa SINOTASHIP.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Januari, 2024 hadi Desemba, 2024 SINOTASHIP ilisafirisha jumla ya tani 615,375 ya mizigo sawa na upungufu wa asilimia 0.73 ikilinganishwa na tani 619,870 zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho katika mwaka 2023. Upungufu huo wa tani za mizigo zilizohudumiwa ni kutokana na mwenendo wa biashara. Pia, SINOTASHIP iliendelea na biashara ya uwakala ambapo katika kipindi cha Januari, 2024 hadi Desemba, 2024 ilihudumia meli na kuwezesha kuhudumia makasha 81,993 sawa na ongezeko la asilimia 11.41 ikilinganishwa na makasha 73,599 yaliyohudumiwa mwaka 2023. Ongezeko hili linatokana na kutanuka kwa biashara ya uwakala na uwepo wa ongezeko la meli zinazoleta na kuondosha mizigo katika bandari za Dar es Salaam na Mtwara.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Tanzania imeendelea kuimarisha ushirikiano na Serikali ya China kupitia Kampuni ya Meli ya China na Tanzania (SINOTASHIP) ambapo kampuni hiyo imeendelea kusafirisha mizigo ya masafa marefu nje ya nchi kwa kutumia meli yake moja pamoja na zile za washirika wake. Katika msimu wa korosho ulioishia Desemba, 2024 jumla ya meli nne (4) za washirika wa Kampuni ya SINOTASHIP zilitia nanga katika bandari ya Mtwara na kubeba zaidi ya tani 29,997.50 za korosho.

B.1.3. UTOAJI MAFUNZO KATIKA VYUO VYA MAFUNZO VYA KISEKTA

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59(i) iliahidi kuboresha na kuvijengea uwezo vyuo vya mafunzo vya kisekta vinavyosimamiwa na Wizara ya Uchukuzi. Kupitia vyuo hivyo, Serikali imeendelea kutoa mafunzo katika nyanja mbalimbali za usafiri na usafirishaji ikiwemo mafunzo ya usafiri wa anga, usafiri ardhini na usafiri majini kwa lengo la kuwa na wataalam toshelevu wa kutoa huduma katika Sekta ya Uchukuzi. Utendaji wa vyuo vya kisekta kwa mwaka wa fedha 2024/25 unajumuisha Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Usafiri wa Anga, Chuo cha Bandari, Chuo cha Hali ya Hewa na Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

138. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) imeendelea kutoa mafunzo, kufanya tafiti, kutoa ushauri wa kitaalam pamoja na kuandaa machapisho kwa lengo la kujenga uwezo wa wataalam katika njia kuu za usafiri na usafirishaji ambazo ni barabara, anga, reli, maji na usafirishaji kwa njia ya bomba.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2024/25, Chuo cha NIT kimeendelea kutoa mafunzo ya kozi ndefu 48 ili kuzalisha wataalam mahiri wa kuendeleza miradi mikubwa ya kitaifa inayotekelezwa na Serikali. Kwa sasa, Chuo kina wanafunzi wa kozi ndefu 17,701 ikilinganishwa na wanafunzi 16,131 kwa mwaka wa masomo 2023/24 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 9.7. Ongezeko hili limetokana na Chuo kuanzisha kozi za kimkakati zinazoendana na miradi mikubwa ya kitaifa inayotekelezwa na Serikali katika sekta ya usafirishaji. Aidha, jumla ya wanafunzi 4,176 walihitimu mafunzo ya kozi za muda mrefu ikilinganishwa na wanafunzi 3,884 waliohitimu katika mwaka wa masomo 2022/23 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 7.51.

140. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka 2024/25, jumla ya washiriki 4,303 walihudhuria mafunzo ya kozi fupi za Menejimenti ya Usafirishaji na Uchukuzi; Ukaguzi wa Magari; na weledi wa madereva ikilinganishwa na washiriki 3,679 waliohudhuria kozi fupi katika kipindi kama hicho katika mwaka

wa masomo 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 17. Ongezeko hili linatokana na utekelezaji wa sheria za uendeshaji wa vyombo vya moto ambapo madereva wanatakiwa wawe wamepata mafunzo wakati wa uhuishwaji wa leseni zao za udereva.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Serikali kupitia Chuo cha NIT kwa kushirikiana na *Ethern Aviation Training Organization* ya Ugiriki imepata ithibati kutoka Wakala wa Usalama wa Anga wa Ulaya (European Aviation Safety Agency - EASA) ya kuwa Kituo cha Mitihani ya Leseni za Kimataifa kwa Wahandisi Matengenezo ya Ndege (EASA part – 66 Aircaft Maintenance License Training) na kuwa Kituo cha Mafunzo ya Uhandisi Matengenezo ya Ndege (EASA Part -147 Maintenance Training Organization). Mafanikio haya ni ya kipekee, ya aina yake kwa nchi yetu na yatawezesha wataalam wetu kuwa na ubora na vigezo stahiki vya ushindani wa soko la ajira kikanda na kimataifa.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha NIT imeendelea kutekeleza mradi wa kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia ambapo ujenzi wa jengo la Kituo cha Rasilimali Mafunzo lenye Maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 450 kwa wakati mmoja, madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,653 na Ofisi za watumishi 190 umefikia asilimia 98; uundwaji wa ndege moja (1) yenye injini mbili (2) kwa ajili ya kufundishia marubani unaendelea kiwandani nchini Marekani na unatarajiwa kukamilika na ndege kuwasili Chuoni mwezi Oktoba 2025. Aidha, Chuo kimekusudia kuongeza ndege mbili (2) zaidi za injini moja (1) kwa ajili ya kutoa mafunzo ya urubani, ambapo taratibu za ununuzi zinaendelea.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha NIT imeendelea na utekelezaji wa mradi wa uanzishwaji wa Kampasi ya NIT Lindi kwa ajili ya kuzalisha nguvukazi mahiri na kujenga uwezo wa kiteknolojia katika sekta ya usafiri majini, mafuta na gesi ambapo taarifa ya Tathmini ya Athari kwa Mazingira na Kijamii (ESIA) imeandaliwa na kuthibitishwa na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Aidha, Upembuzi Yakinifu umefanyika na kuwezesha mradi kusajiliwa kwa Namba 4207 na hatua za maandalizi ya utekelezaji wa mradi zinaendelea.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NIT kinaendelea na utekelezaji wa shughuli za uanzishwaji wa Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Usafiri wa Anga na Operesheni za Usafirishaji chini ya Mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Intergration Project* (EASTRIP) ambapo kazi zifuatazo zimetekelezwa: -

i. Kuendelea na ujenzi wa majengo Matano (5) katika Kampasi ya Mabibo – Dar es Salaam ambapo Mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,504 umekamilika na ujenzi wa majengo matatu (3) yenye madarasa 10, maabara 15, karakana tano (5) na ofisi za watumishi umefikia asilimia 96;
ii. Ujenzi wa jengo la Karakana ya Matengenezo ya Ndege (Aviation Hangar) katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA) litakalotumika kuhifadhia ndege za mafunzo ya urubani na matengenezo ya ndege hizo pamoja na mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege upo kwenye hatua ya kumpata Mkandarasi; na
iii. Ununuzi wa vifaa vya mafunzo ya urubani na uhandisi wa matengenezo ya ndege ikiwemo *Flight Simulators* mbili (2) na programu za Kompyuta (softwares) kwa ajili ya maabara, madarasa na ofisi katika Kampasi ya NIT Mabibo – Dar es Salaam na KIA unaendelea.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Chuo cha NIT kinaendelea na utekelezaji wa kazi za uanzishwaji wa Kituo cha Kikanda cha Umahiri cha Mafunzo ya Usalama Barabarani kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) ambapo mambo yafuatayo yamefanyika: -

i. Kutoa mafunzo ya usalama barabarani na ukaguzi wa usalama wa barabara ambapo jumla ya washiriki 14,638 wakiwemo wanafunzi wa shule za msingi, madereva wa pikipiki (bodaboda), bajaji na magari;
ii. Kuwajengea uwezo wataalam 35 katika masuala ya ukaguzi wa usalama wa barabara (Road Safety Audit); na
iii. Kufunga vifaa vya kisasa vikiwemo *Teleconferencing System, Geographic Information System (GIS), Vehicle Tracking System (VTS), Global Positioning System (GPS)* na *Digital Television* kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa mafunzo

ya usalama barabarani kwa njia ya mtandao na kufanya tafiti za masuala ya usalama barabarani.

145. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuboresha utoaji wa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam, Chuo cha NIT kinaendelea kutekeleza mpango wa mafunzo kwa kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi katika mafunzo ya muda mrefu. Kwa sasa, jumla ya watumishi 65 wanaendelea na mafunzo hayo ikiwa 44 wanasoma Shahada ya Uzamivu, 17 Shahada ya Uzamili, wawili (2) mafunzo ya Urubani (Integrated Commercial Pilot License Course - ICPL) na wawili (2) mafunzo ya Leseni ya Matengenezo ya Ndege (Basic Aircraft Maintenance Technician License).

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

147. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na vyuo vingine, katika mwaka 2024/25, Wizara imeendelea kusimamia utoaji wa mafunzo katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI). Katika kutekeleza azma hiyo, DMI imeendelea kutoa elimu na mafunzo ya bahari nchini. Mafunzo hayo yanajumuisha kozi za muda mrefu na mfupi pamoja na; tafiti mbalimbali, huduma ya ushauri wa kitaalam na masuala mengine yanayohusu elimu ya bahari. Aidha, Chuo kimeendelea kutoa kozi za umahiri (Certificates of Competency) katika sekta ya bahari nchini.

148. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza ahadi ya kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia katika vyuo vya kisekta, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari (TPA) imenunua mtambo maalum wa mafunzo kwa vitendo (Full Mission Bridge and Engine Room Simulator) utakaotumika kutoa mafunzo ya vitendo ili kuongeza ubora na umahiri katika utoaji wa mafunzo ya uhandisi na unahodha wa meli nchini. Mtambo huu ulikabidhiwa kwa Chuo cha DMI mwezi Februari, 2025 na shughuli ya ufungaji imekamilika. Sambamba na hilo, Chuo kimenunua vifaa vya mafunzo vikiwemo vifaa vya Karakana na Maabara ya mafuta na gesi asilia. Katika hatua nyingine, Chuo cha DMI kimeanza taratibu za upanuzi wa Chuo hicho kwa kujenga Chuo kikubwa na cha kisasa katika eneo jipya lililopo Kimbiji katika wilaya ya Kigamboni Jijini Dar es Salaam lenye ukubwa wa ekari 13. Kwa sasa taratibu za kumpata Mshauri

Elekezi atakayefanya zoezi la Upembuzi Yakinifu, Usanifu wa Kina (Detailed Design) na uandaaji wa Mpango Kabambe zinaendelea. Ujenzi wa Chuo hicho unategemea kuanza mwaka wa fedha wa 2025/26.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo kimeendelea kutekeleza mkakati wa kuongeza udahili wa wanafunzi mwaka hadi mwaka ambapo katika mwaka wa masomo 2024/25, Chuo kimeweza kudahili wanafunzi wa kozi ndefu 5,921 sawa na ongezeko la asilimia 14.37 ikilinganishwa na wanafunzi 5,177 waliodahiliwa katika mwaka wa masomo 2023/24 katika kozi ndefu 51 zikiwemo kozi 10 za umahiri kwa Maafisa wa vyombo vya majini (Certificate of Competency). Vilevile, kwa mwaka wa masomo 2024/25, Chuo kimeweza kudahili washiriki wa kozi fupi 7,145 sawa na ongezeko la asilimia 6.34 ikilinganishwa na washiriki 6,719 waliodahiliwa mwaka wa masomo 2023/24 katika kozi fupi 49.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Chuo kimetoa machapisho ya tafiti 23 na kutoa huduma ya ushauri wa kitaalam (consultancy) kwa taasisi za Umma na Binafsi zipatazo tisa (9). Vilevile, Chuo kimeratibu Kongamano la Kimataifa la Uchumi wa Buluu lililofanyika Julai, 2024 Jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na washiriki 1,002 kutoka nchi saba (7) za Ghana, Gambia, Kenya, Liberia, Sierra Leone, Nigeria na mwenyeji Tanzania. Tukio hili lilikuwa fursa kubwa ya kiuchumi na kuitangaza nchi yetu kimataifa katika tasnia ya bahari.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utendaji na utoaji wa mafunzo, Serikali imeendelea kuongeza idadi ya watumishi kutoka 154 kwa mwaka wa fedha 2023/24 hadi kufikia watumishi 166 kwa mwaka wa fedha 2024/25. Kati ya hao watumishi 78 ni wanataaluma na 88 wasio wanataaluma. Aidha, Chuo kimeendelea kuwajengea uwezo na kuwaendeleza watumishi katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi, ambapo watumishi 19 wapo katika mafunzo hayo. Kati ya watumishi hao, wanne (4) wanasoma Shahada ya Uzamivu; saba (7) Shahada ya Uzamili, na watatu (3) wanahudhuria mafunzo ya ukakamavu (Cadetship), watatu (3) wanaohudhuria mafunzo ya muda mfupi ya taaluma na wawili (2) wanahudhuria mafunzo ya vitendo melini.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na vyuo vya NIT na DMI vinavyosimamiwa moja kwa moja na Wizara, vipo vyuo vingine vinne (4) ambavyo vinasimamiwa na Taasisi moja kwa moja. Vyuo hivyo vimekuwa chachu katika kuwezesha Taasisi husika kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi. Vyuo husika na Taasisi zinazovisimamia ni: Chuo cha Usafiri wa Anga (TCAA); Chuo cha Bandari (TPA); Chuo cha Teknolojia ya Reli (TRC); na Chuo cha Hali ya Hewa (TMA). Utekelezaji wa shughuli za vyuo hivyo katika kipindi cha mwaka 2024/25 ni kama ifuatavyo:

Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania

153. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) imeendelea kutoa mafunzo katika taaluma mbalimbali za sekta ya usafiri wa anga. Mafunzo haya yanajumuisha uongozaji wa ndege, mafunzo kwa mafundi wa mitambo ya kuongozea ndege na mawasiliano, pamoja na utoaji wa taarifa za anga. Pia, chuo kimeendesha mafunzo katika kozi za usalama wa usafiri wa anga, usimamizi na uandaaji wa safari za ndege na usafirishaji wa bidhaa hatarishi katika ndege. Aidha, kozi nyingine zilizotolewa ni makosa ya kibinadamu katika usafiri wa anga, urushaji wa ndege zisizokuwa na rubani, usimamizi wa viwanja vya ndege pamoja na mfumo wa usimamizi wa usalama wa anga. Vilevile, Chuo kimeendesha mafunzo ya ufundishaji kwa wakufunzi wa sekta ya usafiri wa anga. Mafunzo yote yameendeshwa kwa mujibu wa taratibu zilizowekwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) ambalo Tanzania ni mwanachama wake.

154. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi hicho, Chuo cha CATC kimefanikiwa kuendelea kuwa mwanachama kamili wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO) kupitia mpango wa TRAINAIR PLUS katika hadhi ya Full MemberGOLD. Mafanikio haya yametokana na ukaguzi uliofanywa na ICAO kati ya tarehe 2 hadi 5 Desemba 2024, ambapo Chuo kilikidhi vigezo vyote stahiki vinavyohitajika kwa hadhi hiyo.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya washiriki wanaopata mafunzo katika Chuo cha CATC imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka, hususan baada ya Chuo hicho kuwa mwanachama

kamili wa ICAO na pia baada ya kupata cheti cha kutoa mafunzo ya Usalama wa Usafiri wa Anga (ICAO Aviation Security Training Centre). Kutokana na utambuzi huo wa chuo katika ngazi ya kimataifa, idadi ya nchi zinazoshiriki mafunzo katika CATC imeongezeka kutoka 16 za awali na kufikia 18 kwa kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi, 2025. Miongoni mwa nchi hizo ni, Angola na Umoja wa Falme za Kiarabu.

156. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha Julai, 2024 hadi Machi 2025, Chuo cha CATC kiliendesha jumla ya kozi 89 zikiwa na washiriki 1,258. Kati yao, washiriki 121 walitoka nje ya nchi, wakiwemo wanaume 88 na wanawake 33, huku washiriki 1,137 wakitoka Tanzania, wakiwemo wanaume 820 na wanawake 317. Washiriki wa ndani wanaoendelea kupata mafunzo katika CATC wanatoka katika mashirika ya ndege, viwanja vya ndege vya Tanzania Bara na Visiwani, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA), mashirika mbalimbali yanayotoa huduma kwenye viwanja vya ndege, Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mabenki pamoja na wananchi kwa ujumla.

157. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia Machi 2025, Chuo cha CATC kilifanikiwa kutengeneza jumla ya kozi mpya mbili (2) ambazo ni *Aerodrome Wildlife Management na Passengers Boarding Bridge*. Kozi hizi zinalenga kuboresha ufanisi wa usimamizi wa viwanja vya ndege kwa kuhakikisha usalama wa anga dhidi ya wanyamapori na kuongeza ufanisi katika usimamizi wa madaraja ya kupandia abiria.

158. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha CATC ni miongoni mwa vyuo vitatu (3) vya ICAO katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini vinavyotoa mafunzo ya Usalama wa Usafiri wa Anga. Aidha, ni miongoni mwa vyuo tisa (9) barani Afrika na moja ya vyuo 35 duniani vinavyotoa mafunzo hayo. Kutokana na uanachama wake, ICAO hutoa kozi mbili (2) bure kila mwaka kwa kugharamia walimu wawili (2) wa kimataifa kuja kufundisha kozi hizo nchini. Hadi kufikia Machi 2025, kozi zilizotolewa na ICAO kupitia mpango huu ni *Basic Aviation Security Validation*, iliyoshirikisha Watanzania 16 pamoja na ICAO Risk Management

Workshop iliyoshirikisha Watanzania 20 zilizofanyika mwezi Agosti, 2024.

Chuo cha Bandari

159. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Bandari kinatoa mafunzo, tafiti na ushauri wa kitaalam katika tasnia ya Usafirishaji kwa njia ya Bahari na Maziwa nchini. Chuo hiki kinatoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na: Usimamizi wa Wakala wa Forodha na Usafirishaji wa Mizigo; Mipango ya Usafiri wa Majini na Nchi Kavu; Usimamizi wa Operesheni za Meli na Bandari; Usimamizi wa Vifaa vya Bandari na Matengenezo na Usimamizi wa masuala ya Zimamoto na Usalama. Mafunzo ya muda mfupi yanayotolewa na chuo ni pamoja na mafunzo maalum ya kuandaa mizigo kwa kutumia mashine mbalimbali.

160. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/25, Chuo hiki kilidahili jumla ya wanafunzi 1,008 wa mafunzo ya muda mrefu. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, Chuo kilidahili jumla ya wanafunzi 1,451, kati ya hao, wanafunzi 1,216 walitoka katika Sekta Binafsi, wanafunzi 235 ni kutoka Taasisi mbalimbali za Serikali, ikiwemo TPA ambayo ilitoa washiriki 82. Aidha, Chuo kimehuisha mitaala minne (4) na kutengeneza mtaala mpya mmoja (1) ambayo yote ilipitiwa na wadau wa Sekta ya Uchukuzi na kutoa maoni ya kuwasilishwa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kwa ajili ya kupata ithibati.

Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania

161.***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania (TIRTEC) kinatoa mafunzo, kufanya tafiti na kutoa ushauri elekezi katika usafiri kwa njia ya reli ili kuleta tija katika Shirika la Reli Tanzania (TRC) na wadau wengine husika katika usafiri kwa njia ya reli. Chuo kina kampasi mbili (2) ya Tabora (Kampasi kuu) na Morogoro ambazo zinatoa mafunzo ya muda mrefu katika fani mbalimbali ikiwa ni pamoja na Usafirishaji kwa njia ya Reli, Matengenezo ya mabehewa, Matengenezo ya miundombinu ya Reli na Fundi Sanifu wa Mifumo ya Umeme kwenye Vichwa vya Treni.

162. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Chuo cha TIRTEC kilidahili jumla ya wanafunzi 559 sawa na ongezeko la

asilimia 19.66 ikilinganishwa na wanafunzi 466 waliodahiliwa katika mwaka wa fedha 2023/24. Ongezeko hili limetokana na Chuo kupandishwa uwezo na kuanza kutoa stashahada mbalimbali ikiwemo stashahada za Teknolojia ya usanifu wa matengenezo ya reli na mabehewa ambazo awali zilikuwa hazitolewi. Halikadhalika, kwa lengo la kuboresha huduma, Chuo kimepata kibali cha kuanza kutoa kozi mpya ya stashahada ya mawasiliano; usafirishaji na udhibiti wa ajali katika mtandao wa reli; na uchumi katika usafirishaji kwa kampasi ya Tabora na stashahada ya teknolojia ya udereva wa treni na usalama kwenye matengenezo ya miundombinu ya Reli na matengenezo ya mabehewa katika kampasi ya Morogoro. Kuanzishwa kwa kozi hizi kutasaidia kuzalisha wataalam mbalimbali wanaohitajika sokoni hususan katika sekta ndogo ya reli ambayo ndiyo mhimili katika usafirishaji wa mizigo mikubwa.

Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa

163. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa (NMTC) kilichopo Kigoma, kimeendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa katika ngazi ya astashahada na stashahada, ambapo katika mwaka wa fedha 2024/25 jumla ya wanafunzi 60 walidahiliwa. Kati ya wanafunzi hao, Wanafunzi 28 ni ngazi ya stashahada (NTA Level 6 na NTA Level 5) na wanafunzi 32 ni ngazi ya astashahada (NTA Level 4). Aidha, Serikali imeendelea na jitihada za kuboresha miundombinu ya Chuo hicho ili kuimarisha utoaji wa mafunzo na kuongeza wigo wa udahili ikiwemo udahili wa wanafunzi kutoka nje ya nchi.

164. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha NMTC pia kilifanikiwa kuandaa mafunzo mahsusi ya matumizi ya data na taarifa za Rada za hali ya hewa kwa watalaam wa hali ya hewa kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika yaliyofanyika Jijini Mwanza tarehe 26 hadi 30 Agosti, 2024. Mafunzo hayo yalifadhiliwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) baada ya kujiridhisha kuwa Serikali ya Tanzania ina uwezo wa kuendesha mafunzo hayo kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika miundombinu ya hali ya hewa ikiwemo ununuzi wa Rada za hali ya hewa.

B.1.4: MASUALA YA KISERA NA MTAMBUKA Maboresho ya Sera, Sheria na Kanuni za Kisekta

165. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Hotuba ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2024/25, niliwasilisha taarifa ya kuanza maandalizi ya kuhuisha Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 baada ya Tathmini iliyokamilika mwaka 2023 ambapo nilieleza kuwa Wizara itakamilisha taratibu na kumpata Mshauri Elekezi atakayeshirikiana na Wizara katika kuhuisha Sera husika. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Mshauri Elekezi amepatikana na zoezi la kufanya mapitio ya Sera husika lilianza rasmi. Hatua zilizokamilika ni pamoja na kukusanya maoni kutoka kwa Wadau wa Sekta ya Uchukuzi wakiwemo: Kamati ya Maandalizi ya Dira ya Taifa ya mwaka 2050; makundi ya wadau mbalimbali yaliyojumuisha: Vyama vya Watoa huduma za Uchukuzi (Associations) vya Bandari, Mabasi, Malori, Daladala, Anga, Bajaji na Bodaboda; Wadau wa Maendeleo; Wizara na Taasisi; Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu; na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti. Zoezi hilo lilikamilika mwezi Februari, 2025. Aidha, Taarifa ya Kitalaam (Technical Report) imekamilishwa ambayo ndiyo msingi wa kuandaliwa Sera husika. Kwa sasa, Rasimu ya Sera hiyo inaandaliwa kupitia Mshauri Elekezi na baada ya hatua hiyo, rasimu ya Sera hiyo itawasilishwa katika ngazi za maamuzi ili kuridhiwa.

166. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendana na mabadiliko yanayotokea katika utendaji wa Sekta ya Uchukuzi, Serikali imeendelea kufanya mapitio ya sheria na kutunga sheria mbalimbali. Kutokana na hali hiyo, Serikali kupitia Wizara iliandaa muswada wa kutungwa kwa Sheria ya Viwanja vya ndege Tanzania ya mwaka 2024 na kuuwasilisha katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa majadiliano na hatimaye Muswada huo ulisainiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 2 Oktoba, 2024 na kutangazwa kuwa Sheria kwenye gazeti la Serikali tarehe 11 Oktoba, 2024 na kuanza kutumika. Madhumuni ya kutungwa kwa sheria hiyo ni kuimarisha usimamizi, uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege vya Serikali nchini. Kutokana na uwepo wa sheria hiyo, mpaka sasa tayari Serikali imeunda Bodi ya Wakurugenzi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania na pia imeendelea kusimamia, kuendesha na kuendeleza Viwanja vya Ndege vya Serikali na

kuhakikisha kunakuwepo na ufanisi na tija katika shughuli za viwanja vya ndege nchini.

167. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuboresha utendaji wa Sekta ya Uchukuzi, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2024 hadi kufikia Machi, 2025, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake imekamilisha kuandaa Kanuni mpya na kufanya marekebisho katika kanuni mbalimbali za Sekta ya Uchukuzi. Kanuni Mpya iliyotungwa ni Kanuni za Bandari, 2024 (Ports Regulations, 2024). Aidha, Kanuni zilizofanyiwa marekebisho ni pamoja na: Kanuni za Ugomboaji na Uondoaji wa Shehena Mahsusi, 2025 (Tanzania Shipping Agencies (Clearing and Forwading of Exclusive Items) (Amendment) Regulations, 2025); Kanuni za Kuzuia Uchafuzi Utokanao na Mafuta, 2025 (Merchant Shipping (Prevention of Oil Pollution (Amendment), Regulations, 2025); Kanuni za Usafiri Majini za Ubebaji wa Shehena ya Yabisi na Fueli, 2025, (Merchant Shipping (Carriage of Soild Bulk Cargoes and Oil Fuels) (Amendment) Regulations 2025); Kanuni za Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024 (The Land Transport Regulatory Authority (Complaint Handling Procedures) (Amendment) Rules, 2024); na Kanuni za Vigezo na Masharti ya Kutoa Huduma zinazodhibitiwa za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini za Mwaka 2024 (The Land Transport Regulatory Authority (Terms and Conditions for Provision of Regulated Services) (Amendment) Rules, 2024).

168. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali imekuwa ikiwasilisha Itifaki na Mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa inayotoa miongozo katika shughuli za usafiri na usafirishaji yenye lengo la kuimarisha ulinzi, usalama, utunzaji wa mazingira na biashara kwa ajili ya kuridhiwa na Bunge lako Tukufu. Hadi kufikia Machi 2025, mikataba iliyoridhiwa ni: Mkataba wa Usalama wa Maisha Baharini (International Convention for the Safety of Life at Sea - SOLAS 1974); Mkataba wa Kuzuia Uchafuzi kutoka kwenye Meli (International Convention for the Prevention of Pollution from Ships-MARPOL, 1973/78); Mkataba wa Kipimo cha Tani za Meli (International Convention on Tonnage Measurement of Ships (TONNAGE, 1969); na Mkataba wa Viwango vya Mafunzo, Vyeti na Uangalizi kwa Mabaharia (International Convention on

Standards of Training, Certification and Watchkeeping for Seafarers (STCW, 1978).

169. ***Mheshimiwa Spika***, Serikali kupitia TASAC imesaini na kuanza taratibu za kuridhiwa Mkataba Mpya wa Usafiri Majini wa Afrika wa Mwaka 2010 (Revised African Maritime Transport Charter, 2010). Kuridhiwa kwa Mkataba huo kutaleta manufaa kwa Taifa ikiwa ni pamoja na: Kuimarika kwa uhusiano wa kidiplomasia na kiuchumi kati ya Tanzania na nchi za Umoja wa Afrika pamoja na Jumuiya za Kimataifa; Kuongezeka kwa wigo wa Tanzania kushiriki kwenye fursa za uongozi, mafunzo, ajira na tafiti zitakazoratibiwa na Nchi Wanachama wa Umoja wa Afrika (AU); Kuimarika kwa usalama na utunzaji wa mazingira katika masuala ya usafiri majini; Kuendelea kuitangaza Tanzania Kikanda na Kimataifa; Kuongezeka kwa wigo wa ushiriki wa Tanzania katika masuala ya Kikanda na Kimataifa yanayohusu usafiri majini; na Kuendelea kuitangaza lugha ya Kiswahili ambayo imekubaliwa kuwa miongoni mwa lugha rasmi za umoja huo wa Afrika.

Ufuatiliaji na Tathmini

170. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) imekuwa na utaratibu wa kufanya tathmini ya utendaji wa Sekta ya Uchukuzi kila mwaka kwa kuendesha mkutano mahsusi wa mapitio ya shughuli zote za kisekta (Joint Transport Sector Review Meeting – JTSR). Mkutano huo hufanyika kila mwaka kwa kuwakutanisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Uchukuzi ikijumuisha Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo. Mkutano uliofanya tathmini ya mwaka wa fedha 2023/24 ambao ulikuwa Mkutano wa 17 ulifanyika Jijini Arusha tarehe 23 - 25 Oktoba, 2024 ambapo tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na changamoto zilijadiliwa kwa kina na kutafutiwa ufumbuzi ikiwa ni pamoja na kuainishwa kwa fursa za uwekezaji katika Sekta ya Uchukuzi. Aidha, Mkutano huo huainisha maazimio yanayohitaji kutekelezwa na wadau mbalimbali na kuyawasilisha kwao kwa utekelezaji.

Mifumo ya TEHAMA

171. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara ya Uchukuzi imeendelea na jitihada mbalimbali za kuhakikisha

matumizi salama, bora na sahihi ya TEHAMA katika utekelezaji wa majukumu yake. Matumizi ya TEHAMA yanaongeza ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato, kuongeza uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma bora na haraka kwa wananchi. Katika kutekeleza hilo na maelekezo ya mamlaka yaliyotolewa katika mikutano mbalimbali kuwa ifikapo tarehe 31 Desemba, 2024 mifumo mbalimbali ya TEHAMA iwe imeunganishwa na kubadilishana taarifa. Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na wadau wengine ikiwemo Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) ilihakikisha mifumo inayotumiwa na Wizara na Taasisi zake imeunganishwa katika mfumo wa kubadilishana taarifa Serikalini (Government Enterprise Service Bus GovESB) ili kuwezesha kubadilishana taarifa na mifumo ya Taasisi za Umma na Binafsi.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** sambamba na hilo, tarehe 01 Agosti, 2024 wakati akizindua rasmi huduma ya usafiri wa treni ya kisasa ya abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alielekeza Wizara ya Uchukuzi kuona namna bora ya kuwezesha upatikanaji wa huduma ya tiketi za abiria kupitia dirisha moja. Katika kutekeleza maelekezo hayo, Wizara ya Uchukuzi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), Shirika la Reli Tanzania (TRC) na wadau wengine iliratibu na kusimamia mchakato wa kujenga dirisha moja la utoaji wa huduma za tiketi za abiria kwa wasafiri wa mabasi ya masafa marefu na wasafiri wa treni za reli ya kisasa (SGR) na reli ya kati (MGR). Kazi hii imeendelea kutekelezwa na kwa sasa dirisha hilo lipo katika hatua za mwisho za kuanza kufanya kazi na inatarajiwa kukamilika mwezi Julai, 2025.

Kuongeza Upatikanaji wa Fedha za Kigeni

173. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2024/25, Wizara iliweka lengo la kukusanya **Dola za Marekani milioni 762.41** kutokana na huduma za uchukuzi zinazotolewa kwa fedha za kigeni ikijumuisha tozo mbalimbali kwa nchi jirani zinatokana na kuhudumia shehena kwenda nchi hizo. Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi kufikia Machi, 2025 jumla ya **Dola za Marekani milioni 435.07** zimekusanywa kutokana na utoaji wa huduma hizo za uchukuzi.

Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Watumishi

174. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhakikisha inakuwa na rasilimaliwatu endelevu na wenye weledi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake katika Idara na Vitengo vyake. Ili kufikia lengo hilo, Wizara imeendelea kutekeleza jukumu la kuwajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali ili waweze kuongeza ujuzi na kuleta tija katika Utumishi wa Umma. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2024 hadi Machi, 2025 watumishi 126 wa Idara na Vitengo vya Wizara walipatiwa mafunzo ndani na nje ya nchi ambapo kati ya Watumishi hao, Watumishi 114 walipata mafunzo ya muda mfupi na watumishi 12 walipata mafunzo ya muda mrefu.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na Taasisi zake imeendelea kutekeleza mwongozo wa kufanya mazoezi mahala pa kazi, unaolenga kuimarisha Afya za Watumishi kwa kuandaa na kushiriki michezo mbalimbali ikiwemo bonanza, mashindano ya maadhimisho ya siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) na kushiriki michezo ya SHIMIWI. Michezo hiyo imeendelea kuhamasisha watumishi kufanya mazoezi ya viungo na kupelekea kuimarisha afya na kupunguza hatari ya kupata magonjwa yasiyoambukizwa pamoja na kujenga uhusiano mwema na Taasisi nyingine. Vilevile, katika kutekeleza mkakati wa kitaifa wa kuzuia na kudhibiti UKIMWI na magonjwa yanayoambukiza, Wizara imeendelea kutoa huduma ya lishe, vifaa vya kujikinga na maambukizi, semina na mafunzo mbalimbali juu ya magonjwa yanayoambukiza na yasiyoambukiza.

Utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa dhidi ya Rushwa

176. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji wa Awamu ya Nne (4), Mkakati huo wenye lengo la kuwa na jamii iliyostawi na yenye mifumo madhubuti ya kukuza uadilifu na isiyovumilia rushwa unatekelezwa kwa kipindi cha Miaka Saba (7) (NASCAP 2023 - 2030). Kupitia Mkakati huo, Wizara imehuisha Kamati ya Uadilifu pamoja na Kamati za Uadilifu za Taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Wizara. Lengo la hatua hii ni kuwajengea uwezo Watumishi juu ya maadili, kudhibiti rushwa na utawala bora ili kuwawezesha Watumishi kushiriki kikamilifu katika kukabiliana na Rushwa mahala pa kazi.

B.1.5: MAFANIKIO YA MIAKA MINNE (4) YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA YA UCHUKUZI

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na maelezo niliyoyatoa kuhusu udhibiti na utoaji wa huduma za uchukuzi pamoja na utoaji wa mafunzo ya kisekta katika kipindi cha mwaka 2024/25 hadi kufikia mwezi Machi 2025, naomba kwa muhtasari niainishe mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Uchukuzi kwa kipindi cha miaka minne (4) ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati inayojumuisha miradi ya reli; viwanja vya ndege; uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania; ujenzi na uboreshaji wa bandari; ujenzi na ukarabati wa meli katika maziwa makuu; ufungaji wa rada za hali ya hewa; na uboreshaji wa vyuo vya mafunzo vya kisekta. Hakika, Serikali ya Awamu ya Sita imepiga hatua kubwa ya kuwaletea maendeleo Watanzania, kwa kuwa utekelezaji wa miradi katika sekta hii umeendelea kuchagiza ukuaji wa sekta nyingine za kiuchumi na kijamii. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita tumeshuhudia mafanikio makubwa na ya wazi katika Sekta ya Uchukuzi kama ifuatavyo:-

Kuanza uendeshaji wa reli ya SGR na Kuendelea kwa Ujenzi katika Vipande mbalimbali vya SGR

179. ***Mheshimiwa Spika,*** kimsingi katika ujenzi wa reli ya SGR nchini, Tanzania imeweka historia nyingine ndani na nje ya Bara la Afrika kwa kujenga na kuanza uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR. Hatua hii ni kubwa na ya kupongezwa kwani imekuwa ya kipekee tangu kupata Uhuru wa nchi yetu. Serikali ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetekeleza kwa vitendo maono ya nchi yetu ambapo uendeshaji wa reli ya kisasa ya SGR ulianza rasmi tarehe 14 Juni, 2024 kwa safari kati ya Dar es Salaam hadi Morogoro na tarehe 25 Julai, 2024 kwa safari kati ya Dar es Salaam hadi Dodoma. Uendeshaji huo ulizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mnamo tarehe 01 Agosti 2024, ambapo hadi kufikia Machi, 2025 abiria 2,054,828

wamesafirishwa na kukusanya jumla ya Shilingi bilioni 60.25. Pamoja na hatua hiyo, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Serikali kupitia TRC inatarajia kuanza uendeshaji wa treni ya mizigo kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma (Ihumwa na Bahi) ifikapo mwezi Juni, 2025. Usafirishaji wa mizigo kupitia reli hii pamoja na manufaa mengine utaongeza mapato ya Serikali na kurahisisha biashara ndani na nje ya nchi na kukuza uchumi na pato la Taifa.

180. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kuanza uendeshaji wa reli ya kisasa katika kipande cha Dar es Salaam – Morogoro - Dodoma, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na ujenzi wa reli ya kisasa ambapo kabla ya kuingia madarakani, TRC ilikuwa imeanza ujenzi wa reli ya kisasa kwa vipande viwili tu ambavyo ni Kipande cha kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro (km 300) na Morogoro hadi Makutupora (km 422). Aidha, Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inatekeleza kwa vitendo ambapo tangu imeingia madarakani imefanikisha kupatikana kwa fedha za kuendelea na kuanza ujenzi wa reli ya SGR kwa vipande vya: Makutupora hadi Tabora (km 368); Tabora hadi Isaka (km 165); Tabora hadi Kigoma (km 506); Isaka hadi Mwanza (km 341); na Uvinza hadi Musongati (km 240). Kazi ya ujenzi katika vipande hivyo inaendelea na ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefungua soko la nje kwa kuhakikisha reli ya SGR inaunganisha nchi jirani ikiwemo Jamhuri ya Burundi na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Katika kutekeleza hili, Serikali imefanikisha kupata fedha za ujenzi wa reli ya SGR kutoka Tabora – Kigoma (Km 506) ambayo itafungua mipaka ya biashara na nchi ya Demokrasia ya Congo kupitia Ziwa Tanganyika (Kigoma) na ujenzi wa reli ya SGR kutoka Uvinza – Musongati (km 240) ambapo mkataba wa ujenzi wa reli hii umesainiwa tarehe 29 Januari, 2025.

Ununuzi wa Ndege

182. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea na ununuzi wa ndege mpya ikiwa ni utekelezaji wa Mpango wa Ufufuaji wa ATCL. Uwekezaji huu umeifanya ATCL kuweza

kutanua mtandao wake kibiashara ambapo tangu Mhe. Rais wa Awamu ya Sita, Dkt. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, ndege saba (7) zimenunuliwa na kuifanya ATCL kuwa na ndege 15 mpya ikiwemo ndege moja (1) ya mizigo zinazohudumia vituo vya ndani, kikanda na kimataifa. Ndege saba (7) zilizonunuliwa katika Awamu hii ya Serikali zinajumuisha ndege moja (1) ya abiria aina ya Dash 8 Q400, ndege mbili (2) za abiria aina ya Boeing 737 Max 9, ndege moja (1) ya mizigo aina ya Boeing 767-300F, ndege moja ya abiria aina ya Boeing 787-8, na ndege mbili (2) aina ya A220-300. Ununuzi huu umeendelea kupanua huduma ya usafiri na usafirishaji wa ndege ndani na nje ya nchi ambapo kwa sasa ndege zetu kupitia ATCL zinatoa huduma katika vituo 27 ikilinganishwa na vituo 23 ilivyohudumia mwezi Machi, 2021.

Kuendelea Kuboresha Huduma za Usafiri na Usafirishaji katika Maziwa Makuu

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji majini, hususan katika Maziwa Makuu, Serikali ya Awamu ya Sita imeweka historia ya kuendelea kujenga na kukarabati meli mbalimbali. Mathalan, katika kuendelea na ujenzi wa meli kwa vitendo, ujenzi wa meli mpya ya MV. Mwanza umeendelea na hadi kufikia Machi, 2025 umefikia asilimia 96 kutoka asilimia 40 iliyofikiwa mwezi Machi, 2021 wakati Serikali ya Awamu ya Sita inaingia Madarakani. Mradi huu unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Mei, 2025. Aidha, meli ya MV. Umoja yenye uwezo wa kubeba kwa wakati mmoja mizigo yenye tani 1,200 ukarabati wake umekamilika na kuanza kutoa huduma, ambapo kwa sasa inafanya safari kwenda nchi za Uganda na Kenya. Serikali pia imeanza ukarabati wa meli ya kihistoria ya MV. Liemba ambayo hadi kufikia mwezi Machi, 2025 umefikia asilimia 15; ukarabati wa meli ya MT. Sangara umefikia asilimia 98; na ukarabati wa meli ya MT. Ukerewe umefikia asilimia 17.

Uboreshaji wa Huduma za Bandari Nchini

183. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuchukua mikakati madhubuti katika kuendeleza bandari nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kufanya maboresho makubwa katika bandari zake za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Bandari za

Maziwa Makuu; na kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari. Kutokana na juhudi hizi mafanikio makubwa yameanza kupatikana. Mathalan, katika kipindi cha kuanzia mwaka wa fedha 2021/22, shehena ya makasha iliyohudumiwa katika bandari za Tanzania imekuwa ikiongezeka kwa wastani wa asilimia 15.23 kwa mwaka kutoka tani milioni 20.78 zilizohudumiwa mwaka 2021/22 hadi kufikia tani milioni 27.55 zilizohudumiwa mwaka 2023/24. Kwa kasi hii, inaonesha kuwa lengo lililowekwa na TPA katika Mpango Kabambe wa Bandari nchini wa mwaka 2021/22 – 2044/45 la kufikia tani milioni 30 mwishoni mwa mwaka 2029/30, litafikiwa kabla ya kipindi hicho kutokana na mikakati madhubuti inayoendelea kutekelezwa chini ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pamoja na mafanikio haya, mikakati ya makusudi inaendelea kuchukuliwa katika kuongeza ufanisi na kuboresha utoaji wa huduma za kibandari nchini ili kuwezesha bandari zetu kuwa za kisasa na kuhimili ushindani.

Miundombinu na Huduma katika Viwanja vya Ndege

185. ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imeendelea kuchukua mikakati mbalimbali ya kusimamia na kuendeleza huduma za viwanja vya ndege nchini. Mikakati hiyo ni pamoja na kuendeleza na kukarabati miundombinu; kununua na kufunga mitambo ya kisasa; na kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Sheria Na. 8 ya Viwanja vya Ndege iliyopitishwa mwaka 2024. Kutokana na mikakati hiyo, Tanzania imekuwa kinara Afrika na Duniani katika uendeshaji na uimarishaji wa usalama wa viwanja vya ndege. Mathalan, mwezi Mei 2023, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA), imewezesha nchi kushika nafasi ya nne (4) barani Afrika kwa ubora wa ulinzi katika viwanja vya Ndege kupitia ukaguzi uliofanywa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) wa masuala ya Ulinzi (ICAO Universal Security Audit Program - Continous Monitoring Approach) kwa kuwa na ufaulu wa asilimia 86.70. Mafanikio haya yameweza kuendelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita na hivyo, hadhi hiyo kutoshushwa tangu itolewe kwa Taifa letu. Hii ni kutokana na ukweli kuwa, wakati wowote nchi husika ikiwa na mapungufu yeyote ya kiusalama katika viwanja vyake vya

ndege hadhi yake hushushwa, hali ambayo haikutokea tangu kuanza kwa Serikali ya Awamu ya Sita.

186. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza mikakati ya kuongeza masoko ya huduma za viwanja vya ndege, katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita kupitia TAA imefanikiwa kuongeza mashirika sita (6) mapya ya ndege ya kimataifa na yaliyoanzisha safari zake nchini. Mashirika hayo ni Air Link, Zambia Airways, Saudia Airline, South African Airways, Air France na Skyward Express. Kwa ujumla, mafanikio haya ya kibiashara pamoja na jitihada zingine yamepelekea idadi ya abiria wanaotumia viwanja vya ndege kuongezeka kutoka abiria milioni 2.4 waliohudumiwa mwaka 2020 hadi kufikia abiria milioni 3.9 waliohudumiwa mwaka 2024 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 62.50.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kufungamanisha sekta zake ili kuleta ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wananchi na wadau wa nje ya nchi. Ni dhahiri kuwa Sekta ya Uchukuzi ni miongoni mwa chachu muhimu katika kufanikisha Sekta ya Utalii nchini. Kupitia utekelezaji wa Mkakati wa Royal Tour, Serikali ya Awamu ya Sita imeanza taratibu za ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti ambapo mnamo Mwezi Februari, 2025 imesaini mkataba na kumkabidhi eneo la mradi Mshauri Elekezi anayefanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa kina (Feasibility Study and Detailed Design) wa Kiwanja hicho. Pamoja na mafaniko mengine, mradi huu utaongeza idadi ya watalii watakaoweza kutembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti kwa kuwa na ndege za moja kwa moja kutoka ndani na nje ya nchi kwa saa 24. Aidha, mradi huu utapunguza miruko ya ndege za kibiashara ndani ya hifadhi na hivyo kulinda ikolojia itakayowezesha Hifadhi ya Serengeti kulinda hadhi ya urithi wa Dunia iliyopewa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Vilevile, uwepo wa Kiwanja hiki utaleta faida mbalimbali ikiwemo kufungua fursa mpya za kiuchumi kwa kuongeza mapato kupitia tozo mbalimbali zikiwemo za utalii na ongezeko la matumizi ya huduma za kijamii.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vya Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano

(FYDP III 2021/22 – 2025/26) kuhusu uboreshaji wa miundombinu ya kimkakati na uongezaji wa thamani ya mazao ya kilimo. Katika kutekeleza kwa vitendo maono haya, Serikali ya Awamu ya Sita imeanza taratibu za ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege katika Mkoa wa Njombe, ambacho pamoja na shughuli nyingine kitakuwa na uwezo wa kuhudumia ndege kubwa za mizigo ikiwemo Boeing 767-300F ya Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) kutua na kuwezesha usafirishaji wa moja kwa moja wa mazao yanayoharibika ndani ya muda mfupi (Perishables) kama maparachichi kwenda masoko ya kimataifa. Hadi kufikia Machi 2025, Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa awali umekamilika na taratibu za kupata fedha za kuanza ujenzi kwa kushirikisha Sekta Binafsi zinaendelea.

Udhibiti wa Usafiri wa Anga

189. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ufungaji wa mfumo wa mawasiliano kwa njia ya sauti baina ya waongoza ndege na marubani katika Viwanja vya Ndege 12 na Vituo 18. Mfumo huo umewezesha kuimarisha usalama wakati wa kutua na kuruka ndege. Aidha, Serikali imekiboresha Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC) na kuwa miongoni mwa vyuo vitatu (3) vya Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO) katika Kanda ya Afrika Mashariki na Kusini vinavyotoa mafunzo ya Usalama wa Usafiri wa Anga. Pia, Chuo hiki ni miongoni mwa vyuo tisa (9) barani Afrika na ni moja ya vyuo 35 duniani vinavyotoa mafunzo hayo. Uboreshaji wa Chuo hicho unaoendelea kutekelezwa una lengo la kuongeza udahili wa wanafunzi ndani na nje ya nchi.

Uimarishaji wa Utoaji wa Taarifa za Hali ya Hewa Nchini

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imekamilisha ufungaji wa Rada tatu (3) za hali ya hewa katika Mikoa ya Mtwara, Kigoma na Mbeya na kufanya Tanzania kuwa na Rada tano (5). Aidha, Rada nyingine mbili (2) zitakazofungwa katika Mikoa ya Kilimanjaro na Dodoma zipo katika hatua za mwisho za uundaji nchini Marekani ili kufikia lengo la muda mrefu la kuwa na mtandao wa Rada saba (7) za hali ya hewa. Aidha, Rada hizi zitachangia kuongeza usahihi wa utabiri wa hali ya hewa nchini.

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeendelea

kuimarisha shughuli za uangazi na utabiri nchini kwa kununua na kufunga mitambo ya kisasa ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na: Mitambo 10 ya uangazi wa taarifa za hali ya hewa katika usafiri wa anga; Mitambo 20 ya kupima hali ya hewa inayojiendesha yenyewe (Automatic Weather Station - AWS) na mitambo 15 kwa ajili ya vituo vya hali ya hewa kilimo (Agrosynoptic AWS) ambapo seti 10 za mitambo hiyo zimefungwa katika vituo vya Kibaha, Naliendele, Kilwa Masoko, Lyamungo, Mlingano, Hombolo, Matangatuwani, Kizimbani, Uyole na Mbinga; Seti ya mfumo wa kisasa wa kuandaa utabiri wa hali ya hewa (Complete Forecasting System); Mitambo miwili (2) kwa ajili ya uangazi wa hali ya hewa katika anga la juu (Upper Air Station); na Mitambo mitatu (3) ya uangazi wa hali ya hewa katika Bahari ya Hindi.

Kuanza Rasmi kwa Mafunzo ya Urubani Nchini na NIT kupewa Hadhi ya Kimataifa

192. ***Mheshimiwa Spika,*** Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 59 (i) ilitoa ahadi ya kukiwezesha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kutoa elimu na kuzalisha wataalam mahiri wa kada ya usafiri wa anga. Katika kutekeleza ahadi hiyo, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu na Watanzania kuwa, Serikali inayoongozwa na jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imewezesha Chuo cha NIT kupata ndege mbili (2) za mafunzo na ithibati ya kuanza kutoa mafunzo ya urubani baada ya kukamilisha maandalizi ya utoaji wa mafunzo ya Urubani kutoka Mamlaka ya Usafiri wa Anga nchini (TCAA). Mafunzo hayo yataanza mwezi Juni, 2025. Hakika haya ni mafanikio makubwa katika nchi yetu kwa kuanza kutoa mafunzo hayo nchini tangu kupata uhuru. Kuanza kwa mafunzo haya hapa nchini kutawezesha Watanzania wengi kupata mafunzo hayo kwa gharama nafuu ikilinganishwa na gharama za mafunzo hayo nje ya nchi. Aidha, kuanza kwa mafunzo haya kutapunguza uhaba wa marubani hapa nchini. Kwa hatua hii, Tanzania itakuwa miongoni mwa nchi chache Afrika zilizothubutu kutekeleza jukumu hili.

193. ***Mheshimiwa Spika,*** Tasnia ya watalaam wa usafiri wa anga inaendelea kukuzwa nchini kwa kubuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo ya kuanzisha kozi stahiki kwa ajili ya kuleta

ufanisi katika uendeshaji wa masuala ya usafiri wa anga nchini. Jitihada hizo zimeiwezesha Tanzania kuendelea kujulikana kikanda na kimataifa. Kutokana na juhudi hizo zilizoendelezwa na Serikali ya Awamu ya Sita, naomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kutokana na umahiri wake kimepewa hadhi kutoka Wakala wa Usalama wa Anga wa Ulaya (European Aviation Safety Agency - EASA) ya kuwa Kituo cha Mitihani ya Leseni za Kimataifa kwa Wahandisi Matengenezo ya Ndege (EASA part – 66 Aircraft Maintenance License Training) na kuwa Kituo cha Mafunzo ya Uhandisi Matengenezo ya Ndege (EASA Part -147 Approved Training Organizations). Hii ni heshima kubwa kwa Taifa letu linaloongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye kwa hakika ameendelea kuwekeza kimkakati katika Sekta ya Uchukuzi.

**Maboresho mahsusi katika Chuo cha Bahari**
Dar es Salaam

194. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita imewezesha ununuzi na ufungaji mtambo maalum wa kufundishia (Full Mission Crane Simulator) ili kuimarisha miundombinu ya kufundishia ya Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI). Mtambo huo umesaidia utoaji wa mafunzo yenye ubora wa hali ya juu na kuzalisha wataalam wa sekta ya bahari wenye weledi mkubwa. Pia, Serikali imewezesha Chuo cha DMI kuwa na Mtambo wa kufundishia Manahodha na Wahandisi wa Meli (Full Mission Bridge and Engine Room Simulator).

Kuanza kwa Mapitio ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003

195. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Awamu ya Sita, kwa namna ya kipekee imeendelea kuboresha miongozo mbalimbali ikiwemo Sera, Sheria na Kanuni ili kuwezesha upatikanaji wa huduma stahiki na ufanisi kwa lengo la kuendana na maendeleo makubwa yanayofanyika ndani ya Sekta ya Uchukuzi yakiwemo: ujenzi wa miundombinu; ushirikishaji wa Sekta Binafsi; na kuimarisha mashirikiano ya kikanda na kimataifa. Katika kutekeleza azma hii ndani ya kipindi hiki, Wizara imeanza kuhuisha Sera ya Taifa ya Uchukuzi ya mwaka 2003 iliyotumika kwa zaidi ya miaka 20 kwa kuhusisha wadau mbalimbali wa Sekta ya Uchukuzi. Zoezi hilo limefanyika kwa kufanya Tathmini ya

Sekta nzima na kukusanya maoni ya wadau wote kwa ajili ya kupata michango na kubaini changamoto za kisekta ili kuweka mikakati bayana ya kuzitatua katika Sera itakayotungwa. Katika mapitio hayo, yapo mambo ya msingi yaliyobainishwa na Wadau ambayo ni pamoja na: umuhimu wa njia za uchukuzi kufungamanishwa (Intermodal Transport); Kuzingatiwa kwa masuala ya ulinzi na Usalama, hususan kulinda na kutunza miundombinu ya uchukuzi; msisitizo wa matumizi ya Teknolojia za kisasa katika utoaji wa huduma za uchukuzi; kuzingatia masuala ya mazingira (green transport); ushirikishwaji zaidi wa Sekta Binafsi katika uendelezaji na utoaji wa huduma za uchukuzi; uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi kwa kuzingatia mahitaji ya makundi yote katika jamii; Kuimarishwa kwa ushirikiano wa Taasisi ndani na nje ya Wizara (coordination); na Kuzingatia haki za watumiaji (Consumer Protection).

196. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali Wizara kupitia Mshauri Elekezi inaendelea kukamilisha mapitio hayo ambayo kwa sasa Rasimu ya Awali ya Sera hiyo imekamilika. Zoezi la ukamilishaji wa Sera hiyo linatarajiwa kuhitimishwa ndani ya mwaka 2025. Sera hii mpya pamoja na mambo mengine, itawezesha utekelezaji wa majukumu ya uanzishaji, usimamizi, uendeshaji na uendelezaji wa mipango na miradi mbalimbali ya Sekta na hatimaye kuwa msingi wa utoaji wa huduma za uchukuzi kulingana na mahitaji ya sasa na baadaye.

197. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mafanikio hayo ya miaka minne (4), Serikali pia imepata mafanikio katika kipindi cha kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 kama ifuatavyo:-

i. Kuwasili kwa vitendea kazi vinavyotumika katika uendeshaji wa Reli ya SGR ambavyo ni vichwa vya treni 17, seti za treni ya umeme za EMU 10 (mchongoko) na mabehewa 264 ya mizigo. Ununuzi huo umewezesha kuendelea kutoa huduma ya kusafirisha abiria kati ya Dar es Salaam na Dodoma;
ii. Kukamilisha ukarabati wa mabehewa ya mizigo 350 kati ya mabehewa 600 na mabehewa ya abiria 33 kati ya mabehewa 37 ambayo yameanza kutoa huduma katika reli ya MGR, hatua hii itasaidia kuboresha huduma za usafirishaji wa mizigo kwa njia ya reli ya MGR;

iii. Kuongezeka kwa mizigo iliyosafirishwa kwa kutumia Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) ambapo hadi kufikia Machi 2025, ATCL imesafirisha tani 5,869.81 ikilinganishwa na tani 3,658.60 za mizigo zilizosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24, ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 60.41;

iv. Kuongezeka kwa idadi ya abiria waliosafirishwa na ATCL ambapo abiria 876,357 wamesafirishwa sawa na ongezeko la abiria 25,707 ikilinganishwa na abiria 850,650 waliosafirishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24;

v. Kuendelea kuboreshwa kwa Kampuni ya Ndege nchini (ATCL) kulikowezesha pamoja na mambo mengine, kurejesha safari katika kituo cha Johanesburg nchini Afrika Kusini mwezi Novemba, 2024, kituo cha Mtwara na kituo cha Iringa mwezi Machi 2025 na kufanya ATCL kuwa na jumla ya vituo 26. Pamoja na hatua hizo, Serikali imekamilisha taratibu za kuanza safari zake nchini DRC katika kituo cha Kinshasa;

vi. Kupokelewa kwa ndege moja (1) aina ya Boeing 787-8 Dreamliner iliyowasili nchini tarehe 20 Agosti, 2024 katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Abeid Amani Karume Zanzibar;

vii. Kuendelea kutoa huduma katika Bandari Kavu ya Kwala ambapo hadi kufikia Machi, 2025 ilihudumia makasha 805;

viii. Kuendelea na ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokozi katika Ziwa Victoria (Maritime Rescue Cordination Centre - MRCC, Mwanza) ambapo ujenzi wake umefikia asilimia 71, Kituo hicho kitaimarisha usalama wa usafirishaji na usalama wa watu na vyombo vya usafiri katika Ziwa Victoria;

ix. Kuendelea na ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokozi vinavyojengwa kwenye eneo la Kanyara - Geita, Ukerewe na Musoma ambapo utekelezaji wake katika eneo la Kanyara – Geita umefikia asilimia 68, Ukerewe umefikia asilimia 71 na Musoma umefikia asilimia 80;

x. Kukamilisha ununuzi wa boti maalum (Ambulance Boat) itakayotoa huduma ya uokozi katika Ziwa Victoria. Boti hiyo tayari imepokelewa nchini tarehe 31 Machi, 2025 kupitia Bandari ya Mtwara na taratibu za kuanza kutoa huduma zinaendelea kukamilishwa;

xi. Kuendelea kuaminiwa kwa nchi yetu na Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) katika utoaji wa mafunzo ya hali ya

hewa. Mathalan, mafunzo mahsusi ya matumizi ya data na taarifa za Rada za hali ya hewa kwa watalaam wa hali ya hewa kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika yalifanyika Jijini Mwanza tarehe 26 hadi 30 Agosti, 2024;

xii. Serikali kupitia TMA imefakiniwa kuzisaidia nchi za Namibia na Burundi katika uboreshaji wa huduma za hali ya hewa kutokana na kuendelea kuimarika kwa ushawishi wa Tanzania katika nyanja ya hali ya hewa kikanda na kimataifa;

xiii. Kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia ya Chuo cha NIT kwa kujenga majengo sita (6) katika Kampasi ya Mabibo jijini Dar es Salaam ikiwemo maktaba yenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 450 kwa wakati mmoja, madarasa yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,528, ofisi za kuhudumia watumishi 215, maabara 15, karakana tano (5) na mabweni mawili (2) yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 1,504;

xiv. Kuanza kwa ujenzi wa majengo ya Chuo cha NIT Kampasi ya Lindi kwa ajili ya kuzalisha Nguvukazi Mahiri na kujenga uwezo wa kiteknolojia katika sekta ya usafiri majini, mafuta na gesi;

xv. Serikali kupitia Chuo cha DMI imefanikiwa kuboresha na kuendeleza miundombinu ya kufundishia mabaharia na wataalam mahiri wa masuala ya Sekta ya Bahari pamoja na Mafuta na Gesi; na

xvi. Serikali kupitia TAA imefanikiwa kupata tuzo ya mshindi wa kwanza kutoka Baraza la Viwanja vya Ndege Afrika (Airport Council International) kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere kwa kuwa kiwanja chenye huduma bora za usalama kwa mwaka 2024 kwa viwanja vya ndege vya Afrika vyenye miruko zaidi ya 50,000..

B.1.6: CHANGAMOTO NA MIKAKATI YA KUZITATUA

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mwaka 2024/25 imekabiliwa na changamoto mbalimbali. Baadhi ya changamoto hizo na mikakati ya kuzitatua ni: -

*i. Mabadiliko ya Tabianchi*

Katika kipindi hiki cha utekelezaji, mabadiliko ya tabianchi (Climate Change) yameendelea kutokea na kusababisha

hali ya hewa kubadilika mara kwa mara na kusababisha uharibifu wa miundombinu ya uchukuzi, hususan miundombinu ya reli.

Mkakati
Kuendelea kuimarisha huduma za hali ya hewa ikiwemo kufunga Rada za hali ya hewa na kuongeza mtandao wa vituo vya hali ya hewa ili kuimarisha utoaji na matumizi sahihi ya taarifa za hali za hewa na tahadhari ya matukio ya hali mbaya ya hewa; na kufanya tafiti mbalimbali zitakazosaidia kubaini athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa ajili ya usanifu wa miundombinu stahiki.

*ii.* *Mdororo wa Uchumi wa Dunia*
Mdororo wa uchumi wa Dunia unaoathiri shughuli za usafiri na usafirishaji nchini, kutokana na uhusiano uliopo kati ya huduma zitolewazo ndani na gharama za huduma hizo katika soko la dunia.

Mkakati
Kuendelea kuchukua tahadhari za athari za mdororo wa uchumi wa dunia kwa kuweka mikakati ya kukabiliana nazo pindi zinapotokea ili kutoleta madhara zaidi katika huduma za usafiri na usafirishaji nchini.

*iii.* *Mahitaji Makubwa ya Fedha za Utekelezaji wa Miradi*
Miradi mingi ya uchukuzi kuhitaji fedha nyingi (capital intensive) katika utekelezaji wake. Mathalan, Mradi wa SGR utagharimu takribani Shilingi trilioni 23 hadi kukamilika kwake.

Mkakati
Kuendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kutekeleza baadhi ya miradi inayohitaji uwekezaji mkubwa na hivyo kupunguza gharama kwa Serikali. Aidha, Serikali imeendelea kuwahusisha Washirika wa Maendeleo katika utekelezaji wa baadhi ya miradi. Mathalan, katika mwaka wa fedha 2025/26 washirika waliokubali kutoa fedha za utekelezaji wa baadhi ya miradi ya Sekta ya Uchukuzi ni pamoja na: JICA, Benki ya Dunia, Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (European Investment Bank -EIB) na AfDB.

iv. *Uchache wa Wataalam wa Kada Adimu, hususan Marubani na Wahandisi Ndege*
Sekta ya Uchukuzi inakabiliwa na uchache wa wataalam katika nyanja mbalimbali za usafiri na usafirishaji, zikiwemo usafiri kwa njia ya anga na majini.

Mkakati
Wizara imeendelea kuimarisha vyuo vyake ili viweze kuzalisha wataalam wa kada adimu katika usafiri wa majini na anga wakiwemo mabaharia, marubani na wahandisi matengenezo ya ndege kupitia vyuo vilivyo chini ya Wizara vikiwemo DMI na NIT.

v. *Uvamizi na Uharibifu wa Miundombinu ya Uchukuzi*
Uvamizi na uharibifu wa miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo reli hususan nyaya za shaba za SGR, mataruma, vifungio na madaraja ya reli.

Mkakati
Kuendelea kushirikiana na vyombo vya dola pamoja na jamii inayozunguka maeneo husika kutoa elimu ya athari za uvamizi, uharibifu na hujuma za miundombinu ya uchukuzi ikiwemo miundombinu ya reli ili kujenga uwezo kwa jamii inayozunguka miundombinu kuwa walinzi wa miundombinu.

C: MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/26

199. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Uchukuzi itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele katika mwaka husika ili kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za uchukuzi nchini. Katika utekelezaji huo, Wizara itazingatia vipaumbele vyake ambavyo ni: Kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR (Standard Gauge Railway) katika Ushoroba wa Kati; Kuendelea kuboresha miundombinu ya reli ya TRC (Metre Gauge Railway - MGR) na reli ya TAZARA – (Cape Gauge Railway - CGR) ikiwemo kipande cha kutoka Kilosa – Kidatu (km 108) kwa ajili ya kuunganishwa na reli ya TAZARA; Kuendelea kuboresha Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL); Kuendelea na ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi

ikiwa ni pamoja na vichwa vya treni, mabehewa na mitambo ya ukaguzi wa reli; Kuboresha miundombinu na huduma katika Bandari za Bahari na Maziwa Makuu na kuendelea na ujenzi wa bandari kavu nchini, ikiwemo Bandari Kavu ya Kwala ambapo lengo ni kuifanya kuwa bandari kavu ya kimkakati; Kuimarisha usalama na mawasiliano kwenye usafiri na usafirishaji katika Maziwa Makuu nchini; Uendelezaji na uendeshaji wa viwanja vya ndege; Kuimarisha usalama na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira katika usafiri wa anga, ardhini na majini; Kuendelea na ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo za kubeba abiria na mizigo katika Maziwa Makuu; na Kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji majini.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** vipaumbele vingine vya Wizara kwa mwaka 2025/26 ni: Kuendelea kuboresha miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha huduma za uchukuzi; Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika uendelezaji na uendeshaji wa Bandari, Reli na Viwanja vya Ndege nchini; Kujenga uwezo wa Taasisi za usafiri wa anga, majini na ardhini; Kuendelea kuimarisha miundombinu na huduma za hali ya hewa; Kuendelea kutoa mafunzo katika masuala ya reli, hali ya hewa, ujenzi wa meli na usafirishaji kwa njia ya maji na anga; Kutekeleza mikakati ya upatikanaji wa mizigo katika reli ya SGR na kuanza kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kwa hatua za awali; Kutekeleza mikakati ya upatikanaji wa fedha za kigeni; Kuendelea kuimarisha miundombinu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika vyuo vya mafunzo vya kisekta; Kuendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma; Kuendelea kuimarisha Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Shughuli za Wizara; na Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi na kuboresha mazingira ya kazi kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa huduma za uchukuzi kwa ufanisi zaidi.

201. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza vipaumbele vyake, Wizara (Fungu 62) na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2025/26 imetengewa jumla ya **Shilingi 2,746,485,018,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 125,438,950,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,621,046,068,000** ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Aidha, Fedha za Matumizi ya Kawaida zilizotengwa zinajumuisha **Shilingi 96,654,340,000** kwa ajili ya

Mishahara ya Watumishi na **Shilingi 28,784,610,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo. Vilevile, Fedha za Miradi ya Maendeleo zilizotengwa zinajumuisha **Shilingi 2,452,512,444,000** fedha za ndani na **Shilingi 168,533,624,000** fedha za nje. Miradi ya maendeleo na shughuli za Wizara na Taasisi zitakazotekelezwa katika mwaka husika ni kama ifuatavyo:

## C:1. MIRADI YA MAENDELEO ITAKAYOTEKELEZWA KWA MWAKA 2025/26

202. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini yake itaendelea kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati. Miradi ya kielelezo iliyotengewa fedha ni mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na uboreshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Aidha, miradi ya kimkakati iliyotengewa fedha ni pamoja na miradi ya miundombinu ya viwanja vya ndege; ukarabati wa reli; miundombinu ya bandari; ujenzi na ukarabati wa meli; ununuzi wa rada za hali ya hewa; ununuzi wa boti za uokoaji; ununuzi wa mitambo ya kuongozea ndege; pamoja na miundombinu na vifaa vya kufundishia.

Mradi wa Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri na Usafirishaji katika Bahari na Maziwa Makuu

203. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi milioni 833.22** fedha za nje kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu wa utafutaji na uokoaji (MRCC) katika Ziwa Victoria;
ii. Kukamilisha ujenzi wa vituo vitatu (3) vya utafutaji na uokoaji (Nansio – Ukerewe, Musoma Mjini, Kanyala – Sengerema) katika Ziwa Victoria;
iii. Kukamilisha ununuzi wa boti (Ambulance Boat) itakayotoa huduma katika Ziwa Victoria;
iv. Kukamilisha ununuzi wa boti mbili (2) za utafutaji na uokoaji katika Ziwa Victoria;
v. Kufanya Upembuzi Yakinifu wa kuboresha shughuli za utafutaji na uokoaji katika Ziwa Tanganyika na Ziwa Nyasa;
vi. Kufanya Upembuzi Yakinifu wa Usanifu wa kina ili kuhuisha ramani za urambazaji na ufungaji wa alama kwenye njia za kuongoza meli katika Maziwa Makuu;

vii. Kuratibu Sensa ya kuhuisha kanzidata ya vyombo vidogo vya usafiri majini; na
viii. Kuunda mfumo wa TEHAMA wa ufuatiliaji na usimamizi wa vyombo vya usafiri majini.

Mradi wa Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam (DMGP)

***204 Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 24.08** fedha za nje kwa ajili ya usimamizi wa utekelezaji wa mradi wa DMGP; ufungaji wa Mfumo wa Umeme katika Gati Na. 1- 7 pamoja na kufanya ukaguzi wa kitaalam wa mradi wa DMGP.

Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mwanza

205. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 13.80** fedha za ndani kwa ajili ya ukamilishaji wa Ujenzi wa Jengo la Abiria na Miundombinu yake; na Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Uboreshaji wa Kiwanja hicho.

Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Arusha

206. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 4.57** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege ya Kilimo Anga, ujenzi wa tabaka la juu la lami la barabara ya kuruka na kutua ndege na ununuzi wa Mtambo mmoja (1) wa Zimamoto.

Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Mtwara

207. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 6.57** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa Jengo jipya la abiria, Jengo la kuongozea ndege, kituo cha zimamoto na kituo cha hali ya hewa.

Mradi wa Ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Kilimanjaro – KIA

208. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu ambao utatekelezwa kupitia TAA umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 35** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo: ukarabati wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na mfumo wa taa za kuongozea ndege; ujenzi wa jengo la wageni mashuhuri; ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la

kiwanja; ujenzi wa Jengo la mizigo; na ujenzi wa jengo la utawala na watoa huduma.

**Mradi wa Uendelezaji wa Viwanja vya Ndege vya** Mikoa

209. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 20.59** fedha za ndani kwa ajili ya: ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lindi; ukarabati na upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Moshi; ujenzi wa jengo la abiria katika Kiwanja cha Ndege cha Musoma; ufungaji wa taa za kuongozea ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Mafia; ununuzi wa magari mawili (2) ya zimamoto kwa Viwanja vya Ndege vya Shinyanga na Sumbawanga.

Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti

210. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 3** fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina na kuanza ujenzi wa Kiwanja kipya cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti. Kiwanja hiki kitajengwa kwa kuzingatia mazingira (ecosystem) na kujulikana kama *Green International Airport* na kitafungamanisha Sekta ya Utalii na kuchagiza shughuli za utalii kwa kuwa kiunganishi na viwanja vya ndege vya kimataifa nchini.

Mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba

211. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 1.90** fedha za ndani kwa ajili ya kukamilisha Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa Kina pamoja na kuanza ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha mkoa wa Kagera.

Mradi wa Uboreshaji na Upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria JNIA

212. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 7.94** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 80.12** fedha za nje kutoka Serikali ya Ufaransa kwa ajili ya uboreshaji na Upanuzi wa Jengo la Pili la Abiria; uboreshaji wa mfumo wa taa za kuongozea ndege; ujenzi wa eneo maalum la usalama kwenye barabara ya kuruka na kutua ndege; Ujenzi wa uzio wa ndani wa usalama pamoja na ujenzi wa Jengo

maalum la viongozi (Presidential Pavilion). Kukamilika kwa jengo hili kutawezesha kuunganishwa na Jengo la Tatu la abiria (Terminal III) na hivyo kuongeza uwezo wa kuhudumia abiria nchini pamoja na kuwa kitovu cha kutolea huduma kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL). Kwa ujumla jengo hilo baada ya kukamilika linakadiriwa kuwa na uwezo wa kuhudumia abiria milioni 3.5 ikilinganishwa na abiria milioni 1.5 wanaohudumiwa kwa sasa, sawa na ongezeko la asilimia 133.33.

Mradi wa kuwezesha Taasisi (Institutional Support)

213. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 33.4** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 4.33** fedha za nje. Kazi zitakazotekelezwa ni:-

i. Uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria JNIA;
ii. Ulipaji fidia kwa maeneo ya viwanja vya ndege;
iii. Kufanya Tathmini ya Kiteknolojia katika viwanja vya ndege; na
iv. Ujenzi wa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya Chuo cha DMI Kampasi ya Kimbiji Dar es Salaam na Kikwetu Lindi.

Mfuko wa Reli (Railway Infrastructure Fund)

214. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka wa fedha 2025/26, Mfuko wa Reli *(Railway Infrastructure Fund)* unatarajia kutumia jumla ya **Shilingi bilioni 294.80** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na ukarabati na matengenezo ya njia ya reli iliyopo ya Meter Gauge Railway (MGR);
ii. Kuendelea na ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi vitakavyotumika kutoa huduma katika njia ya reli ya MGR;
iii. Kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya ishara, mawasiliano na umeme wa majengo ya uendeshaji katika njia ya reli ya MGR;
iv. Kuendelea na uboreshaji wa mifumo ya TEHAMA;
v. Kuendelea na uwekaji wa uzio na alama katika maeneo ya reli;
vi. Ukarabati wa majengo ya uendeshaji na karakana; na
vii. Kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa awali kwa ajili ya ujenzi wa njia za reli ikiwemo reli ya kutoka Mbegani-Kidomole na Kilosa – Kidatu (km 108).

Mradi wa Ujenzi wa Reli ya SGR

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Mradi wa Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) wenye lengo la kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika ushoroba wa kati na kurahisisha biashara kati ya Bandari ya Dar es Salaam na nchi jirani umetengewa jumla ya **Shilingi trilioni 1.51** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kukamilisha ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Morogoro - Makutupora (Km 422);
ii. Kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Makutupora – Tabora (Km 368);
iii. Kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Tabora - Isaka (Km 165);
iv. Kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Isaka - Mwanza (Km 341);
v. Kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Tabora - Kigoma (Km 506);
vi. Kuendelea na ujenzi wa reli ya SGR kwa kipande cha Uvinza - Musongati (Km 240);
vii. Kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi (Vichwa vya treni, mabehewa, mitambo na mashine za matengenezo ya njia ya reli);
viii. Kuendelea kuwezesha mafunzo ya wataalam wa usimamizi na uendeshaji wa reli ya SGR;
ix. Kugharamia matengenezo ya njia ya reli kwa kipande cha kutoka Dar es Salaam - Morogoro;
x. Kugharamia utekelezaji, ufuatiliaji na usimamizi wa masuala ya mazingira na kijamii kwa mujibu wa mkataba;
xi. Kugharamia usimamizi na ufuatiliaji wa ujenzi wa reli ya SGR; na
xii. Kuendelea kubuni na kutekeleza mikakati ya kuzalisha na kutafuta mizigo kwa ajili ya reli ya SGR.

Mradi wa Ukarabati wa Reli ya MGR - Tanzania Intermodal Rail Project – TIRP II

216. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 51.28** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-

i. Kuendelea na ukarabati wa njia ya reli ya MGR kipande cha Dar es Salaam - Tabora (Km 257.4);
ii. kuendelea na ukarabati wa njia ya reli ya MGR kipande cha Tabora – Isaka (Km 135);
iii. Kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya reli Tanga – Arusha (Km 626);
iv. Kufanya Upembuzi Yakinifu na Usanifu wa awali kwa ajili ya ukarabati wa miundombinu ya reli Kilosa-Gulwe-Igandu; na
v. Kugharamia huduma za ushauri (Consultancy) na wataalam katika utekelezaji wa mradi.

Mradi wa Uboreshaji wa Reli ya TAZARA

217. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 12.32** fedha za ndani kwa ajili ya utekelezaji wa kazi zifuatazo:-

i. Kuanza taratibu za ununuzi wa mabehewa 30 ya abiria;
ii. Ununuzi na ufungaji wa Mfumo wa kukatia tiketi;
iii. Kufanya matengenezo ya njia ya reli, hususan maeneo yaliyowekewa ukomo wa mwendokasi;
iv. Ununuzi wa vipuri vya vichwa vya treni vinne (4) vya njia kuu;
v. Kununua vipuri vya kichwa kimoja (1) cha treni cha sogeza (Shunting Locomotive);
vi. Kununua mzani wa kupimia mabehewa ya mizigo katika mpaka wa Tunduma;
vii. Kujenga njia mbili (2) za reli katika stesheni ya Tunduma;
viii. Kununua mashine ya ukaguzi wa abiria na mizigo; na
ix. Kununua mashine (Excavator) moja (1) ya kuchimba udongo.

Mradi wa Rada, Vifaa na Miundombinu ya Hali ya Hewa

218. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 13.50** fedha za ndani na **Shilingi bilioni 1.99** fedha za nje. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kukamilisha uundaji wa Rada zitakazofungwa Dodoma na Kilimanjaro pamoja na ujenzi wa miundombinu yake;

ii. Kuendelea na uundaji wa vifaa vya uangazi kwenye Bahari ya Hindi vitakavyofungwa Zanzibar, Dar es Salaam na Bagamoyo;
iii. Kufunga vifaa vya upimaji wa hali ya hewa ya anga la juu katika mikoa ya Mtwara na Kigoma;
iv. Ununuzi wa vifaa vya hali ya hewa pamoja na mitambo ya mawasiliano na utabiri wa hali ya hewa;
v. Kujenga maabara ya uhakiki, uboreshaji na urekebishaji (Calibration Laboratory) wa vifaa vya upimaji hali ya hewa;
vi. Kukamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Kanda ya Mashariki pamoja na Kituo cha kufuatilia matukio ya Tsunami;
vii. Kuanza ujenzi wa Ofisi za Makao Makuu ya TMA Jijini Dodoma;
viii. Kuanza kazi ya usanifu wa mabweni na majengo ya Utawala katika Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa;
ix. Kujenga Kituo cha hali ya hewa kilimo kilichopo Hombolo, Jijini Dodoma pamoja na ujenzi wa uzio wa Ofisi za TMA Zanzibar; na
x. Kuimarisha ustahimilivu wa Jamii za ukanda wa Pwani ya Tanzania katika uvuvi endelevu na mazingira ya baharini kupitia Mradi wa ECOFISH.

Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji na Ubadilishanaji wa Data na Taarifa Muhimu za Hali ya Hewa – SOFF Project

219. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 2.17** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo:-
i. Kujenga vituo vitano (5) vya hali ya hewa vya kupima hali ya hewa ya anga la juu;
ii. Kununua vifaa na mitambo ya hali ya hewa ya kisasa; na
iii. Kuwezesha uendeshaji wa vituo vya hali ya hewa.

Mradi wa ununuzi wa Ndege za Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

220. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa ununuzi wa ndege una lengo la kuboresha utoaji wa huduma za kusafirisha mizigo na abiria zenye kuhimili ushindani katika soko la kikanda na kimataifa na

kuchagiza shughuli za utalii, kilimo na biashara ndani ya nchi. Katika mwaka wa fedha 2025/26 mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 216.05** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo: -

i. Kukamilisha ununuzi wa ndege nne (4) za masafa mafupi, na moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba hadi tani 23;
ii. Kukamilisha ununuzi wa injini moja (1) ya ziada ya Ndege aina ya Boeing 737-9;
iii. Kununua seti ya injini ya ziada ya ndege aina ya Q400;
iv. Kuwezesha matumizi ya awali ya ndege nne (4) zitakazonunuliwa aina ya Dash 8 Q400 kufika nchi kutoka kwa waundaji pamoja na kuzinunulia vipuri muhimu vya awali kwa kuzingatia matakwa ya waundaji;
v. Kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za ATCL Makao Makuu na jengo lililopo Kiwanja cha Ndege cha JNIA Terminal I ili kuwa na mwonekano wenye hadhi;
vi. Kujenga Ofisi za ATCL katika eneo la Medeli Jijini Dodoma ili kupanua wigo wa utoaji huduma;
vii. Kukamilisha ukarabati wa nyumba 38 za ATCL zilizoko KIA ili kupunguza gharama za malazi za marubani na wahandisi punde kiwanja cha kilimanjaro kitapoanza kutumika kama sub hub;
viii. Kuendelea na ulipaji wa madeni ya nyuma yaliyolimbikizwa kabla ya ufufuaji ili kuweka vizuri mizania ya vitabu vya hesabu za Kampuni na kuimarisha imani miongoni mwa wadau wa ATCL; na
ix. Kuendelea na ukarabati na ununuzi wa vifaa vya karakana (Hangar) za matengenezo ya Ndege kwa Viwanja vya Ndege vya JNIA na KIA.

Mradi wa Uimarishaji wa Uendeshaji wa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL)

221. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu wa kuboresha utendaji wa ATCL kwa ujumla umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 67.00** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi mbalimbali zikiwemo: -

i. Ujenzi wa karakana ya kisasa ya ndege katika kiwanja cha JNIA;
ii. Ujenzi wa jengo la kuhifadhia vipuri;

iii. Kufunga mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya kuboresha uendeshaji wa Kampuni;
iv. Kuwezesha mafunzo kwa marubani na wahandisi wa ndege;
v. Kuendelea na ujenzi wa ghala la kuhifadhia mizigo na bidhaa; na
vi. Ununuzi wa vipuri vya ndege kwa ajili ya matengenezo ya ndege zote.

Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Meli katika Maziwa Makuu
222. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 171.00** fedha za ndani. Fedha hizi ni kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ambayo inajumuisha:-

i. Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,500 katika Ziwa Tanganyika;
ii. Kuanza ujenzi wa meli mpya yenye uwezo wa kubeba abiria 600 na mizigo tani 400 katika Ziwa Tanganyika;
iii. Kuendelea na ujenzi wa meli mpya ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 3,000 katika Ziwa Victoria;
iv. Kugharamia Upembuzi Yakinifu na kuanza taratibu za ujenzi wa meli ya mizigo kwa ajili ya kuiwezesha Kampuni kufanya biashara katika bahari kuu;
v. Kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kujengea meli chenye uwezo wa kubeba meli zenye uzito wa tani 5,000 katika Ziwa Tanganyika;
vi. Kuendelea na ukarabati mkubwa wa meli ya MV. Liemba katika ziwa Tanganyika;
vii. Kulipa gharama za Wahandisi Washauri kwa ajili ya kusimamia miradi ya ujenzi na ukarabati wa Meli;
viii. Kuendelea na ukarabati wa meli za MV. Ukerewe, MT. Nyangumi na MV. Clarias katika Ziwa Victoria;
ix. Ununuzi wa Mabehewa ya kubebea mizigo katika meli ya MV. Umoja kwenye Ziwa Victoria;
x. Kugharamia ununuzi wa boti za uokozi katika Maziwa Makuu;
xi. Kuendelea na ufungaji wa mifumo ya TEHAMA kwa ajili ya ukusanyaji wa mapato katika Maziwa Makuu;

xii. Kuanza ukarabati wa Meli ya MV. Songea katika Ziwa Nyasa;
xiii. Kununua mtambo wa kushusha na kupakia mizigo (crane) katika meli;
xiv. Kuanza ukarabati wa meli ya MV. Mwongozo katika Ziwa Tanganyika; na
xv. Kugharamia mahitaji ya awali (Initial Cost) ya uendeshaji wa meli za MV. Mwanza na MT. Sangara.

Mradi wa Ununuzi wa Mitambo ya Kuongozea Ndege

223. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 1.80** fedha za ndani kwa ajili ya kugharamia ununuzi na ufungaji wa mitambo ya kuwezesha ndege kutua kwa usalama (Instrument landing system - ILS); kuondoa mifumo ya zamani na kufunga mifumo mipya pamoja na Mafunzo ya kiufundi kwa wafanyakazi kuhusu utumiaji wa mitambo ya ILS.

Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga

224. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 20.88** fedha za ndani kwa ajili ya kazi zifuatazo: -

i. Kugharamia ujenzi wa jengo la Utawala lenye sakafu tano (5);
ii. Kugharamia ujenzi wa darasa moja (1) lenye sakafu nne (4) pamoja na ununuzi wa vifaa vya kufundishia;
iii. Kugharamia ujenzi wa jengo la hosteli lenye sakafu tano (5) na ununuzi wa samani; na
iv. Kugharamia ujenzi wa ukumbi wa mikutano na mgahawa wa chakula.

Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Usafiri wa Anga

225. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 3.70** fedha za nje kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Kufanya Utafiti wa Awali wa Tathmini ya IASA pamoja na kupitia nyaraka muhimu;
ii. Tathmini ya Uzingatiaji wa Viwango vya ICAO (Annex 1, 6, na 8);

iii. Kuandaa taarifa ya Tathmini ya Awali na kukamilisha Mpango wa Marekebisho;
iv. Msaada wa kiufundi wa Marekebisho ya Kisheria, Mwongozo wa Ukaguzi, na Mafunzo ya Wakaguzi;
v. Usimamizi na Uratibu wa Kazi kwa Njia ya Mtandao; na
vi. Kuandaa vigezo vya kupata *Category One rating* kutoka FAA.

Mradi wa ujenzi wa Miundombinu na Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia - (NIT)

226. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 8.37** fedha za ndani kwa ajili ya kutekeleza kazi zifuatazo: -

i. Ununuzi wa Ndege mbili (2) zenye injini moja – Complex piston single engine (Piper Arrow);
ii. Kukamilisha ununuzi wa Ndege moja (1) yenye injini mbili (Twin engine aircraft - Beechcraft Baron);
iii. Ununuzi wa kifaa maalum cha kufundishia namna ya kufunga na kufungua mlango wa Ndege (Door Trainer); na
iv. Matengenezo ya ndege za mafunzo ya urubani.

Mradi wa Uanzishwaji wa Kampasi ya NIT Lindi katika Sekta ya Usafiri Majini, Mafuta na Gesi

227. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 6.5** fedha za ndani kwa ajili ya ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) kwa ajili ya Madarasa, Maabara, Ofisi pamoja na Ujenzi wa Jengo la huduma za chakula (Canteen).

**Mradi wa *East Africa Skills for Transformation and Regional Integration* (EASTRIP)**

228. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, mradi huu umetengewa jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** fedha za ndani kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro (KIA).

C.2: SHUGHULI NYINGINE ZITAKAZOTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2025/26 C.2.1. UDHIBITI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI UDHIBITI WA USAFIRI ARDHINI

229. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) katika mwaka wa fedha 2025/26 inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 43.5** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani ili kudhibiti na kuboresha usalama, upatikanaji wa huduma endelevu na rafiki kwa mazingira kama ifuatavyo: -

(a) Usafiri wa Barabara

i. Kuendelea kutoa na kusimamia masharti ya leseni kwa huduma zinazodhibitiwa, kuthibitisha madereva na kusajili wahudumu wa vyombo vya moto vinavyotoa huduma za usafiri kibiashara;

ii. Kuimarisha upatikanaji na uhakika wa huduma za usafiri mijini na vijijini, kwa kuzingatia watu na maeneo yenye mahitaji maalum, na kusimamia tozo za huduma hizo (nauli elekezi za usafiri wa abiria), na viwango vya ubora wa huduma hizo;

iii. Kuendelea na usimamizi wa utekelezaji wa matumizi ya mifumo ya tiketi za kielektroniki kwa mabasi yaendayo mikoani na Nchi jirani pamoja na kuunganisha mifumo hiyo kwenye mfumo jumuishi wa tiketi za kielektroniki;

iv. Kusimamia usalama wa huduma zinazodhibitiwa ikijumuisha kupanua wigo wa mfumo wa ufuatiliaji magari (VTS), kuongeza ufanisi katika kuthibitisha na ufuatiliaji madereva, kuratibu kanzidata ya madereva wa malori na kushirikiana na wadau katika kutatua changamoto za usafiri wa mabasi kwa saa 24;

v. Kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika mawasiliano ya ndani na ubadilishanaji wa taarifa na nyaraka, pia katika utoaji wa huduma kwa wateja ili kuondoa urasimu, kuweka uwazi na kuongeza ufanisi kwenye usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali; na

vi. Kusogeza huduma za utoaji wa leseni za vyombo vinavyodhibitiwa kwa wananchi wengi zaidi kwa kuongeza kutumia mawakala (authorized agents), hususan kupitia vyama vya ushirika (SACCOS) za wamiliki na waendesha pikipiki (bajaji na bodaboda), Taasisi za Umma na Kampuni.

(b) Usafiri wa Reli

i. Kufanya kaguzi za usalama na ubora wa miundombinu, mitambo, vifaa na mifumo ya reli za Shirika la Reli Tanzania (TRC), ikiwemo kutoa ithibati ya mitambo ya reli za MGR na SGR kabla ya matumizi;
ii. Kununua vifaa vya kisasa vya ukaguzi wa miundombinu ya reli ili kuboresha usalama wa usafiri huo na kuongeza ufanisi wa ukaguzi wa reli;
iii. Kukagua miundombinu, mabehewa na vichwa vya treni za TAZARA kwa niaba ya Serikali ya Tanzania (Mkaguzi wa Reli wa Serikali); na
iv. Kuendesha mafunzo kwa watumishi wanaohudumia reli za TRC na TAZARA (Safety Critical Workers) ili kuboresha usalama na huduma za reli.

(c) Usafiri wa Waya

i. Kuanza kutoa vibali na leseni za ufungaji wa miundombinu na utoaji wa huduma za usafiri wa waya Nchini; na
ii. Kusimamia utekelezaji wa Kanuni za LATRA za Usafiri wa Waya kwenye maeneo yenye vivutio vya utalii kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara ya Uchukuzi, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Halmashauri za Miji / Manispaa / Wilaya / Majiji (LGAs), Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), na Wakala wa Huduma za Misitu (TFS).

(d) Majukumu Mengine

i. Kusimamia uzingatiaji wa utunzaji mazingira kwa vyombo vinavyotoa huduma ya usafiri ardhini kibiashara pamoja na watumiaji wa huduma zinazodhibitiwa ikiwa ni pamoja na kuandaa na

kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs);

ii. Kutoa elimu kwa watumishi kuhusu Masuala Mtambuka ya Kitaifa ikiwemo kukuza maadili, kupambana na rushwa, kuimarisha afya na kudhibiti maambukizi ya UKIMWI na magonjwa yasiyoambukiza na athari zake;
iii. Kutoa elimu kwa Umma kuhusu huduma na masuala ya udhibiti wa usafiri ardhini, haki na wajibu wa watoa huduma na watumia huduma, pamoja na taratibu za kushughulikia migogoro katika huduma zinazodhibitiwa;
iv. Kutekeleza sehemu ya miradi ya Benki ya Dunia iliyobuniwa kuboresha Huduma za Usafiri kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na Arusha;
v. Kuanza ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya LATRA Dodoma, na kukamilisha ujenzi wa majengo ya Ofisi kwenye mikoa mawili (2);
vi. Kuendelea kuwezesha Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA-CCC), Baraza la Ushindani (FCT), Tume ya Ushindani (FCC), na kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali;
vii. Kuendeleza watumishi kwa kuwapa mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu ili kuwajengea uwezo, kukuza weledi na ujuzi wa kutekeleza majukumu ya Mamlaka kwa ubora, ufanisi na kwa kuwajali wateja;
viii. Kupata ithibati na kutekeleza Mfumo wa Usimamizi wa Ubora (Quality Management System) kulingana na Viwango vya Kimataifa (ISO 9001:2015);
ix. Kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali kwa kutumia TEHAMA ikiwemo Mfumo Jumuishi wa Tiketi Mtandao; na
x. Kuendelea kutoa na kusimamia masharti ya leseni kwa watoa huduma wanaodhibitiwa.

UDHIBITI WA USAFIRI WA ANGA

230. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Mamlaka ya Usafiri wa Anga (TCAA) inalenga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 110.76** kutoka vyanzo vyake vya ndani kwa ajili ya kusimamia ubora wa huduma za usafiri wa Anga, kulingana

na viwango vya kimataifa vilivyowekwa na Shirika la Usafiri wa Anga Duniani (ICAO). Kazi zitakazotekelezwa ni zifuatazo: -

i. Kuendelea kutoa na kusimamia leseni kwa Mashirika ya Ndege na Wataalam wa Anga;
ii. Kusimamia usalama wa usafiri wa anga kwa kuweka viwango vya usalama vya kitaifa na kimataifa;
iii. Kufanya kaguzi za mara kwa mara kwa Mashirika ya Ndege na huduma zinazotolewa kwa abiria ili kuhakikisha kuwa zinazingatia sheria, taratibu na viwango vya kimataifa vya huduma;
iv. Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Mamlaka ya Usafiri wa Anga ili kuhakikisha kuwa wana ujuzi na maarifa ya kutosha ya kusimamia sekta hiyo kwa ufanisi;
v. Kuweka mazingira ya ushindani ili kuhakikisha huduma za usafiri wa anga zinapatikana kwa uhakika na kwa bei nafuu;
vi. Kuendelea kuboresha huduma za uongozaji Ndege kwa kuboresha mitambo ya uongozaji ndege katika viwanja na vituo vyenye mitambo;
vii. Kuimarisha udhibiti wa sekta ya usafiri wa anga kwa kuendelea kufanya mapitio ya kanuni ili kuhakikisha anga letu linaendelea kuwa salama;
viii. Kuboresha mifumo ya kielektroniki ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato pamoja na kuhakikisha madeni ya zamani yanakusanywa;
ix. Kuimarisha Chuo cha Usafiri wa Anga kwa kuboresha miundombinu pamoja na vifaa vya kufundishia;
x. Kufanya tafiti mbalimbali ili kubaini fursa za uwekezaji kwenye sekta ya usafiri wa anga kwa ajili ya kuvutia mashirika ya ndege ya kimataifa ya usafiri wa Anga; na
xi. Kuendelea kushirikiana na mashirika ya kikanda na kimataifa ili kuwianisha viwango vya usalama na utendaji bora katika Sekta ya Anga.

UDHIBITI WA USAFIRI MAJINI

231. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, TASAC imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 99.73** kutoka

katika vyanzo vya mapato vya ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kutoa leseni kwa watoa huduma zinazodhibitiwa na kusimamia masharti ya leseni;
ii. Kudhibiti gharama, nauli na tozo mbalimbali za usafiri wa majini kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ili kuhakikisha kuwa tozo hizo zinaendana na gharama za uzalishaji na pia zinaleta ushindani katika soko;
iii. Kufanya ukaguzi wa meli za nje zinazokuja katika bandari za Tanzania Bara na meli zilizosajiliwa nchini ili kuhakikisha vyombo hivyo vinazingatia viwango vya ubora kwa ajili ya usalama na utunzaji wa mazingira;
iv. Kuratibu kazi za utafutaji na uokoaji sambamba na mazoezi ya utafutaji na uokozi; v. Kuimarisha mifumo ya utoaji wa Vyeti vya Mabaharia;
vi. Kuweka mifumo thabiti ya kukabiliana na uchafuzi wa mazingira majini utokanao na meli;
vii. Kutoa elimu na uelewa wa masuala yanayohusu usalama, ulinzi na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira utokanao na meli;
viii. Kuendelea kujenga uwezo wa watumishi katika nyanja mbalimbali ikiwa ni pamoja na shughuli za udhibiti ili kuendelea kukidhi haja na kukabiliana na changamoto za kupanuka kwa maeneo ya udhibiti na mabadiliko ya teknolojia;
ix. Kuendelea kutoa huduma za uwakala wa forodha zinazojumuisha ugomboaji na uondoshaji wa shehena mahsusi, ambazo ni silaha na vilipuzi, makinikia, wanyama hai, nyara za Serikali na kemikali zinazotumiwa na kampuni za madini;
x. Kuendelea kuimarisha mifumo ya mapato na matumizi kwa kukuza matumizi ya TEHAMA katika kudhibiti huduma za usafiri na biashara ya usafirishaji kwa njia ya maji;
xi. Kuendelea kutoa huduma na elimu kwa Watumishi kuhusu masuala mtambuka kama vile UKIMWI, rushwa na elimu kwa Umma kuhusu Sekta zinazodhibitiwa na Shirika kwa kupitia njia mbalimbali kama vile Redio, Magazeti, Vipeperushi na Mikutano ya Wadau;

xii. Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma kwa wadau kwa kukuza matumizi ya TEHAMA na mifumo katika utoaji wa huduma hizo;

xiii. Kuendelea kuandaa kanuni na nyenzo za utendaji zitoazo mwongozo kuhusu udhibiti huduma za usafiri kwa njia ya maji, usalama na ulinzi kwa vyombo vya usafiri majini na uchafuzi baharini kutoka katika meli; na

xiv. Kuendelea kusimamia utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa kuhusu Usafirishaji kwa njia ya Maji inayoratibiwa na Shirika la Bahari Duniani (International Maritime Organization - IMO).

HUDUMA ZA HALI YA HEWA

232. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 19.32** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani ikiwa ni pamoja na mapato yatokanayo na tozo za huduma za hali ya hewa, hususan zitumiwazo katika usafiri wa anga na majini. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 ni kama ifuatavyo:-

i. Kuimarisha utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu na hivyo kuongeza usalama na ufanisi kwa shughuli za kiuchumi zinazofanyika kwenye maji;

ii. Kuongeza vyanzo vya mapato kwa lengo la kuboresha huduma za hali ya hewa;

iii. Kuboresha mfumo wa kuandaa utabiri pamoja na kuendelea kutoa utabiri wa hali ya hewa wa kila siku, siku kumi, mwezi na msimu pamoja na tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa;

iv. Kuendelea kutekeleza mfumo wa udhibiti wa ubora wa huduma za hali ya hewa zinazotolewa kwa sekta ya usafiri wa anga pamoja na kuendelea kumiliki cheti cha ubora (ISO: 9001:2015);

v. Kununua vifaa vya kisasa vya uangazi wa hali ya hewa kupitia mradi wa SOFF unaofadhiliwa na mpango wa Umoja wa Mataifa wa kuwekeza katika miundombinu ya uangazi wa hali ya hewa;

vi. Kuboresha utoaji wa huduma za hali ya hewa kwa ajili ya kuongeza ufanisi na usalama kwa Sekta za Nishati, Madini, Rasilimali Maji,
Usafiri, Kilimo, Utalii na Ujenzi;
vii. Kuendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa kupitia Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa kilichopo Kigoma;
viii. Kufanya tafiti za hali ya hewa na mabadiliko ya Tabianchi na matokeo ya tafiti husika kutumika katika kupunguza athari za mabadiliko ya hali ya hewa kwa sekta za kiuchumi na kijamii;
ix. Kuboresha matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na uendeshaji wa shughuli za hali ya hewa hapa nchini;
x. Kuendeleza watumishi waliopo pamoja kuajiri wafanyakazi wapya;
xi. Kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kutumia huduma zinazotolewa na Mamlaka;
xii. Kudhibiti na kuratibu huduma za hali ya hewa zinazotolewa nchini kwa kuhakikisha taratibu na matakwa ya kisheria yanafuatwa katika utoaji wa huduma za hali ya hewa; na
xiii. Kuendesha na kuimarisha mtandao wa vituo vya hali ya hewa hapa nchini kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa data za hali ya hewa.

## C.2.2. UTOAJI WA HUDUMA ZA UCHUKUZI

HUDUMA ZA BANDARI

233. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi trilioni 1.38** kutoka katika vyanzo vya ndani vya mapato vitokanavyo na huduma za kibandari ikiwa ni pamoja na: -

i. Kuhudumia jumla ya meli 6,366 zenye GRT milioni 46.895. Kati ya meli hizo meli 1,382 ni za Kimataifa (Deep Sea) zenye *Gross Register Tonnage* (GRT) milioni 42.101, meli 1,275 ni za mwambao (coastal) zenye GRT milioni 2.272 na meli 3,708 zenye GRT milioni 2.572 zitahudumiwa katika Bandari za Maziwa Makuu; na

ii. Kuhudumia Shehena ya tani milioni 32.742 ikijumuisha tani za shehena ya makasha (TEUs) 1,299,949 zitakazohudumiwa na Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi itakayotekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha zitokanazo na vyanzo vya mapato ya TPA kwa mwaka wa fedha 2025/26 inajumuisha bandari zilizopo katika Bahari ya Hindi, Maziwa Makuu na Bandari Kavu.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi inatambua umuhimu mkubwa wa huduma za bandari katika Uchumi wa nchi yetu. Hii ni pamoja na ukweli kwamba sekta ndogo ya bandari inachangia asilimia 98 ya huduma ya usafiri kwa biashara ya nje na asilimia zaidi ya 40 katika mapato yatokanayo na kodi. Aidha, ni ukweli kwamba uimarishaji wa huduma za bandari kwa kuongeza miundombinu kama gati na vifaa vya kisasa ndiyo njia sahihi na ya haraka katika kuchangia ukuaji wa uchumi. Katika kuhakikisha kuwa bandari inatimiza azma hiyo, Serikali imepanga kuongeza zaidi uwezo wa bandari zetu, hususan Bandari ya Dar es Salaam. Hatua zitakazochukuliwa ni pamoja na kuongeza idadi ya magati na vifaa vya kisasa ili kuwezesha uhudumiaji wa meli za makasha kwa saa 24 badala ya siku tatu (3) za sasa.

236. ***Mheshimiwa Spika,*** Bandari ya Dar es Salaam ndio kitovu cha Ushoroba wa kati unaoundwa na nchi saba (7) zinazotumia bandari ya Dar es Salaam. Lengo kuu la Ushoroba wa kati ni kuongeza na kuimarisha matumizi ya bandari ya Dar es Salaam kama lango (Gateway) la Uchumi na Biashara kwa nchi za DRC, Burundi, Uganda, Rwanda, Malawi, Zambia na Tanzania. Kufuatia maboresho makubwa katika Bandari ya Dar es Salaam pamoja na kuimarisha mifumo ya TEHAMA na usimamizi wa bandari kwa kutumia uzoefu wa kampuni za kimataifa, kiwango cha shehena inayohudumiwa na TPA kimeongezeka kwa kasi kutoka tani milioni 14 miaka minne (4) iliyopita hadi kufikia takribani tani milioni 23 kilichohudumiwa katika mwaka wa fedha 2023/24 na inakadiriwa kuwa ifikapo mwaka 2030 shehena itakayohudumiwa katika bandari hiyo itafikia tani milioni 30.

237. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kujipanga na ongezeko hilo na fursa hii kubwa kwa ajili ya kuimarisha uchumi wetu, Wizara katika mwaka wa fedha 2025/26 itatekeleza mikakati ifuatayo:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa matanki 15 ya kupokelea shehena ya mafuta (Single Receiving Terminal – SRT) kwa kuifanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa ya kisasa na kuiongezea uwezo zaidi katika kuhudumia shehena;
ii. Kuendelea na ujenzi wa eneo la kuhudumia na kuhifadhia shehena eneo la Kurasini;
iii. Kuendelea na ujenzi wa Reli ya SGR pamoja na maboresho ya mtandao uliopo wa reli ya MGR na CGR ya reli ya TAZARA ndani ya Bandari ya Dar es Salaam;
iv. Kuimarisha mifumo ya Reli kuanzia Bandari ya Dar es Salaam kuelekea Bandari za Maziwa Makuu. Baadhi ya hatua ambazo zitatekelezwa ni kufungamanisha bandari zilizopo katika Maziwa Makuu nchini na bandari za nchi jirani tunazozihudumia;
v. Kuanza kutekeleza mkakati mahsusi wa kuongeza gati 10 na hivyo kufanya Bandari ya Dar es Salaam kuwa na gati 22 kutoka gati 12 za sasa;
vi. Kuanzisha utaratibu wa mizigo ya nje (Transit) kupelekwa moja kwa moja katika Bandari ya Kwala. Hivyo, Bandari Kavu ya Kwala itakuwa na huduma zote za kiforodha kwa kushirikiana na TRA na wadau wote muhimu katika kupokea na kusafirisha mizigo na kutoa huduma za moja kwa moja kutokea Kwala; na
vii. Kuendelea kuboresha bandari nchini ili kurahisisha biashara na nchi jirani ambapo, ujenzi wa Bandari ya Karema kwa upande wa Tanzania katika Ziwa Tanganyika umekamilika na uboreshaji wa Bandari ya Kigoma unaendelea. Vilevile, ujenzi wa meli nne (4) za mizigo zenye uwezo wa kubeba tani 2,000 kwa kila moja kupitia ubia baina ya TPA na Sekta Binafsi umeanza. Kwa upande wa DRC, uboreshaji wa Bandari ya Kalemie unaendelea. Maboresho hayo yatawezesha usafiri na usafirishaji wa shehena mbalimbali zikiwemo za madini kupitia bandari ya Kalemie itakayokuwa inahudumia usafirishaji wa madini kutoka migodi mikubwa ya madini iliyoko Mashariki mwa nchi ya DRC. Ujenzi wa meli hizi utakamilika ndani ya miaka miwili (2) na itakuwa kichocheo kikubwa cha biashara kati ya DRC na Tanzania kupitia

Bandari ya Kigoma katika Ziwa Tanganyika na Bandari ya Dar es Salaam.

238. ***Mheshimiwa Spika,*** ni wazi kuwa ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam pia utategemea uwepo wa mtandao imara wa reli inayounganisha bandari hii na zile za Maziwa Makuu. Ili kufikia lengo hilo, Serikali katika mwaka wa fedha 2025/26 itatekeleza mradi mkubwa wa takribani Shilingi bilioni 600 katika kuimarisha reli ya MGR pamoja na ujenzi wa kipande cha MGR kutoka Mpanda na kuunganisha Bandari ya Karema. Hatua nyingine ya kimkakati katika kuongeza uwezo wa bandari kuhudumia mizigo zaidi na kuifanya Tanzania kuwa Kitovu cha biashara na masoko ni kuanza utekelezaji wa Ujenzi wa Bandari ya kimkakati ya Bagamoyo. Bandari hii itakuwa mahsusi kwa ajili ya kuhudumia meli kubwa za kisasa (Post Panamax) ambazo kwa ukubwa wake haziwezi kuingia katika Bandari ya Dar es Salaam. Mradi wa ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo unalenga pia kuchochea shughuli za viwanda na biashara katika eneo la Ukanda Maalum wa Kiuchumi (Special Economic Zone) wa Bagamoyo. Serikali imekamilisha Upembuzi Yakinifu kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbegani – Bagamoyo. Bandari hii itaunganishwa na Reli ya Kisasa yenye urefu wa kilomita 100 kutoka Bandari Kavu ya Kwala.

239. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu mradi wa kuboresha Bandari ya Tanga wenye lengo la kuwezesha Bandari hiyo kuhudumia meli kubwa za makasha na mafuta. Kupitia mradi huu, Serikali itaendelea na shughuli za ujenzi wa Gati Na. 3 kwa ajili ya makasha na miundombinu ya kupokelea na kusafirisha mafuta katika eneo la Raskazone – Tanga. Vilevile, TPA itaendeleza eneo la Mwambani lenye ukubwa wa Hekta 174 ambapo kwa sasa sehemu ya eneo hilo linatumika kuhifadhia shehena mbalimbali ikiwemo shehena za magari. Sambamba na hilo, Serikali inaendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuchangamkia fursa za uwekezaji wa maghala na ICDs katika mkoa wa Tanga ili kuongeza ufanisi wa kuhudumia shehena.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** mradi wa uboreshaji wa Bandari ya Mtwara unalenga kuwezesha Bandari hiyo kuhudumia meli mbalimbali zikiwemo za shehena chafu (dirty cargo). Serikali

itaendelea na shughuli za: usanifu na ujenzi wa Bandari ya Kisiwa Mgao kwa ajili ya kuhudumia shehena chafu (dirty cargo) unaoweza kuchafua mazingira ikiwa ni pamoja na makaa ya mawe na saruji; ukarabati wa maeneo ya kuhudumia shehena; na ukarabati wa miundombinu ya barabara zinazoingia bandarini.

241. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu nchini, Serikali itaendelea na uboreshaji wa Bandari Kavu ya Kwala kwa awamu ya pili ambayo itahusisha ujenzi wa jengo la utawala, barabara za ndani, ghala na karakana. Aidha, Serikali kupitia TPA itahakikisha kuwa huduma zote za kibandari na kiforodha zinatolewa kwenye Bandari Kavu ya Kwala. Mpango huu utawezesha wateja kukamilisha taratibu zote za uhudumiaji wa shehena zao bila kufika Bandari ya Dar es salaam, hali itakayopunguza msongamano katika jiji la Dar es salaam. Vilevile, Serikali inatarajia kuanza ujenzi wa Bandari Kavu ya Ihumwa Dodoma baada ya kukamilika kwa Upembuzi Yakinifu wa Bandari hiyo unaoendelea kwa sasa ikiwa na lengo la kusogeza huduma kwa wateja na kupunguza msongamano katika barabara zinazoelekea Dar es Salaam na ndani ya Jiji hilo.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** kuhusu Bandari za Maziwa Makuu, Serikali itaendelea na uboreshaji wa bandari zilizopo katika Ziwa Victoria ambapo kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na usanifu na ujenzi wa Bandari za Bukoba, Mwanza South na Mwanza North ili kuboresha huduma na kuwezesha meli ya kisasa ya MV. Mwanza inayojengwa na Serikali kutia nanga na kutoa huduma. Aidha, kwa upande wa bandari zilizopo katika Ziwa Tanganyika kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na uboreshaji wa Bandari ya Kigoma kwa kujenga barabara za kiungo, *Cargo Shed*, ujenzi wa jengo la abiria (Passenger Wharf and Lounge).

243. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Ziwa Nyasa, Serikali itaendelea na ujenzi wa Bandari ya Mbamba Bay ambapo kazi zitakazotekelezwa ni kuendelea na ujenzi wa Bandari hiyo ili kuwezesha kuhudumia meli na shehena katika Bandari za Ziwa Nyasa pamoja na kwenda nchi jirani za Malawi na Msumbiji. Aidha, ili kuendelea kuboresha huduma za bandari nchini, Serikali itaendelea na uboreshaji wa miundombinu, ununuzi wa mitambo

na vifaa mbalimbali vitakavyotumika kwa lengo la kuwezesha kuongoza meli na kuhudumia shehena bandarini.

244. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA itaendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika kuendeleza na kuendesha sekta ndogo ya bandari nchini. Lengo ni kuongeza tija katika utendaji wa bandari ili kuifanya ichangie zaidi katika ukuaji wa uchumi na kuipunguzia Serikali gharama za uwekezaji na uendeshaji wa bandari nchini.

HUDUMA ZA USAFIRI KWA NJIA YA RELI

245. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Shirika la Reli Tanzania (TRC) inatarajia kukusanya **Shilingi bilioni 243.28** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani kwa kusafirisha tani 467,200 za mizigo katika reli ya MGR, tani 500,000 za reli ya SGR, abiria 552,038 wa masafa marefu kwa reli ya MGR, abiria 3,067,200 kwa reli ya mjini na abiria 3,046,320 kwa reli ya SGR. Kazi nyingine zitakazotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kuendelea kukarabati na kuimarisha miundombinu ya reli, majengo ya karakana, stesheni na kambi za wafanyakazi;
ii. Kuhakikisha usalama wa huduma za usafiri wa treni kwa kufunga mifumo mbalimbali ikiwemo mfumo wa ufuatiliaji mizigo (cargo tracking system);
iii. Kuhakikisha ulinzi wa mizigo ya wateja kuanzia sehemu ya kupakia hadi kituo cha mwisho;
iv. Kuendelea kutoa huduma za usafiri kwa njia ya reli jijini Dar es Salaam kwa lengo la kupunguza msongamano;
v. Kuendelea kuwezesha Chuo cha Reli kutoa mafunzo ya reli katika kampasi zote za Tabora na Morogoro; na
vi. Kujenga uwezo wa rasilimaliwatu kupitia mafunzo na ajira.

246. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na kazi hizo, Serikali imeendelea kutekeleza uendelezaji wa reli nchini katika maeneo mbalimbali na kwa sasa imefanikiwa kupata fedha kwa vipande vyote vya SGR kuanzia kipande cha kwanza (Lot 1) hadi kipande cha saba (Lot 7). Pamoja na kuendelea kwa utekelezaji wa vipande hivyo, katika mwaka 2025/26, Serikali itaendelea na ujenzi wa SGR kwa kuunganisha mikoa ya Kaskazini. Reli hiyo inaanzia Shinyanga kwenye kipande cha tano (Lot 5) cha Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa reli ya kati ambayo inajengwa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza. Reli hiyo itakayojengwa itaunganisha mikoa ya

Kaskazini kutokea Shinyanga na kupitia katika mikoa ya Simiyu, Singida, Manyara, Arusha, Kilimanjaro na hadi kufikia bandari ya Mwambani Jijini Tanga. Pia reli hiyo ina kipande cha kutoka Arusha hadi Bandari ya Musoma. Kupitia mradi huu, maeneo mengine yenye utajiri mkubwa wa madini muhimu ya kiuchumi yatakayounganishwa na reli hiyo ni pamoja na: eneo la Dutwa lenye Madini ya Kimkakati yakiwemo Nickel na Cobalt; eneo la Minjingu lenye madini ya Phosphate; eneo la Engaruka lenye malighafi za Viwanda vya kisasa vinavyotumia Sodium Carbonate na Magadi Soda; na eneo la Same na Makanya lenye madini ya Gypsum, Limestone, Ceramics na Bauxites. Kukamilika kwa reli hii kutawezesha kuunganisha Bandari za Tanga na Musoma na nchi ya Uganda. Aidha, reli hii itaunganisha Bandari ya Tanga na Bandari Kavu ya Isaka. Mpango wa Serikali ni kutumia utaratibu wa uwekezaji kwa kushirikisha Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP).

247. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na mikakati hiyo ya reli katika Mikoa ya Kaskazini na kufuatia makubaliano ya kuifufua Reli ya TAZARA na ujenzi unaoendelea wa Bandari mpya ya Mtwara na Mbamba Bay. Serikali pia, itaendelea na utekelezaji wa ujenzi wa Reli kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay kwa kiwango cha SGR. Reli hii ina umuhimu katika kuunganisha maeneo ya kiuchumi ya Liganga na Mchuchuma yenye utajiri mkubwa wa chuma na Makaa ya Mawe. Pia, reli hii inapita na kuunganisha maeneo yenye utajiri mkubwa wa mazao ya nafaka.

248. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia TAZARA inatarajia kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 83.23** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kusafirisha tani 250,000 za mizigo;
ii. Kusafirisha abiria 385,000 kwa upande wa safari ndefu na abiria 280,000 kwa treni ya Udzungwa inayosafiri kati ya stesheni za Kidatu na Makambako (km 365) na abiria 2,465,000 wa treni ya jijini Dar es Salaam (Commuter Train);
iii. Kufanya matengenezo kinga ya injini 12, mabehewa 783 ya mizigo na 54 ya abiria; na

iv. Kuendelea kukarabati na kuimarisha miundombinu ya reli, hususan maeneo yaliyowekewa ukomo wa mwendokasi ili kuleta ufanisi katika utendaji.

HUDUMA KATIKA MAZIWA MAKUU

249. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Kampuni ya Meli Tanzania (TASHICO) imelenga kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 17.64** kutokana na utoaji wa huduma ya kusafirisha abiria na mizigo katika Maziwa Makuu. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kusafirisha abiria 349,504 kwa kutumia meli zilizopo katika Maziwa Makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa;
ii. Kusafirisha mizigo tani 196,036 kwa kutumia meli ya mizigo ya MV. Umoja na meli nyingine za mizigo na abiria; na
iii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi wa Kampuni ili kuongeza ufanisi katika utendaji.

HUDUMA ZA VIWANJA VYA NDEGE

250. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) imeweka lengo la kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi bilioni 220.44** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani vya TAA. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 ni pamoja na: -

i. Kuendelea kuhudumia viwanja vya ndege vya Serikali nchini kwa kufanya matengenezo ya miundombinu na kusimamia shughuli za uendeshaji;
ii. Kuhudumia jumla ya abiria 6,073,213 na tani za mizigo 37,085 kupitia viwanja vya ndege vya Serikali;
iii. Kuendelea na ununuzi na ufungaji wa mashine za kisasa za ukaguzi wa abiria na mizigo katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA, Tabora, Iringa na Lake Manyara;
iv. Kukamilisha ufungaji wa Mifumo ya kielektroniki ya kuhudumia abiria katika Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Iringa, Mtwara na Tabora;
v. Kuendelea kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuwaongezea ujuzi na weledi katika utendaji wao wa kazi katika viwanja vya ndege;
vi. Kuboresha matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuongeza ukusanyaji wa mapato; na

vii. Kuendelea na zoezi la upimaji na upatikanaji wa Hati Miliki za Viwanja vya Ndege vya Serikali.

251. ***Mheshimiwa Spika,*** Sekta ya Usafiri wa Anga ni miongoni mwa maeneo mahsusi ambayo yataendelea kutekelezwa katika mwaka 2025/26 ikiwa ni pamoja na: kuendelea na kasi ya ujenzi wa Viwanja vya Ndege vya kimkakati ambavyo vitakuwa na mchango wa moja kwa moja katika kuimarisha na kuchochea shughuli za uchumi na maendeleo ikiwemo: ujenzi wa Kiwanja cha kisasa cha Ndege cha Kimataifa cha Serengeti kwa ajili ya kuchochea shughuli za sekta ya Utalii. Eneo hilo lina fursa kubwa ya uwekezaji katika Hoteli za kuanzia Nyota saba (7), kambi za utalii pamoja na njia maarufu ya uhamaji wa Wanyamapori. Pia, Serikali itaanza taratibu za ujenzi wa kiwanja cha kimkakati cha Njombe ambacho ni mahsusi kwa ajili ya mizigo ya bidhaa zinazoharibika haraka kama vile Parachichi, Maua, Nyama, Matunda na Mbogamboga. Vilevile, kiwanja hicho kitavutia Sekta ya Utalii katika Mkoa wa Njombe kutokana na uwepo wa hifadhi ya Kitulo. Kiwanja kingine kinachotarajiwa kujengwa ni Kiwanja cha ndege kipya mkoani Kagera, katika eneo la Kyabajwa wilayani Misenyi. Kiwanja hicho cha kisasa kimelengwa kutatua changamoto iliyopo ya kiwanja cha ndege cha Bukoba. Kiwanja hiki, kitasaidia katika kutumia fursa ya Mkoa huo kuwa kiunganishi kwa nchi za Uganda, Rwanda, DRC, Burundi na Sudan ya Kusini. Pia, Mkoa huo una fursa kubwa ya shughuli za kiuchumi na utalii ikiwemo uzalishaji wa mazao yanayoharibika ndani ya muda mfupi ikiwemo Samaki, Nyama na Senene.

HUDUMA ZA USAFIRI WA ANGA

252. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia ATCL imeweka lengo la kukusanya jumla ya mapato ya **Shilingi trilioni 1.08** kutoka katika vyanzo vya mapato vya ndani vya ATCL. Mapato hayo yanatokana na huduma za kusafirisha abiria na mizigo ndani na nje ya nchi. Kazi zitakazotekelezwa katika mwaka wa fedha 2025/26 ni pamoja na:-

i. Kusafirisha abiria 1,738,380 katika vituo 31 ndani na nje ya Tanzania, vikijumuisha vituo 16 vya ndani ya nchi, ambavyo ni Arusha, Bukoba, Dar es salaam, Dodoma, Geita, Mtwara, Kigoma, Kilimanjaro, Mbeya, Mwanza,

Mpanda, Iringa, Songea, Tabora, Seronera na Zanzibar; vituo 12 vya kikanda vikiwemo Bujumbura, Entebbe, Hahaya, Harare, Johannesburg, Lubumbashi, Lusaka, Nairobi, Kinshasa, Lagos, Goma na Ndola; na vituo vitatu (3) vya kimataifa ambavyo ni Dubai, Guangzhou, na Mumbai;

ii. Kusafirisha tani 14,940 za mizigo kwa ratiba maalum kwa kutumia ndege ya mizigo aina ya Boeing 767-300F katika vituo vya Sharjah (Umoja wa Nchi za Falme za Kiarabu), Guangzhou (China) Mumbai (India), na Nairobi (Kenya). Pia, ATCL itaendelea kusafirisha mizigo kwa safari zisizo na ratiba maalum kwa kuzingatia mahitaji ya soko;

iii. Kutoa mafunzo kwa marubani na wahandisi ndege pamoja na kuajiri na kuwapandisha madaraja marubani ambao wako kwenye hatua mbalimbali za mafunzo maalum (type rating and initial training) kwa aina mbalimbali za ndege;

iv. Kufanya matengenezo ya ndege ya ratiba maalum pamoja na matengenezo mengine yatakayohitajika;

v. Kuendelea kuboresha viwango vya ubora na usalama katika safari zake zote; na

vi. Kugharamia matangazo, mifumo ya mauzo na uendeshaji, mshahara na michango mbalimbali ya kisheria.

HUDUMA ZA USAFIRISHAJI MAJINI

253. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/26, Serikali kupitia Kampuni inayomilikiwa kwa Ubia kati ya Tanzania na China (SINOTASHIP), imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 20.60** kutokana na vyanzo vya mapato vya ndani ikiwa ni pamoja na huduma ya usafirishaji wa mizigo katika masafa marefu kwa njia ya bahari na huduma ya uwakala wa meli. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuendelea kutoa huduma ya usafirishaji wa mizigo kutoka tani 615,375 mwaka 2024 hadi kufikia tani 620,000 ifikapo Juni 2025;

ii. Kuendelea kuongeza makasha kutoka makasha 81,993 mwaka 2024 hadi kufikia makasha 85,000 mwaka 2025; na

iii. Kushirikiana na taasisi za fedha za ndani na nje ya nchi ili kufanikisha kupata fedha kwa ajili ya kununua meli ya kubeba

mizigo (general cargo vessel) itakayokuwa na uwezo wa kubeba tani 34,000 kwa wakati mmoja na itafanya safari kati ya China na Tanzania.

C.2.3. VYUO VYA MAFUNZO VYA KISEKTA

254. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwa na rasilimali yenye ujuzi wa kutosha na kupunguza gharama za kusomesha wataalam nje ya nchi, Serikali kupitia Wizara itaendelea kutekeleza maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kama ilivyobainishwa katika Ibara ya 59(i) kwa kuboresha na kuvijengea uwezo vyuo vya mafunzo vya kisekta. Vyuo hivyo vya kisekta vinajumuisha Chuo cha Taifa cha Usafirishaji, Chuo cha Bahari cha Dar es Salaam, Chuo cha Usafiri wa Anga, Chuo cha Bandari, Chuo cha Teknolojia ya Reli na Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa.

Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

255. ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia NIT imeweka lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 33.9** kutoka katika vyanzo vya mapato ya ndani yatokanayo na utoaji wa mafunzo, tafiti na ushauri wa kitaalam. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na: -

i. Kuongeza udahili wa wanafunzi wa kozi ndefu kutoka wanafunzi 16,131 hadi wanafunzi 18,320;
ii. Kuendelea na ujenzi wa majengo ya NIT Kampasi ya Lindi kwa ajili ya kuzalisha Nguvukazi Mahiri na kujenga uwezo wa kiteknolojia katika sekta ya usafiri majini, mafuta na gesi;
iii. Ujenzi wa *Aircraft Maintenance Practice Shade, Live Engine Installation Room, Staff Canteen, Civil Laboratory (Phase III)*, ukarabati wa majengo ya Chuo na barabara za ndani kwa kiwango cha lami katika Kampasi ya Mabibo – Dar es Salaam pamoja na ujenzi wa Karakana ya Matengenezo ya Ndege katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa Kilimanjaro (KIA);
iv. Ununuzi wa vifaa vya mafunzo, mafuta ya ndege na vilainishi kwa ajili ya ndege za mafunzo ya urubani pamoja na kukamilisha ununuzi wa samani na vifaa vya kuzimia moto kwa ajili ya majengo mapya yanayojengwa na Chuo;
v. Kuimarisha mafunzo na huduma katika Sekta ya Uchukuzi na nyanja shirikishi ikiwa ni pamoja na uandaaji wa mitaala

mipya na uhuishwaji wa mitaala iliyopo ya kozi ndefu na fupi pamoja na miongozo ya kufundishia (training manuals);

vi. Ununuzi wa ardhi katika Jiji la Dodoma kwa ajili ya upanuzi wa huduma zinazotolewa na Chuo kwa wananchi; na

vii. Kuendelea kuwajengea uwezo watumishi kupitia, mafunzo ya muda mrefu na mfupi, mafunzo ya vitendo, ziara za kitaaluma na kubadilishana wakufunzi na vyuo vya nje ya nchi kupitia mikataba ya makubaliano (MoUs).

Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

256. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka wa fedha 2025/26, Chuo cha Bahari Dar es Salaam kitakusanya **Shilingi bilioni 18.46** kutoka katika vyanzo vyake vya mapato ya ndani. Kazi zitakazotekelezwa ni pamoja na:-

i. Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Chuo katika maeneo ya Kigamboni – Kimbiji, Lindi – Kikwetu, Kiparang'anda - Mkuranga na upatikanaji wa vifaa vya Mafunzo;

ii. Kuongeza udahili kufikia wanafunzi 14,821 ambapo kati yao wanafunzi 6,821 ni wa kozi ndefu na wanafunzi 8,000 ni wa kozi fupi;

iii. Kufanya kongamano moja (1) la kitaaluma la Kimataifa kuhusu Uchumi wa Buluu;

iv. Kuboresha shughuli za kitafiti na utoaji wa huduma za ushauri wa kitaalam;

v. Kuimarisha vyanzo vya mapato ili kutekeleza shughuli za chuo ikiwemo miradi ya maendeleo; na

vi. Kuboresha mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi wa utendaji wa Chuo ikiwemo uanzishwaji wa mafunzo kwa njia ya Mtandao (e - Learning).

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Chuo cha DMI kitakuwa mwenyeji wa Kongamano kubwa la Kimataifa la Uchumi wa Buluu litakalofanyika mwaka wa fedha 2025/26. Kongamano hili litajadili mchango wa Sekta za Uchumi wa Buluu ikiwemo Sekta ya Uchukuzi katika ukuaji wa uchumi wa nchi na kuchochea uwekezaji.

Chuo cha Usafiri wa Anga

258. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TCAA katika mwaka wa fedha 2025/26 itaendelea kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali zinazohusiana na masuala ya usafiri wa anga kupitia Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC). Chuo hiki kinatarajia kudahili wanafunzi 2,500 na kuandaa kozi mpya nne (4).

Chuo cha Bandari

259. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali kupitia TPA katika mwaka wa fedha 2025/26 itaendelea kutoa mafunzo katika kozi mbalimbali zinazohusiana na kuhudumia mizigo katika bandari nchini kupitia Chuo cha Bandari. Aidha, Chuo hiki kinatarajia kudahili wanafunzi 1,175.

Chuo cha Teknolojia ya Reli

260. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Chuo cha Teknolojia ya Reli kitaendelea kutoa mafunzo ya reli katika kampasi zake za Tabora na Morogoro. Aidha, Chuo kinatarajia kudahili wanafunzi 760. **Chuo cha Taifa cha Hali ya Hewa**

261. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali kupitia Chuo cha Hali ya Hewa itaendelea kutoa mafunzo ya hali ya hewa na TEHAMA katika ngazi ya awali na Diploma kwa wanafunzi wa kutoka ndani na nje ya nchi. Aidha, Chuo kitaendelea kuboresha mazingira ya ufundishaji ikiwa ni pamoja na kukamilisha ununuzi wa vifaa vya kisasa vya kufundishia na kuendelea na kazi ya usanifu wa mabweni na jengo la utawala katika Chuo hicho.

**C.2.4: MASUALA YA KISERA NA MTAMBUKA**

Sera, Sheria na Kanuni za Kisekta

262. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuendelea kuboresha zaidi utoaji wa huduma za uchukuzi, katika mwaka wa fedha 2025/26, hadi kufikia Desemba 2025 Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wake. Sera hii inalenga kuzingatia mahitaji ya sasa, maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuiwezesha Sekta ya Uchukuzi kuchochea maendeleo ya sekta nyingine muhimu ikiwemo Kilimo, Madini, Viwanda na Utalii.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na upungufu uliopo katika Usimamizi wa bandari na udhibiti wa usafiri ardhini, katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali itaendelea na taratibu za kufanya marekebisho ya Sheria ya Bandari Sura ya 166 na Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini Sura ya 413 ambazo zote zipo kwenye maandalizi ya kuletwa katika Bunge lako Tukufu kwa hatua zaidi. Aidha, Wizara itaendelea kukamilisha taratibu za utungwaji wa Kanuni za Udhibiti Usafiri wa Waya (Cable Transport Regulations) ili kuwezesha Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri Ardhini (LATRA) kuanza kutekeleza shughuli za udhibiti wa usafiri huo ambao unakusudiwa kuchochea na kukuza shughuli za utalii nchini. Aidha, Serikali itaendelea kuridhia Itifaki na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa inayolenga kuimarisha utoaji wa huduma za Uchukuzi ndani na nje ya nchi. **Ufuatiliaji na Tathmini**

264. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Uchukuzi ni miongoni mwa Wizara ndani ya Serikali zinazotekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati. Katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara itaendelea kuimarisha utaratibu na mifumo ya ufuatiliaji na tathmini kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miradi hiyo inatekelezwa ipasavyo na kwa wakati. Pamoja na miradi hiyo, Wizara itafuatilia kwa karibu utendaji wa Taasisi zilizo chini yake kupitia Mikataba ya Utendaji iliyosainiwa kwa mwaka 2025/26 ili ziwe na ufanisi katika kutoa huduma stahiki kwa Watanzania. **Mifumo ya TEHAMA**

265. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, katika kuunga mkono kauli mbiu ya Serikali ya kidigitali, Wizara ya Uchukuzi itaendelea kusimamia na kuratibu matumizi salama, bora na sahihi ya TEHAMA ili kuongeza uwajibikaji na kuboresha utoaji wa huduma bora na haraka kwa wananchi. Aidha, Wizara ya Uchukuzi itahakikisha mifumo ya TEHAMA inayotarajiwa kujengwa na Taasisi zilizo chini yake inaunganishwa na inabadilishana taarifa na mifumo ya Taasisi zingine za Umma na Binafsi.

Kuongeza Upatikanaji wa Fedha za Kigeni

266. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2025/26, Wizara ya Uchukuzi na Taasisi zake itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni nchini na kupunguza matumizi ya fedha hizo.

Kupitia mikakati hiyo, katika kipindi hicho Wizara inatarajia kukusanya fedha za kigeni jumla ya **Dola za Marekani milioni 792.24** sawa na ongezeko la **asilimia 3.91** ikilinganishwa na **Dola za Marekani milioni 762.41** zilizopangwa kukusanywa kwa mwaka wa fedha 2024/25. Mikakati itakayotekelezwa ya kuongeza fedha za kigeni ni pamoja na: -

i. Kuendelea kushirikisha Sekta Binafsi katika uendeshaji na uendelezaji wa shughuli za Uchukuzi nchini zikiwemo za bandari;
ii. Kuimarisha uunganishaji wa njia ya reli na barabara katika maeneo mbalimbali ikiwemo bandari ya Kwala ili kuwezesha nchi jirani zilizopewa maeneo kuwekeza na kuanza kutumia bandari kavu ya Kwala;
iii. Kujenga miundombinu wezeshi kwa ajili ya kupokelea na kuhifadhi mafuta (Single receiving terminal) yanayoagizwa na nchi jirani;
iv. Kuendelea kutekeleza mikakati ya kukuza soko la usafirishaji wa mizigo nje ya nchi kupitia ATCL kwa kujitangaza ndani na nje ya nchi;
v. Kuboresha viwanja vya ndege ili viweze kuhudumia ndege kwa saa 24 kwa kuweka miundombinu mbalimbali ikiwemo kuweka taa za kuongozea ndege katika viwanja husika;
vi. Kuboresha miundombinu ya reli iliyopo na kukamilisha ujenzi wa reli ya kisasa ya SGR;
vii. Kukarabati na kujenga meli katika Maziwa Makuu na kuwezesha kuhudumia nchi jirani zinazozunguka Maziwa Makuu hayo;
viii. Kukamilisha ukarabati wa karakana za ndege katika viwanja vya ndege vya Kimataifa vya Kilimanjaro - KIA (KIMAFA) na JNIA ili matengenezo madogo ya ndege yafanyike ndani ya nchi na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni;
ix. Kuanza mafunzo ya urubani ndani ya nchi ambapo kupitia Chuo cha NIT, Serikali inaendelea na taratibu za kuanza mafunzo hayo ambapo mikataba ya wakufunzi wawili (2) wa Urubani wenye uzoefu wa kutosha tayari imesainiwa; na
x. Kuendelea kuboresha miundombinu na vifaa vya kufundishia katika vyuo vya mafunzo vya kisekta ili kuwavutia wanafunzi wa kigeni kuja nchini kwa wingi zaidi.

Rasilimaliwatu na Maendeleo ya Watumishi

267. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara na Taasisi zake itaendelea kutekeleza Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji awamu ya Nne (4) unatekelezwa kwa kipindi cha miaka saba (7) kuanzia mwaka wa Fedha 2023/24 hadi 2029/30. Mkakati huo una lengo la kuwa na jamii iliyostawi na yenye mifumo madhubuti ya kukuza uadilifu na isiyovumilia rushwa. Kupitia mkakati huu, Wizara itaendelea kutoa mafunzo yanayohusu maadili, uadilifu na kuzuia vitendo vya rushwa kupitia semina na vikao mbalimbali vya wafanyakazi. Hivyo, natoa rai kwa Watumishi na Wananchi kwa ujumla kuendelea kutoa taarifa katika vyombo husika pale wanapohisi vitendo vya rushwa.

268. ***Mheshimiwa Spika,*** halikadhalika katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa Watumishi ili kujikinga na maambukizi mapya ya VVU ikiwemo kuhimiza upimaji wa hiari wa VVU na magonjwa mengine yasiyoambukiza; na ushiriki wa watumishi kwenye mazoezi ya viungo kupitia bonanza, michezo ya Mei Mosi na SHIMIWI kama njia mojawapo ya kuimarisha afya na uhusiano baina ya watumishi katika mahala pa kazi.

Utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa dhidi ya Rushwa

269. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Serikali itaendelea kuwajengea uwezo Watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa lengo la kuwaongezea ujuzi na weledi katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku. Vilevile, Wizara inatarajia kuwajengea uwezo Watumishi katika kutumia Mfumo wa Usimamizi na ufuatiliaji wa masuala ya Kiutumishi na Ajira (Human Resource Management and Audit System) katika miradi ya maendeleo inayotekelezwa na Wizara. Lengo la hatua hii ni kuhakikisha kuwa taarifa za kiutumishi na ajira katika miradi ya maendeleo zinapatikana ili kuwezesha Wizara kutambua mchango wa miradi hiyo katika kukuza ajira nchini.

D: SHUKRANI

270. ***Mheshimiwa Spika,*** katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2024/25, Wizara imefanikiwa kwa kiasi kikubwa

kutekeleza majukumu yake na kufikia malengo yaliyokusudiwa katika Kipindi husika. Matokeo hayo yamepatikana kutokana na ushirikiano wa wadau wa Sekta ya Uchukuzi wa ndani na nje ya Wizara, wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Wananchi kwa ujumla. Naomba nitumie fursa hii kuwashukuru wadau wote waliotoa michango mbalimbali ya hali na mali na wale walioshiriki moja kwa moja katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Wizara. Shukrani za kipekee ninaziwasilisha kwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa ushauri na michango yao ambayo imewezesha Wizara kuimarisha utendaji katika kutoa huduma za uchukuzi kwa Umma.

271. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatambua juhudi za Waheshimiwa Wabunge zilizowezesha Sekta ya Uchukuzi kuongeza mchango wake wa kuchochea ukuaji wa uchumi ikiwemo kuanza kwa uendeshaji wa reli ya SGR. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge muendelee kuishauri Serikali katika utekelezaji wa masuala mbalimbali, hususan yanayogusa maendeleo ya wananchi moja kwa moja. Aidha, niwaombe wananchi na wadau wengine kuendelea kutoa michango yao ya hali na mali katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo pamoja na kuendelea kushirikiana na Serikali katika kulinda miundombinu ya usafiri na usafirishaji ambayo Serikali imekuwa ikitumia kiasi kikubwa cha fedha za Umma kuijenga, kuitunza na katika uendeshaji wake.

272. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba pia nitumie nafasi hii kuwapongeza na kutambua michango inayotolewa na viongozi wanaonisaidia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, kwa kuanza na Naibu Waziri, Mheshimiwa **David Mwakiposa Kihenzile** (Mb.); Katibu Mkuu, **Prof. Godius Walter Kahyarara** na Naibu Katibu Mkuu **Bw. Ludovick James Nduhiye**. Halikadhalika, napenda kuishukuru Menejimenti ya Wizara, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara na Watumishi wote wa Wizara na Taasisi kwa jitihada zao katika utekelezaji wa Majukumu ya Wizara na Taifa kwa ujumla.

273. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii adhimu, kwa niaba ya Wizara kutoa shukrani na kuwatambua wadau wote wa Wizara ikiwa ni pamoja na Washirika wa Maendeleo ambao

wamechangia rasilimali fedha katika utekelezaji wa Programu, Miradi na Mipango mbalimbali ya Wizara. Kwa namna ya kipekee niruhusu niwatambue wafuatao: Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini (IMO); Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Anga (ICAO); Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); Benki ya Dunia (WB); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japan (JICA); Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Korea Kusini (KOICA); Ujerumani (KfW); Foreign Commonwealth and Development Office (FCDO); Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD); Jumuiya ya Umoja wa Ulaya (EU); Benki ya Uwekezaji ya Ulaya (EIB); Shirika la Chakula Duniani (WFP); Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID); Trade Mark Africa; Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Sekretarieti ya Jumuiya ya Nchi za Kusini mwa Afrika - SADC; Nchi za Urusi; Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE); Uingereza; Marekani; Uholanzi; Japan; India; China; Denmark; Korea Kusini; Ufaransa; Ubelgiji; Ujerumani na Uturuki; Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ya NSSF na PSSSF; Taasisi za fedha za CRDB, NMB, AZANIA BANK, NBC na TCB na Asasi mbalimbali za kiraia; Sekta Binafsi pamoja na wadau wengine wengi ambao sikuwataja hapa si kwa sababu ya umuhimu wao bali ni kutokana na wingi wao.

274. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee kabisa naomba uniruhusu nitoe shukrani zangu za dhati kwako wewe binafsi Mhe. Spika, Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote kwa kunisikiliza.

## E: MUHTASARI WA MAOMBI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUKUZI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2025/26

275. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2025/26, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,746,485,018,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 125,438,950,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,621,046,068,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

276. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Hotuba hii, nimeambatisha majedwali mbalimbali yenye taarifa na takwimu kwa ajili ya kutoa uelewa zaidi kwa Waheshimiwa Wabunge na Watanzania

kwa ujumla kuhusu utendaji wa Sekta ya Uchukuzi. Naomba majedwali hayo yachukuliwe kama sehemu ya hotuba yangu. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara (**www.uchukuzi.go.tz**).

277. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja.

F: MAJEDWALI YENYE TAARIFA NA TAKWIMU MBALIMBALI ZA WIZARA

**Jedwali Na. 1:** Orodha ya miradi ya maendeleo na kiasi cha fedha kilichotengwa kwa mwaka wa fedha 2025/26

| MRADI NA. | JINA LA MRADI | BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26 | | | CHANZO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | JUMLA | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | |
| **KIFUNGU 1003: SERA NA MIPANGO** | | | | | |
| 4201 | Multinational Lake Victoria Maritime Communications and Transport Project | - | 833,215,000 | 833,215,000 | AfDB |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4227 | Dar es Salaam Maritime Gateway Project (DMGP) | - | 24,081,834,000 | 24,081,834,000 | WB |
| 4209 | Construction of Mwanza Airport | 13,800,000,000 | - | 13,800,000,000 | GoT |
| 4210 | Construction of Arusha Airport | 4,575,289,122 | - | 4,575,289,122 | GoT |
| 4220 | Construction of Mtwara Airport | 6,570,000,000 | - | 6,570,000,000 | GoT |
| 4224 | Rehabilitation of Kilimanjaro | 35,000,000,000 | - | 35,000,000,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | International Airport (KIA) | | | | |

| MRADI NA. | JINA LA MRADI | BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26 | | | CHANZO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | JUMLA | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | |
| 4226 | Development of Regional Airports (Moshi, Lindi, Njombe, Musoma, Shinyanga, Sumbawanga | 20,596,800,000 | - | 20,596,800,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | na Singida) | | | | |
| 4237 | Construction of Serengeti Airport | 3,000,000,000 | - | 3,000,000,000 | GoT |
| 4287 | Construction of Bukoba Airport | 1,900,000,000 | - | 1,900,000,000 | GoT |
| 4299 | Modernization and Expansion of Julius Nyerere International Airport | 5,947,200,000 | 80,128,165,600 | 86,075,365,600 | GoT & AFD |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Terminal Building II | | | | |
| | Construction of Presidential Pavilion | 2,000,000,000 | - | 2,000,000,000 | GoT |
| | **Institutional Support** | | | | |
| 6267 | Operationalizati on of TB III JNIA | 15,300,000,000 | - | 15,300,000,000 | GoT |

| MRADI NA. | JINA LA MRADI | BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26 | | | CHANZO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA | FEDHA ZA | JUMLA | |

| | | NDANI | NJE | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | |
| | TAA - Compensation of PAPs at Airports | 15,000,000,000 | | 15,000,000,000 | GoT |
| | TAA - Technology Assesment for TAA'S Airports | - | 4,332,720,000 | 4,332,720,000 | USTDA |
| | Operational aziti on of Msalato Inter. Airport | 2,000,000,000 | | 2,000,000,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Dar Es Salaam Maritime Institute | 1,097,670,878 | - | 1,097,670,878 | GoT |
| **JUMLA NDOGO 1003** | | **126,786,960,000** | **109,375,934,600** | **236,162,894,600** | |
| **KIFUNGU 2005: MIUNDOMBINU YA UCHUKUZI** | | | | | |
| 4213 | Railway Infrastructure Funds | 294,801,622,000 | - | 294,801,622,000 | GoT |
| 4216 | Tanzania Intermodal Railway Project – TIRP II | - | 51,281,048,000 | 51,281,048,000 | WB |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4281 | Construction of New Standard Gauge Railway SGR | 1,511,000,000,000 | - | 1,511,000,000,000 | GoT |

| MRADI NA. | JINA LA MRADI | BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26 | | | CHANZO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | JUMLA | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | |
| JUMLA NDOGO 2005 | | 1,805,801,622,000 | 51,281,048,000 | 1,857,082,670,000 | |
| KIFUNGU 2006: HUDUMA ZA UCHUKUZI | | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4211 | Rail Rehabilitation and SBU Improvement for TAZARA | 12,323,862,000 | - | 12,323,862,000 | GoT |
| 4290 | TMA Radar, Equipment and Infrastructure | 13,500,000,000 | - | 13,500,000,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | TMA – Enhancing Resielence of Coastal Communities Towards Sustainable Fisheries and Healthy Marine Environment (ECOFISH) | - | 1,995,115,000 | 1,995,115,000 | DENMARK |
| 4238 | Enhancing Meteorological | - | 2,177,688,000 | 2,177,688,000 | WMO |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Observation and Data Exchange | | | | |

| MRADI NA. | JINA LA MRADI | BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26 | | | CHANZO |
|---|---|---|---|---|---|
| | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | JUMLA | |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | |
| | in Tanzania through Systematic Observation Financing Facility - SOFF | | | | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 4294 | Acquisition of New Aircrafts - ATCL | 216,050,000,000 | - | 216,050,000,000 | GoT |
| 4236 | ATCL Operational and Infrastructure Improvement | 67,000,000,000 | - | 67,000,000,000 | GoT |
| 4295 | Procurement and Rehabilitation of Marine Vessels - | 171,000,000,000 | - | 171,000,000,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | TASHICO | | | | |
| 4298 | VHF (Navigation Aids) | 1,800,000,000 | - | 1,800,000,000 | GoT |
| 4202 | Development of Civil Aviation Centre | 20,880,000,000 | - | 20,880,000,000 | GoT |
| 4235 | Aviation Safety Technical Assistance | - | 3,703,838,400 | 3,703,838,400 | USTDA |

| **MRADI** | **JINA LA MRADI** | **BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA 2025/26** | **CHANZO** |
|---|---|---|---|

| NA. | | FEDHA ZA NDANI | FEDHA ZA NJE | JUMLA | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 (3+4) | |
| 6377 | Infrastructure Development and Training Equipment (NIT) | 8,370,000,000 | - | 8,370,000,000 | GoT |
| 4309 | East Africa Skills for Transformation and Regional | 2,500,000,000 | - | 2,500,000,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Integration Project (EASTRIP) - NIT | | | | |
| 4207 | Establishment of NIT Lindi Campus for Development of Skilled Workforce and Technology for Maritime, Oil and | 6,500,000,000 | - | 6,500,000,000 | GoT |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Gas Sectors at Kikwetu Lindi Municipality | | | | |
| **JUMLA NDOGO 2006** | | **519,923,862,000** | **7,876,641,400** | **527,800,503,400** | |
| **JUMLA KUU YA MAENDELEO (WIZARA- FUNGU 62)** | | **2,452,512,444,000** | **168,533,624,000** | **2,621,046,068,000** | |

**Jedwali Na. 2:** Orodha ya Viwanja vya Ndege vya Serikali Tanzania Bara

| **Na.** | **Jina la Kiwanja** | **Mahali Kilipo** | **Vipimo vya** | **Aina ya "Runway"** | **Hali ya Uendeshaji** |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | "Runway" (m) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Julius Nyerere | Dar es Salaam | 3000 x 60<br>1000 x 30 | Lami<br>Lami | Kinatoa huduma |
| 2. | Kilimanjaro | Kilimanjaro/Hai | 3600 x 45 | Lami | Kinatoa huduma |
| 3. | Mwanza | Mwanza | 3300 x 45 | Lami | Kinatoa huduma |
| 4. | Songwe | Mbeya | 3340 x 45 | Lami | Kinatoa huduma |
| 5. | Arusha | Arusha | 1860 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 6. | Mtwara | Mtwara | 2800 x 45 1158 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 7. | Kigoma | Kigoma | 1800 x 45 | Lami | Kinatoa huduma |

| Na. | Jina la Kiwanja | Mahali Kilipo | Vipimo vya "Runway" (m) | Aina ya "Runway" | Hali ya Uendeshaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 8. | Dodoma | Dodoma | 2750 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 9. | Tabora | Tabora | 1900 x 30<br>1260 x 23 | Lami | Kinatoa huduma |
| 10. | Tanga | Tanga | 1268 x 30<br>1385 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 11. | Mpanda | Mpanda | 2000 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 12. | Shinyanga | Shinyanga/ Ibadakuli | 2200 x 30 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 13. | Mafia | Kisiwa cha Mafia | 1500 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 14. | Bukoba | Bukoba | 1500 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 15. | Ziwa Manyara | Ziwa Manyara | 1220 x 23 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 16. | Lindi | Lindi/Kikwetu | 1609 x 46 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| | | | 1847 x 46<br>1383 x 46 | Nyasi/Zege<br>Nyasi | |
| 17. | Musoma | Musoma | 1600 x 30 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 18. | Songea | Songea | 1740 x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 19. | Mbeya | Mbeya | 1500 x 30 | Changarawe | Kimefungwa |
| 20. | Iringa | Iringa/Nduli | 2100x 30 | Lami | Kinatoa huduma |
| 21. | Sumbawanga | Sumbawanga | 1600 x 33 | Nyasi | Kinatoa huduma |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 22. | Ngara | Ngara | 1500 x 19 | Changarawe | Kinatoa huduma |

| Na. | Jina la Kiwanja | Mahali Kilipo | Vipimo vya “Runway” (m) | Aina ya “Runway” | Hali ya Uendeshaji |
|---|---|---|---|---|---|
| 23. | Moshi | Moshi | 1268 x 30<br>1480 x 30 | Lami Nyasi | Kinatoa huduma |
| 24. | Nachingwea | Nachingwea | 1793 x 40 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 25. | Kilwa Masoko | Kilwa | 1950 x 30 | Nyasi/ Changarawe | Kinatoa huduma |
| 26. | Kahama | Kahama, Shinyanga | 1530 x 30 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 27. | Ukerewe | Nansio, Ukerewe | 914 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 28. | Morogoro | Morogoro | 1068 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 29. | Manyoni | Manyoni, Singida | 1000 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 30. | Loliondo | Loliondo, Arusha | 1760 x 28 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 31. | Kibondo | Kibondo, Kigoma | 1189 x 40 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 32. | Kasulu | Kasulu, Kigoma | 1400 x 23 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 33. | Uvinza | Uvinza, Kigoma | 9 14 x 46 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 34. | Urambo | Urambo, Tabora | 1524 x 46 | Nyasi | Kinatoa |

| **Na.** | **Jina la Kiwanja** | **Mahali Kilipo** | **Vipimo vya** | **Aina ya "Runway"** | **Hali ya Uendeshaji** |
|---|---|---|---|---|---|

| | | | "Runway" (m) | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | huduma |
| 35. | Maswa | Maswa, Simiyu | 882 x 30 | Nyasi | Kimefungwa |
| 36. | Mombo | Mombo, Tanga | 1285 x 46 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 37. | Mkwaja | Mkwaja, Tanga | 1100 x40 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 38. | Utete | Utete, Pwani | 640 x 60 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 39. | Kilosa | Kilosa, Morogoro | 1154 x 46 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 40. | Ifakara | Ifakara, Morogoro | 1400 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 41. | Tunduru | Tunduru, Ruvuma | 1021 x 23 | Nyasi | Kimefungwa |

| **Na.** | **Jina la Kiwanja** | **Mahali Kilipo** | **Vipimo vya “Runway” (m)** | **Aina ya “Runway”** | **Hali ya Uendeshaji** |
|---|---|---|---|---|---|
| 42. | Liuli | Liuli, Ruvuma | 914 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 43. | Mbamba Bay | Mbamba Bay, Ruvuma | 640 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 44. | Chunya | Chunya, Mbeya | 1332 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 45. | Mafinga | Mafinga, Iringa | 1328 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 46. | Njombe | Njombe | 1890 x 30 | Nyasi | Kinatoa |
| | | | | | huduma |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 47. | Mufindi/Sao Hill | Mufindi, Iringa | 1000 x 40 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 48. | Mpwapwa | Mpwapwa, Dodoma | 674 x 30 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 49. | Mvumi | Mvumi, Dodoma | 914 x 20 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 50. | Kongwa | Kongwa, Dodoma | 1368 x 30 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| 51. | Kirondatal | Kirondatal, Singida | 1097 x 20 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 52. | Biharamulo | Biharamulo, Kagera | 935 x 18 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 53. | Inyonga | Inyonga, Katavi | 914 x 40 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 54. | West Kilimanjaro | Ngarenairobi, Kilimanjaro | 1237 x 37 | Nyasi | Kinatoa huduma |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 55. | Same | Same, Kilimanjaro | 1143 x 46 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 56. | Kondoa | Kondoa, Dodoma | 732 x 50 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 57. | Singida | Singida | 1070 x 30 | Changarawe | Kinatoa huduma |
| **Na.** | **Jina la Kiwanja** | **Mahali Kilipo** | **Vipimo vya "Runway" (m)** | **Aina ya "Runway"** | **Hali ya Uendeshaji** |
| 58. | Masasi | Masasi, Mtwara | 1273 x 40 | Nyasi | Kinatoa huduma |
| 59. | Geita | Nyabilezi, Chato, | 3000 x 45 | Lami | Kinatoa huduma |
| 60. | Liwale | Liwale, Mtwara | | Nyasi | Kimefungwa |
| 61. | Newala | Newala, | | Nyasi | Kimefungw |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | Mtwara | | | a |

**Jedwali Na. 3:** Mashirika ya Ndege yanayofanya Safari za Kimataifa katika Viwanja vya Ndege vya Kimataifa Nchini

**Jedwali Na. 3.1:** Orodha ya Mashirika ya Ndege yanayofanya safari katika Kiwanja cha Ndege cha JNIA

| Na. | SHIRIKA LA NDEGE | AINA YA NDEGE | KITUO | IDADI YA SAFARI KWA WIKI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Emirates (EK) | B773 | DXB | 7 |
| 2. | Air Mozambique™ | B737/E145 | POL APL MPM | 3 |
| 3. | Kenya Airways (KQ) | E190/B738 | NAIROBI | 28 |
| 4. | South African Airline (SA) | A320/A319 | JNB | 7 |
| 5. | Saudia Airline | A320 | JED | 0 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | (SV) | | | |
| 6. | Royal Dutch Air (KL) | B773/B781 | AMS | 7 |
| 7. | Ethiopian Airline (ET) | B738/B737/B787 | ADD | 21 |
| 8. | Qatar Airways (QR) | B787 | DOH | 10 |
| 9. | Air Tanzania Ltd (ATCL) (D) | DH8Q400/B738/ A220 | TKQ MBI ZNZ MWZ/BKZ JRO DOD IRI TBO MYW NPY SGX ARK | 73 |
| | Air Tanzania Ltd (ATCL) (I) | | JNB/HAH/EBB/BJM /LUN-HRE, BOM/CAN/NBO/NLA /DXB | 50 |
| **Na** | **SHIRIKA LA** | **AINA YA** | **KITUO** | **IDADI YA** |

| . | NDEGE | NDEGE | | SAFARI KWA WIKI |
|---|---|---|---|---|
| 10. | Precision Air (PW)DOM. | AT5/AT7 | MYW MWZ TBOTKQ JRO ARK ZNZ MUZ SEU KBH DOD | 40 |
| | Precision Air (PW) INTERN. | | NBO/EBB/HAH/AJN | 24 |
| 11. | EGYPT AIR (MS) | B738 | CAI | 3 |
| 12. | Rwanda Air (WB) | DH8 | KGL | 6 |
| 13. | Oman Air (WY) | B738 | ZNZ MCT | 4 |
| 14. | Turkish Air (TK) | B738/A330 | IST | 9 |
| 15. | Malawian (3W) | DH8 | BLZ/LLW | 7 |
| 16. | Fly Dubai (FZ) | B738 | DXB | 7 |
| 17. | AIR UGANDA (UR) | CRJ | EBB | 7 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 18. | AIR ZIMBABWE(UM) | A320 | HRE | 3 |
| 19. | ZAMBIA AIRWAYS(ZN) | B737 | LUN | 4 |
| 20. | AIR LINK (4Z035) | E190 | JNB | 8 |
| 21. | SKYWARD EXPRESS(OW) | F100 | NBO | 5 |

**Jedwali Na. 3.2:** Orodha ya Mashirika ya Ndege yanayofanya safari katika Kiwanja cha KIA

| Na. | SHIRIKA LA NDEGE | AINA YA NDEGE | KITUO | IDADI YA SAFARI KWA WIKI |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Air Tanzania (ATCL) | DH8Q400/B738/A220 | EBB, DAR, MWZ, ZNZ | 31 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 2. | Precision Air | ATR72, ATR72 | NBO, DAR, MWZ | 21 |
| 3. | Kenya Airways | E190 | NBO | 7 |
| 4. | Ethiopian Airline | A350/B787 | ADD | 11 |
| 5. | Qatar Airways | A330/B787 | DOH | 10 |
| 6. | Turkish Air | B737 | IST | 4 |
| 7. | RwandAir | CRJ 9 | KGL | 3 |
| 8. | Ugandan Airlines | CRJ 9 | EBB | 3 |
| 9. | Royal Dutch Air (KLM) | B787 | AMS | 6 |
| 10. | Air France | A350 | PARIS | 3 |
| 11. | Safari link | C208 | NBO | 7 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 12. | Euro wing Discover | A330 | ZRH | 2 |
| 13. | Edelweiss Air | A343 | ZRH | 2 |

**Jedwali Na. 3.3:** Orodha ya Viwanja vya Ndege vya Serikali vyenye Ratiba Maalum za Safari za Mashirika ya Ndege

| Na. | JINA LA KIWANJA | IDADI | MASHIRIKA YA NDEGE |
|---|---|---|---|
| 1. | JNIA | 23 | ATCL, Emirates, Air Mozambique, Kenya Airways, Saudia Airline, KLM, Ethiopian Airlines, Qatar airways, Precision air, Egyptair, RwandAir, Oman air, Turkish Airlines, Malawian Airlines, Fly Dubai, Ugandan |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | Airlines, Air France, Air Zimbabwe, Ewa, Flightlink,<br>Coastal Travels, Auric Air na Airlink |
| 2. | KIA | 13 | Kenya Airways, KLM, Ethiopian Airlines, Qatar airways,<br>RwandAir, Turkish Airlines, Ugandan Airlines, Air<br>Kenya Express, Safari link, Euro wing Discover,<br>Edelweiss Air, ATCL na Precision air |
| 3. | Mwanza | 3 | ATCL, Precision Air na Auric Air |
| 4. | Arusha | 3 | Precision Air, ATCL na Flightlink |
| 5. | Lake Manyara | 4 | Coastal Travels, Regional Air, Air Excel na Auric Air |
| 6. | Mtwara | 2 | Precision Air na ATCL |
| 7. | Kigoma | 1 | ATCL |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 8. | Tabora | 2 | ATCL na Precision Air |
| 9. | Mafia | 2 | Coastal Travels na Auric Air |
| 10. | Tanga | 1 | Auric Air |
| 11. | Songwe | 2 | ATCL na Precision Air |
| 12. | Bukoba | 2 | ATCL na Precision Air |
| 13. | Songea | 1 | ATCL |
| 14. | Iringa | 2 | Auric Air |
| **Na.** | **JINA LA KIWANJA** | **IDADI** | **MASHIRIKA YA NDEGE** |
| 15. | Dodoma | 3 | ATCL, Precision Air na Flight link |
| 16. | Kahama | 1 | Precision Air |
| 17. | Mpanda | 1 | ATCL |
| 18. | Geita | 1 | ATCL |

**Jedwali Na. 4:** Orodha ya Bandari rasmi zilizo katika Bahari ya Hindi

| Na. | JINA LA BANDARI | MAHALI/MKOA |
|---|---|---|
| **A. Bandari Kubwa** | | |
| 1. | Dar es Salaam | Dar es Salaam |
| 2. | Tanga | Tanga |
| 3. | Mtwara | Mtwara |
| **B. Bandari Ndogo** | | |
| 4. | Mbweni | Dar es Salaam |
| 5. | Kunduchi | Dar es Salaam |
| 6. | Bagamoyo | Pwani |
| 7. | Mafia | Pwani |
| 8. | Nyamisati | Pwani |
| 9. | Kisiju | Pwani |
| 10. | Kirongwe | Pwani |
| 11. | Tumbuju | Pwani |
| 12. | Kipumbwi | Tanga |

| | | |
|---|---|---|
| 13. | Pangani | Tanga |
| 14. | Mkwaja | Tanga |
| 15. | Sahare | Tanga |
| 16. | Korogwe | Tanga |
| 17. | Lindi | Lindi |
| 18. | Kilwa Masoko | Lindi |
| 19. | Songosongo | Lindi |
| 20. | Somanga | Lindi |
| 21. | Mikindani | Mtwara |
| **Na.** | **JINA LA BANDARI** | **MAHALI/MKOA** |
| 22. | Kilambo | Mtwara |
| 23. | Kilongwe | Mafia - Pwani |
| 24. | Kisiju | Pwani |
| 25. | Nyamisati | Pwani |
| 26. | Tumbuju | Pwani |
| 27. | Kilambo | Mtwara |

| | | |
|---|---|---|
| 28. | Sahare | Tanga |
| 29. | Mkwaja | Tanga |
| 30. | Kipumbwi | Tanga |
| 31. | Buyuni Kigamboni | Dar es Salaam |
| 32. | Bushungi | Lindi |
| 33. | Msimbati | Mtwara |
| 34. | Kisiwa Mgao | Mtwara |
| 35. | Hoima - Mradi wa mafuta Chongoleani | Tanga |
| 36. | Changwahela | Bagamoyo - Pwani |
| 37. | Bweni | Mafia - Pwani |
| 38. | Banja | Mafia - Pwani |
| **JUMLA YA BANDARI ZILIZO KATIKA BAHARI YA HINDI** | | **38** |

**Jedwali Na. 5:** Orodha ya Bandari rasmi zilizo katika Maziwa Makuu

| Na. | JINA LA BANDARI | MAHALI/MKOA |
|---|---|---|
| **A. Bandari Kubwa** | | |
| 1. | Mwanza South | Mwanza |
| 2. | Mwanza North | Mwanza |
| 3. | Kemondo | Kagera |
| 4. | Bukoba | Kagera |
| 5. | Kasanga | Rukwa |
| 6. | Kigoma – Cargo Terminal | Kigoma |
| 7. | Kiwira | Mbeya |
| 8. | Itungi | Mbeya |
| 9. | Ndumbi | Ruvuma |
| 10. | Mbamba Bay | Ruvuma |
| **B. Bandari Ndogo** | | |
| 11. | Kyamkwikwi | Kagera |
| 12. | Magarini | Kagera |
| 13. | Ntama | Kagera |

| | | |
|---|---|---|
| 14. | Lushamba | Mwanza |
| 15. | Nyamirembe | Geita |
| 16. | Bukoba Mwaloni | Kagera |
| 17. | Nansio | Mwanza |
| 18. | Musoma | Mara |
| 19. | Mwigobelo | Mara |
| 20. | Kirando | Rukwa |
| 21. | Ilagala | Kigoma |

| **Na.** | **JINA LA BANDARI** | **MAHALI/MKOA** |
|---|---|---|
| 22. | Ujiji | Kigoma |
| 23. | Ikola | Katavi |
| 24. | Karema | Katavi |
| 25. | Wampembe | Rukwa |
| 26. | Lukoma | Kigoma |

| | | |
|---|---|---|
| 27. | Korongwe | Rukwa |
| 28. | Sunuka | Kigoma |
| 29. | Sigunga | Kigoma |
| 30. | Kagunga | Kigoma |
| 31. | Kibirizi | Kigoma |
| 32. | Kipili | Rukwa |
| 33. | Kabwe | Rukwa |
| 34. | Sibwesa | Kigoma |
| 35. | Rukome | Katavi |
| 36. | Matema | Mbeya |
| 37. | Manda | Njombe |
| 38. | Liuli | Ruvuma |
| 39. | Ng'ombo | Ruvuma |
| 40. | Lumbila | Nyasa |
| 41. | Lagosa | Kigoma |
| 42. | Njambe | Ruvuma |

| | | |
|---|---|---|
| 43. | Makonde | Ruvuma |
| 44. | Nsisi | Njombe |
| 45. | Lupingu | Njombe |

| Na. | JINA LA BANDARI | MAHALI/MKOA |
|---|---|---|
| 46. | Lundu | Ruvuma |
| 47. | Ifungu | Ruvuma |
| 48. | Nyakalilo | Mwanza |
| 49. | Ninde | Rukwa |
| 50. | Kapalamsenga | Katavi |
| 51. | Msamba | Mbeya |
| 52. | Kalya | Kigoma |
| 53. | Bukondo | Geita |
| 54. | Kinesi | Mara |
| 55. | Shirati | Mara |
| 56. | Kira | Rukwa |

| | | |
|---|---|---|
| 57. | Kirumo | Mara |
| 58. | Kahunda | Mwanza |
| 59. | Kayenze | Ziwa Victoria |
| 60. | Kirumba Mwaloni | Ziwa Victoria |
| 61. | Kijiweni Chinfufu | Ziwa Victoria |
| 62. | Nkome Kichangani | Ziwa Victoria |
| 63. | Kasenda | Ziwa Victoria |
| 64. | Mnazi Ziwani | Mtwara |
| 65. | Nyamkazi | Bukoba |
| 66. | Katunguru | Muleba - Kagera |
| 67. | Korongwe | Nkasi - Rukwa |
| 68. | Mpasa | Nkasi - Rukwa |
| 69. | Nungwe | Geita |

| **Na.** | **JINA LA BANDARI** | **MAHALI/MKOA** |
|---|---|---|
| 70. | Bunyorwa | Busega - Simiyu |

| | | |
|---|---|---|
| 71. | Ihale | Busega - Simiyu |
| 72. | Nyamikoma | Busega - Simiyu |
| 73. | Tamau | Bunda - Mara |
| 74. | Kibara | Bunda - Mara |
| 75. | Nansimo | Bunda - Mara |
| 76. | Kisorya | Bunda - Mara |
| 77. | Guta | Bunda - Mara |
| 78. | Nyarusurya | Musoma - Mara |
| 79. | Makoko | Musoma - Mara |
| 80. | Bukima | Butiama - Mara |
| 81. | Busekela | Butiama - Mara |
| 82. | Kulwela | Butiama - Mara |
| 83. | Bwai | Butiama - Mara |
| 84. | Kulemela | Rorya - Mara |
| 85. | Kibuhi | Rorya - Mara |

| | | |
|---|---|---|
| 86. | Msasani | Rorya - Mara |
| 87. | Sonjo | Rorya - Mara |
| 88. | Busulwa | Rorya - Mara |
| 89. | Kakukuru | Ukerewe - Mwanza |
| 90. | Mswahili | Nyamagana - Mwanza |
| 91. | Kishimba | Ilemela - Mwanza |
| 92. | Makatani | Geita |
| 93. | Chato Beach | Chato - Geita |
| **Na.** | **JINA LA BANDARI** | **MAHALI/MKOA** |
| 94. | Kibindi | Misenyi - Kagera |
| 95. | Kikumbaitare | Chato - Geita |
| **C. Bandari zenye Waendeshaji Binafsi** | | |
| 96. | Kamanga Ferry | Mwanza |
| 97. | Mkombozi South | Mwanza |
| 98. | Mkombozi North | Mwanza |

| | | |
|---|---|---|
| 99. | Nyehunge | Mwanza |
| 100 | BigiliManoj | Mwanza |
| **JUMLA YA BANDARI ZILIZO KATIKA MAZIWA MAKUU** | | **100** |

**Jedwali Na.**

**6:** Leseni zilizotolewa na LATRA katika usafiri na usafirishaji kwa njia ya barabara kwa mwaka 2021/22 – 2023/24

| Na. | AINA YA LESENI | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Magari ya Abiria | 47,547 | 50,221 | 48,349 |
| 2 | Magari ya Mizigo | 143,011 | 169,942 | 192,996 |
| 3 | Pikipiki za Magurudumu mawili | 23,151 | 31,937 | 46,146 |
| 4 | Pikipiki za Magurudumu Matatu | 20,577 | 25,512 | 22,408 |
| 5 | Taxi za Kawaida | 2,654 | 2,305 | 2,345 |
| 6 | Taxi za Mtandao | 3,013 | 3,523 | 13,402 |
| 7 | Magari ya kukodi | | 718 | 930 |
| | **JUMLA** | **239,953** | **284,158** | **326,576** |

**7:** Mizigo iliyosafirishwa kupitia Reli ya TAZARA kwa mwaka 2018/19 – 2023/24

**Jedwali Na.**

| Na. | JINA LA MSAFIRISHAJI | Tani za Mizigo iliyosafirishwa | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | 2018/19 | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
| 1 | TAZARA (Serikali) | 175,599 | 182,792 | 217,661 | 210,161 | 173,673 | 128,928 |
| 2 | CALABASH – Zambia 2019 (Sekta Binafsi) | 187,113 | 196,676 | 263,772 | 112,249 | 119,883 | 162,827 |
| 3 | AFICD – Tanzania 2021 (Sekta Binafsi) | - | - | - | - | 16,898 | 6,259 |
| | **JUMLA** | **362,712** | **379,468** | **481,433** | **322,410** | **310,454** | **298,014** |

**Jedwali Na.**

**8:** Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kwa mwaka 2020/21 – 2024/25

| Na. | Udahili wa Wanafunzi/Mwaka wa Masomo | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya Wanafunzi (Kozi Ndefu) | 10,988 | 12,942 | 14,920 | 16,131 | 17,701 |
| 2. | Idadi ya Wanafunzi (Kozi fupi) | 3,700 | 3,341 | 2,439 | 5,461 | 4,303 |
| **Jumla** | | **14,688** | **16,283** | **17,359** | **21,592** | **22,004** |

**Jedwali Na.**

**9:** Kozi za muda mrefu zinazotolewa katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

| **Na.** | **JINA LA KOZI** | **AINA YA CHETI** |
|---|---|---|
| 1 | Logistics and Transport Management | Ordinary Diploma |
| 2 | Aircraft Maintenance Engineering | Ordinary Diploma |
| 3 | Auto -Electrical and Electronics Engineering | Ordinary Diploma |
| 4 | Automobile Engineering | Ordinary Diploma |
| 5 | Automobile Engineering and Locomotive Technology | Ordinary Diploma |
| 6 | Civil and Transportation Engineering | Ordinary |

**Jedwali Na.**

| | | |
|---|---|---|
| | | Diploma |
| 7 | Computing and Communication Technology | Ordinary Diploma |
| 8 | Electrical and Railway Electrification Engineering | Ordinary Diploma |
| 9 | Electrical Engineering | Ordinary Diploma |
| 10 | Electronics and Telecommunication Engineering | Ordinary Diploma |
| 11 | Freight, Clearing and Forwarding | Ordinary Diploma |
| 12 | Human Resource Management | Ordinary Diploma |
| 13 | Library and information Studies | Ordinary Diploma |
| 14 | Accounting and Transport Finance | Ordinary |

**Jedwali Na.**

| | | |
|---|---|---|
| | | Diploma |
| 15 | Marketing and Public Relations | Ordinary Diploma |
| 16 | Mechanical Engineering | Ordinary Diploma |
| 17 | Business Administration | Ordinary Diploma |
| 18 | Mechanical Engineering and Railway Vehicle Technology | Ordinary Diploma |
| 19 | Pipe work, Oil and Gas Engineering | Ordinary Diploma |
| 20 | Procurement and Logistics Management | Ordinary Diploma |
| 21 | Records, Archives and information Studies | Ordinary Diploma |
| 22 | Road and Railway Transport Logistics Operations | Ordinary |

**Jedwali Na.**

| | | |
|---|---|---|
| | | Diploma |
| 23 | Shipbuilding and Repair Operations | Ordinary Diploma |
| 24 | Shipping and Port Logistics Operations | Ordinary Diploma |

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|
| 25 | Telecommunication and Railway Signaling Engineering | Ordinary Diploma |
| 26 | Accounting and Transport Finance | Bachelor Degree |
| 27 | Aircraft Maintenance Engineering | Bachelor Degree |
| 28 | Automobile Engineering | Bachelor Degree |
| 29 | Business Administration | Bachelor Degree |
| 30 | Civil and Railway Engineering | Bachelor Degree |
| 31 | Computer Science | Bachelor Degree |
| 32 | Education with Mathematics and Information Technology | Bachelor Degree |
| 33 | Education with Economics and Mathematics | Bachelor Degree |
| 34 | Human Resource Management | Bachelor Degree |
| 35 | Information Technology | Bachelor Degree |
| 36 | Logistics and Transport Management | Bachelor Degree |
| 37 | Marketing and Public Relations | Bachelor Degree |
| 38 | Mechanical Engineering | Bachelor Degree |
| 39 | Naval Architecture and Marine Engineering | Bachelor Degree |
| 40 | Procurement and Logistics Management | Bachelor Degree |
| 41 | Road and Railway Transport Logistics Management | Bachelor Degree |
| 42 | Shipping and Port Logistics Management | Bachelor Degree |

| | | |
|---|---|---|
| 43 | Telecommunication and Railway Signaling Engineering | Bachelor Degree |
| 44 | Electrical and Railway Electrification Engineering | Bachelor Degree |
| 45 | Logistics and Transport Management | Master's Degree |
| 46 | Mechanical and Transportation Machinery Engineering | Master's Degree |
| 47 | Procurement, Logistics and Supply Chain Management | Master's Degree |
| 48 | Shipping and Port Logistics Management | Master's Degree |
| **Jumla ya Kozi Ndefu** | | **48** |

**Jedwali Na. 10:** Kozi za Muda Mfupi zinazotolewa katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT)

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|
| **A. PROFESSIONAL DRIVER COURSES** | | |
| 1 | Passenger Service Vehicle Course (PSV) | Professional Certificate |
| 2 | Heavy Goods Vehicle (HGV) | Professional Certificate |
| 3 | Advanced Driver's Grade II (for Industrial Vehicle Drivers) (ADCG II-IND) | Professional Certificate |
| 4 | Advanced Drivers' Grade II (VIP II) | Professional Certificate |
| 5 | Advanced Drivers Grade I (ADG II) | Professional Certificate |
| 6 | Senior Drivers' Course (SDC) | Professional Certificate |
| 7 | Transport Officers' Course (TOC) | Professional Certificate |
| 8 | Driver Instructor Course (DIC) | Professional Certificate |
| 9 | Driving Examiners Course (DEC) | Professional Certificate |
| 10 | Defensive Driving Training (DDT) | Professional Certificate |
| 11 | Forklift Operator Training (FOT) | Professional Certificate |

| | | |
|---|---|---|
| 12 | Bus Rapid Transport Driving Course (BRT) | Professional Certificate |
| 13 | Airport Vehicle Driving and Operation Courses (AVD) | Professional Certificate |
| 14 | Cabin Crew Course (Ab-Initio) (ABCC) | Professional Certificate |
| 15 | Cabin Crew Qualification Course – Category I (CCQC) | Professional Certificate |
| 16 | Vehicle Inspection (VI) | Professional Certificate |
| 17 | Cargo Tallying for International Shipping Course (CTIS) | Professional Certificate |
| 18 | International Shipping and Practices Course (ISP) | Professional Certificate |
| **B. OTHER SHORT COURSES** | | |
| 1 | Tyre Care and Maintenance (TCM) | Professional Certificate |
| 2 | Vehicle Safety Management and Control (VSMC) | Professional Certificate |
| **Na.** | **JINA LA KOZI** | **AINA YA CHETI** |
| 3 | Bus Passengers Customers Services (BPCS) | Professional Certificate |
| 4 | Engine Overhaul (Petrol and Diesel) (EO) | Professional Certificate |
| 5 | Electronic Fuel Injection (EFI) | Professional Certificate |
| 6 | Fuel Control and Safety Tools Usage (FCSTU) | Professional Certificate |
| 7 | Language Proficiency Course (LPC) | Professional Certificate |
| 8 | Vehicle Fleet Management and Maintenance | Professional Certificate |
| 9 | Airline Marketing | Professional Certificate |
| 10 | Airline Customer Services | Professional Certificate |
| 11 | Airport Operations Fundamentals | Professional Certificate |
| 12 | Global Distribution System Fares and Ticketing - | Professional |

| | | |
|---|---|---|
| | Amedeus | Certificate |
| 13 | Fleet Management in Road Transport Operations | Professional Certificate |
| 14 | Fleet Operations and Maintenance Course | Professional Certificate |
| 15 | Transport Costing and Transport Statistics Analysis | Professional Certificate |
| 16 | Dangerous Cargo Handling Skills | Professional Certificate |
| 17 | Airport /Aviation Security Handling Skills | Professional Certificate |
| 18 | Travel and Tourism Handling Skills | Professional Certificate |
| 19 | Airline/Airport Customer Care Handling Skills | Professional Certificate |
| 20 | Road Safety Awareness | Professional Certificate |
| 21 | Perishable Shipments Handling Skills | Professional Certificate |
| 22 | Introductory Computing Programmes | Professional Certificate |

**Jedwali Na. 11:** Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam DMI) kwa mwaka 2019/20 – 2024/25

| Na. | Maelezo/Mwaka wa Masomo | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya Wanafunzi (Kozi Ndefu) | 937 | 1,590 | 2,299 | 3,505 | 5,177 | 5,921 |
| 2. | Idadi ya Wanafunzi (Kozi Fupi) | 2,544 | 3,859 | 3,764 | 6,692 | 6,719 | 7,145 |
| | Jumla | **3,481** | **5,449** | **6,063** | **10,197** | **11,896** | **13,066** |

**Jedwalii Na. 12:** Kozi ndefu zinazotolewa katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|
| 1. | (NTA Level 9) in International Trade and | Master Degree |

| | | |
|---|---|---|
| | Maritime Law | |
| 2. | (NTA Level 9) in Marine Engineering Management | Master Degree |
| 3. | (NTA Level 9) in Maritime Transport and Nautical Science | Master Degree |
| 4. | (NTA Level 9) in Shipping Economics and Logistics | Master Degree |
| 5. | (NTA Level 9) in Transport and Supply Chain Management | Master Degree |
| 6. | (NTA Level 7/8 in Mechanical and Marine Engineering | Bachelor Degree |
| 7. | (NTA Level 7/8 in Mechatronics Engineering | Bachelor Degree |
| 8. | (NTA Level 7/8 in Oil and Gas Engineering | Bachelor Degree |
| 9. | (NTA Level 7/8) in Marine Engineering Technology | Bachelor Degree |
| 10. | (NTA Level 7/8) in Maritime Transport and Nautical Science | Bachelor Degree |
| 11. | (NTA Level 7/8) in Naval Architecture and Offshore Engineering | Bachelor Degree |
| 12. | (NTA Level 7/8) in Procurement, Logistics and Supply Chain Management | Bachelor Degree |
| 13. | (NTA Level 7/8) in Shipping and Logistics Management | Bachelor Degree |
| 14. | (NTA Level 7/8) in Transport and Supply Chain Management | Bachelor Degree |
| 15. | (NTA Level 6) in Marine Engineering | Ordinary Diploma |
| 16. | (NTA Level 6) in Marine Welding and Fabrication | Ordinary Diploma |
| 17. | (NTA Level 6) in Maritime Transport and Nautical Science | Ordinary Diploma |
| 18. | (NTA Level 6) in Mechanical and Marine Engineering | Ordinary Diploma |
| 19. | (NTA Level 6) in Naval Architecture and Offshore Engineering | Ordinary Diploma |
| 20. | (NTA Level 6) in Oil and Gas Engineering | Ordinary Diploma |
| 21. | (NTA Level 6) in Procurement, Logistics and Supply Chain Management | Ordinary Diploma |

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
| --- | --- | --- |
| 22. | (NTA Level 6) in Shipping and Logistics Management | Ordinary Diploma |
| 23. | (NTA Level 6) in Transport and Supply Chain Management (ODTSM) | Ordinary Diploma |
| 24. | (NTA Level 4) in Cargo Tallying and Supply Chain Management (BTCCTSM) | Basic Technician Certificate |
| 25. | (NTA Level 4) in Marine and Mechanical Engineering (BTCMME) | Basic Technician Certificate |
| 26. | (NTA Level 4) in Marine Operations (BTCMO) | Basic Technician Certificate |
| 27. | (NTA Level 4) in Marine Welding and Fabrication (BTCMWF) | Basic Technician Certificate |
| 28. | (NTA Level 4) in Naval Architecture and Offshore Engineering (BTCNAOE) | Basic Technician Certificate |
| 29. | (NTA Level 4) in Oil and Gas Engineering (BTCOGE) | Basic Technician Certificate |
| 30. | (NTA Level 4) in Procurement, Logistics and Supply Chain Management (BTCPLSM) | Basic Technician Certificate |
| 31. | (NTA Level 4) in Shipping and Logistics Management (BTCSLM) | Basic Technician Certificate |
| 32. | (NTA Level 4) in Transport and Supply Chain Management (BTCTSM) | Basic Technician Certificate |
| 33. | (NTA Level 5) in Naval Architecture and Offshore Engineering (TCNAOE) | Technician Certificate |
| 34. | (NTA Level 5) in Marine Engineering (TCME) | Technician Certificate |

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
| --- | --- | --- |
| 35. | (NTA Level 5) in Marine Welding and Fabrication Engineering (TCMWF) | Technician Certificate |

| | | |
|---|---|---|
| 36. | (NTA Level 5) in Maritime Transport and Nautical Science (TCMTNS) | Technician Certificate |
| 37. | (NTA Level 5) in Mechanical and Marine Engineering TCMME) | Technician Certificate |
| 38. | (NTA Level 5) in Oil and Gas Engineering (TCOGE) | Technician Certificate |
| 39. | (NTA Level 5) in Procurement, Logistics and Supply Chain Management (TCPLSM) | Technician Certificate |
| 40. | (NTA Level 5) in Shipping and Logistics Management (TCSLM) | Technician Certificate |
| 41. | (NTA Level 5) in Transport and Supply Chain Management (TCTSM) | Technician Certificate |
| 42. | Chief and Second Engineer Officer | Certificate |
| 43. | Chief and Second Engineer Officer on Ships between 750kW and 3000kW | Certificate |
| 44. | Electro-Technical Officer | Certificate |
| 45. | Master and Chief Mate | Certificate |
| 46. | Master and Chief Mate on Ships between 500GT and 3000GT | Certificate |
| 47. | Master on Ships less than 500GT (Near Coastal) | Certificate |
| 48. | Officer in Charge of a Navigational Watch on Ships less than 500GT | Certificate |
| 49. | Officer in Charge of a Navigational Watch | Certificate |
| 50. | Officer in Charge of an Engineering Watch | Certificate |
| 51. | Officer in Charge of an Engineering Watch on Ships less than 750kW | Certificate |
| **Na.** | **JINA LA KOZI** | **AINA YA CHETI** |
| | **JUMLA YA KOZI** | **51** |

**Jedwali Na. 13:** Kozi fupi zinazotolewa katika Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI)

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|
| 1. | Able Seafarer Deck | Certificate |
| 2. | Able Seafarer Engine | Certificate |
| 3. | Advanced Fire Fighting | Certificate |

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Advanced Training for Oil Tanker Cargo Operations | Certificate |
| 5. | Basic Training for Oil and Chemical Tanker Cargo Operations | Certificate |
| 6. | Bridge Resource Management | Certificate |
| 7. | Crisis Management and Human Behaviour | Certificate |
| 8. | Crowd Management | Certificate |
| 9. | Dangerous, Hazardous and Harmful Cargoes | Certificate |
| 10. | Electronic Charts Display and Information System (ECDIS) and Automation | Certificate |
| 11. | Electro Technical Rating | Certificate |
| 12. | Elementary First Aid | Certificate |
| 13. | Engine-Room Resource Management | Certificate |
| 14. | Fire Prevention and Fire Fighting | Certificate |
| 15. | GMDSS General Operator (GO) | Certificate |
| 16. | GMDSS Restricted Operator (RO) | Certificate |
| 17. | High Voltage Management Level | Certificate |
| 18. | High Voltage Operational V | Certificate |
| 19. | Leadership and Managerial Skills | Certificate |

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|
| 20. | Leadership and Team Working Skills | Certificate |
| 21. | Automatic Radar Plotting Aid (ARPA) | Certificate |
| 22. | Medical Care | Certificate |
| 23. | Medical First Aid | Certificate |
| 24. | Passenger Safety, Cargo Safety and Hull Integrity | Certificate |
| 25. | Passenger Ship Safety Training | Certificate |
| 26. | Personal Safety and Social Responsibilities | Certificate |
| 27. | Personal Survival Techniques | Certificate |
| 28. | Port Facility Security Awareness | Certificate |
| 29. | Port Facility Security Officer | Certificate |
| 30. | Proficiency in Fast Rescue Boat | Certificate |
| 31. | Proficiency in Survival Craft and Rescue Boats | Certificate |
| 32. | Radar Navigation at Management Level | Certificate |
| 33. | Radar Navigation at Operational Level | Certificate |

| | | |
|---|---|---|
| 34. | Rating Forming Part of a Navigational Watch | Certificate |
| 35. | Rating Forming Part of an Engineering Watch | Certificate |
| 36. | Refresher – Deck Rating | Certificate |
| 37. | Refresher – Engine Room Ratings | Certificate |
| 38. | Refresher and Upgrading – Deck Officers | Certificate |
| 39. | Refresher and Upgrading – Engine Officers | Certificate |
| 40. | Security Awareness Training | Certificate |
| 41. | Ship Security Officer | Certificate |
| 42. | Revalidation Ratings | Certificate |
| **Na.** | **JINA LA KOZI** | **AINA YA CHETI** |
| 43. | Revalidation Officers | Certificate |
| 44. | Hydrogen Sulphide Awareness | Certificate |
| 45. | Small Boat Handling and Maintenance | Certificate |
| 46. | Marine Survey | Certificate |
| 47. | Proficiency in Designated security Duties | Certificate |
| 48. | Ship's Cook Certificate of Competency | Certificate |
| 49. | Ship's Cook Certificate of Competency-Revalidation | Certificate |
| | **JUMLA YA KOZI** | **49** |

**Jedwali Na. 14:** Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC) kwa mwaka 2019/20 – 2023/24

| Maelezo/ Mwaka wa Masomo | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya Wanafunzi | 908 | 1,207 | 2,338 | 2,004 | 2,203 |

**Jedwali Na. 15:** Kozi zinazotolewa katika Chuo cha Usafiri wa Anga Tanzania (CATC)

| Na. | AINA YA PROGRAMU | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|---|
| 1. | Air Traffic Management | Basic Aerodrome Control | Certificate |
| | | Air Traffic Management - Aerodrome Control NTA Level 5 | Certificate |
| | | Aerodrome Control | Certificate |
| | | Approach Control Procedural | Certificate |
| | | Approach Control Procedural Refresher (STP) | Certificate |
| | | Approach Control Surveillance | Certificate |
| | | Approach Control Surveillance Conversion | Certificate |
| | | Area Control Procedural | Certificate |
| | | Area Control Surveillance | Certificate |
| | | Area Control Surveillance Conversion | Certificate |
| | | ATM Supervisory Management | Certificate |
| | | Performance Based Navigation | Certificate |
| | | Pre- Search and Rescue | Certificate |
| 2. | Aeronautical Information Management | Aeronautical Information Officer | Certificate |
| | | AIS Digital Cartography | Certificate |
| | | AIS Supervisory Management | Certificate |
| | | AIP Aerodrome Management and Provision | Certificate |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Transition from AIS to AIM | Certificate |
| | | Aeronautical Charts Management | Certificate |
| | | AIS Refresher | Certificate |
| | | NOTAM Information Management | Certificate |
| 3. | Aviation Security | Basic Aviation Security | Certificate |
| | | Basic Screeners | Certificate |
| | | Screeners Refresher | Certificate |
| | | ICAO Airport Security Supervisors | Certificate |
| | | ICAO AVSEC National Instructors | Certificate |
| | | ICAO Air Cargo and Mail Security | Certificate |
| | | ICAO AVSEC National Inspector | Certificate |
| | | ICAO Crisis Management Workshop | Certificate |
| | | ICAO Risk Management Workshop | Certificate |
| | | ICAO Behaviour Detection Course | Certificate |
| | | ICAO AVSEC Managers Course | Certificate |
| | | AVSEC Professional Management | Certificate |
| | | Behaviour Detection Course | Certificate |

| Na. | AINA YA PROGRAMU | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|---|
| | | National Civil Aviation Security Quality Control Programme | Certificate |
| | | X Ray Image Interpretation Workshop | Certificate |
| | | AVSEC awareness | Certificate |
| 4. | Communication Navigation and Surveillance | ATSEP Competency Based Initial Training | Certificate |
| | | VHF Communication (TCAA) | Certificate |
| | | ATSEP Competency Based Initial Training – | Certificate |
| | | VHF Radio Maintenance | Certificate |
| | | CNS/ATM Concept | Certificate |
| | | ADS-B Refresher Course | Certificate |
| | | DS-B Refresher Course ATM Systems Maintenance | Certificate |
| 5. | Airport Operations | Basic Airport Operations | Certificate |
| | | Advanced Airport Operations | Certificate |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Apron Management | Certificate |
| | | Aircraft Marshaller Refresher | Certificate |
| | | Basic Cargo Operations | Certificate |
| | | Flight Operations / Flight Dispatchers | Certificate |
| | | Crew Resource Management | Certificate |
| | | Crew Resource Management Awareness | Certificate |
| | | Dangerous Goods Regulations (Initial) – Category 6 | Certificate |
| | | Perishable Cargo Regulations | Certificate |

| Na. | AINA YA PROGRAMU | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|---|
| | | Live Animals Regulations | Certificate |
| | | Unit Load Devices Regulations | Certificate |
| | | Dangerous Goods Regulations | Certificate |
| | | Flight Operations / Flight Dispatch Refresher | Certificate |
| | | Safety Management System Awareness | Certificate |
| | | Ground Service Equipment | Certificate |
| | | Basic Airside Safety | Certificate |
| | | Turn Round Coordinator | Certificate |
| 6. | Other Programmes | Human Factors in Aviation | Certificate |
| | | Pre-Basic Procedure Design | Certificate |
| | | Drone Pilot Training | Certificate |
| | | Passenger Boarding Bridge | Certificate |
| | | Customer Service | Certificate |
| | | Radio Telephony Procedures | Certificate |
| | | Safety Management System | Certificate |
| | | Integrated Safety Management System | Certificate |
| | | Quality Management System | Certificate |
| | | QMS Internal Auditors Training | Certificate |
| | | Aerodrome Planning, Operations and Maintenance | Certificate |
| | | Heliport Design and Construction | Certificate |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | Team Resource Management | Certificate |

**Jedwali Na. 16:** Idadi ya Wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania kwa mwaka 2022/23 -2024/25

| Na. | JINA LA KOZI | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Stashahada ya Usafirishaji na Menejimenti ya Lojistiki kwa njia ya Reli | 30 | 44 | 52 |
| 2. | Astashahada ya Usafirishaji na Menejimenti ya Lojistiki kwa njia ya Reli | 57 | 62 | 77 |
| 3. | Astashahada ya Awali ya Usafiri: Menejimenti ya Lojistiki kwa njia ya Reli | 69 | 80 | 85 |
| 4. | Stashahada ya Teknolojia ya Miundombinu ya Reli | - | - | 19 |
| 5. | Astashahada ya Teknolojia ya Miundombinu ya Reli | 40 | 32 | 39 |
| 6. | Astashahada ya Awali ya Teknc Miundombinu ya Reli | - | 22 | 25 |
| 7. | Stashahada ya Kawaida ya Teknolojia ya Uhandisi Mitambo kwenye Mabehewa | - | - | 27 |
| 8. | Astashahada ya Teknolojia ya Uhandisi Mitambo kwenye Mabehewa | 34 | 25 | 38 |
| 9. | Astashahada ya Awali ya Teknolojia ya Uhandisi Mitambo kwenye Mabehewa | 14 | 36 | 23 |
| 10. | Stashahada ya Kawaida ya Teknolojia ya Mifumo ya Umeme kwenye Vichwa vya Treni | 27 | 35 | 57 |
| **Jumla** | | **271** | **336** | **442** |

**Jedwali Na. 17:** Kozi zinazotolewa katika Chuo cha Teknolojia ya Reli Tanzania

| Na. | AINA YA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|

| Kozi zinazofundishwa Kampasi ya Tabora | | |
|---|---|---|
| 1. | Railway Transport and Logistics Management NTA Level 4-6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| 2. | Carriage and Wagon Mechanical Technology NTA Level 4-6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| 3. | Track Technology NTA level 4 -6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| 4. | Electronics and Communication Engineering NTA Level 4-6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| 5. | Transport Safety and Railway Accident Management NTA Level 4-6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| 6. | Diploma in Railway Transport Economics NTA level 4 - 6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| **Kozi zinazofundishwa Kampasi ya Morogoro** | | |
| 7. | Locomotive Mechanical Technology NTA level 4 - 6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma |
| 8. | Locomotive Electrical Technology NTA level 4 – 6 | Basic Technician Certificate to ordinary Diploma 2 |
| 9. | Locomotive Driving Technology NTA level 5 - 6 | Diploma certificate |

**Jedwali Na. 18:** Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Bandari Dar es Salaam kwa mwaka 2019/20 – 2023/24

| Na. | IDADI YA WANAFUNZI/MWAKA | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Idadi ya Wanafunzi (Kozi Ndefu) | 586 | 884 | 937 | 986 | 1,025 |
| 2. | Idadi ya Wanafunzi (Kozi Fupi) | 345 | 675 | 616 | 1,717 | 2,212 |
| **JUMLA** | | **931** | **1,559** | **1,553** | **2,703** | **3,237** |

**Jedwalii Na. 19:** Kozi zinazotolewa katika Chuo cha Bandari Dar es Salaam

| Na. | JINA LA KOZI | AINA YA CHETI |
|---|---|---|
| 1. | Basic Technician Certificate in Freight Clearing Forwarding, and Shipping Management (NTA Level 4) | Basic Technician |
| 2. | Technician Certificate in Freight Clearing, Forwarding and Shipping Management (NTA Level 5) | Technician Certificate |
| 3. | Ordinary Diploma in Freight Clearing, Forwarding and Shipping Management (NTA Level 6) | Ordinary Diploma |
| 4. | Basic Technician Certificate in Shipping and Port Operations Management (NTA Level 4) | Basic Technician |
| 5. | Technician Certificate in Shipping and Port Operations Management (NTA Level 5) | Technician Certificate |
| 6. | Ordinary Diploma in Shipping and Port Operations Management (NTA Level 6) | Ordinary Diploma |
| 7. | Basic Technician Certificate in Maritime Transport and Logistics (NTA Level 4) | Basic Technician |
| 8. | Technician Certificate in Maritime Transport and Logistics (NTA Level 5) | Technician Certificate |
| 9. | Ordinary Diploma in Maritime Transport and Logistics (NTA Level 6) | Ordinary Diploma |

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri, ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwitwa Mheshimiwa Mwenyekiti hapa, wapo wageni wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambao ni wadogo zake saba sijui wamekaa upande gani. Karibuni sana Bungeni. Wanaongozwa na ndugu Gulamali Jamali Gulamali. Karibuni sana.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na utaratibu wetu Mheshimiwa Mwenyekiti, atakuja kunipokea.

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Namuita Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Miundombinu, katibu Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Selemani Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ifuatayo ni Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka kwa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge – *Hansard* kama ilivyowekwa Mezani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo:-

(a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inaeleza kuhusu Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;
(b) Sehemu ya pili inahusu uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kwa kutathimini makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;
(c) Sehemu ya tatu inahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026;

(d) Sehemu ya nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati na;
(e) Sehemu ya tano ni Hitimisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha 2024/2025. Utekelezaji wa maoni na ushauri wa Kamati. Napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri uliotolewa na Kamati, Mkutano wa Bunge uliojadili makadirio ya mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Moja kati ya masuala yaliyotekelezwa kikamilifu, ni kuanza kwa huduma rasmi za usafiri wa treni katika reli ya *SGR* kati ya Dar es Salaam na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza uendeshaji wa treni za *SGR,* na inathamini hatua hiyo, ambayo imechangia urahisi wa usafirishaji wa abiria kati ya Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli. Katika mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi trilioni 3.31. Hadi kufikia Februari, 2025 makusanyo yalikuwa ni shilingi trilioni 1.695 sawa na 51.21% ya lengo. Kwa wastani, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ni wa kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo wa upatikanaji wa fedha, Matumizi ya Kawaida; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi ilitengewa shilingi bilioni 114.74 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha shilingi bilioni 86.66 za mishahara ya watumishi na shilingi bilioni 28.08 za matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya fedha za matumizi ya Kawaida zilizotolewa ni shilingi bilioni 81.51 sawa na 71.04% ya bajeti yote ya matumizi ya kawaida iliyotengwa kama ambavyo kielelezo namba moja kinaonesha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za miradi ya maendeleo. Kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Kamati imebaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2025, kati ya shilingi trilioni 2.61 zilizotengwa kuteleza miradi, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 910.27 sawa na 34.81% ya makadirio. Kielelezo namba mbili kinatoa mchanganuo wa hali ya mapokezi hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati haikuridhishwa na hali ya mapokezi ya fedha za maendeleo kwa kuwa inaathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tathmini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kamati ilipokea taarifa na kukagua miradi katika Mikoa ya Morogoro, Tanga, Dar es Salaam kati ya tarehe 12 na 19 Machi, 2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa tathimini wa baadhi ya miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi namba 4227 - Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi Bilioni 51.10. Lengo la Mradi lilikuwa ni kuongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam kuhudumia mizigo kwa kuboresha miundombinu ambapo mradi utakapokamilika ifikapo mwaka 2027 na kutawezesha bandari hiyo kuhudumia meli kubwa zaidi Duniani inatarajiwa kuwa shehena itakayohudumiwa itaongezeka hadi kufikia tani milioni 30. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya shilingi bilioni 3.72 zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inapongeza juhudi ambazo Serikali inafanya katika kuboresha miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na uwekezaji unaoendelea kufanyika. Ni dhahiri kwamba uwekezaji huo umeboresha huduma mbalimbali na kuongeza pato la Taifa, hasa kwa kuwa sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* inakusanya fedha nyingi zaidi kupitia mapato yatokanayo na shughuli za Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mendeleo ya mradi wa reli ya kisasa *(Standard Gauge Railway)*. katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali ilitenga shilingi trilioni 1.51 kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa ya *SGR* pamoja na ununuzi wa vitendea kazi. Hadi kufikia Februari, 2025, jumla ya shilingi bilioni 250.66 sawa na 16.59% zilikuwa zimetolewa kutekeleza mradi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua mbalimbali ambazo zimefikiwa na Serikali katika kutekeleza mradi huu ikiwemo kipande cha kwanza (Dar es Salaam - Morogoro) kufikia 99.68%, kipande cha pili (Morogoro – Makutupora) kufikia 97.85% na kwa huduma za treni kuanza kati ya Dar es Salaam na Morogoro. Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikisha 63.10% za ujenzi wa kipande cha tano (Mwanza – Isaka).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo, Kamati haikuridhishwa na kiwango cha fedha kilichopokelewa na bado hairidhishwi na maendeleo ya mradi huu hususan katika kipande cha tatu (Makutupora – Tabora) pamoja na kipande cha nne (Tabora – Isaka) ambavyo maendeleo yake ni 14.53% na 6.61% mtawalia. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuja na mpango ambao utawezesha vipande hivyo vya reli ya *SGR* vinakamilika kwa wakati ili njia ya reli ya kati ianze kufanya kazi kwa ukamilifu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya Reli ya *TAZARA*; Kamati imebaini kwamba, Reli hiyo kwa sasa haifanyi kwa ufanisi kutokana na uchakavu wa miundombinu yake. Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia ambapo mnamo Septemba, 2024 ziliingia Mkataba wa Makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ya kufufua reli hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Makubaliano hayo unafanyika haraka ili reli hiyo, ambayo ni muhimu kwa uchumi wa nchi zetu Jirani, ijiendeshe kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miundombinu na huduma katika viwanja vya ndege nchini; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika viwanja vya ndege nchini. Mathalani, katika mradi wa miundombinu na uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere *(JNIA),* kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali ilitenga shilingi bilioni 30.3 ambapo sehemu ya fedha hiyo ilikusudiwa kulipa fidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na umuhimu wa kulipa fidia uliojitokeza, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali imefanya uhamisho wa shilingi bilioni 114 ili kulipa fidia ya eneo la Kipunguni ya shilingi bilioni 129.03. Fedha hizo zitalipwa kwa awamu na ulipaji wa fidia hiyo ulikuwa unaendelea. Hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya shilingi bilioni 9.6 zimetolewa kwa ajili ya uendeshaji wa jengo la tatu la abiria *(TB III)* na shilingi bilioni 20 kwa ajili ya ulipaji fidia awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati inapongeza Serikali kwa kuanza kulipa fidia ya wakazi wa Kipunguni. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, fidia kwa wakazi ambao wamepisha miradi yote ya viwanja vya ndege nchini inalipwa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya utendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania *(ATCL)*. Kamati imebaini kwamba, katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa bajeti ya shilingi bilioni 324.5 kwa ajili ya ununuzi wa ndege; na kuboresha miundombinu wezeshi ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na majengo, karakana na ukarabati wa nyumba zilizopo katika Kiwanja cha *KIA*. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya shilingi bilioni 355.04 ikiwa ni sawa na 109.41% zimetolewa baada ya kufanyika kwa uhamisho wa ndani kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha utoaji wa huduma za usafiri wa ndege za shirika, na kuhakikisha kwamba uwekezaji unaofanyika unaleta tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Umbile la bajeti, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishiwa shilingi 2.74 ikiwa ni ongezeko la 0.61% ukilinganisha na bajeti ya shilingi trilioni 2.72 iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha 2024/2025.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi hususan katika Matumizi ya Kawaida, ambapo kuna ongezezo la wastani wa 9.32%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, makusanyo ya maduhuli; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi imepanga kukusanya jumla ya shilingi trilioni 3.39 ikiwa ni sawa na ongezeko la 2.69% ukilinganisha na malengo ya kukusanya shilingi trilioni 3.31 waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha unaoisha kama ambavyo kielelezo namba nne kinaainisha. Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha makadirio ya makusanyo ya maduhuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishwa shilingi bilioni 125.43 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 96,654,340,000 ni mishahara na shilingi bilioni 28.78 ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inayoombwa ni sawa na ongezekeko la asilimia 9.32 ukilinganisha na Bajeti kama hiyo kwa Mwaka unaoisha kama ambavyo Kielelezo Na. 5 kinaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha za utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambayo inaongeza motisha kwa Watumishi wa Umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kwa weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Bajeti ya Maendeleo. Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inaomba kuidhinishiwa shilingi trilioni 2.62 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha

inayoombwa ni sawa na ongezeko la asilimia 0.23 ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha kama ambavyo Kielelezo Na. 6 kinaonesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaipongeza Serikali kuongeza fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inagusa moja kwa moja vipaumbele vya Wizara ambavyo vimeidhinishwa katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya nne - Maoni na Ushauri wa Kamati. Umuhimu wa kujenga reli ya kisasa ya *SGR* katika ushoroba wa Kusini. Kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali kujenga reli ya kisasa *(Standard Gauge Railway)* kutoka Mtwara hadi *Mbamba Bay* inayokadiriwa kuwa na urefu wa kilometa 1,000. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba, reli hiyo inaunganishwa pamoja na matawi ya reli itakayofika Liganga na Mchuchuma ili kuchechemua shughuli za kiuchumi katika Ushoroba wa Kusini *(Southern Corridor)* hususan uzalishaji wa makaa ya mawe na chuma katika maeneo hayo. Hatua hii pia itasaidia Serikali kupunguza gharama za uagizaji wa chuma nje ya nchi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaamini kwamba, iwapo Serikali itafanikisha kujengwa kwa reli hiyo, kutaongeza utendaji wa Bandari ya Mtwara na Bandari ya *Mbamba Bay,* na hatimaye kupunguza shughuli katika Bandari ya Dar es Salaam, kuongeza biashara na nchi jirani na pia kupunguza uharibifu wa barabara zetu unaosababishwa na malori yanayobeba mizigo mizito. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukarabati wa meli nchini. Katika kuhakikisha kwamba huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika Maziwa Makuu nchini unaimarika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha ujenzi na ukarabati wa meli zote nchini. Ili ushauri uweze kutekelezwa kwa ufanisi zaidi, ni vyema Serikali kupitia *TASHICO* ikabajeti kwa namna ambavyo shughuli za ujenzi na ukarabati wa meli hizo utakamilika kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umuhimu wa kuendeleza Bandari Kavu. Kwa kuzingatia maboresho ya huduma na miundombinu ya bandari yanayoendelea kufanyika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutafuta fedha za kuendeleza bandari kavu katika maeneo mbalimbali ya kimkakati nchini. Ujenzi wa bandari kavu, utasaidia katika kuongeza ufanisi wa bandari zilizopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inatambua mipango ya Serikali ya kuendeleza bandari kavu za Kwala (Pwani), Ihumwa (Dodoma), Fela (Mwanza), Katosho (Kigoma), Kurasini (Dar Es Salaam) na Isaka (Shinyanga). Pamoja na jitihada hizo, Kamati inaishauri Serikali kubainisha maeneo mengine ya kimkakati kama vile Tunduma (Mbeya) na kuanza kuweka mipango ya muda mrefu kwa kuziunganisha bandari kavu hizo na miundombinu ya sasa na ijayo ya njia kuu za reli nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uendeshaji wa shughuli za reli kwa Kushirikisha sekta binafsi. Kamati inaendelea kupongeza Serikali kwa hatua za kuendeleza miundombinu ya reli hususan *SGR* nchini. Kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Reli Na. 10 ya Mwaka 2017, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango kazi ambao utaliwezesha Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* kuendesha shughuli zake kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mpango kazi huo uainishe manufaa yatakayopatikana kulingana na uwekezaji uliofanywa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya tano, hitimisho. Kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, tunamshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi Vikao vya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara

ya Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao kwa majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Makame Mnyaa Mbarawa Mbunge kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile - Mbunge. Aidha, ninawashukuru watendaji wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Godius Walter Kahyarara. Kamati inatambua mchango wao katika sekta na inaendelea kuwatia moyo kufanya kazi kwa bidii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, msimamo wa Kamati Kuhusu hoja. Baada ya maelezo haya, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**15 MEI, 2025**

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA UCHUKUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

***[Imetolewa kwa mujibu wa Kanuni 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023]***

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati Kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**Mheshimiwa Spika**, ili kukidhi matakwa yaliyokusudiwa na Kanuni ya 118 (9) na bila kuathiri masharti yanayopatikana katika Kanuni ya 142, Taarifa hii imegawanyika katika sehemu zifuatazo: -

a) Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi ambayo inaeleza kuhusu Muundo wa Taarifa pamoja na namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake;
b) Sehemu ya Pili inahusu Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kwa kutathimini makusanyo ya maduhuli, mwenendo wa upatikanaji wa fedha, utekelezaji wa miradi ya maendeleo na uzingatiaji wa ushauri na maoni ya Kamati;
c) Sehemu ya Tatu inahusu Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;
d) Sehemu ya Nne ni majumuisho ya maoni na ushauri wa Kamati; na

e) Sehemu ya Tano ni Hitimisho.

1.2 Namna Kamati Iliyotekeleza Majukumu Yake

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu hutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti mbalimbali yaliyoainishwa katika Katiba, Sheria mbalimbali pamoja na Kanuni za Kudumu za Bunge.
**Mheshimiwa Spika**, katika kufanyia kazi utekelezaji wa Bajeti ya **Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilifanya yafuatayo: -

a) Kupokea taarifa na kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 (Kanuni ya 117 (1));
b) Kujadili utekelezaji wa Bajeti ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025;
c) Kupokea na kufanya uchambuzi wa Randama ya Wizara (Kanuni ya 115 (1)); na
d) Kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara pamoja na taasisi zake kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

SEHEMU YA PILI

2.0 UCHAMBUZI WA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

2.1 Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, katika Mkutano wa Bunge uliojadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kamati ya Kudumu ya Bunge iliwasilisha Maoni yake kuhusu Bajeti ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** ili kutimiza masharti yaliyowekwa na Kanuni ya 118 (9).

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge lako kwamba, kwa sehemu kubwa Serikali imeyafanyia kazi maoni na ushauri

uliotolewa na Kamati.[1] Moja kati ya masuala yaliyotekelezwa kikamilifu, ni kwa kuhakikisha kwamba, huduma rasmi za usafiri wa treni katika reli ya SGR kati ya Dar es Salaam na Dodoma zinaanza ili kutoa huduma kwa wananchi na kuongeza pato la Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanza uendeshaji wa treni za SGR kwa safari kati ya Dar es Salaam na Morogoro zilizoanza tarehe 14 Juni, 2024, pamoja na safari kati ya Dar es salaam na Dodoma ambazo zilianza tarehe 25 Julai, 2024. Kamati inatambua na kuthamini hatua hiyo, ambayo imechangia urahisi wa usafirishaji wa abiria kati ya mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Dodoma.

**Mheshimiwa Spika**, suala lingine ambalo limefanyiwa kazi kwa kiwango cha kuridhisha, ni kwa Serikali kutenga bajeti maalum kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC). Kamati imeridhishwa na inapongeza hatua ambazo Serikali imechukua kwa kubajeti **Sh. Bilioni 78** ambapo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 **Sh. Bilioni 23.2** zimetengwa kwa ajili ya kuanza mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande mwingine, baadhi ya maoni na ushauri uliotolewa na Kamati hayakufanyiwa kazi kwa ukamilifu na kwa sababu hiyo Kamati inapenda kuweka msisitizo kuhusu umuhimu wa utekelezaji wake. Kwa mfano, Serikali ilishauriwa kuchukua hatua thabiti na za haraka ili kuhakikisha kwamba Usafiri wa Meli katika Ziwa Tanganyika unaimarishwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi kufikia Februari, 2025, ukarabati wa meli ya **MT. Sangara** ulikuwa umefikia **asilimia 98** na kwamba Mkandarasi alikuwa anasubiriwa kukabidhi meli. Kwa upande wa **MV Liemba**, ukarabari wake ulianza tarehe 13 Julai, 2024 baada ya mkandarasi kulipwa malipo ya awali, ambapo hadi kufikia Februari, 2025, utekelezaji wake ulikuwa umefikia **asilimia 15**, na kwa upande wa **MV Mwongozo**, ukarabati wake ulikuwa haujaanza.

[1] Randama ya Mpango na Bajeti ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Uk. 3 - 13

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada hizo za Serikali, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa ushauri huu kwa kuwa changamoto ya usafiri katika Ziwa Tanganyika imekuwa ya muda mrefu. Kwa muktadha huo, ni vema Serikali ikaweka mkazo wa utekelezaji wa ushauri huo kwa haraka zaidi ili usafiri wa maji katika ziwa hilo uwe wa uhakika na wenye tija.

2.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 **Fungu 62 - Wizara ya Uchukuzi** pamoja na taasisi zake iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya jumla ya **Shilingi 3,310,021,435,500**. Hadi kufikia Februari, 2025 makusanyo yalikuwa ni **Shilingi 1,695,043,812,011.58** sawa **na asilimia 51.21** ya lengo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa wastani, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ni wa kuridhisha.

2.3 Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha

2.3.1 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** ilitengewa **Shilingi 114,744,476,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizo zinajumuisha **Shilingi 86,661,930,000** za Mishahara ya Watumishi (P.E.) na **Shilingi 28,082,546,000** za Matumizi Mengineyo (O.C.).

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya fedha za matumizi ya Kawaida zilizotolewa ni **Shilingi 81,510,144,771.45** sawa na **asilimia 71.04** ya bajeti yote ya Matumizi ya Kawaida iliyotengwa kama ambavyo **Kielelezo Na. 1** kinaonesha. Kati ya fedha hizo zilizotolewa, **Shilingi 27,579,944,896.17** ni fedha za Matumizi Mengineyo (O.C.) sawa na **asilimia 98.21** ya Bajeti yote ya Matumizi Mengineyo iliyotengwa na **Shilingi 53,930,199,875.28** ni Mishahara (P.E.) sawa na **asilimia 62.23** ya Bajeti yote ya mishahara iliyotengwa.

*KIELELEZO NA. 1 – MCHANGANUO WA HALI YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KUFIKIA FEBRUARI, 2025*

| BAJETI | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 86,661,930,000 | 53,930,199,875.28 | 62.23% |
| MATUMIZI MENGINEYO (O.C.) | 28,082,546,000 | 27,579,944,896.17 | 98.21% |
| **JUMLA KUU** | **114,744,476,000** | **81,510,144,771.45** | **71.04%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha za matumizi ya kawaida kwa kiwango kinachoridhisha.

### 2.3.2 Fedha za Miradi ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Bajeti ya Maendeleo, Kamati imebaini kwamba, hadi kufikia Februari, 2025, kati ya **Shilingi 2,614,931,941,000** zilizotengwa kuteleza miradi, Wizara ilikuwa imepokea **Shilingi 910,278,902,672** sawa na **asilimia 34.81** ya Makadirio. **Kielelezo Na. 2** kinatoa mchanganuo wa hali ya mapokezi ya fedha za Bajeti ya Maendeleo.

*KIELELEZO NA. 2 – MCHANGANUO WA HALI YA MAPOKEZI YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO KUFIKIA FEBRUARI, 2025*

| BAJETI YA MAENDELEO | MAKADIRIO 2024/2025 | MAPOKEZI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | % |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 2,524,369,202,000 | 899,465,783,861 | 35.63% |
| FEDHA ZA NJE | 90,562,739,000 | 10,813,118,812 | 11.94% |
| **JUMLA KUU** | **2,614,931,941,000** | **910,278,902,672** | **34.81%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati haikuridhishwa na hali ya mapokezi ya fedha za maendeleo kwa kuwa inaathiri utekelezaji wa miradi mbalimbali ya Sekta ya Uchukuzi.

### 2.4 Ukaguzi wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo
### 2.4.1 Maelezo ya Awali

**Mheshimiwa Spika**, ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, ni sehemu ya usimamizi wa Bunge kwa Serikali kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (1) kwa lengo la kutathmini hali ya mapokezi ya fedha, hatua ya utekelezaji pamoja na kubainisha changamoto za utekelezaji wa miradi hiyo. Kamati ilifanya ukaguzi wa miradi katika mikoa ya Morogoro, Tanga na Dar es Salaam kati ya tarehe 12 – 19 Machi, 2025.

### 2.4.2 Miradi Iliyokaguliwa

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitoe ufafanuzi wa miradi hiyo kwa muhtasari kama ifuatavyo: -

(a) Mradi Na. 4228 – Uboreshaji wa Miundombinu ya Bandari ya Tanga

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Tanga umetekelezwa kwa awamu mbili (2) ambapo Awamu ya Pili *(Phase II)* ilianza Disemba, 2020. Shughuli zilizotekelezwa ni pamoja na ujenzi wa gati *(berth)* kwa kuongeza mita 50 upande wa Mashariki kuelekea baharini na mita 92 upande wa Magharibi kuelekea baharini. Shughuli nyingine ni ujenzi na usimikaji wa miundombinu ya maji, umeme, mifumo ya TEHAMA na zimamoto.

**Mheshimiwa Spika**, hadi wakati inakagua mradi huu katika utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025, **Shilingi Bilioni 256.8** zilikuwa zimetumika ambapo mradi ulikuwa umekamilika kwa **asilimia 100**.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kukamilisha mradi huo ambao umechangia Bandari ya Tanga kuongeza

uwezo wa kuhudumia shehena na kuongezeka kwa meli. Maboresho hayo yamechangia ufanisi na kuongezeka kwa mapato ambapo katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 bandari hiyo ilikusanya **Shilingi Bilioni 45.69** sawa na **asilimia 200** ya lengo la kukusanya **Shilingi Bilioni 22.79**.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio yaliyoainishwa, Bandari ya Tanga inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

i. Ufinyu wa eneo ambao kwa sasa bandari hiyo ina jumla ya hekta 17; na
ii. Kutokuwa na kituo cha kuhudumia shehena ya mafuta.[2]

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia kuwa Bandari ya Tanga ni moja kati ya bandari za kimkakati nchini hususan katika kuchochea maendeleo na shughuli za kiuchumi katika Ushoroba wa Kaskazini *(Northern Corridor)*, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za haraka kutatua changamoto zilizoainishwa hususan kuwa na mpango endelevu wa kutumia kwa ufanisi eneo lililopo na maeneo mengine ambayo tayari yanamilikiwa na Bandari.

(b) Mradi Na. 4227 - Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa jumla ya **Shilingi Bilioni 51.10**. Lengo la Mradi lilikuwa ni kuongeza uwezo wa Bandari ya Dar es Salaam (Lango Kuu la Biashara) kuhudumia mizigo kwa kuboresha miundombinu ambapo utakapokamilika ifikapo mwaka 2027 na kuwezesha bandari hiyo kuhudumia meli kubwa zaidi duniani *(postpanamax ships)* na shehena itakayohudumiwa itaongezeka hadi kufikia tani milioni 30.[3]

---

[2] Taarifa ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Kuhusu Mradi wa Maboresho ya Bandari ya Tanga Kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tarehe 13 Machi, 2025 Uk. 11 - 12

[3] Randama ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Uk. 27 - 28

**Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia Februari 2025, jumla ya **Shilingi Bilioni 3.72** zimetolewa kwa ajili ya kutekeleza shughuli zifuatazo: -

i. Kuboresha Gati Na. 8 – 11 na Ujenzi wa Gati Na. 12 -15
ii. Kujenga matanki 15 ya kupokelea mafuta pamoja na miundombinu yake *(Single Receiving Terminal - SRT)* Kuendeleza Eneo la Kurasini *(EX - EPZA Logistic Centre)*
iii. Kujenga mtandao wa reli katika Bandari ya Dar es Salaam kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC)

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na kwamba Kamati haikuridhishwa na hali ya mapokezi ya fedha kutekeleza mradi huo, Kamati inatambua kwamba maboresho ya Bandari ya Dar es Salaam ni mradi endelevu ambao umekuwa ukitekelezwa kwa awamu tofauti.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza juhudi ambazo Serikali inafanya katika kuboresha miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam na uwekezaji unaoendelea kufanyika. Ni dhahiri kwamba uwekezaji huo umeboresha huduma mbalimbali na kuongeza pato la Taifa, hasa kwa kuwa sasa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) inakusanya fedha nyingi zaidi kupitia mapato yatokanayo na shughuli za Bandari ya Dar es Salaam.

(c) Mradi Na. 4213 - Ukarabati wa Miundombinu na Njia ya Reli (MGR) Kipande cha Tanga – Arusha

**Mheshimiwa Spika**, Reli ya Kaskazini (Tanga – Arusha) inayojulikana pia kama Reli ya Usambara, ni mojawapo ya njia kuu za reli nchini, na ina umuhimu katika kuchochea ukuaji wa uchumi hasa kwa kuzingatia maboresho katika Bandari ya Tanga. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Kamati ilitaarifiwa kwamba, mwaka 2018 Serikali ilianza jitihada za kufufua njia ya reli hii kwa sababu ya uchakavu wake baada ya kutofanya kazi kwa zaidi ya miaka 30.

**Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa jitihada hizo, Kamati ilitaarifiwa kwamba, ufufuaji wa awali ulianza kwa **Shilingi Bilioni 5.7** ambapo kufikia mwaka 2019, ukarabati huo ulikamilika na

huduma kuanza. Hata hivyo, katika ziara ambayo Kamati ilifanya kukagua utekelezaji kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Kamati ilibaini kuendelea kuwepo kwa changamoto zifuatazo: -

i. Uchakavu wa miundombinu ya reli; na
ii. Kukosekana kwa mifumo ya kisasa ya ishara na mawasiliano kwa ajili ya uendeshaji wa reli

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia changamoto hizo, Kamati ilitaarifiwa na Serikali kwamba, Shirika la Reli Tanzania (TRC) limeandaa mipango ya muda wa kati na muda mrefu wa kukarabati reli hiyo ili kuhakikisha kwamba huduma za usafirishaji zinaboreshwa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kununua vifaa mbalimbali, na kuingia mkataba na Kampuni ya *China Civil Engineering Construction Corporation* (CCECC) wenye thamani ya **Dola za Kimarekani Milioni 56.27** ambao ulisainiwa mwezi Aprili, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua zilizochukuliwa na Serikali. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inaongeza kasi ya kutekeleza mradi huu na kuboresha masharti yake ili huduma katika reli hiyo zianze mapema hususan katika mpango wa muda wa kati. Kwa upande wa mpango wa muda mrefu, kama ambavyo Serikali inakusudia kujenga reli ya kisasa ya SGR, Kamati inashauri kwamba, mpango huo uharakishwe kwa kuzingatia kwamba, tayari maboresho ya bandari yameanza kufanyika. Miradi hii ikifanya kazi kwa pamoja, kutapunguza msongamano wa shughuli za kibandari katika Bandari ya Dar es Salaam.

(d) Mradi Na. 4202 – Ujenzi wa Miundombinu ya Chuo cha Usafiri wa Anga (CATC)

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu unatekelezwa na Mamlaka ya Anga Tanzania (TCAA) kwa lengo la kujenga chuo cha kisasa cha usafiri wa anga kwa gharama ya **Shilingi Bilioni 78.066** kwa kipindi cha miaka mitatu. Katika Mwaka wa Fedha wa 2024/2025 Serikali pia imetenga **Shilingi Bilioni 23.2**.

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara iliyofanywa, Kamati iliridhishwa na maandalizi ya utekelezaji wa mradi ikiwemo hatua ya Serikali kusaini Mkataba na Mshauri Elekezi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza jitihada za kuboresha chuo hicho ambacho kinatarajiwa kuongeza udahili wa wanafunzi wa ndani na nje ya nchi, na vilevile kuongeza ufanisi wa utoaji wa mafunzo ili kuongeza wataalam wa sekta ya usafiri wa anga nchini.

2.5 Masuala Mahsusi Yaliyobainika Katika Utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025

*2.5.1 Mendeleo ya Mradi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway)*

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali ilitenga **Sh. Trilioni 1.51** kwa ajili ya ujenzi wa Reli ya Kisasa ya SGR pamoja na ununuzi wa vitendea kazi. Hadi kufikia Februari, 2025, jumla ya **Shilingi Bilioni 250.66** sawa na **asilimia 16.59** zilikuwa zimetolewa kutekeleza mradi huo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza hatua mbalimbali ambazo zimefikiwa na Serikali katika kutekeleza mradi huu ikiwemo **Kipande cha Kwanza** (Dar es Salaam - Morogoro) kufikia **asilimia 99.68**, **Kipande cha Pili** (Morogoro – Makutupora) kufikia **asilimia 97.85** na kwa huduma za treni kuanza kati ya Dar es Salaam na Morogoro. Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufikisha **asilimia 63.10** za ujenzi wa **Kipande cha Tano** (Mwanza – Isaka).

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na pongezi hizo, Kamati haikuridhishwa na kiwango cha fedha kilichopokelewa na bado hairidhishwi na maendeleo ya mradi huu hususan katika **Kipande cha Tatu** (Makutupora – Tabora) pamoja na **Kipande cha Nne** (Tabora – Isaka) ambavyo maendeleo yake ni **asilimia 14.53** na **asilimia 6.61** mtawalia. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuja na mpango ambao utawezesha vipande hivyo vya reli ya SGR vinakamilika kwa wakati ili njia ya reli ya kati ianze kufanya kazi kwa ukamilifu wake.

*2.5.2 Maboresho ya Reli ya TAZARA*

**Mheshimiwa Spika**, reli ya TAZARA yenye mtandao wa kilomita 1,860 unaoanzia Dar es Salaam (Tanzania) hadi New Kapiri Mposhi (Zambia) ni moja kati ya njia kuu za uchumi wa nchi yetu. Kamati imebaini kwamba, Reli hiyo kwa sasa haifanyi kwa ufanisi kutokana na uchakavu wa miundombinu yake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua jitihada zinazofanywa na Serikali ya Tanzania na Serikali ya Zambia ambapo mnamo Septemba, 2024 ziliingia Mkataba wa Makubaliano na Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China ya kufufua reli hiyo.[4] Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba utekelezaji wa Makubaliano hayo unafanyika haraka ili reli hiyo, ambayo ni muhimu kwa uchumi wa nchi zetu Jirani, ijiendeshe kwa ufanisi zaidi.

*2.5.3 Miundombinu na Huduma katika Viwanja vya Ndege Nchini*

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025 Serikali ilitenga fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali katika viwanja vya ndege nchini.[5] Mathalani, katika Mradi wa Miundombinu na Uendeshaji wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere (JNIA), kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali ilitenga **Sh. Bilioni 30.3** ambapo sehemu ya fedha hiyo ilikusudiwa kulipa fidia.

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na umuhimu wa kulipa fidia uliojitokeza, Kamati ilitaarifiwa kwamba, Serikali imefanya uhamisho wa **Sh. Bilioni 114** ili kulipa fidia ya Eneo la Kipunguni ya **Sh. Bilioni 129.03**. Fedha hizo zitalipwa kwa awamu na wa kulipa fidia hiyo ulikuwa unaendelea. Hadi kufikia Februari, 2025 jumla ya **Shilingi Bilioni 9.6** zimetolewa kwa ajili ya uendeshaji wa Jengo la Tatu la Abiria (TB III) na **Shilingi Bilioni 20** kwa ajili ya ulipaji fidia awamu ya kwanza.

---

[4] https://www.tazarasite.com/successful-signing-mou-concession-tazara

[5] Randama ya Mpango wa Bajeti ya Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi kwa Mwak wa Fedha 2025/2026 Uk. 22 - 24

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa kuanza kulipa fidia ya wakazi wa Kipunguni. Pamoja na pongezi hizo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, fidia kwa wakazi ambao wamepisha miradi yote ya viwanja vya ndege nchini inalipwa kwa wakati.

*2.5.4 Maboresho ya Utendaji wa Shirika la Ndege la Tanzania (ATCL)*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Serikali kwa kuendelea kufanya maboresho ya utendaji wa Shirika la Ndege Tanzania. Maboresho hayo yanalenga kuhakikisha kwamba Shirika linawezeshwa kutoa huduma za kusafirisha mizigo na abiria ili kuhimili ushindani katika soko la kikanda na kimataifa na kuchagiza shughuli za utalii, kilimo na biashara ndani ya nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, mradi huu ulitengewa bajeti ya **Shilingi Bilioni 324.5** kwa ajili ya ununuzi wa ndege; na kuboresha miundombinu wezeshi ya kutolea huduma ikiwa ni pamoja na majengo, karakana na ukarabati wa nyumba zilizopo katika Kiwanja cha KIA. Hadi kufikia Februari 2025, jumla ya **Shilingi Bilioni 355.04** ikiwa ni sawa na **asilimia 109.41** zimetolewa baada ya kufanyika kwa uhamisho wa ndani kwa kuzingatia taratibu zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kutoa fedha kwa wakati. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha utoaji wa huduma za usafiri wa ndege za Shirika, na kuhakikisha kwamba uwekezaji unaofanyika unaleta tija.

*2.5.5 Udhibiti wa Usafiri Ardhini*

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa ratiba za safari za usiku, kupitia LATRA, kwa mabasi ya abiria yaendayo mikoani na nchi jirani kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Hatua hii imerahisisha upatikanaji wa usafiri huo wakati wote (24/7) na kuwezesha abiria kujipangia muda anaopenda kusafiri. Aidha,

hatua hii, pamoja na kuondoa mabasi kukimbizana barabarani na misongamano ya abiria kwenye stendi kuu, imesaidia kukuza shughuli za kiuchumi na kijamii nchini.

**Mheshimiwa Spika**, hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba udhibiti wa mwendokasi unasimamiwa kwa ufanisi zaidi hasa kwa kuzingatia kwamba, kumekuwepo na matukio ya ajali ambazo zimesababisha vifo na majeruhi katika siku za hivi karibuni.

### 2.5.6 **Mafunzo ya Kimkakati Katika Sekta ya Uchukuzi**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza Serikali kwa Kuanzishwa kwa kozi za mafunzo za kimkakati katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) zinazoendana na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo Ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) na ujenzi na ukarabati wa meli katika Maziwa Makuu.

**Mheshimiwa Spika**, inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, mafunzo yanayotolewa katika chuo hiki na vyuo vingine vya sekta ya uchukuzi, yaboreshwe kwa namna ambayo itachochea matumizi ya vifaa na teknolojia ya kisasa.

### 2.5.7 **Udhibiti wa Huduma za Usafiri na Usafirishaji Majini**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuimarisha udhibiti wa huduma za usafiri na usafirishaji majini. Kwa mfano, katika **Sh. Bilioni 1.78** zilizotengwa katika Mradi wa Kimataifa wa Mawasiliano na Uchukuzi katika Ziwa Victoria, ambapo hadi kufikia Februari, 2025 ulitumia jumla ya **Shilingi Milioni 711.98** kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo zifuatazo: -

i. Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu na Masuala ya Utafutaji na Uokoaji katika Ziwa Victoria ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 71
ii. Ujenzi wa vituo vidogo vitatu (3) vya utafutaji na uokozi *(Search and Rescue - SARs)*
iii. Ununuzi wa boti za huduma za kitabibu *(Ambulance Boat)*

iv. Ununuzi wa boti za utafutaji na uokozi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua mbalimbali za kuimarisha udhibiti wa huduma za usafiri na usafirishaji majini kupitia TASAC. Kamati inaendelea kushauri kwamba, Serikali ihakikishe kwanza inawekeza zaidi ili jitihada za udhibiti wa huduma hizo, zifanyike katika maziwa yote nchini, mito na eneo lote la bahari. Jitihada hizi zitaimarisha usalama wa vyombo vya majini na watumiaji wa usafiri wa maji nchini.

SEHEMU YA TATU

3.0 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

3.1 Umbile la Bajeti na Vipaumbele vya Wizara

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, **Wizara ya Uchukuzi** inaomba **kuidhinishiwa Sh. 2,746,485,018,000** ikiwa ni ongezeko la **asilimia 0.61** ukilinganisha na Bajeti ya **Sh. 2,729,676,417,000** iliyotengwa katika Mwaka wa Fedha unaoisha.
**Mheshimiwa Spika**, **Kielelezo Na. 3** kinaonesha Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2025/2026.

*KIELELEZO NA. 3 – ULINGANISHO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026*

| BAJETI | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI YA KAWAIDA** | 114,744,476,000 | 125,438,950,000 | +9.32 |
| **BAJETI YA MAENDELEO** | 2,614,931,941,000 | 2,621,046,068,000 | +0.23% |
| **JUMLA KUU** | **2,729,676,417,000** | **2,746,485,018,000** | **+0.61%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi hususan katika Matumizi ya Kawaida, ambapo kuna ongezezo la wastani wa **asilimia 9.32**.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti inayoombwa ina lengo la kutekeleza vipaumbele mbalimbali vya Wizara ya Uchukuzi ikiwemo vifuatavyo: -

a) Kuboresha miundombinu na huduma katika Bandari za Bahari na Maziwa Makuu na kuendelea na ujenzi wa bandari kavu nchini, ikiwemo Bandari ya Kwala ambayo lengo ni kuifanya bandari kavu ya kimkakati;
b) Kuimarisha usafiri, usalama na mawasiliano katika Maziwa Makuu nchini;
c) Kujenga uwezo wa Taasisi za usafiri wa anga, majini na ardhini;
d) Kuhamasisha Sekta Binafsi kushiriki katika uendelezaji na uendeshaji wa Bandari, reli na viwanja vya ndege nchini; na
e) Kuendelea na ujenzi wa Reli ya Kisasa *(Standard Gauge Railway)* katika Ushoroba wa Kati *(Central Corridor)*.

3.2 Makusanyo ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi imepanga kukusanya jumla ya **Shilingi 3,399,148,152,880 ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 2.69** ukilinganisha na malengo ya kukusanya **Sh. 3,310,021,435,500** waliyojiwekea katika Mwaka wa Fedha unaoisha kama ambavyo **Kielelezo Na. 4** kinaainisha.

**KIELELEZO NA. 4 - ULINGANISHO WA MAKADIRIO YA MAKUSANYO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026**

| CHANZO CHA MAKUSANYO | MAKADIRIO YA MWAKA 2024/20245 | MAKADIRIO YA MWAKA 2025/2026 | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|
| ATCL | 717,967,025,000 | 1,079,765,510,000 | +50.39% |
| TAA | 161,180,246,500 | 220,444,636,200 | +36.77% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| DMI | 16,353,876,000 | 18,462,234,000 | +12.89% |
| LATRA | 43,890,000,000 | 43,531,147,000 | -0.82% |
| TASAC | 82,849,799,000 | 99,730,879,000 | +20.37% |
| NIT | 27,500,000,000 | 33,961,790,000 | +23.49% |
| TCAA | 98,701,888,000 | 110,764,490,000 | +12.22% |
| SINOTASHIP | 19,700,170,000 | 20,600,000,000 | +4.57% |
| TASHICO | 17,646,048,000 | 17,646,048,000 | 0% |
| TPA | 1,837,781,845,000 | 1,380,530,561,000 | -24.88% |
| TRC | 118,894,300,000 | 243,281,140,680 | +104.62% |
| TAZARA | 111,113,717,000 | 111,113,717,000 | 0% |
| TMA | 15,980,000,000 | 19,316,000,000 | +20.87% |
| **JUMLA** | **3,310,021,435,500** | **3,399,148,152,880** | **+2.69%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza kiwango cha makadirio ya makusanyo ya maduhuli. Sambamba na hilo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 taasisi zote ambazo ziko chini ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** zinakuwa na mkakati Madhubuti wa ukusanyaji wa maduhuli na kuwasilisha taarifa Bungeni mara kwa mara kuhusu mwenendo wa makusanyo hayo.

3.3 Matumizi ya Kawaida

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Uchukuzi inaomba kuidhinishwa **Sh. 125,438,950,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Sh. 96,654,340,000** ni Mishahara (P.E.), na **Sh. 28,784,610,00** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (O.C.).

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Matumizi ya Kawaida inayoombwa ni sawa na ongezekeko la **asilimia 9.32** ukilinganisha na Bajeti kama hiyo kwa Mwaka unaoisha kama ambavyo **Kielelezo Na. 5** kinaonesha.

**KIELELEZO NA. 5** – ULINGANISHO WA FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

| MATUMIZI YA KAWAIDA | BAJETI YA 2024/2025 | BAJETI YA 2025/2026 | TOFAUTI (TZS) | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|---|
| MISHAHARA (P.E.) | 86,661,930,000 | 96,654,340,000 | 9,992,410,000 | +11.53% |
| MATUMIZI MENGINEYO | 28,082,546,000 | 28,784,610,000 | 702,064,000 | +2.5% |
| **JUMLA KUU** | **114,744,476,000** | **125,438,950,000** | **10,694,474,000** | **+9.32%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kuongeza fedha za utekelezaji wa Bajeti ya Matumizi ya Kawaida ambayo inaongeza motisha kwa Watumishi wa Umma kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi na kwa weledi.

3.4 Bajeti ya Maendeleo

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara inaomba kuidhinishiwa **Sh. 2,621,046,068,000** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Fedha inayoombwa ni sawa na ongezeko la **asilimia 0.23** ukilinganisha na Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha kama ambavyo **Kielelezo Na. 6** kinaonesha.

*KIELELEZO NA. 6 – ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 NA MWAKA WA FEDHA 2025/2026*

| BAJETI YA MAENDELEO | MWAKA WA FEDHA 2024/2025 | MWAKA WA FEDHA 2025/2026 | TOFAUTI (%) |
|---|---|---|---|
| FEDHA ZA NDANI | 2,524,369,202,000 | 2,452,512,444,000 | -2.84% |
| FEDHA ZA NJE | 90,562,739,000 | 168,533,624,000 | +86.09% |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **JUMLA KUU** | **2,614,931,941,000** | **2,621,046,068,000** | **+0.23%** |

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuongeza fedha za kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo inagusa moja kwa moja vipaumbele vya Wizara ambavyo vimeainishwa hapo juu. Hata hivyo, Kamati imebaini kwamba, ongezeko la Bajeti ya Maendeleo kwa kiasi kikubwa limetokana na kuongezeka kwa Fedha za Nje ambayo imeongezeka kwa **asilimia 86.09** ukilinganisha na kupungua kwa **asilimia 2.84** kwa Fedha za Ndani.

**Mheshimiwa Spika**, katika uchambuzi wake, Kamati ilitathmini juu ya uwezo wa Serikali kutenga fedha za ndani katika kugharamia miradi ya maendeleo bila kuendelea kutegemea fedha za nje. Tathmini hii ina lengo la kuishauri Serikali kuweka mkakati Madhubuti wa kuongeza fedha za ndani ili kuwa na uhakika wa kukamilisha miradi kwa wakati kwa sababu fedha za nje zina masharti yenye mchakato mrefu wa upatikanaji wake.

SEHEMU YA NNE

4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

4.1 Maoni ya Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali ambayo kwa ufanisi mkubwa imeendelea kutoa fedha za kutekeleza majukumu mbalimbali ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi,** hususan katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. kwa muktadha huo, na kwa kuthamini mtaji wa fedha za maendeleo unaotokana na kodi za wananchi, Kamati inaishauri Serikali ifanye yafuatayo: -

a) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika utendaji kazi utakaochochea kuboresha huduma za Sekta ya Uchukuzi nchini, kwa kuwa sekta hiyo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi;
b) Kusimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi yake yote ili iweze kuakisi viwango bora, uendelevu na kuwepo kwa thamani ya fedha; na

c) Kuongeza ufanisi na ubunifu katika kukusanya maduhuli kutokana na vyanzo vilivyopo, na kubaini vyanzo vipya ambavyo vitaongeza wigo wa makusanyo hayo. Sambamba na hilo, Serikali ihakikishe kwamba, huduma zitolewazo na taasisi zake, zinakuwa bora ili kukidhi matarajio ya wadau muhimu wa Sekta ya Uchukuzi.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, Kamati inaishauri Wizara kuzisimamia taasisi zake kwa ukaribu zaidi ili kuhakikisha kwamba zinatekeleza majukumu yake yote kwa ufanisi. Kamati inaamini kwamba, iwapo kutakuwepo na usimamizi madhubuti, taasisi hizo zitaweza kujiendesha bila kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na wakati huo huo zitaongeza tija na hatimaye kuboresha huduma za na kuongeza mapato ya Serikali.

4.2 Maoni Mahsusi

*4.2.1 Umuhimu wa Kujenga Reli ya Kisasa ya SGR Katika Ushoroba wa Kusini*

**Mheshimiwa Spika,** kwa mara nyingine tena, Kamati inaishauri Serikali kujenga reli ya kisasa *(Standard Gauge Railway)* kutoka Mtwara hadi Mbamba Bay inayokadiriwa kuwa na urefu wa kilometa 1,000. Aidha, Serikali ihakikishe kwamba, reli hiyo inaunganishwa pamoja na matawi ya reli itakayofika Liganga na Mchuchuma ili kuchechemua shughuli za kiuchumi katika Ushoroba wa Kusini *(Southern Corridor)* hususan uzalishaji wa makaa ya mawe na chuma. Hatua hii pia itasaidia Serikali kupunguza gharama za uagizaji wa chuma nje ya nchi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaamini kwamba, iwapo Serikali itafanikisha kujengwa kwa reli hiyo, kutaongeza utendaji wa Bandari ya Mtwara na Bandari ya Mbaba Bay, na hatimaye kupunguza shughuli katika Bandari ya Dar es Salaam, kuongeza biashara na nchi za Jirani, na pia kupunguza uharibifu wa barabara zetu unaosababishwa na malori yanayobeba mizigo mizito.

*4.2.2 Maboresho ya Reli ya MGR na CGR*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuongeza fedha za Mfuko wa Reli, ili kuongeza kasi ya ukarabati na kuboresha miundombinu ya reli ya TRC *(Metre Gauge Railway - MGR)* na reli ya TAZARA – *(Cape Gauge Railway - CGR)* ikiwemo kipande cha kutoka Kilosa – Kidatu (Km 108) kwa ajili ya kuunganishwa na reli ya TAZARA.

**Mheshimiwa Spika**, maboresho hayo yataongeza tija katika uendeshaji na kuongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo. Aidha, Serikali iweke mkakati madhubuti wa kukarabati na kununua vichwa vya treni, mabehewa pamoja na kuboresha miundombinu ya mifumo ya kiufundi ya reli hizo.

*4.2.3 Maboresho ya Huduma na Miundombinu ya Viwanja vya Ndege Nchini*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua na kupongeza Serikali kwa kuweka mipango mbalimbali ya kuboresha huduma na miundombinu ya viwanja vya ndege nchini. Pamoja na jitihada hizo, Kamati inashauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kukamilisha zoezi la upatikanaji wa hati za maeneo yote yanayomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA) na kuhakikisha kwamba inamaliza migogoro yote inayohusu mipaka au fidia;
b) Kuboresha miundominu ya Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, ili iendane na ubora wa kimataifa kwa kuzingatia mahitaji ya watumiaji wa kiwanja hicho;
c) Kujenga haraka Kiwanja cha Ndege cha Bukoba, na viwanja vingine vya mikoa;
d) Kufanya tathimini ya kina kuhusu uwezekano wa TAA kuanza kukusanya *Passenger Service Charge* kwa mujibu wa sheria, bila kuathiri mtiririko na utaratibu wa makusanyo ya Serikali; na
e) Serikali kuweka vipaumbele vya kuendeleza viwanja vichache vya kimkakati, badala ya kuingia mikataba na wakandarasi katika viwanja vingi bila kuwa na uhakika wa fedha za utekelezaji wa miradi hiyo.

*4.2.4 Umuhimu wa Kuendeleza Bandari Kavu*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia maboresho ya huduma na miundombinu ya bandari yanayoendelea kufanyika, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kutafuta fedha za kuendeleza bandari kavu katika maeneo mbalimbali ya kimkakati nchini. Ujenzi wa bandari kavu, utasaidia katika kuongeza ufanisi wa bandari zilizopo.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua mipango ya Serikali ya kuendeleza bandari kavu za Kwala (Pwani), Ihumwa (Dodoma), Fela (Mwanza), Katosho (Kigoma), Kurasini (Dar Es Salaam) na Isaka (Shinyanga). Pamoja na jitihada hizo, Kamati inashauri Serikali kubainisha maeneo mengine ya kimkakati kama vile Tunduma (Mbeya), na kuanza kuweka mipango ya muda mrefu kwa kuziunganisha bandari kavu hizo na miundombinu ya sasa na ijayo ya njia kuu za reli nchini.

*4.2.5 Uendeshaji wa Shughuli za Reli kwa Kushirikisha Sekta Binafsi*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaendelea kupongeza Serikali kwa hatua za kuendeleza miundombinu ya reli hususan SGR nchini. Kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Reli Na. 10 ya Mwaka 2017, Kamati inaishauri Serikali kuandaa mpango kazi ambao utaliwezesha Shirika la Reli Tanzania (TRC) kuendesha shughuli zake kwa kushirikiana na sekta binafsi. Mpango kazi huo uainishe manufaa yatakayopatikana kulingana na uwekezaji uliofanywa na Serikali.

*4.2.6 Uwekezaji Katika Elimu*

**Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia uwekezaji unaofanywa na Serikali katika miundombinu ya uchukuzi nchini, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inawekeza zaidi katika taasisi zake zote zinazotoa elimu kuhusu masuala ya uchukuzi, anga na hali ya hewa. Uwekezaji huo ufanyike kwa namna ambayo, vyuo vyote vya Serikali vipatiwe vifaa vya kisasa vya kufundishia, kuwasomesha waalimu katika vyuo mbalimbali duniani ili kupata

maarifa bora, na kuboresha maslahi ya waalimu, wakufunzi na watumishi wa taasisi hizo.

*4.2.7 Ujenzi na Ukarabati wa Meli Nchini*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatambua kwamba, huduma za usafiri wa abiria na mizigo zinazotolewa katika Maziwa makuu ya Victoria, Tanganyika na Nyasa zitawezesha muingiliano wa shughuli za kijamii na kiuchumi kati ya Tanzania na nchi jirani za Uganda, Kenya, Sudan Kusini, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Zambia na Malawi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kwamba huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo katika maziwa makuu nchini unaimarika, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha ujenzi na ukarabati wa meli zote nchini. Ili ushauri uweze kutekelezeka kwa ufanisi zaidi, ni vyema Serikali kupitia TASHICO ikabajeti kwa namna ambayo shughuli za ujenzi na ukarabati wa meli hizo utakamilika kwa haraka zaidi.

**4.2.8 Mkakati wa Kuimarisha Usalama wa Usafiri na Usafirishaji Majini**

**Mheshimiwa Spika**, katika kuhakikisha kwamba Serikali inaimarisha usalama wa usafiri na usafirishaji majini, hususani katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo: -

a) Kushirikiana na nchi jirani zinazotumia maziwa hayo kuona iwapo utaratibu uliotumika katika Mradi wa Ziwa Victoria, unaweza kutumika katika maziwa hayo hasa ujenzi wa vituo vya uokozi;
b) Kuimarisha ukaguzi wa mara kwa mara wa vyombo vya usafiri majini ili kuhakikisha viwango vya ubora vinazingatiwa; na
c) Kundelea kutoa elimu kwa watumiaji wa huduma za usafiri na usafirishaji majini ili kuwapatia ufahamu kuhusu tahadhari za kiusalama.

*4.2.9 Kuboresha Huduma za Hali ya Hewa*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba, inaongeza uthabiti wa upatikanaji wa taarifa za uhakika za hali ya hewa katika maeneo mbalimbali nchini. Ili kufanikisha hili, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kusimika vituo vipya na vya kisasa vya kufuatilia taarifa ya hali ya hewa ikiwa ni pamoja na vituo vya kupima uwingi wa maji kwenye mabonde ya mito. Kamati inaamini kwamba, kwa Serikali kuwa na uhakika wa upatikanaji wa taarifa zote muhimu za hali ya hewa, itasaidia vyombo vyake kuwa tayari kukabiliana na maafa pindi dalili zinapojitokeza.

4.2.10 **Udhibiti wa Huduma za Usafiri wa Anga Nchini**

**Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kuboresha usalama wa usafiri wa anga nchini, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba inakamilisha majaribio ya mitambo *(Site Acceptance Test)* kwenye viwanja vyote nchini, ikiwemo vituo vipya ambavyo vilihitaji kujengwa kwanza kabla ya kusimika mitambo husika.

SEHEMU YA TANO

5.0 HITIMISHO

5.1 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya kipekee naendelea kukushukuru wewe binafsi kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu na kwa maelekezo yako ambayo yamekuwa msaada mkubwa katika uendeshaji bora wa shughuli za kila siku za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Aidha, namshukuru Naibu Spika, kwa namna anavyokusaidia kutekeleza majukumu yako, pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kukusaidia kuendesha kwa ufanisi Vikao vya Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, kwa moyo wa dhati kabisa, niwashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ambao wamekuwa mstari wa mbele katika kuendelea kuisimamia Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zilizo chini yake

kwa niaba ya Bunge lako tukufu. Kwa hakika, maoni, ushauri na mapendekezo yao vina mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Serikali. Naomba niwatambue Wajumbe hao ili majina yao yaingie katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Moshi Selemani Kakoso, Mb. | **Mwenyekiti** |
| 2. | Mhe. Anne Kilango Malecela, Mb. | **Makamu** |
| 3. | Mhe. Kapt. Abbas Ali Hassan Mwinyi, Mb. | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo, Mb. | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Abubakar Damian Asenga, Mb. | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Ahmed Mabkhut Shabiby, Mb. | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Ally Anyigulile Mlaghila Jumbe, Mb. | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Amina Ali Mzee, Mb. | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb. | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Fredrick Edward Lowassa, Mb. | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Geoffrey Idelphonce Mwambe, Mb. | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Ghati Zephania Chomete, Mb. | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Innocent Edward Kalogeris, Mb. | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Prof. Joyce Lazaro Ndalichako Mb. | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb. | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Mbarouk Juma Khatib, Mb. | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Miraji Jumanne Mtaturu, Mb. | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Mohamed Maulid Ali, Mb. | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Eng. Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, Mb. | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Mwatumu Dau Haji, Mb. | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Stella Simon Fiyao, Mb. | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Sylvia Francis Sigula, Mb. | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Uchukuzi, Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb) kwa ushirikiano ambao ameipatia Kamati katika kipindi chote cha Utekelezaji wa Majukumu ya Kamati akisaidiwa na Naibu Waziri wa Uchukuzi, Mhe. David Mwakiposa Kihenzile (Mb). Aidha, niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi pamoja na taasisi zake chini ya uongozi wa Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Godius Walter Kahyarara. Kamati inatambua mchango wa watendaji hao katika maendeleo ya Sekta ya Uchukuzi na inaendelea kuwatia moyo kwamba wafanye kazi kwa bidii.

**Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini sio kwa umuhimu, nawashukuru sana watendaji wote wa Ofisi ya Bunge chini ya uongozi wa Katibu wa Bunge, Bw. Baraka I. Leonard kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake hadi kukamilika kwa Taarifa hii.

5.2 Msimamo wa Kamati Kuhusu Hoja

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, naomba Bunge lako likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Moshi Selemani Kakoso, Mb.
**MWENYEKITI**
Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu
15 Mei, 2025

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Selemani Kakoso.

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wachangiaji wetu, Mchangiaji wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, ajiandae.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema ambaye ametujalia na kutuwezesha kuendelea kuwepo humu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee ninampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri lakini kwa kazi kubwa na nzuri inayofanyika kwenye sekta anayosimamia kwenye Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wako mnafanya

kazi nzuri pamoja na watendaji kule Wizarani, tunawapongeza sana tunaendelea kuwatakia kila lakheri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mchango kwenye maeneo machache. Eneo la kwanza, Mheshimiwa Rais alipokuwa kwenye ziara kwenye Mkoa wa Tanga, Tarehe 24 Februari alipokuwa Korogwe tulimuomba kwamba Serikali itukumbuke ujenzi wa Reli ya kisasa kwa upande wa kaskazini, lakini watu wa Korogwe tuliomba kwa namna jiografia ya Korogwe ilivyo tunafaa kuwa na *logistics centre* ya uhakika kwenye lile eneo kwa ajili ya kukuza biashara kwenye maeneo yale. Tunaomba Mheshimiwa Waziri maombi haya tuliyompa Mheshimiwa Rais muendelee kuyafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili na la mwisho ninalotaka kuchangia ni kuhusu bandari, kwenye bandari nina maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza Mheshimiwa Rais akiwa Tanga aliahidi kwamba barabara ya kutoka Handeni kwenda Kibirashi itakwenda kujengwa kwa ushirikiano kati ya Bandari na wenzetu wa *TANROADS* wakae waone namna ya kujenga barabara hii ili iweze kusaidia Bandari ya Tanga iweze kufanya kazi vizuri. Tunaiomba Bandari na *TANROADS* mkae pamoja timizeni ahadi aliyoitoa Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili kwenye upande wa bandari, kipekee ukichukua takwimu za mafanikio na ufanisi wa bandari yetu kwa sasa hasa bandari ya Dar es Salaam, tuna kila sababu ya kukiri kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan, hakika ni mzalendo namba moja wa nchi yetu, lakini ni kiongozi mwenye maono makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa mchakato wa uwekezaji kwenye bandari kulikuwa na maneno mengi, mengine ya hovyo, mengine ya kusadikika, mengine ya kufikirika lakini ukisikiliza na ukipata takwimu ya mafanikio ya bandari yetu kwa sasa, Mheshimiwa Rais ni mzalendo wa kweli na ni kiongozi jasiri

aliyesimamia maono haya, tunampongeza sana Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa zinaonesha mapato kwenye bandari yameongezeka kwa zaidi ya shilingi trilioni moja katika kipindi hiki cha mwaka mmoja tu huu, lakini siyo hivyo tu, muda wa meli kusubiri dangani umepungua kwa kiwango kikubwa sana, lakini muda wa kuhudumia meli kutoka wastani wa siku saba mpaka siku tatu, muda wa meli kupungua dangani umepungua kutoka wastani wa siku 46 mpaka leo tunavyozungumza tuko kwenye siku saba, haya ni mafanikio makubwa sana kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio haya na kwa uzoefu wa kazi hii kubwa ya kijasiri aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, mimi nakuja na ushauri mmoja leo kwenu, inawezekana muda wa mwaka mmoja usitoshe kuufanyia kazi lakini mna muda wa kuufanyia kazi. Tunaomba tuishauri, kwa kutumia uzoefu wa kazi hii aliyoifanya Mheshimiwa Rais, Wizara na Serikali anzeni kutafuta namna ya kuanzisha na kukuza biashara mpya kwenye bandari, biashara ya kufaulisha mizigo na ili biashara hiyo ifanyike vizuri tunawapa wito, tafuteni wawekezaji wengine tukajenge bandari mahsusi kwa ajili ya jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunalo eneo zuri sana kule Tanga. Tukishindwa kujenga kwenye Bandari ya Tanga ilipo sasa tuna eneo la Pangani *Deep Sea* zuri kabisa, tuna eneo la Mwambani, tutafute uwekezaji, tuanzishe ujenzi wa bandari nyingine kwa ajili ya biashara mahsusi ya kusafirisha mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukichukua jiografia ya Bara la Afrika liko katikati ya Mabara hayo mengine yote kwa maana ya Asia, Amerika, lakini ukichukua Tanzania ambayo iko katikati ya Bara la Afrika Pwani ya Mashariki, huu uzuri wa jiografia yetu unazifanya bandari zetu kuwa sehemu na kitovu muhimu sana kwenye biashara ya kufaulisha mizigo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatujatumia vizuri uzuri wa jiografia tulionao, tunazo nchi ambazo hazina uzuri wa jiografia kama

Tanzania lakini zimetumia mbinu hii ya biashara na zinafanya vizuri na nitakupa mfano wa nchi mbili. Nchi ya kwanza ni Singapore, wakati Singapore inapata uhuru mwaka 1964, *GDP* ya Singapore ilikuwa ndogo kuliko *GDP* ya Tanzania. Singapore imepata uhuru *GDP* yake ni *dollar* milioni 894.15 wakati huo *GDP* ya Tanzania ilikuwa *dollar* bilioni 3.75, lakini mpaka mwaka 1979 *GDP* ya Tanzania ilikuwa kubwa kuliko Singapore, lakini leo Singapore *GDP* yake ni mara sita ya *GDP* ya Tanzania, na sekta zinazokuza uchumi wa Singapore ni tatu tu, kwanza ni bandari, pili ni utalii na ya tatu ni huduma za kifedha. Kwa sasa bandari ya Singapore ni bandari ya pili kwa ukubwa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu za mwaka 2023 bandari ya Singapore, imehudumia meli 193,016, lakini bandari ya Singapore imehudumia shehena milioni 41.12 katika shehena milioni 41.12 asilimia 90 ya shehena hizi ni *transshipment* ni kufaulisha tu. Ukiacha hiyo tunayo bandari ya Salalah iko Oman imeanzishwa mwaka 1998 kwa mkataba wa *PPP* kati ya Serikali ya Oman na Shirika la *AP Terminals,* Kampuni ya Meli. Kwa mwaka 2023, Bandari ya Salalah imehudumia meli milioni 3.8 katika meli milioni 3.8 asilimia 98 ya mizigo iliyohudumiwa, shehena zilizohudumiwa na bandari hii ni za kufaulisha, sisi tunakwama wapi kufanya jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba Wizara tuanze kubuni namna ya kupata mwekezaji, *very strategic investor* tukajenge bandari Tanga mahsusi kwa ajili ya biashara ya kufaulisha mizigo na tukijenga hii bandari, bandari yetu hii itakumbana na ushindani wa maeneo mawili tu, kwanza itakuwa ni bandari hii ya Salalah lakini ya pili itakuwa ni Bandari ya Djibout. Ukienda kwenye ushindani Bandari ya Salalah haitatusumbua sana pamoja na kwamba ina *advantage* nyingi, ikiwemo *advantage* ya kuwa karibu na Bahari ya Sham kwa hiyo kuwa karibu na masoko ya Amerika na Ulaya lakini wako mbali sana na *Route* ya *Cap of Good Hope* ambapo sisi bandari zetu kwa jiografia yetu ziko karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushindani ya pili inawezekana ukawa Bandari ya Djibout, hauwezi kuwa mkubwa kwa sababu

Bandari ya Djibout sasa hivi haina mwekezaji baada ya *DP World* kuondoka, lakini pia ina hudumia meli chache, wastani wake ni meli 350,000 kwa mwaka. Mtu pekee ambaye ni tishio kwetu kwenye jambo hili ni nchi moja jirani ambayo siitaji, bandari yao iko karibu na sisi jiografia yetu ni moja, *location* yetu ni moja. Wakituwahi kwenye jambo hili wenzetu watafanya biashara nzuri zaidi kuliko sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sisi tuanze kutafuta wawekezaji, na kwenye kutafuta wawekezaji kwenye miradi mikubwa kama ilivyokuwa kwenye *DP World* huwezi kuanza kutangaza, ukitangaza huwezi kupata *strategic investor* unachotakiwa kufanya ni kutafuta makampuni makubwa duniani, tunakaa nayo, tunazungumza nayo, tuna *negotiate terms,* kwa sababu haya makampuni makubwa mengi yao yenyewe yana miliki meli kwa hiyo yatakuwa na uhakika wa kuleta meli, yana uhakika wa mizigo. Niombe sana Serikali ni wakati sahihi tuanze kuwaza jambo hili na mimi naona eneo sahihi sana kwenye jambo hili ni eneo la Tanga, tuna eneo la Pangani na tunalo eneo la Mwambani, maeneo yote mawili haya yanafaa kwa ajili ya ujenzi wa bandari hii kwa ajili ya kufanya kazi ya kufaulisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naendelea kumpongeza Mheshimiwa Waziri, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, nilimtaja Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde ajiandae.

**MHE. KILUMBE S. NG'ENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi ninaanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia afya na uhai na vilevile nichukue nafasi hii kabisa kutoka kwenye sakafu ya moyo wangu kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kiongozi wetu, mwenye maono na mwenye kusimamia vyema Serikali yake kiasi cha kutoa matumaini makubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niruhusu pia nimshukuru na kumpongeza sana Mheshimiwa Pofesa Makame Mnyaa Mbalawa, Waziri wa Uchukuzi, Naibu wake Mheshimiwa Kihenzile, Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara ya Uchukuzi kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya inayoleta matumaini kwa Watanzania kuongeza, na kuchechemua uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimepata bahati juzijuzi hapa ya kwenda kutembelea Bandari ya Kalema iliyoko katika Ziwa Tanganyika kwenye Mkoa wa Katavi na kule tumekwenda kuangalia sekta binafsi ambao wanajenga meli nne za mizigo ambapo kila meli moja itakuwa inachukua tanai elfu mbili, kwa hiyo, meli hizo nne zitakuwa zinachukua tani 8,000. Hawa wawekezaji wanaweka zile meli kwenye Ziwa Tanganyika kwa ajili ya kuchukua mzigo wao wa madini kutoka Congo, kuuleta kwetu kwenye bandari zetu na kuuleta Bandari ya Dar es Salaam na kusafirisha kwenda nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanachosema, wenyewe mzigo wao ni wa kutoka Congo tu, mzigo wa kupeleka Congo watachukua mizigo ya watanzania na wafanyabiasha wengine, iwe ni mahindi, iwe ni karanga, chochote kile watabeba kwa gharama nafuu kukipeleka Congo kwa sababu wao tayari gharama zao zitakuwa zimejilipa katika kuleta madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninapongeza hatua hii kwa sababu siku zote tumekuwa tukisema hapa katika Bunge hili, Serikali haiwezi kufanya kila kitu, Serikali ni lazima ihusishe sekta binafsi katika kuhakikisha kwamba huduma kwa wananchi zinapatikana. Serikali inajenga barabara lakini haina mabasi, mabasi ni ya watu binafsi ndiyo yanapita kwenye barabara na hata hii *SGR* huko tunakokwenda itafika mahala miundombinu ni ya Serikali lakini itakuwa inapita Treni ya Kuchauka inapita hapo, Treni ya Prof. Manya inapita hapo, analipa miundombinu. (Na nyie hamumshukuru Mungu ninawaombea mambo mema hayo au mpaka niseme ya Mheshimiwa Bakhresa. *(Kicheko&Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niunge mkono juhudi zinazoendelea za Bandari ya Dar es Salaam, watanzania mmeona. Tulisimama katika Bunge hili tukawatoa hofu tukawaambia kinachokwenda kufanyika ni kikubwa kutoka *TICTS* iliyokuwa inaendesha bandari kuja *DP World* tumeongeza shilingi trilioni moja, trilioni moja ni karibu asilimia nne hadi tano ya bajeti ya nchi yetu imeongezeka kutokana na uwekezaji mzuri uliyofanywa pale. Kwa hiyo, tunapongeza sana Serikali kwa hatua hii na hasa tunampongeza Rais wetu, aliziba masikio akasema mimi sitaki kusikia kelele, ninafanya mambo kwa manufaa ya watanzania, wakiyaona watanipongeza na leo tunampongeza Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uchukuzi ni kazi ya *chain,* unatoka kwenye reli, reli ikifika kwenye bandari, bandari inachukua, bandari ikikoma inachukua barabara inapeleka mpaka inapokwenda, ni kazi ya *chain*. Sasa ni lazima tuongeze kasi ya ujenzi wa reli, hasa *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninasema hivyo kwa nini? Kwenye *SGR* pesa mnazo; mbona tunasuasua? Hebu tuongeze kasi! Mheshimiwa Profesa Mbarawa wewe tunakuamini siyo Profesa wa maneno, wewe ni Profesa wa vitendo na umeonyesha kazi kubwa sana, ongeza kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ikiweza kufika Kigoma mizigo inayotoka Kongo ya madini itakwenda kwenye Bandari ya Dar es Salaam; kwa hiyo tutakuwa na *chain*. Kwenye reli tutapata, kwenye meli tutapata, na Bandari ya Dar es Salaam tutapata, kwa hiyo ongezeni kasi. Hizi kilometa 506 za Tabora - Kigoma ambazo sasa hivi mmefikia 7.88%, mimi ninaamini katika kipindi kisichozidi miezi sita mkiamua tunaweza tukaenda mpaka 40%; hebu ongezeni kasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine niwapongeze kwa hatua mliyoanza nayo ya kujenga kiwanda cha meli kule Kigoma. Nimesikia tayari mmempa *advance* yule mkandarasi na kazi imeanza pale eneo la Katabe katika ufukwe wa Ziwa Tanganyika. Hii nayo itatusaidia sana; meli zote za Zambia, Kongo, Burundi na

Tanzania tukiwa na *ship yard* pale imekamilika watakuja kufanya ukarabati pale, tutapata fedha na hiyo itasaidia sana kuongeza mzunguko wa fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie na suala la meli ya MV. Liemba na MV. Mwongozo. Mheshimiwa Waziri ninarudia kukupa maua yako. Uliahidi katika Bunge hili kwamba utafanya kila namna uwezavyo utoe fedha ili kazi ile ianze. Ninashukuru nimeona kazi ile imeanza. Sasa hivi meli ile imepandishwa kwenye cherezo na mpaka sasa kazi ninaambiwa iko kwenye asilimia karibu 24. Ninakupa hongera sana kwa kazi hiyo na nikuombe endelea na kazi ya Mwongozo kwa sababu kazi ya Mwongozo ni ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya Mwongozo ni *stability* tu. Kila kitu kiko sawasawa; *engine* iko sawasawa na vitu vingine vyote viko sawasawa. Hebu anza na kazi ile ya Mwongozo, Mwongozo inaweza ikatoka haraka na wananchi wetu wakaweza kupata huduma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninarudia tena kutoa pongezi nyingi kwa Mheshimiwa Rais wetu kwa haya mambo ambayo wananchi wetu wameyaona wenyewe sasa. Ninarudia tena kutoa pongezi nyingi kwako Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Naibu wako na Wizara nzima ya Uchukuzi; endeleeni kupiga kazi na sisi tunawaunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda. Nilimtaja Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde na Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga wajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Uchukuzi ambayo ni Wizara muhimu sana kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2020 tuliweza kuwasilisha kitabu kwa Watanzania kinachoitwa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi. Ilani hii ilikuwa na kurasa zipatazo 303. Ilani hii pamoja na mambo mengi kwenye Sekta ya uchukuzi ilizungumza maneno mazito sana kwenye ibara ya 58 kwenye sehemu ile ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ilieleza kwa uwazi kabisa kwamba Sekta ya Uchukuzi, Chama Cha Mapinduzi kinatambua kuwa uendelezaji wa miundombinu ni hitaji la msingi katika kuchochea na kuwezesha Uchumi na kuwezesha maendeleo ya Sekta ya kiuchumi na kijamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ambayo ni kitabu ambacho ni mwongozo wa maendeleo ilieleza waziwazi. Wanasema siku zote tembea kwenye maneno yako. Kwa hiyo kwenye hili ninaomba niseme wakati ninaenda kuchangia, Chama Cha Mapinduzi na Serikali yake imetembea kwenye maneno yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, imetembea kwenye maneno yake kwamba itaboresha Sekta ya Uchukuzi na kweli imeboresha. Kwenye hili ninaomba niseme waziwazi kwa hakika Mheshimiwa Rais ameonekana wazi kwamba yeye anasimamia vizuri maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Sekta ya Uwekezaji mimi nitachangia kama maeneo matatu; nitachangia upande wa bandari, nitachangia reli lakini nitamalizia upande wa anga kwa maana ya Sekta ya Usafirishaji wa Anga ambayo nitaeleza kwa ufupi sana katika maeneo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kama nilivyosema kwenye Sekta hii amefanya kazi kubwa, fedha nyingi zimetolewa na tunaona namna ambavyo Sekta hii inachochea Uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye Ibara ile ya 59 imesema chama kitaelekeza Serikali kuendelea kuwekeza katika

miundombinu ya kimkakati. Miundombinu hiyo inajumuisha reli, viwanja vya ndege pamoja na bandari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili la bandari niseme kwa uwazi kabisa nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri ndugu yetu Mheshimiwa Profesa Mnyaa Mbarawa pamoja na Naibu Waziri na Katibu Mkuu na watendaji wote kwa namna walivyosimamia kwa dhati maono ya Mheshimiwa Rais. Kwa hakika Mheshimiwa Profesa Mbarawa hongera sana kazi umefanya nzuri ninajua kuna kipindi *weight* ilipungua lakini Mungu atakuongeza *weight* kwa kazi kubwa uliyofanya ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri alisimama kidete katika kusimamia jambo hili lilikuwa na kelele nyingi lakini leo wanaona aibu kwa kazi kubwa aliyofanya. Leo ameeleza hapa kwamba katika kipindi cha mwaka huu tumeongeza zaidi ya bilioni 1.7 ambayo kimsingi haijawahi kupatikana katika eneo lolote. Hayo ni mafanikio makubwa katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi tumeona uwekezaji mkubwa kwenye eneo hili. Bandari ya Dar es salaam ilikuwa na maneno mengi kwa miaka minne iliyopita. Ilikuwa na maneno mengine kwamba magari ambayo yanahifadhiwa pale sehemu haitoshi, kwenye ile *row* ambayo inapokea magari lakini kama haitoshi gati namba moja mpaka namba tatu imeboreshwa, gati namba nne na namba saba imeboreshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunavyoongea ushushaji wa shehena umeongezeka kwa kiwango kikubwa ambayo ni tofauti na huko nyuma ambayo ilikuwa ni kero kubwa kwa ajili ya Bandari yetu ya Dar es salaam na hata ilitishia baadhi ya wateja kutokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi tumeenda kukaribisha Sekta Binafsi. Kazi hii kama Kamati tumeiona ni kazi kubwa. Leo hii tunavyoongea tumepunguza gharama za uendeshaji kwa 30% ambazo zilikuwa zinafanyika wakati inaendeshwa na Serikali. Kwa hiyo maana yake ni kwamba

mwekezaji amekuja kuwa ni sehemu ya uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam ambayo imekuwa ni kimbilio katika nchi zinazotuzunguka katika ukanda huu wa nchi nane. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilitaka niseme nini? Niendelee kuwaomba sana Wizara endeleeni kusimamia mipango ambayo ipo kwa ajili ya gati namba 8 – 11 pamoja na 12 na 15 ikiwemo pale eneo la kupokelea mafuta matanki 15 yale ambayo yatasaidia kuwa na hifadhi ya mafuta nchini hata likiyumba soko la mafuta duniani bei itabakia palepale na itaendelea kuongeza uchumi wa nchi. Kazi hii endeleeni kuifanya kwenye lile eneo la *single receiving terminal* iendelee kwa kasi ambayo imeanza na kwa hakika najua Mheshimiwa Waziri utaendelea kusimamia jambo hili. Hongera sana kwa kazi nzuri ya Bandari ya Dar es salaam lakini tunaona Bandari ya Tanga na Mtwara kazi nzuri inafanyika. Endeleeni kufanya hivyohivyo ili kuongeza uchumi wa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo hili la pili tumekuwa na gharama za uendeshaji zilizopungua. Tumeweza kuongeza bakaa la mapato. Bakaa la mapato lilikuwa shilingi bilioni 45 lakini leo bakaa la mapato limekuwa bilioni 142. Ni jambo kubwa ambalo halijawahi kutokea fedha hizi zitaenda kufanya kazi kubwa ya kujenga hospitali, kujenga shule, kujenga barabara ambazo Wabunge wote wamekuwa wakisema hapa kwa sababu mapato yatapatikana kwa wingi katika eneo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana tunaposikia watu wanasema "*no reforms no election*" si kwa bahati mbaya. Hata wewe huogopi kwa maendeleo haya? Lazima useme "*no reforms no election*" kwa sababu ukiingia uwanjani unapigwa asubuhi bado kweupe. Hauna sababu ya kupata aibu bora uweke mpira kwapani ondoka usije ukapatwa na aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningekuwa hata mimi ningesema "*no reforms*" kwa hali iliyofanywa na Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Kingu.

**TAARIFA**

**MHE. ELIBARIKI I. KINGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ninaomba nimpe taarifa mchangiaji anayechangia kwa uzalendo mkubwa sana Mbunge pacha na jirani yangu kwamba kilio cha *"no reforms no election"* lazima kitaendelea kwa sababu kwa *impact* hii ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo Shirika la Ndege peke yake sasa hivi linaingiza jumla ya mapato ya dola milioni 354 kwa miaka minne, Sekta ambayo inaelekea kuwa Sekta ya tatu katika kuleta *forex* za nchi. Nani atakuja kwenye uchaguzi kushindana na CCM? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninampa mchangiaji taarifa ya kwamba kwa namna ambavyo uchukuzi wameupiga mwingi, kwa kweli *"no reforms no elections"* wataendelea kuisema kwa sababu hakuna wa kuja ku-*compete* na Chama cha Mapinduzi kwenye uchaguzi ujao. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu unaipokea hiyo taarifa ya Mheshimiwa Kingu?

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapokea taarifa kwa heshima ya pacha wangu Mheshimiwa Elibariki Kingu lakini ninaomba niseme tu kwamba hata wale wanaosema kwamba "Hatuchezi" nao pia naona ni haohao. Wanafanana na hao ambao wanasema *"no reforms no election"* kwa sababu hali ya mziki wa Mpanzu na wengine ni mkubwa sana pale watakapoona tunaenda kubeba kombe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtaturu malizia nusu dakika.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie eneo la reli. Reli imefanyika vizuri sana na uwekezaji mkubwa tumepata zaidi ya shilingi bilioni 60 katika muda mfupi. Hili ni jambo kubwa lakini hata Balozi wa Marekani alipopanda kwenye

ile treni aliona ni bora kuliko ya Marekani maana yake ni kazi kubwa iliyofanywa na Serikali yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, dakika moja. Niombe sana eneo moja tu la viwanja vya ndege. Viwanja vya ndege vilisemwa vitajengwa katika viwanja 11 vya Songea, Iringa, Musoma, Tanga, Dodoma pamoja na Singida lakini naona viwanja vingine vinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe na kiwanja cha Singida kiko karibu na Makao Makuu ya nchi na chenyewe kiangaliwe. Nitaomba Mheshimiwa Waziri kwa sababu nimechangia kwa uzalendo kwenye eneo hili, nikuombe unaposimama uwaambie watu wa Singida kiwanja cha Singida kimekwama nini ili na sisi wale watoto wa Dar es Salaam ambao hawajawahi kuja Singida warudi nyumbani waje wapande ndege kwa sababu wengine wamesema bila ndege hawarudi nyumbani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya ninaomba kuunga mkono hoja, ahsante sana. Asilimia 100 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan mitano tena. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu; nakushukuru sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde, Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ajiandae.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kupata nafasi hii na mimi niweke mchango wangu mdogo kwenye Wizara nyeti kabisa Wizara ya Uchukuzi. Nikupongeze sana Mheshimiwa Profesa Mbarawa kwa kazi nzuri, Katibu Mkuu, Naibu Waziri ndugu yetu Kihenzile kwa namna ambavyo mmekuwa mkichapa kazi bila kulala kuhakikisha kwamba nchi inakwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisia miamba watatu hawa wawili walionitangulia kuzungumza wamesema maneno mazito sana kuhusu maono ya Mheshimiwa Rais wetu, msimamo wake kuhakikisha kwamba bandari inawekezwa na hii inatufanya Taifa letu liwe Taifa la kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata wale waliokuwa wanabisha walikuwa sehemu ya kufanikisha jambo hili kwa sababu wakati mwingine ikitokea mtu akibisha mwingine ndiyo anafanya vizuri zaidi. Kama unavyoona hata kwenye michezo jamaa wakibisha sisi tunafanya vizuri zaidi, sisi tukibisha wanafanya vizuri zaidi, hivyo ndiyo inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais alifumba macho akasema twende tuwekeze. Mabingwa wamezungumza kwa umakini sana namna ambavyo mapato yameongezeka lakini ninataka kusema nini kwako Mheshimiwa Waziri, Naibu wako pamoja na Katibu Mkuu? Namna mnavyosimamia utendaji wa kazi wa siku hadi siku kupunguza uzembe, uwajibikaji kuwa wa kiwango cha juu kumetufikisha kwenye mafanikio haya makubwa, tunawashukuruni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo mengi yamezungumzwa hapa watu hawajui tu. Mapato haya ongezeko lake yametupa faida gani? Mpaka sasa hivi ndani ya mwaka mmoja Bandari ya Mbamba Bay inajengwa, ujenzi wa matanki ya kuhifadhia mafuta tulilisema sana kwenye Bunge hili; Serikali sikivu imeanza kujenga na *speed* yake ni kubwa na ni nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kuna ujenzi wa bandari ya mizigo michafu Mtwara inajengwa kwa nguvu kubwa sana. Ujenzi wa gati mbili za mita 500 Dar es Salaam unajengwa kutokana na mafanikio haya. Kwa hiyo mimi hapa ninataka kuunganisha tu watu wasiseme mbona kumeongezeka hatuoni kitu? Mapato yameongezeka na shughuli za ujenzi zimeongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kazi inatakiwa kufanywa Mheshimiwa Waziri. Kweli Mheshimiwa Rais alisema aliwapa *timeframe* kwamba lazima treni ianze kazi na imeanza na

tumeona namna ambavyo watu wanasafiri kwa haraka wanaboresha shughuli zao. Juzi mimi kuna mtu alikuwa na mgonjwa Muhimbili lakini uji ameupika Dodoma mgonjwa akaenda kunywa Muhimbili kitu ambacho zamani kisingewezekana. Zamani isingewezekana uji umepikwa Dodoma umenywewa Muhimbili - Dar es salaam halafu jioni karudi anasema nilikuwa Dar es Salaam kumwona mgonjwa. Yaani watu wanakwenda wanateleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, kuna mambo ya kufanywa. Tunawapongeza sana kwenye reli *Engineer* Kadogosa, tunampongeza sana kwenye bandari *Engineer* Mbosa pamoja na Menejimenti yote wamefanya kazi kubwa sana watu wa manunuzi. Tumeona *Engineering* ikifanya kazi ya watoto wazalendo wazawa wa Taifa hili. Ndugu zangu tukiaminiana tunaweza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumeona namna ambavyo treni yetu inasimamiwa kwa usafi mkubwa na mabinti zetu wako hapa juu. Wamefanya kazi nzuri, wanatunza mazingira, wana lugha nzuri, yaani ukisafiri ni kama unasafiri Ulaya, hili ndiyo tulikuwa tunalitaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ya kufanya Mheshimiwa Waziri; kwanza elimu itolewe sehemu zote ambazo treni inapita. Kuna baadhi ya maeneo watu wanarusha mawe kwenye treni. Vitengo vyetu vya elimu, madiwani wa maeneo yale, wenyeviti wa Serikali za vijiji, sisi Waheshimiwa Wabunge tunayo *training* ya kutosha; kule ambako treni imeanza kazi na kule ambako itaenda kuanza kazi elimu itangulie kutolewa ili watu wajue hii treni ni mali yetu. Treni siyo ya kurushia mawe, mtu anataka kupima kasi ya treni na kasi ya jiwe, kidogo hivi vitu vinatuletea shida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo mimi ningeomba nishauri kwenye reli yetu ya kati kumekuwa na hujuma nyingi sana. Watu wanang'oa vyuma chakavu sana, wanapeleka abiria kuchukua muda mrefu sana kusubiri chombo; hii inakuwa si sawa. Kwa hiyo tunawaomba sana Serikali

muanzishe *operation* kwa watu wanaouza vyuma chakavu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila muuzaji wa chuma chakavu aweke bango kwenye Ofisi yake kwamba vyuma vya reli vya aina hii marufuku kuvileta hapa ili watu waelewe kabisa kwamba chuma cha reli uuzwaji wake una taratibu, hakiwezi kuuzwa hovyohovyo na hivyo kusababisha watu ku-*sabotage* reli yetu. Hii itatupelekea watu tukiheshimu miundombinu, tukaheshimu utaratibu, Taifa letu litasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya mambo mengine madogo madogo haya yasikuumizeni Waheshimiwa Wabunge. Mtu akisema *"no reforms no election"* wewe badilisha kidogo tu mwambie *"no election no reforms"* basi yaani inakuwa imekaa mahali pake. Hakuna uchaguzi hakuna mabadiliko. Uchaguzi ndiyo unaoleta nini mabadiliko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yatakujaje bila uchaguzi? Haiwezekani! Ni sawasawa unalazimisha umefunga jembe la kulimia na ng'ombe au umefunga mkokoteni na punda halafu unataka mkokoteni utangulie; mkokoteni utavuta punda? Haiwezekani. Ni lazima punda ndiyo atangulie kuvuta mkokoteni. Kwa hiyo lazima uchaguzi utangulie ili ulete mabadiliko. Jambo rahisi sana wala lisitupotezee muda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Livingstone Joseph Lusinde. Nilimwita Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge, ajiandae. *(Makofi)*

**MHE. ABUBAKARI D. ASENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa nafasi ya kupata dakika hizi chache na mimi kuchangia katika Wizara yetu ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama walivyosema wenzangu ni bahati iliyo njema kupata nafasi hii na mimi nataka kuanza kwa kutoa pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwanza kwa kuzigawa Wizara hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana leo tumesahau lakini nyuma Wizara ya Ujenzi na Wizara ya Uchukuzi zilikuwa ni Wizara moja na hapo ndipo ninapomuonea huruma Mheshimiwa Profesa Mbarawa wakati ule alipokuwa Waziri alikuwa akibeba mzigo wote katika ujenzi na katika uchukuzi. Sisi ambao tuko katika Kamati ya Bunge ya Miundombinu tunajua mzigo mkubwa ambao walikuwa nao lakini kwa maoni ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amezigawanya na leo tunapata matunda makubwa sana katika Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Profesa Mbarawa na Naibu Waziri wake hapa, *ex - DAS* kaka yetu mpole kabisa Mwakiposa na watumishi wote wa Wizara ninawapongeza sana. Pia, Wakurugenzi wote kuanzia *LATRA, TASAC, TPA, TRC, ATCL, TASHICO, TMA, TCAA, TAA, TAZARA, DMI* na Wakurugenzi wote kwa ujumla mnafanya kazi nzuri tumeiona kwenye Kamati na tunawapongeza sana katika utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa utekelezaji huu mzuri wa Chama cha Mapinduzi na Ilani yake kwa hakika tutashinda mechi zote zilizobaki japokuwa ile mechi moja ya "*no reform*" hatutaicheza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana Mheshimiwa Waziri kwa kubadilisha Sera ya Uchukuzi. Tumeona kwenye Kamati na mlitupatia semina kuna Sera ya Uchukuzi ya mwaka 2003 kwamba mtaibadilisha sasa safari hii mifumo yote ya usafirishaji itasomana. Hili ni jambo kubwa sana ambalo kwa kweli tunawapongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza katika shilingi 2,746,485,000,000 mnazoziomba na ulizozisema hapa, 95% inaenda katika bajeti ya maendeleo na 4.5% peke yake ni matumizi ya kawaida. Mkifanya kazi hii vizuri na kwa bidi mtaunga

mkono kauli ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kwamba tukiwekeza vizuri katika Uchukuzi, katika Bandari tutapata nusu ya bajeti ya nchi yetu na tutajikwamua sana kiuchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka kusema kidogo kwenye *SGR, TRC* na *TAZARA*. Nikwambie tu, nilikuwa ninarudia hotuba za nyuma za Wabunge kwenye Mabunge yaliyopita hapa. Nimeiangalia hotuba ya Mheshimiwa Heche akiwa Mbunge hapa, anaizodoa Serikali ya CCM kwamba, hiyo *SGR* hamtaijenga; rudieni hotuba zake mtasikia, anawaambia jengeni hiyo *SGR* muone. Ukiniruhusu nitakutumia *video,* nimesafiri kwenye *SGR* na Mheshimiwa Heche, alisinzia, na pembeni alikuwa na mtoto mzuri, mpaka tunashuka Dar es Salaam, anateremka kwenye *belt* zile mpaka chini. Ukiniruhusu nitakutumia hizo picha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ninataka nimwambie Mheshimiwa Heche, anazunguka huko anatapika maneno, anamkebehi Rais, familia yake na uongozi huu, lakini *SGR* kapanda na alivyokuwa Mbunge hapa alikuwa anabeza. *SGR* sasa inapendeza, kama alivyosema Mheshimiwa Lusinde, ina maua mazuri siyo kama yale ya *ATCL* ya malalamiko zamani, maua yanapendeza, safari inakuwa fupi. Hata Mheshimiwa Musukuma alikuwa analalamikia kwamba, maua yale yako mengi, lakini maua yale yana faida zake, na sote tunayaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini *SGR* imetusaidia kutoka saa tisa za Dar es Salaam – Dodoma kwa basi, sasahivi ni saa tatu; hilo ni jambo la msingi sana na halijawahi kutokea. Ushauri wangu kwa *SGR,* Dodoma, mnajaza foleni kwa kupeleka treni kule mwisho, Barabara ya Iringa, nimewaambia kuna mchakato wa kuweka kituo Stendi ya Mabasi ya Nanenane; wekeni na shusheni hata dakika tano pale kwa sababu, wananchi wengi wanatoka Dar e Salaam wanapanda mabasi ya kwenda mikoani hapa Dodoma. Unavyowapitisha unawapeleka Stendi ya Iringa inabidi warudi tena mjini, wanatengeneza foleni kubwa; shusha pale Nanenane dakika tano, lami imeshaungwa pale kwenda kwenye Kituo cha Mabasi cha Nanenane, halafu wengine wanaobaki

kwenda njia ya Iringa huko, Singida, wanaweza wakaendelea. Kwa hiyo, nataka kutoa ushauri huo, ni muhimu mkalizingatia jambo hilo kwa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maendeleo yanaletwa na mikakati na mipango. Nimeangalia hotuba za Wabunge wa CHADEMA wa nyuma, kaka yangu Nassari, ambaye sasahivi Mheshimiwa Rais kamteua kuwa, mkuu wa wilaya, nilikutananae juzi hapa akiwa *DC*. Nilimsalimia, "Kaka Nassari mambo vipi?" Akaniambia, "Salama ndugu yangu"; nikamwambia, "maendeleo vipi?".

Mheshimiwa Mwenyekiti, akasema, "aah bwana, maendeleo ni mchakato. Sasahivi nimekuwa mkuu wa wilaya ndiyo ninajua kwamba, kupiga kelele peke yake bila mipango hakutoshelezi maendeleo".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sasahivi yuko vijijini kule anahamasisha maendeleo na anaona ugumu wa maendeleo. Alitamani wagombea ubunge wote wa upinzani wawe ma-*DC* kwanza kabla ya kuanza kupiga kelele na kukosoa siku zote kwa sababu, kukosoa ni rahisi, lakini kujenga ni kugumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRC* wakamilishe kipande cha Mwanza – Tabora ambacho kiko 63% na Makutupora – Tabora kiko 14%; kamilisheni hivi, ili Watanzania wote waweze kupata raha. Nimeona kwenye taarifa yenu mnaboresha *MGR* na *SGR* na nimeona kwenye bajeti kuna kipande cha Kidatu – Kilosa, kilometa 108 kitaunganishwa na *SGR*. Hili ni jimbo langu, Kidatu imepooza, tunaamini mkiunganisha pale patakuwa na stendi nzuri na patachangamka sana. Kwa hiyo, tunawaomba sana mkamilishe jambo hili, ili tuendelee kukuza sekta ya uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa Mkataba wa *TAZARA*. Septemba 2024, *TAZARA* sasa itafufuka na wananchi wetu watapata mafanikio makubwa. Katika hii *TAZARA,* na Katibu Mkuu ananisikiliza, ardhi ya *TAZARA* iko Tanzania japokuwa tuna ushirikiano na Zambia, nimeleta barua kwako kuomba *temporary* ekari moja ya ardhi katika eneo lenye ekari 20; kuna soko, zaidi ya miaka 30 halmashauri haiwezi

kuendeleza soko lile kwa sababu, haijapata ruhusa ya kumiliki ardhi ile. Tumeomba kwa barua, tunaomba ekari moja katika soko la miaka mingi ambalo lipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halmashauri wapewe barua ya kutumia ekari moja, ili Mkurugenzi wa Halmashauri apate uhalali wa kutumia fedha za Serikali kujenga choo na mabanda. Hatutaki kujenga soko la ghorofa wala soko la nini, tunataka kujenga choo *temporary* na mabanda kwa sababu, ardhi ya *TAZARA* iko kwetu Tanzania tunaweza kuitumia, yatakapokuja mabadiliko baadae, mtabadilisha na mtatumia kwa vitu vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu bandari. Mmefanya uwezeshaji mkubwa wa bandari na Wabunge wengine wamesema hapa. Sasa ninajiuliza, mimi niko Kamati ya Bunge ya Miundombinu, hapa kuna taarifa kibao za kuboresha Bandari ya Nyasa, Dar es Salaam, Tanganyika, Ziwa Victoria, Mbegani Bagamoyo na Mtwara, sasa ule uongo ulikuwa unasemwa kwamba, bandari zimeuzwa katika nchi hii uko wapi? Mbona bandari zote ziko kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania ni lazima wawe makini na watu hawa. Nchi nzima walisema bandari zimeuzwa na kuna watu wamewaamini watu hawa, lakini Serikali inazimiliki bandari zote na inaendelea kuziboresha; za kuambiwa changanya na za kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *TPA* ni vizuri sana mkakamilisha, nimesema mara kadhaa hapa kuhusu reli ndani ya bandari. Tunaboresha bandari kavu ya Kwala, lakini kama treni haitoi makontena pale ndani bandarini tutaendelea kupata hasara kubwa sana katika nchi yetu kwa maana ya kwamba, hakuna *connection* ya reli ndani ya bandari na Bandari Kavu ya Kwala na hii ya Ihumwa. Kamilisheni jambo hilo, ili muweze kuleta maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASHIKO*. Ninapenda kusema kwamba, mnafanya kazi nzuri, pamoja na *TASAC* kwa kumalizia… ninaomba dakika moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninataka nisisitize, tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba, hatujapata ajali za maji, lakini hii *TASAC,* tumeona katika bajeti na mipango ya Serikali, inatakiwa ijiongeze itumie mapato ya ndani kununua maboti ya uokozi; lolote likitokea, sasahivi wanaweza kutafuta miili? Wanaweza kufanya uokozi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona boti moja limenunuliwa Uturuki, la *ambulance,* ndiyo linafika sasahivi kwenda Mwanza; waongeze, wanunue mengi kwa sababu, yanachukua muda mrefu kuyajenga. *TASAC* ipewe uwezo, itumie mapato ya ndani iweze kujenga ofisi na uokozi, lolote likitokea tuokoe maisha ya watu wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ila *no reforms,* hatuchezi. Japokuwa mechi zilizobaki tutashinda.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abubakari Damian Asenga, ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ng'anzi Ulenge na Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji ajiandae.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa nafasi ya kuchangia. Nimshukuru Mwenyezi Mungu mwenye enzi na utukufu kwa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo moyo wangu umejawa na shukrani. Natumia fursa hii kumpongeza sana na kutoa shukrani nyingi za dhati kwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa Profesa Makame Mbarawa, kwa Katibu Mkuu, pamoja na mtendaji wa Mamlaka ya Bandari kwa mapinduzi na mageuzi makubwa ya Sekta ya Bandari na Uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka ya karibuni tu Bandari ya Tanga tulikuwa tunatajwa tuna mwamba usiochimbika uliosababisha Bandari ya Tanga kujiendesha bila faida kwa sababu, meli zilikuwa hazifiki gatini, leo hii tunavyozungumza Bandari ya Tanga, ndani ya miezi sita, imezalisha shilingi bilioni 45. Moyo wangu umejawa na shukrani na hakika Mheshimiwa Rais amejivua gamba la *business as usual,* ameonesha ni Rais ambaye

hakubali kucheza kama vile watu wa zamani walivyokuwa wakisema, tumewaona baba zetu, kama hivi, wanafanya na yeye kuji-*limit* na kuji-*confine* hapo. Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mbarawa hakika mmefanya mageuzi makubwa katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaizungumzia Bandari ya Tanga, ambayo ninakwenda kujengewa barabara ya lami kutoka Handeni – Kiberashi, kama *toll road,* kutokana na mapinduzi na mageuzi makubwa ya Mamlaka ya Bandari. Kwa kweli, moyo wangu umejawa na shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni miaka ya karibuni tu tulikuwa tunazungumzia ma-gati ya bandari zetu kuu yamejengwa kwa *sheet piles* ambazo zilikuwa ni lazima ufanye *electrolysis* uondoe *hydroxyzine irons,* ili kuzuia chumvi isiweze kuharibu *sheet piles* zile. Leo tunazungumzia miundombinu ambayo ma-gati yamejengwa kwa zege nzuri na zimeongezwa meta kumi ndani ya maji, hakika ni mageuzi makubwa katika sekta hii ya bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mwaka 2000 tu tulikuwa tunazungumzia wizi wa mafuta bandarini; tulikuwa tunazungumzia upotevu wa mafuta na mapato bandarini. Leo tunazungumzia bandari zetu zenye *flow meter* za kidijiti, hakika ni mapindduzi makubwa katika Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka hivi karibuni tulikuwa hatuna chelezo, tunabeba meli tunazipeleka Mombasa. Leo hii hiyo imekuwa historia, hakika ni mageuzi makubwa katika sekta hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni juzi tu, ninakumbuka ambavyo tulikuwa tunahangaika na *cranes* zisizokuwa na uwezo wa upakuaji; tunatumia *cranes* ambazo mara kwa mara zinaharibika, tunapoteza fedha nyingi kwenye matengenezo. Leo hii tunazungumzia *ship to shore gantry cranes* ambazo zinaweza kuingia zenyewe mita 50 ndani ya maji kutokana na *rail space* yake. Hakika ni mageuzi makubwa kwenye sekta ya bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka vizuri tangu Awamu ya Kwanza ya Profesa Mbarawa katika sekta hii akiwa ni Waziri, enzi za Magufuli, alivyokuwa king'ang'anizi na mfuatiliaji wa karibu mpaka *Mr.* DK. Qube akawa anamuona nuksi pale bandarini, lakini leo tunayaona mageuzi makubwa kwenye Sekta hii ya Uchukuzi. Hakika moyo wangu umejawa na shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hivi karibuni tulikuwa tunazungumza namna ambavyo tunaweza tukapunguza muda wa utekelezaji, ili mtu ambaye yuko kwenye hoteli anakunywa kikombe chake cha kahawa anaiona meli yake namna ambavyo inasogea kwenye gati na namna ambavyo inahudumiwa. Leo tumeingiza TEHAMA katika utekelezaji wa shughuli za kibandari na tunayaona mafanikio yake. Moyo wangu umejawa na shukrani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiukweli ninaona fahari kubwa kwa mapinduzi makubwa yaliyofanyika katika Sekta hii ya Bandari na kipekee, hili la kuhakikisha tumepata *private sector* kuweza kuiendesha bandari. Vijana wa bandari walikuwa wanabembelezwa kuingia *DP World* mpaka mkurugenzi mkuu anawaongezea mishahara, nendeni mkahudumu; kwa kweli, ni mapinduzi makubwa kwa sababu, mimi nimekuwa pale, nilikuwa ninaona *treatment* ya wafanyakazi ikoje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii bandari imetulia. Hakika ni mapinduzi makubwa na ni pongezi kwake kijana, ambaye yuko *very well composed,* Plasduce Mbossa. Anafanya kazi kubwa vizuri zaidi na niwaambie vijana wengine mlioaminiwa katika nafasi hizi, jitahidini kujifunza kupitia Mbossa, yuko *very well composed* na bandari imetulia; bandari ilivyokuwa juzi, sivyo ilivyo sasa hivi. Hakika mmeleta mageuzi makubwa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikumbushe, nilisema haya wakati wa mchango wangu wa kwanza katika Sekta ya Bandari, leo ninakwenda kutimiza miaka mitano, mmefanya mengi makubwa ya kimapinduzi katika sekta hii. Ninaomba niikumbushe bandari, mengi mmefanya, lakini bado tusipotafuta *mechanism* na kufanya tafiti ya kujua namna ambavyo tunaweza ku-*control sedimentation* na kina cha bahari kupungua, bado

kutakuwa na *challenge* mbele yetu. Niwaombe sana Mamlaka ya Bandari pamoja na Wizara husika kuwekeza katika kujua ni kwa nini kuna *sedimentation rate* kubwa na kwa nini kina kinapungua katika bandari zetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje na *mechanism* ambayo italinganisha *dragging* na kuchimba. Tuone ipi ina thamani ndogo, kuweza kuleta matumizi yaliyosahihi katika sekta ya bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa reli ya kisasa na kwa ujenzi mkubwa unaoendelea, ambao kidunia ni nchi mbili tu ndizo zinaweza kutekeleza mradi mkubwa kama huu wa reli wa nchini Tanzania, ni China na Saud Arabia pekee ndiyo zinaweza kutekeleza mradi huu ambao ukikamilika kilometa zake 4,700 hakika Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mama wa Kizimkazi, ambao walimchukulia poa, aisee wakae kisawasawa. Inabidi tu wazoee kwamba, Dkt. Samia Suluhu Hassan mambo yake siyo ya kitoto, anashindana na China na Saud Arabia kuwa na mradi mkubwa kama huu. Hakika ni mageuzi makubwa katika sekta ya uchukuzi na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kumalizia. Ninaomba nizungumzie viwanja vya ndege; ninaomba nikizungumzie Kiwanja cha Ndege cha Msalato. Kiwanja kinajengwa, ombi langu ni kuhakikisha hatukifanyi kikawa kama Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam; hakiwi *Vingungutilised,* lazima tuweke miundombinu inayoendana na kiwanja cha ndege cha kimataifa. Ni lazima kuwe na *land use plan* nzuri kuzunguka Msalato *Airport* kwa maana ya hoteli, *business centres* na mambo mengi, ili kuendana na kiwanja cha ndege cha kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuhitaji Msalato *Airport* iwe *Vingungutilised,* tunahitaji Msalato *Airport* iwe *airport* ya Kimataifa, ya mfano. Tujifunze kutokana na makosa ya kiwanja cha ndege kingine cha kimataifa ambacho tunacho nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalize kwa kusema kwamba, *design* ya Kiwanja cha Ndege cha Msalato

inazungumzia kubeba *passengers* milioni moja na laki tano kwa mwaka, wakati kiwanja ambacho kipo sasahivi tunazungumzia *passengers* laki moja na hamsini mpaka laki mbili na hamsini kwa mwaka. Maana yake ni lazima kuweka mikakati ya namna gani tutaongeza *capacity* ya *passengers* hao ku-*attract more investors* Mjini Dodoma kwa ku-*attract* vivutio zaidi Mjini Dodoma, ili kiwanja cha ndege kile kiweze kuingiza idadi hiyo ya *passengers* kwa ku-*return* mapato ambayo yatawekezwa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, moyo wangu umejawa na shukrani. Hongera sana Profesa Makame Mbarawa, Dkt. Samia Suluhu Hassan na Kadogosa kwa kazi kubwa kwenye miundombinu yetu ya reli. Mnaupiga mwingi, *big up* sana. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja 105%.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile ajiandae.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Awali ya yote kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kuwa na hali ya uzima na afya, lakini ninawashukuru na wenzangu wote humu Bungeni, sasahivi ninawaona wako wazima na wana afya njema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Waziri wangu, kaka yangu, Makame Mnyaa pamoja na Naibu wake kwa kazi kubwa anayoifanya katika Wizara hii; mimi niko Kamati hii ya miundombinu, nimetembelea mambo mbalimbali katika miundombinu. Nimetembelea bandari, nimetembelea viwanja vya ndege, lakini pia nimetembelea treni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana ndugu yangu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa hatua kubwa aliyoichukua na

anaendelea kuchukua. Ni Mheshimiwa mwenye maono, anayeona mbali na kisha anatekeleza. Mwenyezi Mungu amwondolee shari na ampe heri, amjalie uzima yeye na wanaoongoza nyuma yake, ili aweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wengi wamezungumzia mazuri sana na mimi niseme ukweli, mazuri yapo, lakini kitu chochote kilicho kizuri hakikosi kasoro. Kitu kikiwa kizuri ni lazima na kasoro itakuwepo, mimi katika kusafiri kwangu, sasahivi ninatembelea sana treni, ninatoka hapa mchana ninaingia kwenye treni jioni na usiku; ukiingia treni ya usiku tu unaambiwa uvutaji wa sigara hautakiwi, lakini pombe inanywewa na inakuwa hatari. Sijui hii Serikali kama inalitambua hili jambo au vipi? Kutuharibia katika safari zetu za treni! Tunapendeza mule wenyewe tukikaa, vichwa vinatulia tu mpaka usingizi unakuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pombe mule imezidi, Mheshimiwa Waziri unanisikia? Kaa kitako na wenzio, wafanyakazi, uwaambie watulie, wanywaji wanapiga kelele na wanacheza ngoma wala hazimo! Mheshimiwa Waziri hili nimeliona, changamoto hii ni kubwa katika treni zako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa kweli, wenzangu wamezungumza treni zinafanya kazi vizuri, ni za kisasa na wala hapa Tanzania haijapata kutokea. Yote hayo msimamizi ni Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**MBUNGE FULANI:** Endelea, endelea.

**MHE. MWANTUMU DAU HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, jingine ninazungumzia kuhusu ndege. Ndege zetu sasahivi hazina matatizo, zinakwenda vizuri. Yaani utasema hizi ndege ni kama zinajipangilia kwa sababu, wanaona kuna ushindani wa safari. Watu wengi wanakwenda kwenye treni na huku ndani ya ndege sasahivi hata zile nauli kidogo zimepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kuna huku ku-*delay,* ndege unaambiwa saa tatu, unaenda, matokeo yake huondoki mpaka saa tano za usiku, hili nalo lirekebishwe. Ndiyo maana nikasema

panapo uzuri hapakosi kasoro, hiyo ndiyo kasoro niliyoiona katika ndege sasahivi. Unaenda safari yako ufike kwa wakati, lakini hufiki kwa wakati, unabaki kukaa pale mpaka unachoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, inakuja ndege pale saa tano ndiyo unaondoka unaenda zako nyumbani, hilo ndilo nililoliona. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ukae kitako na wenzio wajitahidi, hizi ndege zinapotoka hizo safari zije huku kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala langu la tatu, ni kuhusu bandari: bandari zetu zimesifiwa hazina wasiwasi. Kuna bandari za nchi kavu, lakini pia kuna bandari za baharini. Hapa kwenye Bunge lako Tukufu lilitoa suala la kuhusu habari ya maboti na Naibu Waziri Kihenzile akaniambia kuna maboti yatatengenezwa na kuletwa tuondokane na urasimu wa maboti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aboti tunatoka nayo Zanzibar kuja nayo huku Dar es Salaam yanajaa sana, mtitiriko wa maboti haujawahi kutokea nalisema hili na wenzangu wanalijua ni kweli. Kwa hiyo, tunafika pale mbanano watu hawatulii kwenye maboti wamesimama, hata tukifika pale taabani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba Serikali hilo boti walililotaka kutulea la kuanzia bahari ya maziwa mpaka kuja kwenye bahari hii watuletee itakuwa ya Serikali, labda itakuwa afadhali na upandaji wetu itakuwa afadhali. Halafu na wale wasimamizi wanaoangalia yale maboti kwa sababu niliuliza, je, hawa watu wanaoangalia haya maboti hawapo au hawafanyi kazi vizuri? Kwa hiyo, Naibu Waziri, Kihenzile akaniambia hawa watu wapo na hii meli haiwezi kuondoka kama haijaangaliwa lakini naona si kweli hawapo! Kwa hiyo, tuletewe meli yetu tuingie mle kwa usalama na amani ili tuweze kusafiri vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja, 100% ahsante sana Waziri, ahsante sana Naibu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwantumu Dau Haji. Kabla sijamtaja mchangiaji anayefuatia tuna wageni ambao wapo muda huu hapa Bungeni.

Tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni wa Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa ambaye ni Waziri wetu wa Uchukuzi hawa ni Wakurugenzi na Wakurugenzi Wasaidizi na Maafisa kutoka Wizara ya Uchukuzi, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wawakilishi kutoka Taasisi za fedha *NMB, NBC, TBC* na Azania Bank karibuni sana wawakilishi wa taasisi zetu za fedha. *(Makofi)*

Tunao wawakilishi wa mashirika, makampuni, taasisi na vyama vya kitaalam na wasafirishaji, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao wawakilishi wa Klabu ya Michezo ya Wizara ya Uchukuzi iliyofanya vizuri katika mashindano ya Mei 1, 2025 na kupata makombe mbalimbali, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Marubani na Wahudumu wa Kampuni ya Ndege ya Tanzania *(ATCL)* karibuni sana. *(Makofi)*

Makofi ya Waheshimiwa Wabunge yanaashiria huduma yenu njema Mwenyezi Mungu awajalie muendelee vizuri.

Tunao Wahudumu wa Treni ya Kisasa ya Umeme *(SGR)* kutoka Shirika la Reli Tanzania. Karibuni sana Wahudumu wetu wa Treni hayo ni maua yenu kutoka kwa Waheshimiwa Wabunge naamini huduma yenu itaendelea kuwa nzuri kwa Watanzania na Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi/Vigelegele)*

Wawakilishi wa Manahodha kutoka Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania, Kampuni ya Meli ya Tanzani *(TASHICO)* na Chuo cha Bahari Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao mgeni wa Mheshimiwa Daktari Florence George Samizi Ndugu Doreen Lyimo Mdau wa Taasisi ya Wanawake na

Maendeleo kutoka Kibondo Mkoa wa Kigoma, karibu sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Simon Songe Lusengekile, Mheshimiwa Amina Ali Mzee ajiandae.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kunipa nafasi nami nichangie Hotuba ya Waziri wa Uchukukuzi. Kwanza, nianze kwa kumpongeza sana Waziri wa Uchukuzi pamoja na Naibu wako kwa kazi kubwa mnazofanya kwenye Wizara yetu ya Uchukuzi. Pia, nimpongeze sana Katibu Mkuu na Watumishi mbalimbali waliopo kwenye Wizara hii ya Uchukuzi, kwa kweli kazi kubwa zinaonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzangu wamezungumza sana habari ya bandari, nami niungane nao kupongeza sana kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa iliyofanyika kwenye bandari yetu hasa ya Dar es Salaam. Kwa kweli, kazi kubwa imefanyika na tumeona upanuzi wa uboreshaji wa miundombinu ya bandari umeendelea kuongezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakika Mama Samia amefanya kazi kubwa, hakika Watumishi wa bandari zetu wamefanya kazi kubwa, wakiongozwa na Kaka yetu Mbosa wamefanya kazi kubwa sana kwenye bandari yetu ya Dar es Salaam. Kwa kweli tunawapongeza sana na Mama Samia tunampongeza sana kwa maamuzi aliyoyachukua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia, nilipongeza sana Bunge mwaka jana 2024, kwenye Bajeti Kuu tulipitisha kwamba makusanyo ya *Wharfage* sasa yaanze kukusanywa na *TPA*. Tumeona maendeleo makubwa baada ya makusanyo haya kuwa yameanza kukusanywa na *TPA,* tumeona makusanyo yameongezeka kutoka bilioni 476 kwa mwaka 2023/2024 kwa maana ya kuanzia Julai - Machi, pia kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Julai – Machi makusanyo yameongezeka kwa bilioni 22 kwa maana ya kuleta jumla ya bilioni 499. Haya ni mapinduzi makubwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam na bandari zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona uboreshwaji wa maeneo, wenzangu wamesema Bandari ya Mwanza imeendelea kuboreshwa, Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa matenki, pia gati namba moja mpaka gati namba saba, upembuzi yakinifu wa gati namba nane mpaka 11, gati namba 12 mpaka gati namba15 tunaona maendeleo makubwa sana yamefanywa na nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Mama Samia ananikumbusha hadithi moja ya Yohana Mbatizaji alipokuwa gerezani baada ya kutembelewa na wafuasi wake, na aliamini kwamba kwa kuwa Yesu anaweza kila kitu aliamini atatoka gerezani kwa miujiza. Na akauliza akawaambia wale wafuasi nendeni mkamuulize Yesu je, ni yeye au tunasubiri ajaye? Yesu akawajibu akawaambia nendeni mkamwambie wafu wanafufuka, viwete wanatembea pia vipofu wanaona. Kiongozi mzuri hapimwi kwa maneno, kiongozi mzuri anapimwa kwa kazi na Mama Samia tumempima kwa kazi kubwa na amefanya kazi kubwa kwenye Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Watanzania leo tukiulizwa kwamba, nendeni mkamuulize yeye ndiye au tusubiri ajaye tutasema yeye ndiye kwa sababu ya maendeleo makubwa ambayo tumeendelea kuyaona kwenye Taifa letu hasa kwenye bandari na kwenye *SGR*. Wenzangu wamechangia sana suala la *SGR* kwa kweli hapa ndipo tumeona maendeleo makubwa ya nchi yetu na sasa tunaenda kwenye uchumi, tunaamini kazi itaendelea kufanyika, tuendelee kumuunga mkono Mama Samia, tuendelee kukiunga mkono Chama Cha Mapinduzi, makubwa yanaendelea kuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo moja kwenye eneo la *SGR*. nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri pamoja na wasaidizi wako Kaka yangu Kadogosa, umeendelea kufanya kazi kubwa kwenye eneo la *SGR* hongera sana endelea kufanya kazi hii kwa sababu ni eneo ambalo tunalihitaji kwenye nchi yetu na kazi hii inakuhusu wewe kama maandishi ya Biblia yanavyosema Ezra 10:4 kwamba kazi inakuhusu wewe, nyanyuka nenda na kaitende. Kadogosa unafanya kazi njema sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna *study* zimefanyika huko nyuma za ujenzi wa reli ya kisasa kuanzia Arusha kuja Makuyuni, kuja Simiyu pale Dutwa, kupita Lamadi Busega, Bunda kwenda mpaka Musoma. *Study* hizi sasa nendeni mkazifanyie kazi tunatamani huko mbeleni kuona mpango wa Serikali kwenye ujenzi wa reli ya kisasa kwa maana ya *SGR* kutoka Arusha kwenda mpaka Musoma kupitia Simiyu Mkoani kwangu, Busega Jimboni kwangu, Bunda kwa Bwana Getere na hadi Musoma. Na tunaamini ujenzi wa reli hii utakapokamilika uchumi wa wananchi utaongezeka, uchumi wa nchi utaongezeka, usafirishaji wa mizigo, usafirishaji wa mazao pia utaongezeka na utawarahisishia wananchi wetu Watanzania katika suala zima la kusafirisha mizigo na usafiri wa wao kwa wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Kaka yangu Kadogosa, niombe sana mkubwa wangu Mheshimiwa Prof. Mbarawa kuangalia *study* hii ambayo imefanyika huko ili tuwe na mpango wa ujenzi wa reli ya kisasa kuanzia kule Arusha kuja Simiyu na kwenda mpaka Musoma. Mafananikio makubwa tutayapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wakati tunasoma shule ya msingi tulikuwa tukiangalia zile sinema anakuambia hiyo *trailer* muziki baadaye. Tumeona *trailer* ya *SGR* hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam, tumeona mafanikio makubwa haya, tumeona wananchi wananufaika na *SGR* hii. Tuna imani kubwa *SGR* pia ya kutoka Arusha kwenda Musoma itawanufaisha Watanzania, itawanufaisha wananchi wa Simiyu na wananchi wa Jimbo la Busega.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale Dutwa kuna madini ya *Nickel* nafikiri pia usafirishaji utaendelea kupitia *SGR* na kwa sababu mapato yetu yatazidi kuongezeka kupitia aina hii ya usafirishaji kwa kutumia *SGR*. Ni imani yangu kubwa *study* hii mtakapoifuatilia na kuja na mpango sisi kama Wabunge tutawapitishia mpango na kwa sababu wananchi wa Jimbo la Busega wamesema bado wanatamba nami najua nitakuwa hapa nitaendelea kuwapitia bajeti yenu ili muende kufanya kazi ya ujenzi wa reli ya kisasa kuanzia kule Arusha kwenda Musoma. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nusu dakika ni kwamba nimemuona hapa Kaimu Waziri Mkuu mzee wangu Mkuchika niseme tu jambo moja. Wizara ya Katiba na Sheria walikuja na kampeni ya Samia *legal campaign*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba msimamizi wa shughuli za Serikali hapa Bungeni, siku ya tarehe 15 Juni, 2025 *Derby* ya Simba na Yanga tuipe jina ya Samia *Derby campaign* ili tuendelee kumuunga mkono Mama Samia ili tuendelee kuunga mkono michezo katika nchi yetu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika achukue hilo alipeleke mje na mpango, mje na Sami *Derby Campaign* na ambaye hatapeleka timu tutaona ana matatizo.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. SIMON S. LUSENGEKILE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Hatuchezi.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana nilimtaja Mheshimiwa Amina Ali Mzee, Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane ajiandae.

**MHE. AMINA ALI MZEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia uhai na uzima nami kupata nafasi hii ya kuchangia Bajeti hii ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na Watendaji wote wa Sekta ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mapinduzi makubwa ambayo ameyaleta ndani ya sekta hii ya uchukuzi. Leo hii Tanzania tunajionea, tuna reli, tuna ndege, tuna meli, Daktari Samia ndio ambaye amezileta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapinduzi haya makubwa katika sekta ya uchukuzi Daktari Samia amedhamiria dhahiri kuhakikisha Tanzania inaendelea ndani ya sekta ya uchukuzi. Tuna kila hatua ya kuhakikisha Daktari Samia tunamrudisha tena katika urais 2025. Nimpongeze sana Daktari Samia kwa kuendelea kuhakikisha sekta ya uchukuzi inaendelea kupiga hatua katika nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijikite katika mchango wangu. Sekta ya Uchukuzi ina vyuo mbalimbali. Vyuo ambavyo vinazalisha elimu na ujuzi mbalimbali kwa vijana wetu. Ndani ya sekta hii ya uchukuzi kuna Chuo cha *NIT*, Chuo cha DMI, Chuo cha Usafirishaji, vyuo vyote hivi vinazalisha nguvu kazi ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Chuo cha Usafirishaji, Serikali imeeleza ndani ya bajeti hii juu ya ununuzi wa *flight simulator* kwa ajili ya wananfunzi. *Flight simulator* hii itakwenda kuchochea, kukuza uelewa wa wanafunzi wetu ambao wanazalishwa ndani ya Chuo cha Usafirishaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Watendaji ambao wapo ndani ya sekta ya uchukuzi mchukue tahadhari na jitihada za makusudi kuhakikisha mnakwenda kutoa elimu juu ya uzalishaji wa marubani katika Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona na mmeeleza juu ya uchache wa Marubani ambao wapo ndani ya Taifa hili. Twende tukatumie vifaa ambavyo vimeletwa ili kuhakikisha tunazalisha

Marubani wanaoweza kuendesha ndege ambazo Rais wetu ameendelea kuzinunua ndani ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna Chuo cha Reli. Tuna reli ambayo inaendelea ya *SGR*. Reli yetu ya *SGR* inahitaji ujuzi na uelewa na ufanisi mkubwa. Teknolojia inayotakiwa kuendeshwa ndani ya reli hii ni ya hali ya juu, tuendelee kutoa elimu kwa vijana wetu juu ya matumizi mazuri ya reli, uendeshaji pia utunzaji wa miundombinu ya reli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli yetu Serikali imetumia fedha kubwa kuhakikisha reli inaijengwa. Kwa hiyo, kwa makusudi tuhakikishe reli hii inajengwa lakini inatunzwa, vipi itatunzwa na vipi itatunzwa na vipi itaendelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu kubwa inahitajika kuwekezwa kwa Chuo chetu cha Reli kuhakikisha wanawapa *training* ya kutosha juu ya ujenzi wa miundombinu ya reli, vichwa vya treni pia uharibifu utakapotokea jinsi gani hatua za haraka za kuhakikisha wanaweza kutengeneza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuhakikisha jinsi gani wanaweza kuendeleza ujenzi wa meli. Tuna ujenzi ambao unaendelea wa meli ndani ya Maziwa Makuu. lakini tuchukue jitihada za makusudi kuwawezesha vijana, kuwajengea elimu juu ya kuweza kutengeneza meli hizo. Meli zitakuwepo na zitaendelea kubakia, wataalam wataondoka. Tuhakikishe wataalam ambao wamekuja kutengeneza meli zile wanawapa *knowledge* ya kutosha vijana wetu ili waweze kuhakikisha wakiondoka *knowledge* ile itaendelea kubakia na kuliendeleza Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kuipongeza Serikali inayoongozwa na Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kuleta maendeleo ndani ya sekta hii ya uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina mengi naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Amina Ali Mzee, nilimtaja Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Davis Mwakiposa Kihenzile Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia kuhusu Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitangulie kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa uwekezaji mkubwa ambao ameufanya katika sekta hii ya uchukuzi. Kwa kweli Serikali yetu ya Awamu ya Sita imetumia fedha nyingi kuwekeza katika Bandari ya Mtwara, Dar es Salaam pia bandari zilizoko katika maziwa makuu kwenye upande wa usafirishaji, vyombo vya usafiri kama meli pia hata bandari zenyewe na mazingira yake pamoja na viwanja vya ndege vimeboreshwa. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Rais Daktari Samia Suluhu Hassan, kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikupongeze Mheshimiwa Waziri, wewe ni Waziri Makini, Profesa Mbarawa umefanya kazi kubwa kwa kushirikiana na msaidizi wako Mheshimiwa Kihenzile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina jambo moja kubwa la msingi ni kuhusu shughuli za usafirishaji na usafiri katika mikoa ya Kusini. Kwa muda mrefu hadi Bunge hili tulipokuwa tunachangia kwenye Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu na bajeti zingine ikiwemo ya Wizara ya Ujenzi. Wabunge wengi wa mikoa ya Kusini tulikuwa tukihimiza kwamba, kipaumbele chetu cha kwanza katika huduma ya uchukuzi ni suala la barabara. Kipaumbele cha pili tulisema ni barabara, kipaumbele cha tatu ni barabara. Na hii ilitokana na kutokuwa na usafiri wa aina nyingine katika hiyo mikoa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa nafikiri sasa kupitia Wizara ya Uchukuzi, twende na vipaumbele vitano. Kipaumbele chetu cha kwanza kibaki kuwa barabara, kipaumbele cha pili, kiwe ujenzi wa *SGR* kutoka Dar es Salaam kwenda mpaka Mtwara, kutoka Mtwara mpaka Mbamba bay.

Pia, kuwe na *branch* kutoka kule Mbamba bay kwenda Liganga na Mchuchuma, kwenda Songwe hadi Kiwira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu wilaya zetu za Mikoa ya Lindi, Mtwara, Ruvuma sasa hivi zina *resources* nyingi na kuwepo kwa usafiri wa barabara peke yake tulishuhudia mwaka jana 2024 na mwaka huu 2025, barabara yetu ikiwa imekatika sana, imeharibika mara kwa mara na kwa hivyo kusababisha shughuli za usafiri kusimama kwa wakati fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *volume* au wingi wa mizigo umekuwa ukiongezeka hasa baada ya kufunguliwa Kiwanda cha *Cement* cha Dangote lakini yanapatikana madini ya jasi kule Kilwa kwa wingi sana yanatumia barabara hiyo hiyo. Pia hata makaa ya mawe yanayopatikana kule Ruvuma nayo yanapita katika barabara hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii imesababisha barabara kuchakaa mapema na kuharibika mara kwa mara hasa baada ya tufani ya Kimbunga Hidaya na Mvua za *El Nino*. Kwa hiyo, niombe wizara iangalie haya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa *SGR* kama nilivyosema hayo maeneo yaangaliwe kwa mara ya kwanza tupate *SGR* inayotoka Lindi kwenda mpaka Mtwara kupitia Kilwa. Itaweza kubeba hizo rasilimali zote zilizopo pamoja na mazao ya korosho na ufuta kuweza kuyapeleka bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa bandari, tunayo bandari yetu ya Kilwa ya uvuvi ya kisasa kabisa inajengwa pale na iko zaidi ya 80% imeishakamilika. Wizara yetu ya Uchukuzi iliwahi kutufahamisha Wanakilwa kwamba ile bandari itajengewa gati ya kuweza kuchukua abiria na ikipatikana ile gati itakuwa na umuhimu mkubwa kwa ajili ya usafirishaji wa mizigo na abiria kwenda nchi ya jirani ya Comoro. Pia itawezesha usafirishaji na usafiri kwenda Mafia, Zanzibar, Pemba, Dar es Salaam, Tanga na mwambao wote wa Bahari ya Hindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mheshimiwa Waziri atakapokuja ku-*wind up* hotuba yako tunaomba utupe neno kidogo litakalowaletea faraja wana kusini kupitia bandari hii. Gati hii mpya ambayo ilipangwa kujengwa katika Bandari ya Kilwa. Lakini pia Bandari ya Lindi kwa miaka mingi hatujaona ikifanyiwa uendelezaji niombe Serikali iangalie pia Bandari ya Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kwenye usafirishaji uundaji wa meli. Hizi bandari zote zinazoboreshwa nyingi Taasisi yetu *TASHICO* imekuwa ikitumika kujenga meli hasa kwenye maziwa makuu, kule Ziwa Victoria kuna meli mbili zipo katika hatua mbalimbali za uundaji wake. Ukienda Ziwa Tanganyika *MV* Liemba inakarabatiwa lakini kuna *MV* Mwongozo inafanyiwa matengenezo. Kwa hiyo, msisitizo kupitia taasisi yetu ya *TASHICO* pia ijenge meli katika Mwambao wa Bahari ya Hindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili hizi bandari tunazozijenga ikiwemo ya Dar es Salaam, Tanga na uhimarishaji wake unaofanyika, ukarabati wake unaofanyika uweze kuleta tija kubwa zaidi kwenye usafirishaji wa mizigo, abiria na kadhalika ili kupunguza lile tatizo barabara ikikatika basi mambo yanakuwa hayaendi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la viwanja vya ndege. Nimesoma hapa katika *Paragraph No*. 126 sijaona Viwanja vya Ndege vya Kilwa, Nachingwea, Lindi kama kuna chochote kimetengwa kuhusiana na hivyo viwanja. Imezungumzwa tu kwa ujumla wake maboresho ya *ITCL* tunashukuru yanaenda vizuri na mambo yanakwenda vizuri. Lakini bado nilifikiri Serikali ingekuja na jambo katika viwanja vya ndege hivi nilivyovitaja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ukienda pia kwenye viwanja vya ndege tunashukuru wenzetu wa *TAWA* kule Miguruwe – Kilwa Kaskazini wanajenga kiwanja chao cha ndege. Lakini pia nilifikiri wanapaswa kuungwa mkono na Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla nilikuwa na hayo naipongeza sana Serikali, nampongeza sana Mheshimiwa Rais na

niwaombe Watanzania wote tukampe miaka mitano tena Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nasema naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Kumba Ndulane, haya ahsante sana. Nilimtaja Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mheshimiwa Naibu Waziri ajiandae.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana nami kwa kunipa nafasi niweze kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu ili niweze kuchangia hii Bajeti ya Wizara ya Uchukuzi. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wetu, Makame Mbarawa na Naibu wake Kihenzile lakini na timu nzima ya hii Wizara ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza kwa hatua kubwa hatua mbalimbali ambazo wameendeleanazo katika kuhakikisha kwamba wanatuletea mapinduzi makubwa katika hii Sekta ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimewahi kufanya kazi na Mheshimiwa Waziri Profesa Mbarawa kwa kweli ni Waziri ambaye msikivu yeye hasubiri kukaa ofisini ili mtu aende kupeleka hoja. Mahali popote unapokutananae unapomweleza hoja yako wakati huo anaisikiliza na kuweza kuifanyia kazi. Mwenyezi Mungu aendelee kubariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kumpongeza Dkt. Samia Suluhu Hassan, Mheshimiwa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa namna ambavyo ameleta mapinduzi makubwa katika sekta hii na ukiangalia hotuba ambayo imesomwa na Waziri hapa kwa kweli hatuna cha kusema zaidi ya kuendelea kumuombea Mheshimiwa Rais wetu ili Mwenyezi Mungu aendelee kumwongoza. Kwa sababu sasa

tunaelekea katika mapinduzi makubwa ya hii Sekta ya Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu Mradi wa *SGR* umekuwa mkombozi mkubwa sana lakini tumeona hatua mbalimbali ya kuendeleza *SGR* hata kule Kusini kutoka Mtwara kilomita 371 kwenda Mbamba *bay* pamoja na maunganisho ya maeneo mengine. Sisi kwetu tunaona kwamba ni mapinduzi makubwa na tunaamini kwamba mradi huu kadri ambavyo unaendelea na sisi wana Lindi kutoka Lindi kwenda Kibiti kuja Dar es Salaam kiunganishi cha kutoka Mtwara tutakwenda na *SGR*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme tu ya kwamba niishukuru Serikali kwa hatua mbalimbali ya kutuletea mradi huu wa Ujenzi wa Chuo cha *NIT,* chuo hiki tulikata tamaa lakini tunashukuru kwa hatua mbalimbali ambazo zimesimamiwa kupitia hii Wizara ya Uchukuzi na sasa chuo hiki kinakwenda kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Waziri nikushukuru sana kwa sababu nilikuwa ninakukera sana juu ya ujenzi wa chuo hiki lakini sasa nimeona katika taarifa ambayo leo umeisoma sasa tunaelekea kwenye utekelezaji wa ujenzi wa chuo hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wana Lindi tunaona kwetu ni mapinduzi makubwa, kwa sababu tulikuwa na kilio cha muda mrefu Lindi tangia ianze ilikuwa haina chuo hata kimoja. Lakini leo tunazungumza tuna vyuo karibia vinne, vitatu viko katika hatua mbalimbali za ujenzi lakini tuna chuo cha madaktari pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi kwetu tunaona kwamba tunaendelea kupiga hatua mwaka hadi mwaka na tunasema ya kwamba sisi tuna deni kubwa na Dkt. Samia Suluhu Hassan. Dkt. Samia Suluhu Hassan siyo wakuja kuomba kura Lindi, sisi wana Lindi tuna kila namna ya kuhakikisha kwamba Dkt. Samia Suluhu Hassan anashinda kwa kura nyingi za kishindo. Kwa sababu hatuna cha kumshukuru zaidi ya kwenda kumpigia kura nyingi na

endelee kuwa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uboreshaji wa Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Lindi. Nimeona katika taarifa ya bajeti na nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri sasa ninaona kwamba tunaelekea kwenda kwenye utekelezaji wa uboreshaji wa uwanja huu, kwa sababu kwa miaka minne mfululizo unawekwa ndani ya bajeti lakini utekelezaji wake hauonekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe uwanja huu una historia yake. Kwanza tumerithi kutoka kwa wakoloni lakini uwanja una *run way* nane ni uwanja mkubwa kuliko uwanja mwingine. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Waziri ninajua kwamba anatamani kuhakikisha kwamba uwanja ule unaboreka. Changamoto kubwa iliopo ni upatikanaji wa fedha lakini ninaamini kwa sababu sasa hivi upo katika hatua nzuri ya utekelezaji na umeishapitia hatua mbalimbali, maana yake sasa unakwenda kwenye utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Ndulane ameongea, kipaumbele chetu cha Wabunge wote wa Mkoa wa Lindi na Mtwara ni Barabara. Sisi tuna changamoto kubwa sana ya barabara na hatuna njia nyingine mbadala ya kusafiri kwa sababu hatuna ndege inayokuja Lindi na uwanja haueleweki. Lakini hatuna bandari japokuwa bandari ipo. Miaka ya ukoloni ya nyuma ilikuwa *MV* Mapinduzi inafunga gati Lindi lakini leo hatuna cha kuzungumza juu ya bandari ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Waziri. Kwanza kuhakikisha kwamba barabara yetu inayotoka Dar es Salaam – Kibiti – Lindi – Mtwara tuendelee kuiboresha kwa kiwango kikubwa. Hali ya barabara imekuwa mbaya mno, watu wanashindwa kusafiri, watu wanashindwa kusafirisha mizigo pamoja na kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sisi tuliamini kwamba sasa tunakwenda kwa hatua kubwa kupiga hatua kubwa za kiuchumi katika kuufanya Mkoa wetu wa Lindi sasa usonge mbele kimaendeleo lakini tunarudi nyuma kwa sababu ya barabara siyo nzuri hakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyabiashara wadogo wadogo sasa wameamua kutumia Bandari ya Lindi, Lindi kuna meli ndogo ndogo ambazo zinafunga gati pale kupakia. Wanapakia mbuzi, kuku, nazi, maembe, mihogo na bidhaa mbalimbali zinakwenda Comoro. Kutoka Lindi kwenda Comoro ni pafupi kuliko Dar es Salaam kwenda Comoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana Serikali itusaidie kuhakikisha kwamba pamoja na udogo wake uliopo watukarabatie Bandari ya Lindi sasa tufungue fursa za kiuchumi ambazo tunazitarajia Lindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua kwamba uchumi wetu utakua lakini bandari yetu itatumika mapato ya Serikali yatapatikana lakini kuhakikisha kwamba ajira kwa vijana wetu zitapatikana. Kwa hiyo, nimuombe sana Profesa Makame Mbarawa aone namna gani ya kuweza kutusimamia kuhakikisha kwamba tunaboresha bandari ile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho nimuombe katika kuzunguka uwanja wa ndege palikuwa na wananchi ambao wamekaa kwa muda mrefu zaidi ya miaka thelathini, arobaini. Lakini wamewekeza shughuli za kilimo pale kwa muda mrefu, sasa hivi mnawahitaji waondoke wale wananchi. Niwaombe sana Serikali wafanye namna yoyote ya kuona namna gani wanawatoa waweze kwenda kutafuta ardhi maeneo mengine kufanya shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru sana na ninaunga mkono hoja 100%. na nimtakie kila la kheri Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana kwenda kutekeleza miradi ambayo imeainishwa katika kupitia kitabu chake cha Hotuba ya Bajeti. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ZULFA MMAKA OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru *Allah* kwa kutujalia uzima na kuweza kuchangia leo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kazi kubwa ya kuijenga nchi yetu. Hakika ni Rais mwenye maono ya mbali. Pia nimpongeze Waziri na Naibu Waziri wake kwa jinsi wanavyoiongoza Wizara kwa umakini mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitajikita kwenye reli ya kisasa za *SGR*. Naamini reli hii imekuja kutatua shida za usafiri kwa Watanzania. Ila kuna shida pale unaposafiri na kamzigo chako cha zawadi kama vile korosho, ubuyu na vitafunwa vingine ambavyo sisi Watanzania tuna utamaduni wa kupelekeana zawadi. Ila kwa upande wa stesheni wanalazimisha uviache pale kwa sababu hairuhusiwi kubeba chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe muweke utaratibu maalum ili tuweze kubeba zawadi zetu, kwani kuna wanafunzi pia wanapotoka majumbani kuelekea *boarding* wanabeba chakula chao yaani vitafunwa kwa ajili ya kuwasaidia siku kadhaa, ila wanapofika stesheni wanaambiwa hairuhusiwi kubeba. Naomba hili liangaliwe kwa huruma sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JOSEPH Z. KAMONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya meli Ziwa Nyasa upande wa Ludewa tunaomba vibanda vya kupumzika abiria na vyoo. MV Songea ikarabatiwe ili ikahudumie wananchi Ziwa Nyasa, MV Mbeya iongeze safari Ziwa Nyasa walau kila wiki ili kuwaepushia wananchi hatari za kusafiri kwa mitumbwi na maboti ambayo mengine hayajahakikiwa ubora wake. Na pia Bandari ya Manda wananchi wa Igalu tunaomba walipwe fidia na ujenzi uanze.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namtanguliza Mwenyezi Mungu katika mchango wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri mno inayofanywa nchini kutokana na Wizara ya Uchukuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii Profesa Mbarawa kwa kuongoza Wizara na utekelezaji wa miradi mbalimbali na kazi nzuri tumeiona. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuendelee na pongezi nyingi kwa Naibu Waziri David Kihenzile, pia Katibu Mkuu, Naibu Katibu na watendaji wote wa Wizara hii. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu nitaanza na ujenzi wa viwanja vya ndege nchini; pongezi nyingi sana kwa Serikali kwa ujenzi wa viwanja vya ndege nchini kikiwepo kiwanja cha ndege cha Iringa, hongera sana. Tunaiomba sasa Serikali kabla haijaanza ujenzi wa viwanja vingine ufanyike upembuzi yakinifu ili kukamilisha majengo ya abiria. Uwanja wetu wa Mkoa wa Iringa umekuwa na abiria wengi sana na kumekuwa na changamoto kwa abiria hasa miundombinu ya vyoo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ATCL* napongeza uteuzi wa kiongozi wa shirika hilo Bwana Simbaulanga, kwa kipindi kifupi amefanya kazi nzuri sana na kwa niaba ya wananchi wa Iringa tunashukuru kwa kuanza kuleta ndege ya abiria katika kiwanja chetu cha Iringa, lakini hayo marekebisho yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa ushauri wangu hapa Dodoma ni makao makuu ya nchi yetu, ni vizuri ndege zote kuwe na safari za kuunga kutoka Dodoma mfano Mwanza - Dodoma, nia ya ushauri wangu kuwepo na ndege za kutoka maeneo yote lakini *connection* iwe hapa Dodoma ili kuwapa wepesi abiria wa maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa reli ya kisasa nchini ya *SGR;* pongezi nyingi sana kwa Mtendaji Mkuu wa Shirika la Reli Bwana Kadogosa kwa kazi nzuri sana aliyoifanya katika

shirika hili kwa sababu ujenzi wa reli nchini unakwenda kuponya hata barabara zetu, pia kuleta urahisi kwa huduma za usafiri na usafirishaji. Tunaomba sasa ujenzi uendelee kwa kasi kubwa na niungane na Kamati kuomba sasa Serikali inaaza ujenzi wa reli ya kisasa na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo baadhi ya malalamiko kwa abiria tunaomba yaangaliwe na yafanyiwe kazi ikiwemo mizigo inayozidi bei ni kubwa kuliko hata bei ya ndege, hili liangaliwe upya. Pia ikiwezekana kuwe na *open ticket* kama katika nchi nyingine ili kama utachelewa treni na hakutumia tiketi iweze kutumika kwa kubadilisha tiketi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niombe reli ya *TAZARA* ipewe kipaumbele kusimamiwa, pia naomba kujua yale malipo ya wafanyakazi wa *TAZARA* yalifikia wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kubwa sana kwa Serikali kuhusiana na uendeshaji bandari yetu kwa kweli ni mapinduzi makubwa sana, tumeona ongezeko kubwa la mapato. Hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja.

**MHE. MWANTUMU M. ZODO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa aliyoifanya kwenye Taifa letu kuhakikisha anatutoa sehemu moja kutupeleka sehemu nyingine.

Pia tunamshukuru Mheshimiwa Rais kwa kuendelea kuboresha viwanja vya ndege na usafiri wa anga kwa ujumla, kuendelea kuboresha vivuko pamoja na usafiri wa reli kwa ujenzi wa reli ya kisasa ambayo inakwenda kuleta mageuzi makubwa ya kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali yangu tukufu na sikivu kuendelea kuboresha viwanja vyetu vya ndege kikiwemo kiwanja cha ndege cha Tanga.

Pia naiomba Serikali kuendelea kuboresha vivuko vyetu hasa kivuko chetu cha Pagani, kivuko hiki kina changamoto kubwa na kinasababisha adha kubwa na kuhatarisha maisha ya wananchi wetu. Kivuko hiki mpaka sasa hakifanyi kazi, imekuwa changamoto sana kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee ninaomba kuungana na Watanzania wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kutimiza vyema miaka minne kwa kuongoza nchi yetu akiwa Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeshuhudia mafanikio makubwa katika kuimarisha miundombinu hususan barabara, reli, viwanja vya ndege, bandari, huduma za kiuchumi na kijamii kama vile ujenzi wa madarasa, hospitali, zahanati na vituo vya afya, huduma za maji, utawala bora, pamoja na kuhamasisha uwekezaji na utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi nzuri iliyotukuka ya kumsaidia Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, kwa kuteuliwa kuwa Mgombea Mwenza wa nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa uzoefu na weledi wake, kama ilivyo kwa Watanzania walio wengi, nina imani kubwa kwa Mheshimiwa Dkt. Nchimbi na kumtakia afya njema na kila la heri kwenye mchakato ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mbunge), Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati kwa kutekeleza majukumu ya kumsaidia Waziri Mkuu, ikiwa na pamoja na jukumu la kuendelea kuisimamia ipasavyo sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Spika na Naibu Spika na pia uongozi wote wa Bunge kwa uongozi mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi, kwa hotuba nzuri iliyojaa ubunifu mkubwa na imedhihirisha utayari wa Taifa letu katika ushindani wa kimataifa *(national competitiveness)*. Bajeti hii ambayo ni ya mwisho, inaenda sambamba na Dhima ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambayo ni "Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu."

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi chake akiwa Waziri wa Uchukuzi, tathmini zinathibitisha mafanikio makubwa ya utekelezaji na usimazi wa Mpango wa Kwanza na wa Pili na kupelekea Taifa letu la Tanzania kufanya vizuri mno kuinua uchumi katika kipindi hiki kigumu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha miezi tisa ya bajeti inayoishia Juni, 2025 Serikali kupitia Wizara ya Uchukuzi, imetekeleza miradi mingi ya miundombinu ya reli, bandari na uimarishaji wa safari za anga ikiwemo ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa hatua nzuri za utekelezaji wa mradi wa kihistoria wa ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR* pamoja na uboreshaji wa bandari utaimarisha kwa kiasi kikubwa uchumi wa nchi yetu. *SGR* na bandari ni nguzo imara ya kiushindani katika biashara ya usafirishaji wa ndani na nchi za Maziwa Makuu na hata za Kusini mwa Afrika na Kati. Bandari za

Tanzania ni lango la usafirishaji kwa Zambia, Malawi, DR Congo, Uganda, Burundi, Rwanda, Sudan ya Kusini na hata Zimbabwe na Msumbiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imefanya kazi kubwa kuhakikisha ujenzi wa *SGR* unaendelea kwa kasi ile ile na pia napongeza jitihada za kuendelea kutafuta vyanzo vya fedha vya masharti nafuu kugharamia ujenzi huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na ujenzi wa reli ya kisasa, Serikali imefanya maboresho makubwa ya miundombinu na huduma katika bandari zetu hususana Bandari ya Dar es Salaam ili kukabiliana na ushindani mkubwa wa bandari zingine za ukanda huu wa Afrika Mashariki na Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Dar es Salaam inakumbana na ushindani mkubwa toka Bandari za Mombasa (Kenya), Beira (Msumbiji), Nacala (Msumbiji), Durban (Africa Kusini), Lobito (Angola) na Walvis Bay (Namibia). Maboresho ya bandari zetu iendane na kuondoa changamoto zingine ambazo zinasababisha gharama kubwa za usafirishaji kwa bandari zetu na kusababisha kupoteza biashara ya usafirishaji kwa bandari shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufanisi wa bandari unategemea pia maboresho ya barabara, reli ya kati *(TRL)*, reli ya *TAZARA*, utendaji wenye tija wa wadau wote wa bandari na hata watumishi ili kupunguza gharama za usafirishaji kwa wateja wa bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa karibu 72% ya mzigo wote wa nchi za nje unasafirishwa kwa kupitia Dar es Salaam *Corridor* ambapo DR Congo ni 36%, Zambia 31% na Malawi 5%. Pamoja na fursa za kijiografia ya bandari zetu, mzigo unaopita sasa kwenye Bandari ya Dar es Salaam, ni 50% tu ya biashara yote ambayo kwa sasa inashikiliwa na bandari shindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ajili ya kunusuru biashara hii inayopotea kwa bandari shindani, Serikali ichukue hatua za

haraka kuboresha huduma za *TAZARA* ikiwa ni pamoja ya maboresho ya miundombinu ya reli, ununuzi wa vichwa vya reli, mabehewa na vitendea kazi vingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza Serikali kwa haraka ishughulikie maboresho ya mkataba wa *TAZARA* na kisha kutafuta washirika kutoka sekta binafsi kuwekeza katika uboreshaji wa miundombinu ya reli na hata uendeshaji kwa mfumo wa *PPP*. Katika kipindi hiki cha ushindani mkubwa na hata mfumuko wa bei wa mafuta ya petroli, mbolea na bidhaa mbalimbali, usafirishaji wa reli ni mojawapo ya suluhisho kubwa kupunguza mzigo wa bei kubwa kwa wateja wa bandari zetu na hata wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na maboresha ya reli ya *TAZARA,* napendekeza kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu Mbeya ambayo ina fursa kubwa katika kipindi hiki katika kuwezesha kupunguza gharama za kusafirisha kwa wateja wa bandari na hata kupunguza bei za mafuta ya petroli, pembejeo na mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari Kavu ya Mbeya ni njia panda kwa wateja wa nchi za Malawi, Zambia, DRC, Lubumbashi na hata kwa Zimbabwe na Msumbiji. Serikali ichukue hatua za haraka kuinusuru reli ya *TAZARA* hata ikibidi kurekebisha mikataba ya umiliki na uongozi ili mradi iendeshwe kwa tija. Kuna kuchukua hatua za makusudi kwa kutumia zaidi *TAZARA* kusafirisha mizigo ambayo imeelemea hata uwezo wa barabara zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa mizigo kwa kutumia *TAZARA* ilenge kupunguza gharama za mafuta ya petroli, pembejeo kwa wakulima na wakati huo kupunguza gharama za kusafirisha mazao ya wakulima. Pamoja na kuboresha *TAZARA,* napendekeza kukamilisha taratibu za ujenzi wa Bandari Kavu ya Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na changamoto za mfumuko wa bei za mafuta na pembejeo, kuna fursa kubwa na hasa mahitaji makubwa ya mazao ya kilimo kwa soko la ndani na

nje. Uzalishaji kwa tija unategemea kwa kiasi kikubwa ubora wa miundombinu ya reli na viwanja vya ndege ikiwa ni pamoja na uwanja wa ndege wa Songwe kwa usafirishaji wa mazao yetu kwa soko la ndani na nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboresho ya uwanja wa ndege wa Songwe uende sambamba na ujenzi wa maghala mahususi wa maua, mbogamboga, parachichi, nyama, viwanda vya kutengeza thamani za mazao na madini na *EPZ/Industrial Park*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa (Mbunge) na Naibu wake Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile (Mbunge), Profesa Godius W. Kahyarara - Katibu Mkuu, Bwana Ludovick J. Nduhiye - Naibu Katibu Mkuu, watumishi wote wa Wizara na taasisi zake kwa kazi kubwa wanazofanya kwenye kusimamia Wizara ya Uchukuzi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu wa leo utahusu mradi wa *Standard Gauge Railway (SGR)* hapa nchini Tanzania na changamoto zilizojitokeza kwenye utekelezaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uchumi wa nchi yoyote ile duniani, sekta ya uchukuzi na usafirishaji ni muhimu sana katika maendeleo ya kiuchumi. Hivyo basi, Serikali iliyo makini huchukua hatua madhubuti za kuimarisha sekta ya usafirishaji kwa kujenga miundombinu mbalimbali ya usafirishaji kama vile reli, kuimarisha usafiri wa majini na angani ili kuifungua nchi kushiriki katika shughuli mbalimbali za kijamii na uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu iliyo na viongozi makini, ilichukua maamuzi ya kimkakati kujenga reli ya kisasa ya *SGR* kusafirisha mizigo na abiria huu ukiwa ni mwarobaini wa kutatua changamoto ya usafirishaji na kulinda usalama na maisha ya barabara zetu hapa nchini. Pamoja na gharama kubwa za mradi huu, reli hii ya *SGR* ikikamilika itafanya mageuzi makubwa katika

sekta ya usafirishaji kwa maslahi makubwa ya kiuchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali kwa uamuzi huu makini wa ujenzi wa reli ya hii ya kisasa ya *SGR*. Historia inaonesha kwamba ujenzi wa reli ya kwanza hapa nchini ulifanyika mwaka 1912 takribani miaka 113 iliyopita ambapo Serikali ya kikoloni nchini iliamua kuimarisha sekta ya usafirishaji na kujenga reli kwa lengo la kuunganisha miji katika maeneo ya kilimo, uzalishaji na kibiashara ambapo reli hiyo iliunganisha Dar es Salaam yenye bandari na miji ya Mwanza, Kigoma, Tanga na Arusha. Reli ya pili ya *TAZARA* ilijengwa na Serikali ya Awamu ya Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *SGR* ni mradi mkubwa wa kihistoria ambao unatekelezwa na Serikali kwa kutumia fedha za walipa kodi wake kwa gharama ya shilingi trilioni saba. Mradi huo ni mkubwa na uwezo wake ni wa juu na sasa matatizo ya usafarishaji nchini yatapata suluhu kubwa kwani unakwenda kuimarisha na kulinda miundombinu ya barabara zetu zilizokuwa zimeelemewa na mizigo kupitia malori makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwekezaji katika sekta hii ya uchukuzi umeimarisha sana usafirishaji wa abiria kwani *SGR* yenye kasi ya kilometa 160 kwa saa inachukua saa tatu kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma na inakadiriwa itachukua saa nane kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Reli hii imeleta furaha kubwa kwa watu kwani wasafiri walikuwa wanatumia saa tisa hadi 10 kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma kwa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mizigo, tunaishukuru Serikali kwani katika hotuba ya bajeti iliyosomwa leo tarehe 15 Mei, 2025 Serikali imesema huduma hiyo itaanza mwezi Juni, 2025. Reli hii ya *SGR* itakuwa na uwezo wa kubeba tani milioni 10,000, kwa mkupuo sawa na malori 500 yenye tani 20, treni tano zenye tani 10,000 na kuwa na kasi kubwa ya kilometa 160 kwa saa, tofauti na ya sasa ambayo ina kasi ya kilometa 30 kwa saa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inasemekana kwamba katika Bara la Afrika itakuwa ni reli pekee yenye uwezo mkubwa kama huo, tani milioni 10 -17 zitasafirishwa kwa mwaka, kwa hiyo, *SGR* itakuwa mwamba katika sekta ya usafirishaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli ya *SGR* inaweza kuwa njia rahisi na nafuu ya kusafirisha mazao kwenda masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa yale mazao yanayoharibika haraka, ni muhimu Serikali iwekeze kwa kununua mabehewa ya kubeba mazao haya na kuboresha miundombinu ya kuhifadhi mazao yanayosafirishwa nje kama mbogamboga au nyama ili kuhifadhi ubora. Katika zile stesheni za kimkakati, ni vyema Serikali ikajenga *cold rooms* zitakazotumia kuhifadhi mazao yanayoharibika haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya usafirishaji wa mizigo hasa ile mikubwa inayotoka bandarini kwenda sehemu zingine za nchi na nyingine nje ya nchi, uwepo wa reli imara kama hii ya *SGR* itasababisha utendaji kazi wa bandari zetu za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Zanzibar kuwa na ufanisi mkubwa. Ufanisi wa bandari hizi unategemea sana uwepo wa miundombinu imara kwa upande wa nchi kavu, kama reli imara. Serikali yetu yenye viongozi imara imeliona hilo ndiyo maana ikatekeleza ujenzi wa reli ya kisasa ya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa reli ya *SGR* umetupeleka kwenye teknolojia mpya kabisa ya reli na katika sekta ya usafirishaji, kwani matatizo mengi ya barabara yanatokea kwa sababu ya mizigo mizito na ilikuwa hakuna reli imara ya kubeba mizigo hiyo. Kwa hiyo, ujenzi wa reli hii ni maamuzi sahihi yaliyofanywa na Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali yetu kwa maono haya. Ili kwenda sambamba na teknolojia hii mpya. Naishauri Serikali kuwapa mafunzo wataalam wa ndani watakaosaidia kutatua changamoto za kiufundi kwenye uendeshaji wa mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hiyo ambayo inatumia nishati ya umeme imekuja wakati muafaka ikiwa Serikali inatekeleza mradi mkubwa wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji *(Rufiji Hydroelectric Power)* wenye kutoa megawati 2,115, kwa hiyo, kama mipango itawekwa sawa, treni hiyo itapata umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza sana Serikali kwani hadi sasa ujenzi wa kipande cha kuanzia Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma kimekamilika na kuanza kutumika. Serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa mradi huo kuelekea Mwanza (kilometa 1219) na baadaye Tabora - Kigoma (kilometa 506), na Uvinza - Musongati (kilometa 240). Ninaishauri Serikali iendelee kuwekeza kwenye mradi huu kama ilivyopangwa ili tupate suluhisho la usafirishaji abiria na mizigo kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na nchi jirani za DRC Congo, Burundi, Rwanda na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kukamilika kwa mradi huo kutakuwa na ufanisi mkubwa kwenye sekta ya usafirishaji nchini kwa kubeba mizigo tani nyingi, lakini pia kasi yake katika kusafirisha abiria, kutoka Dar es Salaam - Dodoma ambapo treni inafanya safari mara nane kwa siku, hivyo kuleta mafanikio makubwa katika sekta ya usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mradi huu kuelekezwa Kanda ya Kati na Kanda ya Ziwa, ninaiomba Serikali ijenge reli ya *SGR* itakayounganisha Mikoa ya Kaskazini (Tanga, Kilimanjaro na Arusha). Ninaleta ombi hili kwa sababu upanuzi wa reli kuelekea Mikoa ya Kaskazini italeta faida kubwa sana za kiuchumi. Mikoa ya Kaskazini ina malighafi za kutengeneza cementi *(gypsum),* madini ya *soda ash* ambayo inasemekana yatachimbwa kwa zaidi ya miaka 100. Usafiri wa uhakika unahitajika kubeba shehena za mizogo hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa utalii kuna vivutio maarufu kama Milima ya Kilimanjaro na Meru, mbuga maarufu za wanyama za Kilimanjaro, Arusha, Tarangire, Mkomazi, Manyara, Serengeti na Ngorongoro. Ujenzi wa reli ya *SGR* itakuwa

chachu ya maendeleo kwa Mikoa ya Kanda ya Kaskazini kwa kurahisisha kusafirisha mizigo na watalii kwenda maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafanikio tuliyoyapata, ninaishauri Serikali iboreshe mambo yafuatayo ili kuondoa baadhi ya kero zilizojitokeza kwenye kuwahudumia wasafiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kawaida kitu kipya mara nyingi huwa na changamoto. Huduma za usafiri wa *SGR* zimekabiliwa na changamoto za kukatikakatika umeme mara kwa mara. Ninaishauri Serikali ihakikishe kuwa umeme unakuwa wa uhakika katika mradi huu wa kielelezo ili usiwe mradi wa kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye vituo vya kupanda na kushusha abiria, maeneo ya kukaa abiria ni madogo sana. Hii imekuwa kero na inasababisha msongamano mkubwa wa watu jambo ambalo siyo jema kiafya. Ninaishauri Serikali ijenge maeneo ya kutosha kwa ajili ya abiria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye stesheni za *SGR* kuna viti vichache vya kukalia abiria. Kwenye vituo hivi kuna abiria wengi ambapo wengine hawawezi kusimama muda mrefu kutokana na umri au magonjwa. Ninaishauri Serikali ihakikishe kila stesheni inakuwa na viti vya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wasafiri wengi wa *SGR* wanaopenda kusafiri na mizigo, lakini menejimenti ya *SGR* imeweka kikwazo cha kusafiri na mizigo ya ziada. Ninaishauri Serikali iruhusu mizigo kwa kulipia kila uzito unaozidi kama wanavyofanya kwenye ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto nyingine kubwa ni ile ya ukosefu wa usafiri wa uhakika na unaoeleweka wa kuchukua na kuleta abiria stesheni. Kuna malalamiko makubwa ya shida ya usafiri kutoka na kuingia vituo vya *SGR*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaishauri Serikali ishirikishe wadau mbalimbali ili wachangamkie fursa hii ya kuondoa shida ya usafiri wa kuingia na kutoka katika vituo vya *SGR*. Ni vyema viongozi wa

mikoa husika ambako *SGR* inapita wahakikishe unakuwepo usafiri wa uhakika ili wananchi wasipate shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nihitimishe kwa kusema kwamba ujenzi wa reli ya *SGR* unaenda kuimarisha sekta ya usafirishaji hapa nchini. Tumeonesha kwamba nchi yetu inaweza kufanya makubwa ikiwa tutajipanga vizuri. Ujenzi wa reli hii ukikamilika, Taifa litanufaika kwa kiwango kikubwa. Nisisitize kwamba kuna umuhimu wa kujenga reli ya *SGR* kuelekea mikoa ya Kanda ya Kaskazini ili pia iwe chachu ya maendeleo katika maeneo haya na nchi yetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo yangu hapo juu, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida Mohamed, ahsante sana. Sasa namkaribisha Mheshimiwa Naibu Waziri, Wizara ya Uchukuzi Mheshimiwa David Mwakiposa Kihenzile.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia katika mjadala wa hotuba yetu leo na kabla sijaanza nitumie nafasi hii kumshukuru Rais wetu mpendwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ambaye kimsingi ndiye ambaye ametuamini lakini ndiye anayetoa fedha na anayetoa miongozo yote katika sekta yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kuwashukuru Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri wetu Mkuu, Mheshimiwa Naibu Waziri Mkuu ambao ndiyo viongozi na wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais katika kazi yetu hii ya kujenga taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee pia nitumie nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri wetu mpendwa, Mheshimiwa Profesa Makame Mbarawa Mnyaa ambaye ndiye ambaye anayetuongoza kwenye sekta kwa kutusaidia na kutuongoza wakati wote ili kutimiza malengo ambayo Mheshimiwa Rais ameweza kutukabidhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hiyo pia kumshukuru Katibu Mkuu wa Wizara yetu Mheshimiwa Kahyarara na Naibu wake Mheshimiwa Nduhiye pamoja na watendaji wote, Wakurugenzi Makao Makuu pamoja na Watumishi kwa ujumla, Wakuu wa Taasisi, Wenyeviti wa Bodi pamoja na Wajumbe wa Bodi Mbalimbali ambao kimsingi tunashirikiana nao katika shughuli za kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimeona Watumishi wenzetu wako hapa, wahudumu kwenye sekta zetu mbalimbali, wapo wa kwenye ndege, wapo wa kwenye meli, wapo wa kwenye treni. Wote tunawashukuru sana kwa sababu wanatupa ushirikiano mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kipekee pia nitumie nafasi hii kuwashukuru viongozi wenzangu katika wilaya yetu ya Mufindi kwa kutuongoza, Chama Cha Mapinduzi na Serikali lakini Wanaccm wenzangu na Wananchi wa Jimbo la Mufindi Kusini kwa kuendelea kuniamini na kunisaidia katika kutimiza majukumu yangu haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kushukuru familia yangu kwa kazi ambayo wananisaidia kunivumilia kwenye majukumu ya kila siku. Aidha, Mheshimiwa Spika mwenyewe ambaye ndiye kiongozi wetu akisaidiwa na Naibu Spika na wewe mwenyewe Mheshimiwa Mwenyeti na Wenyeviti wengine kwa kazi kubwa mnayomsaidia katika kuongoza kazi hii pamoja na Kamati yetu ya kisekta na Kamati zingine na Wabunge wote wa Bunge hili kwa kazi ambayo wanaifanya ya kujenga Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji katika kikao cha leo walikuwa wengi lakini pia siku za huko nyuma tulipokea michango mbalimbali ambayo inagusa sekta yetu. Mheshimiwa Waziri yote kwa umoja wake ameweza kuipokea amejipanga kama sekta kwa ajili ya kufanyia kazi. Nishukuru kipekee waliochangia kwa maandishi na waliochangia moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, michango ya leo inadhihirisha mambo mengi lakini kwa uchache inadhihirisha umakini na uhimara wa Bunge letu Tukufu la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwamba ni Bunge la vitendo, Bunge la matokeo lakini pia inathibitisha umadhubuti wa CCM kuwa tayari katika kuendelea kuongoza nchi yetu leo, kesho na kesho kutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia Bunge hili linazidi kudhihirisha kwamba ni Bunge la maslahi ya wananchi. Bunge la matokeo zaidi. Lakini mwisho wa michango hii imepeleka sifa nyingi sana kwa Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ambaye kipekee kupitia anavyotuongoza kwa miaka hii minne ameonyesha kipaji cha uongozi, ameonyesha upekee katika uongozi, ameonyesha maono katika uongozi, utulivu wa hali ya juu hata pale kunapokuwa na kelele nyingi katika nchi yetu. Lakini yeye amekuwa ni mtulivu akiendelea kuchapa kazi zake vizuri, tumuombee Mheshimiwa Rais maisha marefu na afya njema ili aendelee kuipaisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu imebahatika kuwa katika nafasi nzuri ya kimkakati na imekuwa ni maombi ya wananchi pamoja na Wabunge mbalimbali hapa wakati wote kwamba tutumie faidi hii ya kuwepo kwetu kimkakati kuweza kulisha au kuhudumia karibu nchi nane ambazo hazina bandari zinatutegemea sisi. Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhihirisha hilo amefanya maamuzi mbalimbali ni mashahidi mwaka juzi tu hapa tulipokuwa tunazungumzia habari ya kuongeza wawekezaji binafsi katika sekta yetu ya bandari kulikuwa na kelele nyingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kelele zile maamuzi aliyoyafanya ya kuingiza wawekezaji hawa pamoja na faida nyingine nyingi naweza kuongea mambo makuu mawili. Kwanza kama ilivyozungumzwa na wenzangu ni kuongezeka kwa fedha za kikodi, mapato ya kikodi karibu trilioni 1.2 ambayo kutoka 7.08 mpaka kufikia 8.2 ngapi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukiacha hiyo imeongezeka pia gharama za matumizi kwenye bandari za uendeshaji

zimeshuka kwa takribani bilioni 290, ukichukua kipengele hiki peke yake unaona karibu trilioni 1.5 imeweze kutengenezwa katika mwaka huu mmoja. Ndiyo maana napata ujasiri sasa wa kuongeza mishahara ya wafanyakazi, anapata ujasiri sasa wa kuongeza fedha kwenye barabara, anapata ujasiri sasa wa kupeleka fedha kwenye maji huu ni utulivu na umakini wa hali ya juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jambo hilo kubwa ambalo limefanyika Dkt. Samia Suluhu Hassan ameamua kubadili hii Sekta ya Uchukuzi kwa kufanya maboresho katika maziwa makuu. Limezungumzwa hoja ya kwanza hapa namna ya kuongeza usafirishaji kwenye upande wa bahari. Baharini tayari alishatoa maelekezo tumeishampata mkandarasi hivi ninavyozungumza anafanya usanifu kutazama biashara iliyopo katika ukanda wa bahari yetu pamoja na maeneo jirani kama kina Visiwa vya Comoro na maeneo mengine. Itakapokamilika katika mwaka wa fedha utakaofuatia tutaanza maandalizi kwa ajili ya kujenga meli hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pili katika maziwa makuu amezungumza Mheshimiwa Kilumbe pale Dkt. Samia Suluhu Hassan kazi kubwa aliyoifanya ya kihistoria moja ni kukarabati meli zote zilizopo katika Ziwa Tanganyika. Hivi navyozungumza Meli ya *MV* Mwongozo tayari Mkandarasi amepatikana, hivi navyozungumza Meli ya Liemba tayari Mkandarasi amepatikana na anajenga yuko asilimia 15. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi navyozungumza MT Sangara ipo asilimia 98 pamoja na hilo tunajenga kiwanda kikubwa cha kujengea meli na kukarabati meli katika Ziwa Tanganyika na hii ni kwa sababu kwenye Ziwa Tanganyika nchi kubwa ambazo zinamiliki ziwa hilo ni Tanzania pamoja na Congo. Maana yake ni nini? Tukiyafanya haya yote usafiri wa reli ya *SGR* utakaofungamanishwa na bandari ambazo zimejengwa kwenye Ziwa hilo utarahisishwa sana na meli hizi ambazo zinajengwa. Hii ni habari njema sana kwa wenzetu wa Mikoa ya Kigoma, Katavi pamoja na Rukwa kwa namna ambayo itakwenda kuwanufaisha zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika kuvutia wawekezaji Serikali imefanyakazi kubwa kuvutia wawekezaji. Ninapozungumza hapa tayari tunaye mkandarasi ambaye anajenga meli nne kwa mkupuo za tani elfu mbili mbili na inategemewa ndani ya miaka miwili kuanzia tarehe 01Aprili, 2025 zitakuwa zimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi yake itakuwa ni kuchukua madini kutoka Kalemi ambako bandari inajengwa kuja mpaka bandari zetu na kisha zitasafirishwa kwenda mpaka Dar es Salaam na mwaka wa kwanza tutakuwa na *almost* tani laki sita, maboresho haya yanakwenda sambamba kwenye maziwa, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa David Kihenzile Mwakiposa, Naibu Waziri wa Uchukuzi. Sasa hivi ninamkaribisha mtoa hoja, Profesa Makame Mbarawa, Waziri wa Uchukuzi aweze kuhitimisha hoja yake.

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kukutana katika hili Bunge letu Tukufu la Bajeti ili kukamilisha kazi tuliyoanza leo asubuhi ambapo niliwasilisha hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii pia kuanza kumshukuru Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, wewe mwenyewe na Wenyeviti wote wa Bunge kwa jinsi mlivyoongoza na kusimamia majadiliano haya, hii ni pamoja na hoja nyingine zilizotangulia. Aidha, nichukue fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuwa wazi na kutoa michango yao ya kina wakati wa majadiliano haya yaliyopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninathibitisha kwamba michango ya Waheshimiwa Wabunge yote tumeichukua kwa uzito mkubwa

na tunakwenda kuifanyia kazi ili iendelee kuleta ufanisi kwenye sekta ya uchukuzi pamoja na sekta ya usafiri na usafirishaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kipekee nimshukuru Mwenyekiti wetu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Sulemani Moshi Kakoso na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa maoni yao mazuri waliyoyatoa pamoja na michango yao. Ninakiri kwamba hoja hizo na maoni yao ni muhimu sana kwa maendeleo na ukuaji wa miundombinu, huduma za usafiri na usafirishaji hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kutumia fursa hii pia kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia katika bajeti hii. Waheshimiwa Wabunge 15 wamechangia wakati wa majadiliano ya hoja hii, ambapo Waheshimiwa 14 wamechangia kwa kuaongea na Mheshimiwa mmoja amechangia kwa maandishi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mchache uliopita Mheshimiwa Naibu Waziri amemalizia kuchangia na kutoa ufafanuzi wa baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa ufasaha na weledi mkubwa. Ninakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi ambavyo umejibu baadhi ya hoja za Waheshimiwa Wabunge na mimi nitajikita zaidi kuzungumzia hoja zilizosalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nianze kuhitimisha hoja yangu kwa kutoa ufafanuzi wa kiujumla kwa maoni ya Kamati ya Miundombinu na baadhi ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge. Tunafahamu kwamba sekta ya uchukuzi ni muhimu sana, katika mwaka wa fedha 2024/2025, sekta ya uchukuzi iliendelea kutoa mchango chanya katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. Mchango huo umewezesha kuendelea kukua kwa sekta nyingine za uzalishaji kama vile sekta ya kilimo, madini, utalii, viwanda na biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka 2023 sekta hii ilikua kwa 4.1% na kuchangia takribani Pato la Taifa 7.2%. Aidha, kwa

kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2024 – Machi, 2025, sekta ya uchukuzi ilichangia mauzo ya kiasi cha dola za Kimarekani bilioni 2.48 ya fedha za kigeni, sawa na ongezeko la 8.30%, ikilinganishwa na dola za Kimarekani bilioni 2.29 zilizopatikana katika mauzo ya kipindi kama hicho mwaka 2023/2024.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sasa nijikite kwenye maoni ya Kamati yetu ya Kudumu ya Miundombinu. Kwanza, tumekubali kwamba tumeyachukua na tunaenda kuyafanyia kazi, ni maoni mazuri. Pia, kuna maoni machache ambayo ninatamani niyazungumzie kwa ufupi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la kwanza kuhusu kuboresha miundombinu ya viwanja vya ndege. Kamati yetu imetoa maoni ya kukamilisha zoezi la upatikanaji wa hati. Serikali kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imeendelea na jitihada za upangaji, upimaji na ukamislishaji wa maeneo katika maeneo ya viwanja vya ndege nchini, ambapo hadi hivi sasa imefanikiwa kupata jumla ya hati ya vya ndege 35. Aidha, zoezi la upimaji na upangaji wa viwanja vya ndege Nane vya Tabora, Dodoma, Manyoni, Kondoa, Ngara, Mwanza, Mafia, na Masasi lipo katika hatua ya mwisho ambapo hatimiliki za viwanja hivyo zinatarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa huu Mwaka wa Fedha 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya pili ilikuwa ni kuboresha miundombinu ya Kiwanja cha Ndege cha *KIA*. Katika kuhakikisha kwamba miundombinu ya Kiwanja cha Ndega cha *KIA* inaboreshwa ili kuendana na ubora wa kimataifa Serikali inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali katika kiwanja cha ndege hicho. Kwanza, mradi ambao tunaendelea kuujenga ni ukarabati mkubwa wa njia ya kurukia na kutua ndege ili iendane na ndege kubwa zinazokuja sasa hivi. Kazi ya pili inayofanyika ni; ujenzi wa Jengo Wageni Mashuhuri *(VIP* na *CIP)*. Mradi wa tatu utakofanyika hapo ni ujenzi wa jengo la kuhifadhia mizigo pamoja na ukarabati mpya wa jengo la abiria ili kuendana na hali halisi ilivyo sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufanikisha yote haya kwenye bajeti ya mwaka huu tumetenga takribani shilingi bilioni 35. Tunaamini kazi ya kuwapata wakandarasi itaanza hivi karibuni na baada ya hapo kazi ya ujenzi itaendelea. Maoni ya tatu yaliyotolewa na Kamati yetu ni kuhusu uendeshaji wa shughuli za reli kwa kushirikana na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzoefu umeonesha hasa tukichukua bandari kwamba, sekta binafsi ndiyo inakuwa ni *engine* ya maendeleo ya nchi. Leo hapa Wabunge wote wamesema na kuzungumzia juu ya maendeleo na faida iliyopatikana kwa uwekezaji wa sekta binafsi katika bandari ya Dar es Salaam. Kwa hiyo, ninaomba niwahakikishie Kamati yetu kwanza na Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwenye upande wa *SGR* tunakwenda kushirikisha sekta binafsi. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari Sheria ya *Open Access* tulishapitisha hapa Bungeni na sisi Wizara tayari tumeshatayarisha Kanuni za *Open Access* kwa ajili ya kufanya kazi hiyo. Tayari wapo Kampuni za Watanzania mbalimbali ambao wameonesha nia ya kufanya kazi ya uendeshaji wa *SGR* ya kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma hasa kwenye eneo la mizigo, kwa sababu biashara kubwa sana ipo kwenye mizigo. Kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba itakapofika Mwezi Juni, kazi hiyo ya usafirishaji wa mizigo kutoka bandarini Dar es Salaam – Dodoma itaanza rasmi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya Kamati pamoja ya baadhi wa Wabunge wamezungumzia kuhusu Reli ya Kusini. Reli ya Kusini ni muhimu sana kwa sababu kule kuna madini mengi na ninaamini tukijenga reli hiyo itafungua sana uchumi wa nchi yetu hasa kwenye sehemu ya upande wa kusini. Jambo hili tunalifahamiu na tumeshalifanyia kazi, tumeshafanya *feasibility study.* Hivi ninavyozungumza Serikali ipo katika hatua ya kutafuta fedha kwa ajili ya ujenzi wa hiyo Reli ya Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru Wabunge wengi waliochangia kuhusu *SGR*. *SGR* kwa sasa kutoka Dar es Salaam – Dodoma imebadilisha maisha ya watanzania. Zamani watanzania

walikuwa wanatumia saa Tisa Dar es Salaam – Dodoma, leo wanatumia saa tatu. Hii ni rekodi mpya ninafikiri kwenye Nchi za Afrika ukiondoa Morocco kwa sababu wana *high speed train,* lakini nchi zote nyingine hizi *speed* ya treni ya Tanzania ipo juu sana. Watanzania wote wanafurahia, sisi sote Wabunge karibu kila siku hapa tunapanda *SGR* kutoka Dar es Salaam – Dodoma na Dodoma – Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua faida hizo, Serikali inaendelea kujenga kwa kasi vipande vilivyobakia, hasa kipande cha kutoka Makutopora – Tabora ambayo sasa hivi ipo 14.53%; kipande cha nne cha kutoka Tabora – Isaka ambacho kipo 6.5%; na kipande cha tano kutoka Mwanza – Isaka ambacho kipo 63.16%. Vilevile, kipande cha Tabora – Kigoma ambacho kipo 7.88%. Serikali inaenda kujenga na kwenye bajeti hii wote ni mashahidi. Serikali imetenga takribani Shilingi trilioni 1.8 kwa ajili ya ujenzi wa vipande hivyo. Tunaamini kila Wakandarasi watakavyomaliza kufanya kazi yao, wakileta *certificate* tutalipa kwa wakati ili kuhakikisha kwamba mradi huo unamalizika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwenye hotuba yangu kwamba Mwezi wa Juni tutaanza kazi ya usafirishaji mizigo kutoka Dar es Salaam – Dodoma. Tumejipanga vizuri, mabehewa yapo na tunaamini tukifanya hivyo tutapunguza sana ule msongamano kwenye Bandari pamoja na Jiji la Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia kuhusu ushirikishwaji wa sekta binafsi katika miundombinu. Ushirikishwaji wa sekta binafsi ndiyo njia pekee ambayo itatutoa hapo tulipo. Kwenye bandari tumefanya na tumeona mafanikio makubwa. Kama nilivyosema kwenye *TRC* tunakwenda kufanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nigusie haraka Mheshimiwa Mnzava alikuja na hoja barabara ya Tanga – Handeni – Kibirashi – Chemba. Barabara hii ni muhimu, Bandari ya Tanga sasa hivi imeunganishwa na barabara mbili, Barabara ya Chalinze na Arusha. Ukitumia barabara kutoka Tanga – Handeni –

Kibirashi – Chemba hasa kwa mizigo inayokwenda *DRC*, Zambia, Burundi na maeneo mengine, unapunguza takribani kilomita 100 ukilinagnisha na barabara ya Chalinze. Kwa vile barabara hii kama Mheshimiwa Rais alivyotuelekeza tunaenda kuijenga kwa *PPP,* ushirikiano kati ya *TPA* na *TANROADS*. Tayari tumeanza vikao kwa ajili ya kuona jinsi gani tutaanza kuijenga lakini barabara hii ni muhimu. Tunaamini tukijenga barabara hii itajiendesha yenyewe kwa sababu mzigo upo na ni barabara ambayo italeta faida kubwa kwa watumiaji wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Mnzava vilevile amezungumzia kuhusu Bandari za *Trans-shipment* ni kweli na sisi kwa kulitambua hilo, tumeanza Bandari ya Bagamoyo na tunaenda bandari zingine kuhakikisha kwamba, tunazijenga bandari kubwa kwa ajili tu ya mizigo ya *trans-shipment* kutoka eneo moja kupeleka lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala la Kiwanja cha Ndege cha Lindi tumeshapata Mkandarasi na gharama yake ni takribani bilioni 120. Sasa hivi tunatafuta fedha kwa ajili ya kulipa *advance payment* ili kazi hiyo iweze kufanyika mara moja. Kuna hoja ya viwanja vya ndege vya Mkoa wa Simiyu, Njombe, Singida na Manyara, hivi vilevile tumetenga kwenye bajeti. Ukienda kwenye kitabu chetu utakuta tumetenga bilioni 22 kwa ajili ya kazi hiyo ili kuhakikisha kwamba na viwanja vya ndege vyote vya Mikoa ya Tanzania vinajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na hoja ya Mheshimiwa Mwantumu kuchelewa kwa safari ya ndege ya *Air* Tanzania, tumelichukua na tunaenda kulifanyia kazi ili kuhakikisha kwamba sasa *delays* zilizokuwepo hizi zimepungua. Kwa ufupi *delays* hasa kwa ndege kubwa zimepungua bado tuna changamoto kidogo kwa *delay* kwenye *Q400* kunapokuwa na matatizo, lakini tumelichukua hili na tunaenda kulifanyia kazi kuhakikisha kwamba sasa *delays* zote zinamalizika kwa asilimia kubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kilumbe yupo hapa, Mheshimiwa Naibu Waziri amezungumza *MV* Mwongozo tayari ameshapatikana Mkandarasi na kwenye bajeti ya mradi huo ni

bilioni 9.1 na kwenye bajeti hii tayari tumetenga bilioni Nane kwa ajili ya kuanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ufafanuzi huo sasa ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Profesa Makame Mnyaa Mbarawa. Hoja imeungwa mkono.

Katibu, tuendelee.

**NDG. NEEMA MSANGI – KATIBU MEZANI:** Kamati ya Matumizi

## KAMATI YA MATUMIZI

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaingia Kamati ya Matumizi.

*Hapa Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:**

## KITABU CHA PILI

## MATUMIZI YA KAWAIDA

### Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resources Management*…….............................Sh. 3,344,871,000
Kifungu 1002 – *Finance and Accounts Unit*…......…..Sh. 823,923,000
Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*……….....…Sh. 1,538,086,000

Kifungu 1004 – *Government Communication Unit*….Sh. 409,489,000
Kifungu 1005 – *Procurement Management Unit*........Sh. 718,665,000
Kifungu 1006 – *Internal Audit Unit*…………….............Sh. 576,567,000
Kifungu 1007 – *Legal Services Unit*……………….…….Sh. 595,697,000
Kifungu 1008 – *Information and Communication Technology Unit*…………..……………Sh. 639,525,000
Kifungu 1009 – *Monitoring and Evaluation Unit*…..…Sh. 814,788,000
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*........Sh.1,504,824,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*...........Sh. 113,110,496,000
Kifungu 2007 – *Air Transport Accidents Investigation Unit*……………………..……………Sh. 216,972,000
Kifungu 5002 – *Transport Safety and Environment Division*………………………………Sh. 1,145,047,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**KITABU CHA NNE**

**MIPANGO YA MAENDELEO**

**Fungu 62 – Wizara ya Uchukuzi**

Kifungu 1003 – *Policy and Planning Unit*…………Sh. 236,162,894,600
Kifungu 2005 – *Transport Infrastructure Division*.Sh. 1,857,082,670,000
Kifungu 2006 – *Transport Services Division*……....Sh. 527,800,503,400

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

**NDG. MONICA MWAGA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

**MWENYEKITI:** Bunge linarejea.

*(Bunge Lilirejea)*

**SPIKA:** Waheshimiwa tuketi. Mtoa Hoja, Taarifa.

**T A A R I F A**

**WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa taarifa kwamba, Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, limekamilisha kazi yake, ninaomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, ninaafiki.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, hoja imeungwa mkono. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Sasa, nitawahoji Waheshimiwa Wabunge wanaoafiki hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Wote mmeafiki. *(Makofi)*

*(Hoja ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Wizara ya Uchukuzi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 Yalipitishwa na Bunge)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuhojiwa na ninyi kuitika ndiyo, sasa nitangaze rasmi kwamba Bunge limepitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Uchukuzi kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi, Naibu waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii tunawapongeza sana kwa bajeti hii ambayo Bunge limeamua kupitisha siku ya leo, pia tunawatakia kila la kheri katika utekelezaji wa yale ambayo mmeyasema humu kwamba mnaenda kutekeleza kwa ajili ya kuwaletea wananchi wa Tanzania maendeleo kwenye hili eneo la uchukuzi. *(Makofi)*

Pia nitumie fursa hii kumshukuru sana Mwenyekiti wetu wa Kamati yetu ya Miundombinu, Mheshimiwa Kakoso pia Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Anne Kilango wanafanya kazi nzuri sana ya kuisimamia Kamati hii na sasa tunaona mambo mazuri yanaendelea kufanyika pia tuna matumaini ya mazuri zaidi kuendelea kufanyika. Kwa hiyo, Mwenyekiti na Kamati yako tunakushukuru sana kwa kazi nzuri ya kuisimamia sekta hii ya uchukuzi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, wote mawazo yenu kama alivyohitimisha hapa Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, mawazo mliyoyatoa, mapendekezo na maoni mliyoyatoa yamepokelewa, basi bila shaka yataendelea kufanyiwa kazi. Hivyo basi, nitumie fursa hii kuwashukuru wote kwa pamoja katika ushiriki wenu kwa kuhakikisha sekta hii wanashauriwa ipasavyo.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo basi ninaahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 7.23 Mchana Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Ijumaa, Tarehe 15 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*